Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Kumi na Nane - Tarehe 4 Julai, 2003**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU (k.n.y. MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO - MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU):**

Taarifa ya Kamati ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi katika mwaka uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2003/2004.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 170

**Kampuni ya *Tanzania Parking System***

**MHE. OMAR S. CHUBI** aliuliza:-

Kwa kuwa tangu kuanzishwa kwa Kampuni ya *Tanzania Parking Systems* kumekuwa na vitendo vingi vya kero kwa waegesha magari kama vile kuvutwa kwa magari na kupelekwa trafiki kwa uegeshaji bila taarifa, kudaiwa gharama za *Breakdown* na kutumika kwa lugha chafu upande wa wahudumu wa kampuni husika:-

(a) Je, tangu kampuni hiyo ianzishwe imechangia kiasi gani cha fedha kwenye Pato la Taifa?

(b) Je, ni huduma gani imeboreshwa kwenye maegesho hayo hadi kuhitaji watoze kodi?

(c) Je, ni kwa nini kampuni hiyo isichukue jukumu la kuhakikisha usalama wa magari yanayoegeshwa kwenye *Parking Systems* zake ili pindi yakiibiwa iweze kuwajibika moja kwa moja?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Chubi, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 1997 hadi sasa Kampuni ya *Tanzania Parking Systems* imekusanya shilingi bilioni 4.7 na imeilipa Halmashauri ya Jiji shilingi milioni 763 bado shilingi milioni 415.6 sawa na asilimia 25 ya makusanyo yote yaliyopaswa kulipwa. Fedha zilizopatikana zimeisaidia Halmashauri ya Jiji kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo Jijini Dar es Salaam. Aidha, Kampuni hiyo inalipa kodi ya mapato kwa Serikali na watumishi 250 katika kampuni hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Jiji imelazimika kutoza ushuru baada ya kuboresha huduma zifuatazo katika maeneo yaliyotengwa rasmi kwa ajili ya maegesho ya magari:-

(i) Mashine maalum za kukatia tiketi zimewekwa katika mitaa mbalimbali ya katikati ya Jiji ya Samora, Sokoine, Libya, Stesheni, Posta ya Zamani, Posta Mpya, Lumumba, Kitumbini, Kivukoni, maeneo ya *Oysterbay* na Muhimbili.

(ii) Alama maalum zilizowekwa kuonyesha sehemu na mipaka ya maegesho ili kuimarisha usalama.

(iii) Wapo Wasimamizi wa maegesho katika maeneo ya mitaa yaliyotengwa kwa ajili ya maegesho ya magari.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mkataba uliopo Kampuni ya *Tanzania Parking System* haina jukumu la kulinda magari ya wateja. Hata hivyo, watumishi wa *TPS* wanasaidia kutoa ulinzi wa jumla wanapokuwa katika maeneo yao ya kazi na kwa

mujibu wa Kifungu cha 11-12 cha Sheria Ndogo ya Maegesho ya magari ya mwaka 1998, Wakala wa kukusanya ushuru anao wajibu wa kumhoji mtu anayetaka kutoa gari sehemu ilipoegeshwa endapo ana wasiwasi na mtu huyo kama ndiye aliyeegesha gari hilo au hapana. Hivyo, ulinzi wa gari lililoegeshwa ni jukumu la mwenye gari. Endapo katika hali isiyotegemewa, wizi au uharibifu ukitokea, basi Sheria ya Bima ya Magari itatumika.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kusema kwamba katika zoezi kubwa kama hili linalofanywa na *TPS* inawezekana kabisa hapa na pale pametokea hali ya kutoelewana kati ya mwegesha gari na mkusanyaji ushuru. Ili kuondokana na kutoelewana huko tutaendelea kutoa elimu na kuwataka wanaokusanya fedha za maegesho waheshimu wateja. Lakini tunaomba vile vile na kwa wale wote wanaoegesha magari nao watimize wajibu wao ili kuondokana na bughudha yoyote.

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Moja, kwa kuwa mwenendo wa utendaji wa kazi ya hawa watumishi ni kama vita hasa kwa kukimbilia kufunga minyororo na kuchukua magari kupeleka *Traffic* halafu udaiwe ulipe zile gharama. Je, huu siyo unyanyasaji katika hali ambayo nchi hii inasifiwa yenye amani, utulivu wakati hali hiyo inaendelea?

Pili, katika idadi kubwa ya wafanyakazi 250 nahisi kama wafanyakazi huenda 175 wametoka Mkoa mmoja ambao Kiswahili chao ni cha kijeshi jeshi, hakuna tafadhali, wala nini yaani misukumo sukumo tu kama vita. Je, Wizara itajaribu kufanya utaratibu wa kuwapatia angalau masomo ya lugha ili yaoane na utamaduni wetu wa Tanzania? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, mara zote ambapo unakuta gari limefungwa mnyonyoro na kupelekwa sehemu ya Polisi, itakuwa imetokana na mambo mawili. Moja, ulipoegesha gari uliondoka bila kulipa ushuru na uliporudi ukakuta hiyo hali imejitokeza.

Lakini pili, inawezekana kabisa ukaegesha gari sehemu ambayo haitakiwi na kwa hiyo, vile vile utakutana na hali kama hiyo kutokana na Polisi ambao nao wanasaidia katika kuhakikisha magari yanawekwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, kama nilivyosema katika maelezo ya awali inawezekana kabisa tunao watumishi baadhi yao ambao wana lugha ambayo hairidhishi kwa wateja. Ndiyo maana tumesema tutaendelea kutoa elimu na kuitaka Halmashauri ya Jiji kuchukua hatua zinazostahili pale inapoonekana kwamba kwa kweli majibu na lugha iliyotumika haifai. Lakini naomba nisisitize tena mpaka mnapofikishana hapo ni dhahiri kabisa kwamba na wewe mwegesha gari bila shaka utakuwa umetumia lugha au namna nyingine ambayo imefanya mkakorofishana.

Na. 171

**Utaratibu wa Uegeshaji wa Magari Mjini**

**MHE. RAYNALD A. MROPE** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilianzisha utaratibu wa uegeshaji wa magari mijini kupitia Kampuni ya *Tanzania Parking Systems* kwa lengo la kuwa na utaratibu mzuri wa kuegesha magari na kuondoa msongamano katika uegeshaji:-

(a) Je, Serikali imefanya uchunguzi gani wa kuridhisha kuona kuwa utaratibu huo ni mzuri wenye kunufaisha wananchi na si watu binafsi?

(b) Je, tangu utaratibu huo uanzishwe Kampuni hiyo ya *TPS* imejenga maeneo gani mapya au kukarabati sehemu zipi za kuegeshea magari katika Jiji la Dar es Salaam?

(c) Je, ni sahihi kwa kampuni hiyo kutoza kodi sehemu yoyote ile ambayo haikutengenezwa kwa ajili ya kuegesha magari kama eneo la barabara mbele ya Wizara ya Afya lililopo Mtaa wa Samora ama eneo la Barabara nyuma ya *Kilimanjaro Hotel* na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niseme hili ni swali la tatu sasa linalofanana kuhusiana na tatizo hili. Lakini nitajitahidi kutoa tena maelezo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mwaka 1997 Serikali ilianzisha utaratibu wa uegeshaji magari mijini ili kuondoa msongamano wa magari. Maeneo yaliyohusika ni katikati ya Jiji la Dar es Salaam na eneo la Kariakoo.

Katika kutekeleza hili, Serikali iliingia mkataba na Kampuni ya *Tanzania Parking System* na tangu imeanza muda wote Halmashauri imekuwa ikifanya tathmini ya mwaka hadi mwaka ili kuona maendeleo ya utendaji kazi wa Kampuni hiyo na kwa ujumla imeridhika kabisa kwamba utaratibu kimsingi ni mzuri na umepunguza sana kero na misongamano mbalimbali iliyokuwepo hapa Jijini.

Mheshimiwa Spika, katika mkataba kama nilivyosema asilimia 25 ya makusanyo inabaki katika Halmashauri ya Jiji. Kwa hiyo, hadi sasa ni jumla shilingi bilioni 4.7 zimekwisha kusanywa na asilimia 25 ya kiasi hicho ni shilingi 763. Lakini kama nilivyosema bado wanadaiwa shilingi milioni 415.6.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mkataba uliopo jukumu la *TPS* ni kukusanya ushuru na kuwasilisha asilimia 25 ya mapato yake katika Halmashauri ya Jiji.

Kwa upande wa Halmashauri ya Jiji inawajibika kutenga maeneo ya maegesho, kuyaendeleza na kuweka huduma muhimu. Kwa hiyo, kutokana na fedha zinazokusanywa Halmashauri ya Jiji itaendelea kuboresha na kupanua zaidi huduma hii ya maegesho. Kwa hiyo, Kampuni hii ya *TPS* tangu iingie mkataba haijajenga maeneo yoyote mapya kwa sababu si jukumu lake.

(c) Katika mkataba niliotaja hapo juu, Kampuni hii ya *TPS* ilionyeshwa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya maegesho ambayo yanastahili kutozwa ushuru. Maeneo hayo ni katikati ya mji na eneo la Kariakoo, Mitaa inayohusika ni Samora, Sokoine, Libya, Stesheni, Posta Mpya, Posta ya Zamani, Lumumba, Kitumbini, Kivukoni, *Oysterbay* na Muhimbili. Hivyo kwa maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge, ni sahihi kwamba magari yanayopaki katika maeneo hayo yanastahili kutozwa ushuru.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa karibu Wabunge watatu katika Mkutano huu wamekerwa na suala la *Tanzania Parking System.* Hii inaonyesha kwamba kuna wengi wanaokerwa na tatizo hili. Je, kwa nini Serikali kuanzia leo isitoe amri kwa kampuni hii kuacha kuwatoza wananchi na wageni na kuwabughudhi wanapopaki katika maeneo ambayo hayakutengenezwa, yaani vichochoro tu, penye majani, kwenye mavumbi. Hii ni haki? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya kuegesha magari katika Jiji la Dar es Salaam nimeyataja na nimesema katika maeneo hayo ukiegesha gari ni lazima utozwe ushuru.

Kama kuna maeneo mengine nje ya hayo ambayo Mheshimiwa Mbunge anasema kwenye majani, vichochoro, vumbi sasa ili mradi hayapo katika maeneo haya, unayo haki kabisa kwenda kwenye Halmashauri ya Jiji na kutoa taarifa kwa wahusika kuonyesha hali ya kutoridhishwa na utendaji wa Kampuni hiyo kwa sababu amekwenda nje ya makubaliano na mkataba, lakini kwa sasa kwa kweli maeneo yan yanayotozwa ni hayo.

Na. 172

**Uongozi, Uendeshaji na Usimamizi wa Elimu**

**MHE. FAUSTINE K. RWILOMBA (k.n.y. MHE. ELIACHIM J. SIMPASA)** aliuliza:-

Kwa kuwa uongozi, uendeshaji na usimamizi wa elimu katika ngazi zote muhimu sana katika kipindi hiki cha mabadiliko ya sayansi na teknolojia na kwa kuwa kwa mtu asiyekuwa na upeo mpana wa elimu hataweza kusimamia vizuri elimu hiyo:-

(a) Je, Serikali inao maafisa elimu wangapi wenye Shahada ya Chuo Kikuu *(University Degree),* Stashahada *(Diploma)* na ni wangapi wasio na viwango hivyo vya elimu?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuinua kiwango cha elimu kwa wasimamizi na viongozi wa elimu kuendana na teknolojia ya sasa katika viwango vya *DEO's School Inspectors, Ward Education Coordinators* na *Head Teachers* ili waweze kuendesha masuala ya elimu kitaalm kuliko ilivyo sasa?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwalimu Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mafisa Elimu wenye shahada ya Uzamili kwa ngazi ya Mkoa ni 7 kati ya mikoa 21 kwa Tanzania Bara ambayo ni sawa na asilimia 33.3%. Maafisaelimu 14 wa Mikoa mingine wana Shahada ya kwanza ya Chuo Kikuu ambao ni asilimia 66.6%. Kwa upande wa ngazi ya Wilaya, tuna Afisa Elimu mmoja mwenye Shahada ya Udaktari *(Ph.D),* Maafisa Elimu 6 wenye Shahada ya Uzamili yaani *Masters* ambao ni asilimia 5.2%. Maafisa Elimu 49 ambao ni asilimia 43 wana Shahada ya Kwanza ya Chuo Kikuu. Maafisa Elimu waliobakia 58 ambao ni asilimia 51 wana Stashahada ya Elimu.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuendana na teknolojia ya sasa, Serikali ina mikakati ya kuinua kiwango cha elimu kwa wasimamizi na viongozi wa elimu katika ngazi mbalimbali kuanzia kwa Maafisa Elimu wa Wilaya, Wakaguzi, Waratibu Elimu Kata na Walimu Wakuu. Wizara yangu kwa kushirikiana na TAMISEMI huwapatia mafunzo ya kujenga uwezo *(Capacity Building)* wa kusimamia elimu kwenye ngazi zao kwa ufanisi zaidi.

Aidha, Wizara yangu imetayarisha muhtasari wa mafunzo ya menejimenti yanayotolewa na Wakala wa Maendeleo ya Elimu *(ADEM)* kule Bagamoyo, kwa wasimamizi wa elimu kuanzia ngazi ya Mkoa hadi ngazi ya shule. Sambamba na hilo Wizara inasisitiza Maafisa Elimu kujiendeleze kitaaluma na kitaalam na hadi sasa Maafisa Elimu wengi wamejisajili Chuo Kikuu Huria *(Open University).* Kuhusu ukaguzi kila wanapoteuliwa wakaguzi wapya hupewa mafunzo maalumu ya ukaguzi.

Waratibu Elimu Kata na Walimu Wakuu hupata mafunzo mbali mbali ya muda mfupi na mrefu hususan yaendanayo na utendaji wa kazi za kila siku katika kuboresha elimu. Kuhusu uteuzi mpya utaratibu wa sasa ni kuwa nafasi iliyo wazi inatangazwa pamoja na sifa zake na usaili wa waombaji unafanywa na Kamati inayozingatia sifa zinazotakiwa na kutoa mapendekezo kwa Mamlaka ya Uteuzi kutegemea na kila ngazi ya uongozi wa elimu.

**MHE. FAUSTINE K. RWILOMBA:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kuniruhusu niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa hapo awali Vyuo vya Ualimu vilikuwa vinachukua walimu walio kazini iliendesha mafunzo ya *in-service* na sasa hivi yamesimama na kwa kuwa nia yetu ni kuweza kuendeleza Walimu. Je, Wizara sasa haioni kwamba kuna umuhimu wa kutenga baadhi ya Vyuo kwa ajili ya kuendesha mafunzo ya *in-service* kwa upande wa *Diploma* ambao baadaye wataenda Chuo Kikuu?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kulikuwa na kipindi ambacho kwa sababu nafasi ilikuwepo kilikuwa kimetengwa Chuo maalum kwa ajili ya mafunzo kazini yaani *In-service Training* ya Walimu. Lakini katikati kipindi cha sasa kutokana na utekelezaji wa MMEM, tunahitaji katika miaka hii mitano ya utekelezaji wa MMEM kuwafundisha na kuwaajiri Walimu wapya 45,000. Kwa hiyo, tumelazimika Vyuo vyote kuvitumia kwa kazi ya mafunzo ya Walimu hawa ambao tunawahitaji kuendana na mpango. Lakini Serikali tunalifanyia kazi suala hili la mafunzo ya Ualimu wa *Diploma* kuwawezesha kufikia hatua ya Chuo Kikuu na mazungumzo yako katika hatua kubwa, hatua iliyoendelea kujaribu kubadilisha Vyuo vyetu vitatu vya mafunzo ya *Diploma* viweze kuwa ni Vyuo Shirikishi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili waweze kutoa *Diploma* lakini pia ile *Diploma* iwe imeandaliwa kwa namna ambayo wakati wanafanya ile *diploma* miaka miwili wanakuwa pia wamefanya miaka miwili ya mwanzo ya Shahada ya Kwanza ya Elimu.

Hii itawawezesha walimu hao watakapokuwa kazini wakirudi tena Chuo Kikuu wanahitaji kukaa miaka miwili kumalizia ile miaka miwili iliyobakia. Kwa hiyo, wataalam wa Chuo Kikuu wanashirikiana na Wizara kufanya maandalizi hayo. *(Makofi)*

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana umenipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Lakini pia nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri katika swali la msingi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ili kuimarisha mpango wetu huu wa Elimu kwa Wote *(UPE),* ni lazima tuwe na walimu bora, walimu ambao wameendelezwa na kwa kuwa bado tuna wale walimu wa daraja la A mpaka daraja B, je, Serikali ina mpango gani kuwapa mafunzo ili watoke daraja la *IIIB* waende daraja *IIIA* kabla ya mwaka 2006? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, swali analolizungumzia la Walimu wa *Grade* B na C kupewa mafunzo ili kupanda kuwa *grade* A limeangaliwa na Wizara yangu kwa ushirikiano na TAMISEMI kwa makini sana na hata tukafikia uamzi kwamba ule utaratibu wa zamani ambao ulikuwa unawapeleka kwanza wafanye mitihani ya *O-Level* yaani wafanye Mtihani wa Kidato cha nne ndipo waende kwenye mafunzo ya miaka miwili kuwa *grade* A tukaona haufai.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kwanza wengi wao walikuwa wanafaulu katika masomo ambayo siyo yale wanayofundisha katika shule za msingi na tulikuta wengi kama nilivyowahi kusema hapa wanafaulu ya *Bible Knowledge, Islamic Studies* na

wanaweza kufikia akapata daraja kwa masomo kama hayo ukichanganya pengine na Uraia na Kiswahili walikuwa wanaweza kufaulu halafu wanakwenda kusomea Ualimu. Sasa tukaamua kwamba si kazi ya Wizara hii kufundisha Makatekista. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo *route* ya kupita *O-Level* tumeibadilisha na sasa hivi tumeandaa mafunzo ya Walimu hao ambayo yatawawezesha kupata sifa inayoitwa *In-service Grade A* na *module* zilizoandaliwa zinawafanya wasome masomo wanayofundisha katika shule za msingi na wafaulu kwa sababu wao ni walimu wafaulu kwa wastani wa B katika masomo manne na wakiweza kufikia hapo watapandishwa kuwa *In-service Grade A* ndiyo utaratibu unaotumika sasa.

Na. 173

**Ubinafshishaji wa Majengo Yaliyokuwa Yanatumiwa na Misheni**

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI (k.n.y. MHE. THOMAS NGAWAIYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilibinafsisha majengo yaliyokuwa yakitumiwa na misheni kwa ajili ya shule za msingi na kwa kuwa majengo hayo hayajafanyiwa ukarabati kwa zaidi ya miaka 30 na kwamba tangu shule hizo zichukuliwe na Serikali kiwango cha taaluma kimeshuka kwa kiasi kikubwa na nyingine hazijafaulisha mwanafunzi ye yote kwa kipindi cha miaka 20 wakati kabla ya kubinafsishwa kwa shule hizo zilikuwa zinafaulisha wanafunzi kwa zaidi ya asilimia 70:-

(a) Je, Serikali haioni haja ya kurudisha shule hizo na majengo kwa wahusika lakini ziwe chini ya uangalizi na msaada wa Serikali yenyewe ili kuboresha elimu?

(b) Je, kwa nini Serikali haikuzifidia misheni husika kutokana na majengo yao?

(c) Je, Serikali inasema nini juu ya shule za msingi zilizomaliza zaidi ya miaka mitano au zaidi mfululizo bila kufaulisha hata mwanafunzi mmoja na ziko shule za aina hiyo ngapi hapa nchini?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu swali lake Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbunge wa Moshi Vijijini, lenye sehemu (a), (b) na (c) ningependa kutoa maelezo ya kiujumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara haiweki kumbukumbu za shule zilizokuwa za *Mission* peke yake kuhusu matokeo ya mitihani. Kwa hiyo, sijui Mheshimiwa Mbunge amezitoa wapi, hadi kufikia madai ya ubovu wa shule hizi anayoyafanya mwanzoni mwa

swali lake. Nahitaji usahihi wa madai hayo ili niweze kumjibu vizuri ama kukubaliana au kutokubaliana na madai yake.

Mheshimiwa Spika, namwomba anipatie ushahidi wa kitakwimu na majina ya shule. Baada ya ombi hilo ningependa sasa kutoa majibu ya sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua ya kuziboresha shule hizo katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) kwa mwaka 2002 hadi 2006 unaohusu shule zote za msingi za Serikali, zikiwemo hizo anazozizungumzia, unaoendelea kwa mafanikio makubwa nchini kote.

(b) Suala la kufidiwa halikuwepo kwa sababu Serikali ilichofanya ni kubeba mzigo zote wa kuziendesha shule hizo pamoja na ile sehemu waliyokuwa wanaibeba *Mission* na majengo husika yakaendelea kutumiwa kwa madhumuni yale yale ya kuelimisha watoto wa nchi yetu na kwa sababu hiyo wenye majengo hayo hawakuidai Serikali fidia yoyote.

(c) Mheshimiwa Spika, zipo shule 240 ambazo ni asilimia 2.2 ya shule zote za Msingi nchini ambazo hazijafanikiwa kupeleka wanafunzi kidato cha kwanza katika Sekondari za Serikali kuanzia mwaka 1995-2002. Kitendo cha shule ya Msingi kutokupeleka wanafunzi wao Sekondari huchangiwa na sababu nyingi kama vile upungufu wa vyumba vya madarasa, walimu na vifaa vya kujifunzia na kufundishia na utoro wa wanafunzi. Mpango wa MMEM ambao Wizara yangu inausimamia kwa kushirikiana na TAMISEMI umebuniwa kwa lengo la kuondoa kasoro hizo, kwa kuongeza idadi ya walimu 45,796 ifikapo mwaka 2006, kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa kuongeza madarasa, kuongeza nyumba za walimu na kuongeza maliwato na pamoja na Ofisi za shule na pia kupunguza uwiano wa kitabu kimaoja kwa wanafunzi hadi kufikia uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja kwa mwaka 2006 na kuboresha ikama ya walimu katika kila shule zote.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa katika utangulizi wa Mheshimiwa Waziri, amemshutumu Mheshimiwa Mbunge kwa kutokuuliza swali lake vizuri. Lakini kwa kuwa ni wajibu wa Serikali kujua kwani ninapouliza swali hutuma kwa wataalam wake Wilayani, Mkoani na Serikalini kujua ni shule ngapi zilitaifishwa hapo mwanzo. Je, Waziri yuko tayari kukiri kwamba jibu hakulifanyia kazi na badala yake anataka Mbunge ndiyo alifanyie kazi?

Pili, kwa kuwa hizo shule 42 alizozisema kwamba hazijapeleka wanafunzi sekondari, sasa baada ya kugundua hiyo, anao mkakati gani muhimu ili wanafunzi na wazazi wa sehemu hiyo waweze kufaidi kushinda kwenda shule za sekondari kama wengine?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza kuwa nimemshutumu Mheshimiwa Mbunge kwa kuuliza, ningefanya utafiti. Kusema kweli, namshauri Mheshimiwa Mbunge alisome kwa makini lile swali. *(Makofi)*

Serikali haikuulizwa itoe takwimu. Kama ingeulizwa lazima tungefanya utafiti na kutoa takwimu hizo, ila Mheshimiwa Mbunge, kafanya *conclusion* zake yaani kasema yuko hivi yeye mwenyewe, bila kutaka usahihi wa takwimu ambao tungeweza kumpatia na kama hazipo tungeweza haziko na kama anataka tuzifanyie utafiti tuzilete tungeweza kufanya utafiti. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge alipange swali vizuri liweze kumpa majibu kama anachotaka ni kupata hizo takwimu kutoka kwa watunza takwimu ambayo ni Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, shule hizi ambazo hazipeleki wanafunzi sekondari kwa hivi sasa ni sehemu ya shule zetu za msingi ambazo katika mpango wa MMEM tunazifanyia kazi kwa kuongeza walimu, vitabu na kadhalika na kadhalika. Kwa hiyo, ndiyo hatua muhimu inayochukua ili kuziwezesha shule zetu zote ziwe zinapeleka watoto sekondari.

Mheshimiwa Spika, ningependa nichukue nafasi hii kusema pia kwamba sio kila wakati shule isipopeleka mtoto sekondari wamefeli wote. Tunalo tatizo pia la uhaba wa nafasi za sekondari. Kwa sababu tunazo nafasi za kupeleka Sekondari asilimia 10 tu. Mwaka 2003 tumefikia asilimia 10 tu ya rika lengwa kwa elimu ya sekondari.

Kwa hiyo, vijana wetu wanashindania nafasi hizo. Kwa hiyo, jawabu la kudumu pamoja na kuboresha ufundishaji katika shule za msingi kwa hatua tunazochukua katika MMEM lazima pia tuweke jitahada kupanua elimu ya sekondari katika Wilaya zetu zote.

Na. 174

**Uhaba wa Chakula Nchini**

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika hotuba yake kwa Taifa hapo tarehe 31 Machi, 2002 alilitahadharisha Taifa juu ya tarajio la uhaba wa chakula mwaka 2003 pamoja na hatua za kukabiliana na tatizo hilo:-

(a) Je, hali ya akiba ya chakula ikoje sasa hadi kufikia wakati wa kujibu swali hili?

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani kabambe za kununua akiba ya chakula cha ziada kilichoko mikononi mwa wananchi?

(c) Je, ni maeneo gani ambayo yanatarajiwa kuathirika sana kwa uhaba wa chakula hapa nchini na Serikalini inafanya nini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mbunge wa Lushoto, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Hadi tarehe 2 Julai, 2003 Hifadhi ya Chakula ya Taifa ilikuwa ina tani 51,060 za mahindi. Akiba hiyo ipo katika Kanda saba ambazo ni Kipawa (Dar es Salam) tani 4,986, Arusha tani 18,624, Dodoma tani 11,281, Shinyanga tani 7,489, Makambako tani 4,661, Songea tani 3,201 na Sumbawanga tani 810.

Mheshimiwa Spika, akiba iliyokuwa mikononi mwa wafanyabiashara hadi tarehe 26 Juni, 2003, ilikuwa tani 113,484, tani 81,862 za ngano, tani 24,409 za mahindi, tani 6,373 za mchele, tani 11 za mtama na tani 829 za mikunde.

(b) Katika Bajeti ya mwaka wa 2003/2004, Serikali imetenga shilingi bilioni 3.6 ili kuiwezesha Hifadhi ya Chakula ya Taifa kununua tani 20,800 za mahindi kutoka kwenye maeneo yenye ziada ya chakula na kuyauza kwenye maeneo yatakayokuwa na upungufu wa chakula. Ununuzi huo utaipa Hifadhi ya Chakula ya Taifa uwezo wa kusambaza zaidi ya tani 73,950 za mahindi katika mwaka wa 2003/2004.

Aidha, wafanyabiashara binafsi wanahimizwa kununua chakula kutoka maeneo ya ziada na kukiuza kwenye maeneo yenye upungufu. Endapo kitahitajika chakula zaidi Serikali imetenga shilingi bilioni nane za dharura ambazo zitatumika kuagiza chakula kutoka nje.

(c) Kutokana na taarifa zilizopokelewa kutoka Mikoani na kwenye Wilaya na kutokana na taarifa zilizowasilishwa na timu za wataalam wa Wizara zilizotumwa Mikoani kutathmini hali ya chakula, maeneo yenye upungufu mkubwa wa chakula yako kwenye Mikoa ya Manyara (Wilaya ya Simanjiro, Hanang na Kiteto), Dodoma (Wilaya ya Dodoma Vijijini, Kongwa na Kondoa), Singida (Wilaya za Manyoni, Singida Vijijini na Iramba) na Shinyanga (Wilaya ya Meatu na Kishapu). Mikoa ya Morogoro, Mtwara, Lindi na Pwani itajitosheleza kwa chakula ijapokuwa itakuwa na maeneo yenye upungufu.

Ufafanuzi zaidi unapatikana kwenye jedwali Na. 1 lililoko kwenye ukurasa wa 9 wa hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2003/2004. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wairejee.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningeomba kwanza nifanye masahihisho kwamba Mheshimiwa Rais alilihutubia Taifa tarehe 31 Machi, 2003. Baada ya marekebisho hayo ningeomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa thamani ya shilingi inashuka kwa kulinganisha na thamani ya hela za nje; na hii ni dhahiri kwamba kama chakula kitanunuliwa nje kitakuwa ghali; na Serikali imetamka kwamba imetenga shilingi bilioni nane na ni dhahiri kwamba kutakuwa na njaa.

Je, Serikali isingeona busara kuzipeleka shilingi bilioni nane, moja kwa moja zikanunue chakula kwa bei rahisi kuliko kusubiri kununua kutoka nje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, mwaka 2002 Serikali ilitoa tani 500 kwa Wilaya ya Lushoto tulipopungukiwa na chakula, napenda kuishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Lakini lilitoka sharti la kwenda kukichukua chakula hicho kutoka Bohari ya Akiba ya Chakula, Halmashauri ndiyo ingepaswa kufanya kazi hiyo, lakini kutokana na uwezo mdogo wa Halmashauri ilishindwa kwenda kuchukua chakula hicho. Je, mwaka 2003 kutokana na njaa kubwa ambayo inategemewa kutokea, Serikali imeandaaje kuagiza chakula kisambazwe kwa gharama ya Serikali Kuu kuliko kutegemea Halmashauri? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, thamani ya shilingi inaweza ikashuka. Tukumbuke kuwa wananchi wenyewe wana chakula tayari mikononi ambacho sikukitaja hapa, kiasi fulani kipo. Kwa hiyo, siyo kusema kuwa tunaponea chakula kilichopo kwenye maghala tu, hapana. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, pili, katika jibu la msingi nilisema kuwa zipo shilingi bilioni tatu na kitu kwa ajili ya chakula, sasa nasema kama hazitatosha tutafanya hivyo. Zaidi ya hayo Serikali imewahimiza wananchi na viongozi kuhamasisha ulimaji katika mabonde na kadhalika. Kwa hiyo, tunategemea chakula kitakuwepo kama hali ilivyo. Zaidi ya hayo Kitaifa, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, kila asubuhi hufanya kikao ili kutathmini hali ilivyo. Inaonekana hofu siyo kubwa sana kwa sababu hali si mbaya sana kama inavyoonekana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kusambaza chakula. Suala hili litashughulikiwa na Serikali kutegemeana na hali itakavyoonekana. Kwa hiyo, Halmashauri itakayoonekana haina uwezo Serikali itashughulikia. *(Makofi)*

Na. 175

**Mradi wa Kilimo - *KAEMP***

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mradi wa Kilimo na Mazingira Kagera *(Kagera Agricultural and Environmental Management Project (KAEMP)* umekuwa ukitengeneza barabara Mkoani Kagera ili kusaidia usafirishaji wa mazao ya kilimo:-

(a) Je, *KAEMP* imetengeneza barabara za urefu gani katika Mkoa mzima wa Kagera?

(b) Je, mpaka sasa zimetumika fedha kiasi gani katika utengenezaji wa barabara hizo?

(c) Je, ni barabara za urefu gani kila Wilaya zimetengenezwa na *KAEMP* na kwa Jimbo la Kyerwa ni kilometa ngapi zimetengenezwa kwa gharama kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mbunge wa Kyerwa, naomba kutoa maelezo mafupi ya utangulizi.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Usimamizi wa Kilimo na Mazingira Mkoani Kagera *(Kagera Agricultural and Environmental Management Project - KAEMP)* ulikuwa wa miaka sita kuanzia mwaka 1997/1998 hadi mwaka 2002/2003 na ulianzishwa na Serikali ya Tanzania, *IFAD,* Mfuko wa Maendeleo ya Serikali ya Ubelgiji, *OPEC* na nguvu za wananchi kwa lengo la kurekebisha na kukarabati maeneo yaliyoathiriwa na wimbi la wakimbizi kutoka Rwanda na Burundi na kuondoa kasoro zilizosababisha kushuka kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo. Matengenezo ya baadhi ya barabara za Mikoa na Wilaya yalikuwa moja ya sehemu ya mradi huo.

Mheshimiwa Spika, mradi ulipanga kukarabati barabara zenye urefu wa kilomita 518.3 katika Wilaya za Biharamulo, Muleba na Bukoba zikiwa na kilomita 123.9 za barabara za Mkoa na kilomita 393.2 za barabara za Wilaya (Biharamulo km. 116, Bukoba km. 131.2, Muleba km. 99.2, Karagwe km. 26 na Ngara km. 22). Wilaya za Karagwe na Ngara hazikuwa zimejumuishwa kwenye mradi kwa kuwa barabara zake zilikuwa zinashughulikiwa na *UNHCR* hadi wakimbizi waliporudi makwao mwaka 1999 ambapo *UNHCR* waliacha kuendelea na matengenezo ya barabara kwenye Wilaya hizo na ikabidi ziunganishwe kwenye Mradi wa *KAEMP.*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mradi umetengeneza barabara zenye urefu wa kilomita 516 zikiwemo kilomita 122.8 za barabara za Mkoa na kilomita 393.2 za barabara za Wilaya.

(b) Hadi tarehe 18 Juni, 2003 jumla ya shilingi 7,164,208,366.40 zilikuwa zimetumika.

(c) Barabara zilizotengenezwa kwa kila Wilaya ni kama ifuatavyo:-

Biharamulo kilomita 115.1, Bukoba kilomita 130.9, Muleba kilomita 99.2, Karagwe kilomita 26 na Ngara kilomita 22 jumla kilomita 393.2. Katika Wilaya ya Karagwe ni kilomita 26 tu za barabara za Nyakagoyegoye kwenda Rwabwere zilizotengenezwa chini ya Mradi wa *KAEMP.* Kama nilivyotangulia kueleza, Mradi wa *KAEMP* haukujumuisha Wilaya ya Karagwe hadi *UNHCR* na *NGOs* zilizokuwa zikishughulikia barabara za Wilaya hizo zilipoondoka.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kila mmoja katika Taifa hili anajua kwamba ni Wilaya ya Ngara na Karagwe zilizowatunza wakimbizi wa Rwanda na Burundi; na kwa kuwa Mradi huu wa *KAEMP* ulianza mwaka 1997/1998; na kwa kuwa *UNHCR* waliondoka Karagwe na Ngara mwaka 1996; je, hizi hela zote zilizoombwa kwa ajili ya kukarabati maeneo

hayo ambayo yalikaliwa na wakimbizi ikiwepo Ngara na Karagwe, kitendo cha kutengeneza kilomita 26 siyo dhuruma kwa wananchi wa Karagwe na Ngara?

Mheshimiwa Spika, pili, kama Mheshimiwa Waziri anasema siyo dhuruma au ni dhuruma; je, sasa Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba barabara hizo za Karagwe na Ngara zinatengenezwa kwa sababu hazikutengenezwa kama ilivyokusudiwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kusisitiza kuwa wakimbizi walitoka mwaka 1999, narudia kwamba ni mwaka 1999 lakini wakati mpango huu unapangwa kama nilivyozungumza na waliohusika huko, wameniambia kuwa wakati ule Ngara ilikuwa inashughulikiwa na hili shirika la wakimbizi pamoja na Taasisi ambazo zilihusishwa na hilo shirika la wakimbizi. Ndiyo maana wakati ule *KAEMP* haikujumuishwa katika maeneo haya lakini baada ya wao kuondoka mwaka 1999 ikaonekana kuna haja ya kufanya masuala hayo na wamefanya mengi tu, siyo tu kushughulika na barabara moja hii ila kuna miradi ya kilimo, miradi ya mazingira na miradi ya afya. Hata hivi tunavyozungumza siyo kuwa barabara zitaachwa kabisa, hapana, barabara bado zinashughulikiwa na Wizara ya Ujenzi, *Road Toll* na Halmashauri na mipango ya kushughulikia masuala haya kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kuwa hakuna dhuruma kwa sababu ingekuwa ni dhuruma kwa sababu hii na ile sidhani kama wangedhurumu Wilaya mbili. Maana iko Ngara vile vile na Karagwe na sioni kama Serikali ya CCM ina mradi wa aina hii, kudhurumu Wilaya wanakotoka Waheshimiwa Wabunge.

Na. 176

**Makusanyo ya Mapato ya Serikali**

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mamlaka ya Ukusanyaji kodi katika nchi jirani ya Kenya *(KRA)* inakusanya kodi mara mbili ya kiwango kinachokusanywa na *(TRA)* hapa nchini; na kwa kuwa vyanzo vya ukusanyaji wa mapato vimeongezeka na kukua kama vile uchimbaji wa madini, utalii na kadhalika; na kwa kuwa maslahi ya watumishi wa *TRA* yanaboreshwa ili kuwa kichocheo cha kuongeza tija na ufanisi:-

(a) Je, ni sababu gani zinazosababisha Serikali kutokusanya mapato sahihi kutoka kiwango cha sasa bilioni 100 - 105 kwa mwezi hadi kiwango halisi kulingana na vyanzo halisi vilivyopo?

(b) Je, ukwepaji ushuru uliokithiri kwenye bidhaa kama mafuta ya nishati, mafuta *(crude)* ya kupikia inaathiri kwa asilimia ngapi makusanyo ya Serikali na ni nini malengo ya Serikali *(projections)* kuhusu makusanyo ya mapato kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo?

(c) Je, ajira za wafanyakazi wa *TRA* huwa zinatangazwa kwenye vyombo vipi vya habari ili kuwepo na ukweli na uwazi katika ajira kwenye Taasisi hiyo nyeti kwa maendeleo ya Taifa hili?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba nitoe maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, utozaji wa kodi katika nchi yetu hufanywa kwa mujibu wa Sheria zilizopitishwa na Bunge. Sheria za kodi hueleza kianzio cha kodi, viwango *(rates)* na taratibu za kulipa kodi hiyo. Kwa mfano, Sheria ya Ushuru wa Forodha inafafanua kwamba ushuru utatozwa kwa kuzingatia thamani ya bidhaa iliyoingizwa nchini kutoka nje na kwa kiwango kilichotajwa katika Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, uwezo wa nchi kukusanya mapato kutokana na vianzio vya kodi hutegemea vigezo vilivyomo katika Sheria ya Kodi, uwezo wa Serikali kusimamia Sheria hiyo *(Tax Administration)* na mfumo wa uchumi *(Structure of the Economy).* Kwa kiasi kikubwa, tofauti ya ukusanyaji mapato kati ya nchi yetu na Kenya inatokana na tofauti zilizopo katika mifumo ya uchumi wa nchi hizi mbili. Kwa mfano, Sekta ya Kilimo ambayo sera yetu ni kutokuitoza kodi kwa kadri inavyowezekana, inachangia karibu nusu ya Pato la Taifa kwa mwaka, wakati mchango wa Sekta ya Kilimo nchini Kenya ni chini ya theluthi moja.

Aidha, Kenya ina sekta kubwa za kisasa za uzalishaji na huduma hasa viwanda na utalii ukilinganishwa na nchi yetu. Licha ya kodi zinazolipwa moja kwa moja na viwanda na mahoteli, sekta hizi hutoa nafasi za ajira na hivyo kuongeza mchango wa kodi zinazolipwa na waajiriwa na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Sheria nzuri za kodi na uchumi wa kisasa usimamizi madhubuti wa Sheria hizo ni muhimu ili kuongeza mapato ya Serikali. Ndiyo maana, pamoja na ukweli kwamba mengi ya marekebisho yaliyofanywa katika mfumo wetu wa kodi katika miaka saba iliyopita yalihusisha kufuta baadhi ya kodi na kushusha viwango vya kodi zilizobakia, mapato ya Serikali yaliongezeka kutoka wastani wa shilingi milioni 25 kwa mwezi mwaka 1995/1996 hadi takriban shilingi milioni 100 mwaka 2002/2003. Pamoja na kukua kwa uchumi, kuimarika kwa usimamizi baada ya kuanzishwa Mamlaka ya Mapato kumetoa mchango muhimu katika kufikia ongezeko hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kiwango cha mapato kinachokusanywa sasa kinatokana na hali halisi ya uchumi wetu na Sheria zetu za kodi. Hata hivyo, Serikali inaendelea kuimarisha Mamlaka ya Mapato ili isimamie kwa ufanisi zaidi Sheria zilizopo na kuondoa kabisa mianya inayotumiwa kukwepa kodi. Vile vile, jitihada za Serikali kuongeza uwekezaji

nchini zinalenga kuboresha hali ya uchumi wa nchi, kupanua sekta ya kisasa ya uzalishaji na huduma ziwe za kisasa, kuongeza nafasi za ajira na kuongeza uwezo wa kiuchumi wa kulipa kodi.

(b) Serikali imetambua kuwepo kwa ukwepaji wa kodi katika sekta ya mafuta ya petroli. Inakadiriwa kuwa ukwepaji huo unapelekea Serikali kutokusanya hadi asilimia 20 ya kodi zilizostahili kulipwa na sekta hiyo. Ili kukabiliana na tatizo hili, Serikali hivi sasa inatekeleza hatua zilizotangazwa kwenye hotuba ya Bajeti ya mwaka huu ambazo ziko ukurasa wa 70 mpaka 72 kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Aidha, Serikali haina taarifa ya ukwepaji wa kodi katika mafuta ghafi ya kula *(crude edible oil).* Hata hivyo, Serikali imechukua hatua za kupunguza uagizaji wa mafuta hayo kwa nia ya kuwalinda wazalishaji wa ndani wa mbegu za mafuta. Bila shaka, kupungua kwa mafuta hayo yanayoingizwa kutoka nje kutapunguza pia tatizo alilolielezea Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, kama lipo.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mitatu ijayo, Serikali inatarajia kukusanya mapato kama ifuatavyo:-

| Mwaka | Mapato (bilioni) |
|---|---|
| 2003/2004 | 1,393 |
| 2004/2005 | 1,573 |
| 2005/2006 | 1,774 |

(c) Mheshimiwa Spika, nafasi za ajira kwa watumishi wa *TRA* hutangazwa kwa njia mbalimbali kutegemea ngazi husika. Nafasi za watumishi wa ngazi za chini kama madereva na kadhalika hutangazwa katika Mikoa ambako nafasi imetokea. Aidha, nafasi katika ngazi za kati hutangazwa katika magazeti ya hapa nchini. Nafasi katika ngazi za Menejimenti hutangazwa katika magazeti ya nchini na ya Kimkoa *(Regional Papers)* ili kuwapa nafasi Watanzania wanaofanya kazi nchi jirani kutuma maombi yao iwapo wanazo sifa zinazotakiwa.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:**Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha; je, Serikali inakiri kwamba mianya iliyopo katika ukusanyaji wa mapato yetu unatusababishia tunakosa kukusanya zaidi ya asilimia 50 ya mapato ambayo tulistahili tuyakusanye? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, kwa sababu Wizara ya Fedha na Taasisi hii ya *TRA* ziko pamoja; na kwamba kuna manung'uniko kwamba watumishi wengi wa Taasisi hii wanatoka sehemu moja ya nchi; je, Serikali haioni kwamba hili linaweza kuwa ni tatizo kubwa ambalo linaondoa uadilifu na uaminifu katika Taasisi hii ya *TRA?* *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nilijibu kwamba Serikali inapoteza takriban asilimia 20 ya mapato ambayo yalitakiwa kukusanywa kwenye sekta ya mafuta na siyo asilimia 50 kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema.

Mheshimiwa Spika, uwezo wa nchi kukusanya kodi kama nilivyoeleza unatokana na sababu nyingi lakini mojawapo ni ule uwezo wa nchi ama Serikali kusimamia vizuri Sheria za Kodi yaani *Tax Administration*. Kwa hiyo, Serikali inachofanya ni kwamba inaboresha mfumo wa kodi na pia inaboresha taratibu za kukusanya kodi ili *compliance* watu waweze kulipa kodi kwa urahisi zaidi. Pia Serikali ama Wizara ya Fedha kupitia *TRA* inapunguza sana misamaha ambayo ilikuwa inatumika pia kukwepa kodi na mojawapo ya mikakati ilikuwa ni Serikali pamoja na Taasisi zake kulipa kodi. Lakini pia tumejitahidi sana kupunguza rushwa katika utaratibu mzima wa kukusanya kodi na hivyo kupunguza zaidi mianya ya kodi.

Kama nilivyosema katika ukurasa wa 70 mpaka 72 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, imeelezwa mikakati gani ambayo imebuniwa katika kupunguza mianya ya ukwepaji kodi siyo tu katika mafuta lakini pia katika sehemu nyingine. Tunaimarisha *TRA* zaidi na mategemeo yetu ni kwamba tutakusanya kiasi kikubwa zaidi mwaka huu na miaka inayofuata.

Mheshimiwa Spika, pili, utaratibu unaotumika kuwaajiri watumishi *TRA* hauangalii jinsia wala kabila na wala sehemu moja ya nchi. Kama nilivyosema, matangazo ya ajira yanatangazwa kwenye magazeti na wanaoajiriwa ni wale wenye sifa zinazotakiwa.

**WABUNGE FULANI:** Aah!!

**SPIKA:** Nashindwa kupokea maswali ya nyongeza kwa sababu bado nina maswali matatu na dakika kumi tu zimebaki lakini majibu ya nyongeza nayapokea, Mheshimiwa Waziri wa Utumishi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Spika, naomba kuongezea jibu kwenye majibu mazuri ya nyongeza ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, kuhusu ajira ya watumishi wa umma na hususan wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera ya Ajira na Menejimenti, nafasi zote za kazi katika Serikali lazima zitangazwe na utaratibu wa usaili wa kuajiri watumishi lazima ufuatwe. Kwa mujibu wa Sheria mpya ya utumishi wa umma, viongozi wote wa sehemu za kazi ambao hawatafuata utaratibu mzuri na kuwaeleza wale wote walioomba kazi wakati wowote wanapotaka kuona zile taratibu, watakuwa wamekosea na Tume ya Utumishi mpya itakuwa inafuatilia wale wote ambao hawatafuata taratibu ambazo zinatakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nilijulishe Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali itasimamia ipasavyo haki katika ajira na kwa hiyo hatuna sababu ya kuwa na wasiwasi. *(Makofi)*

Na. 177

**Riba Zitolewazo na Taasisi za Fedha**

**MHE. ABDULA SULEIMAN LUTAVI** aliuliza:-

Kwa kuwa Benki ya *NMB, NBC* na *CRDB* na Benki nyinginezo ni Taasisi za kibiashara; na kwa kuwa wateja huweka fedha zao Benki ili wanufaike na kiwango cha riba inayotolewa na Benki:-

(a) Je, kwa sasa ni kiasi gani cha riba anacholipa mteja aliyekopa na ni kiasi gani kinacholipwa kwa anayewekeza?

(b) Kwa tathmini ya jumla; je, tofauti iliyopo ya viwango vya riba inasaidiaje kujenga uwezo wa Mtanzania wa kawaida katika kujiendeleza kwa kutumia huduma za kifedha zitolewazo na Benki hizo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdulla Lutavi, Mbunge wa Tandahimba, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Riba katika Benki za kibiashara zinapangwa kutegemea na nguvu ya soko huria. Kwa mantiki hii, kila Benki hupanga riba zake kutegemea na soko ikiwa ni pamoja na kuzingatia sifa za kibiashara za mkopaji. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili, 2003, mikopo yote ya Kibenki kwa ujumla ilikuwa na riba ya wastani wa asilimia 15.2. Aidha, amana zote za Kibenki kwa jumla zilikuwa na riba ya wastani wa asilimia 3.5 katika kipindi hicho.

(b) Mheshimiwa Spika, tathmini ya jumla inaonyesha kuwa riba wanayolipwa wanaowekeza amana katika Mabenki ya biashara iko chini ya kiwango cha mfumuko wa bei. Hali hii inawafanya waweka amana kuathirika kimapato kwa vile wanapoteza thamani ya fedha yao zinapokuwa Benki na hivyo wanaweza kukatishwa tamaa kuweka akiba katika Mabenki. Vile vile, riba kubwa inayotozwa na Mabenki ya biashara wanapokopesha wateja wao inawaumiza Watanzania wenye kipato kidogo wanaotaka kukopa kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza miradi ya kuwaondolea umaskini.

Mheshimiwa Spika, napenda ieleweke kuwa riba kubwa ya mikopo inayoambatana na riba ndogo kwa amana, ni hali inayotokana na matatizo ya kimsingi katika uchumi wetu. Matatizo hayo ni pamoja na miundombinu hafifu ambayo huongeza gharama za uendeshaji, shughuli za Benki, matatizo yanayoifanya ardhi yetu isitumike

kama dhamana ya mikopo, kwa mfano matatizo katika usajili wa nyaraka za mikopo *(registration of title deeds),* matatizo katika utoaji wa *court injunctions* katika Mahakama na matatizo ya utoaji wa hatimiliki za ardhi *(title deeds).* Vile vile kuna udhaifu katika kurejesha mikopo kwa baadhi ya wakopaji.

Mheshimiwa Spika, tofauti iliyopo ya viwango vya riba haisadii kujenga uwezo wa Mtanzania wa kawaida katika kujiendeleza kwa kutumia huduma za Mabenki. Ili kuwasaidia wananchi wasiathirike zaidi na hali hii, Serikali inaweka mazingira mazuri yatakayowezesha vyombo vya fedha kutoa mikopo kwa riba nafuu zaidi ikiwa ni pamoja na kuimarisha Taasisi za fedha zinazotoa mikopo midogo midogo *(Microfinance Institutions).* Pia mkazo unawekwa katika kuondoa vikwazo vinavyoifanya ardhi isiweze kutumika kama dhamana katika uombaji wa mikopo ikiwa ni pamoja na kuiangalia upya Sheria ya ardhi.

Vile vile Serikali inaendelea kuboresha miundombinu hususan njia za mawasiliano ili kupunguza gharama za uendeshaji wa Mabenki. Hali kadhalika, Serikali imeanza kuhamasisha uanzishwaji wa Benki za wananchi. Hadi kufikia Mei, 2003 Benki Kuu imeshatoa leseni sita kwa *Mufindi Community Bank, Mwanga Community Bank, Kagera Farmers Cooperative Bank, Dar es Salaam Community Bank, Kilimanjaro Cooperative Bank* na *Mbinga Community Bank* ambazo tayari zimeshaanza kutoa huduma ya mikopo kwa riba nafuu.

**MHE. ABDULA S. LUTAVI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Baada ya maelezo haya ya Mheshimiwa Naibu Waziri, bado nina maeneo madogo mawili ninahitaji ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa vielelezo vilivyopo vya ukuaji wa uchumi wetu, vinaonyesha kwamba sekta ya fedha inakua kwa asilimia ndogo sana ukilinganisha na sekta nyingine; na kwa sababu hiyo basi inaathiri kasi ya ukuaji wa uchumi kwa jumla ambayo kwa sasa tuko kwenye asilimia 6.2 tu; na kwa kuwa sababu zinazotolewa ni ile tofauti iliyo kubwa sana iliyopo baina ya riba ya kukopa na ile ya kuweka; je, kwa nini Serikali haioni sasa kwa busara kutumia vyombo vyake kama inavyofanywa kwenye nchi nyingine ili kudhibiti mwenendo mzima wa viwango hivi vya riba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, ni kwamba kama Serikali bado inataka kuendeleza imani yake ya kwamba riba hizi ziwekwe au zijiweke zenyewe kwa kutumia nguvu za soko huria, iniambie yenyewe inaamini itachukua miaka mingapi kupatikana ahueni inayotarajiwa ili wananchi hawa wapate kuwa na kichocheo cha kuweka akiba kwenye Mabenki yetu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Benki Kuu huchukua hatua mbalimbali za kufanya vigezo mbalimbali vya kiuchumi kama ilivyokubaliwa katika malengo yetu ya Kitaifa ya uchumi jumla ili kurekebisha hali hizo. Hatua zinazochukuliwa na Serikali ni pamoja na kufanya ama kuchukua hatua ambazo zitafanya fedha nyingi ambazo ziko kwenye Mabenki ziweze kukopeshwa. Tatizo tulilonalo ni kwamba amana zinazowekwa Benki

zinalipwa fedha kidogo kwa sababu Mabenki yana fedha nyingi ambazo ziko kwenye shelve hazikopeshi. Kwa hiyo, *basically,* kimsingi Benki hazihitaji fedha zile ndiyo maana wanakupa riba kidogo. Lakini pia kwa upande mwingine wanatoza riba kubwa kwa sababu ya matatizo ambayo yanasababisha mikopo isirudi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuanzisha guarantee scheme kwa ajili ya *Export Great Grant Scheme* na nyingine kwa ajili ya *SMS* pamoja na *SIDO* ambayo itakuwa *administered* na Benki Kuu ili kuhakikisha kwamba fedha zilizoko kwenye Mabenki zinakopeshwa. Pia kuboresha ushindani katika soko la fedha, kuboresha soko la hisa nchini, kuboresha miundombinu kama njia za mawasiliano na kuanzisha *Credit Reference Bureau* na kuhamasisha uanzishwaji wa Benki za wananchi na Benki za mikopo midogo midogo. Hizi ni hatua mbalimbali ambazo zinafanywa.

Kwa hiyo, Serikali inachukua hatua na Benki Kuu inatumia mbinu mbalimbali kama kutumia *Treasury Bills, Foreign Exchange Market Provisions* pamoja na *Repurchase Agreements Record* katika kurekebisha hali hii. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba Serikali inakaa kipya na inaliachia soko huria ndiyo lifanye kazi yake. Inafanya *open market interventions* lakini siyo kuweka vigezo kwamba riba itakuwa hiki ama itakuwa hivi.

Mheshimiwa Spika, itachukua miaka mingapi hali kurekebika? Naamini kwamba baada ya hatua zinazochukuliwa na Serikali haitachukua muda mrefu hali hii kurekebishwa. Kwa mfano, kwa mwaka ujao lengo letu ni kwamba mikopo kutoka kwenye Mabenki ya biashara kwenda kwenye sekta binafsi ikue kwa asilimia 24.5 kwa mwaka mmoja. Kwa hiyo, ni lengo la Serikali kuzitoa hizi fedha ili ziweze kuingia kwenye sekta binafsi.

Na. 178

**Kupeleka Madaktari Kamili Kwenye Vituo vya Afya**

**MHE. JOHN E. SINGO (k.n.y. MHE. CHARLES H. KAGONJI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania ni nchi kubwa sana na magonjwa mbalimbali yanawaandama wananchi huko waliko kwa sababu baadhi ya vituo vya afya viko mbali sana na zilipo Hospitali Kuu za Wilaya:-

(a) Je, ni lini Serikali itafikiria kupeleka madaktari kamili kwenye vituo vya afya hapa nchini ili kupambana na maradhi mabaya yanayowasumbua wananchi waishio mbali na Hospitali Kuu za Wilaya?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kama itapeleka madaktari hao kwenye vituo vya afya itapunguza wingi wa wagonjwa wa rufaa kwenye hospitali za juu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Kagonji, Mbunge wa Mlalo, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inayo azma ya kupeleka madaktari kamili kwenye vituo vya afya haraka iwezekanavyo. Hata hivyo azma hii inakwamishwa na idadi ndogo ya madaktari tuliyonayo.

Kwa kuzingatia tatizo hili la ubaha wa Madaktari, Serikali imeongeza idadi ya wanafunzi wanaoingia Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya Muhimbili toka 50 hadi 100 kwa mwaka ili kuongeza idadi ya Madaktari.

Mheshimiwa Spika, aidha, vyuo vingine vya binafsi vya *KCMC, Herbert Kairuki Memorial University* na *Bugando University* vinategemewa kuongeza idadi ya wahitimu wa Udaktari. Hivi sasa Vituo vya Afya vilivyo vingi vinahudumiwa na Maafisa Tabibu *(Clinical Officers)* na vichache vinahudumiwa na Madaktari Wasaidizi *(Assistant Medical Officers).*

Mheshimiwa Spika, tutakapokuwa na Madaktari wa kutosha, Serikali itafikiria kuwapeleka Madaktari wa Shahada ya Chuo Kikuu kwenye Vituo vya Afya. Hivi sasa Madaktari wa Shahada ya Chuo Kikuu hupelekwa katika Hospitali za Rufaa, Mikoa na Wilaya.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kupeleka Madaktari hao kwenye Vituo vya Afya kutapunguza wingi wa wagonjwa wa rufaa kwenye hospitali za juu kwani matatizo mengi yatatatuliwa na Madaktari hao kwenye ngazi ya Kituo cha afya. Lakini kama nilivyosema awali, suala hili linashindikana kutokana na uchache wa Madaktari tulionao.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na mpango mzuri wa Serikali, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Serikali ina mpango gani wa kuboresha utaratibu huu kwa kuweka wazi mpango wa sasa wa kusomesha Madaktari katika Vyuo Vikuu?

(b) Serikali ina mpango gani kuboresha mishahara ya Madaktari pamoja na vitendea kazi katika ngazi ya Vituo vya Afya?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kujiendeleza au kuingia kwenye masomo ya Udaktari uko wazi. Utaratibu huu unahusu wale wanafunzi waliomaliza Kidato cha Sita kuomba nafasi zilizopo katika Vyuo nilivyovitaja.

Mheshimiwa Spika, huko nyuma, Serikali ilikuwa ina-*sponsor* wanafunzi wanaoingia Muhimbili peke yake, lakini kama tulivyoelezwa hapa hivi karibuni ni kwamba kuanzia sasa Serikali itaanza ku-*sponsor* wanafunzi hata wale wanaokwenda kwenye vyuo vya binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuboreshwa mishahara ya Madaktari, suala hili limekuwa likifanyika mwaka hadi mwaka. Mtakumbuka kwamba mwaka jana katika *Civil Service Pay Reform* Madaktari pia wanahusika na kila mwaka mishahara yao itaendelea kuongezeka kadri uwezo wa Taifa utakavyoruhu.

Na. 179

**Maambukizo ya UKIMWI Hospitalini**

**MHE. ESHA H. STIMA** aliuliza:-

Kwa kuwa baadhi ya wanawake wajawazito hupata maambukizo ya virusi vya Ukimwi wakati wanapojifungua Hospitalini kwa sababu ya kuwa na wazazi wengi mahali penye nafasi finyu, mazingira na vyombo visivyo salama wakati wanaposaidiwa kujifungua:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza vyombo kwenye *Labour Ward* ili wanawake wajawazito waweze kujifungua kwa nafasi na mazingira salama zaidi?

(b) Endapo itabainika kuwa mwanamke aliyejifungua ameathirika na virusi vya Ukimwi kutokana na mazingira yasiyo salama wakati wa kujifungua, je, Serikali au Hospitali husika itamhudumia na kulimpa fidia mwathirika huyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Esha Stima, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), ninapenda kutoa maelezo ya jumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya hutoa huduma za afya katika hali ya usafi na utakaso *(sterility)* ili kudhibiti kuenea kwa magonjwa ya kuambukiza kati ya wahudumu wa afya na wagonjwa na baina ya wagonjwa wenyewe kwa wenyewe. Mazingira hayo huwezeshwa kwa kufanya usafi wa kawaida na kwa kutumia mbinu mbalimbali za kuua vimelea vya magonjwa katika mazingira ya utoaji huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esha Stima, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika mpango unaoendelea wa mabadiliko ya sekta ya afya, ambao lengo lake kuu ni kuboresha huduma za afa, Wizara yangu inaendelea kufanya maboresho katika maeneo mbalimbali ya utoaji huduma. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

- Kutoa mafunzo kwa watumishi wote wa afya ili kuleta ufanisi katika kazi zao.

- Kuboresha miundombinu ya afya ikiwa ni pamoja na kuimarisha majengo, ununuzi wa vifaa na madawa.

- Kuimarisha shughuli za usimamizi ili kuhakikisha kuwa huduma za afya zinatolewa katika viwango vinavyokubalika.

(b) Mheshimiwa Spika, katika hali ya kawaida si rahisi kwa mgonjwa mmoja kumuambukiza virusi vya Ukimwi, mgonjwa mwingine kwani ili maambukizi yatokee ni sharti kuwe na mwingiliano wa aina fulani wa maji ya mwili *(body fluids)* kati ya wagonjwa husika.

Uwezekano wa kuambukizwa upo zaidi kwa watumishi wa afya kwani ndio wanaoshika *body fluids* hizo wakati wanawasaidia wagonjwa. Kwa kuzingatia ukweli huu, Serikali inajitahidi kutoa vitendea kazi vya kuzuia maambuzi kwa mfano mipira ya mikononi *(gloves), aprons* na dawa za kuulia vimelea *(disinfectants)*

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wa afya wanapewa mafunzo ya kuwawezesha kujua njia za kuzuia kuambukizwa kutokana na kuwahudumia wagonjwa na pia kuzuia maambukizi kwa wagonjwa.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya lakini nina swali la nyongeza ambalo naomba anisaidie. Ni dawa gani ambayo inaua vijidudu vya Ukimwi wakati wazazi wanaposhirikiana vyombo vya uzalishaji na damu zinachanganyika wakati wanazalishwa kwa wale ambao wanazalishwa kwa vyombo maalum baada ya kushindwa kuzaa wao wenyewe?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba vijidudu au vimelea vya Ukimwi vina muda maalum wa kuishi nje ya mwili wa binadamu. Kwa hiyo, hata kama hapatatokea kusafisha, muda ukiwa mwingi nje ya mwili wa binadamu basi haviwezi tena kumwambukiza mtu mwingine, hilo moja.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, kuna utaratibu mzima wa kuchemsha *(sterilization).* Tunaelewa wazi kabisa vijidudu vingi vinashindwa kuishi katika kiwango fulani cha joto ndio maana vifaa vingi vya hospitali huwa vinafanyiwa sterilization kwa kuchemshwa. Lakini tatu, bado kuna *disinfectants,* hizi ni dawa ambazo zinaua kwa kiwango kikubwa *bacteria* na *viruses* ambao wanaweza kusababisha madhara kwa watumiaji.

Mheshimiwa Spika, nataka nimwondoe wasiwasi kwamba kuchemsha na *disinfectants* zinazotumika kwa kiwango kikubwa sana vinaweza kuondoa tatizo la kuambukizwa kutoka mgonjwa mmoja kwenda mgonjwa mwingine.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yamemalizika. Kuna tangazo moja tu la kikao cha Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mwenyekiti wake Mheshimiwa William Shellukindo, anawaomba wajumbe wa Kamati

hiyo wakutane saa tano na nusu mara baada ya kusikiliza hotuba ya Waziri anayewasilisha makadirio yake leo kwenye chumba Na. 56, vyumba vya Kamati.

Baada ya tangazo hilo, nataka kuwafahamisha Wasemaji Wakuu wa Kambi ya Upinzani kwamba zoezi la kuwapanga kwa kwenye Kamati kwa kuwa ni Wabunge wapya lilifanywa na Idara yangu kabla ya Kiongozi wa Upinzani hajawapanga Wasemaji wake. Kwa hiyo, imetokea kwamba kuna baadhi ya Wasemaji wamewekwa kwenye Kamati ambazo hazishughulikiwi na Wizara yake. Napenda kuwafahamisha kwamba tutalirudia zoezi hilo ili kila Msemaji awe kwenye Kamati inayohusika na Wizara yake. *(Kicheko)*

Tunaendelea na *Order Paper,* Katibu!

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2003/2004
### Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya wa Chama cha Mapinduzi Mheshimiwa Abu Kiwanga, wa Jimbo la Kilombero, Mheshimiwa Nazir Karamagi wa Jimbo la Bukoba Vijijini, Mheshimiwa Ndeka Nziriye wa Jimbo la Kigoma Kusini, Mheshimiwa Sumri Mohamed wa Jimbo la Mpanda Magharibi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya wa *CUF,* Mheshimiwa Karim Said Othman wa Jimbo la Chambani, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim wa Jimbo la Mtambile, Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib wa Jimbo la Chonga, Mheshimiwa Ali Said Salim wa Jimbo la Ziwani, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma wa Jimbo la Micheweni, Mheshimiwa Salim Omar Ali wa Jimbo la Tumbe, Mheshimiwa Mchande Salim Mchande wa Jimbo la Konde, Mheshimiwa Khamis Ali Saleh wa Jimbo la Mgogoni, Mheshimiwa Mohamed Ali Said wa Jimbo la Wingwi, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa wa Jimbo la Gando, Mheshimiwa Khalifa Mohammed Issa wa Jimbo la Mtambwe, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki wa Jimbo la Ole, Mheshimiwa Mwadini Abass Jecha wa Jimbo la Utaani, Mheshimiwa Ali Said Juma, Mbunge wa Kojani na Mheshimiwa Omar Juma Omar wa Jimbo la Pandani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, kwa kuteuliwa kuwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani katika masuala ya Mawasiliano na Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maelezo ya hoja ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, napenda pia kuchukua fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wenzangu walionitangulia kuwasilisha hoja zao kwa hotuba nzuri zenye ufafanuzi wa kina kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa sera, kukua kwa uchumi, maendeleo ya jamii na matarajio yetu kwa kipindi kinachokuja cha mwaka 2003/2004.

Vile vile, napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliochangia hoja za sekta zilizotangulia. Kwani michango yao imesaidia kwa kiwango kikubwa kuboresha hotuba ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, zimefafanua kwa kina hali na mwelekeo wa uchumi na fedha nchini kwa kipindi cha mwaka 2002/2003. Pamoja na mafanikio ya kutia moyo yaliyoelezewa katika hotuba hizo, bado tunatakiwa kuboresha mikakati yetu ya utekelezaji wa sera na programu zilizopangwa ili kufikia kiwango kizuri zaidi cha ubora wa maisha ya jamii. Sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi zitaendelea kutoa mchango wake kwa kuendelea kuboresha miundo mbinu na kuimarisha mifumo ya uendeshaji wa sekta kwa kuishirikisha sekta binafsi na wananchi katika kupanga, kuendeleza na kutoa huduma. Wizara itaendelea kutumia vyombo vyake vya udhibiti ili kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa ni bora, zenye kuzingatia viwango vinavyokubalika na za gharama nafuu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imefafanua vizuri kuhusu utekelezaji wa programu mbalimbali za Serikali zenye lengo la kukuza na kuboresha hali za wananchi hususani kuwaondolea kero ikiwa ni pamoja na umaskini, elimu duni, maradhi na mazingira yasiyoridhisha. Ni matarajio yangu kuwa Waheshimiwa Wabunge wataendelea kuishauri Serikali pamoja na Wizara yangu njia bora za kuyafikia maendeleo tunayoyatarajia.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kueleza hali ya utendaji ilivyokuwa katika kipindi kilichopita, napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, Mbunge wa Tabora Mjini kwa kuyachumbua kwa undani na kuyapitisha makadirio ya matumizi ya Wizara kwa mwaka 2003/2004. Naadhidi kwamba maoni, maelekezo na ushauri mzuri ambao umeiwezesha Wizara yangu kusahihisha dosari mbalimbali katika mipango na utendaji wa kazi za sekta zetu.

Kamati ya Miundombinu ilipata nafasi ya kutembelea taasisi zifuatazo, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA),* Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga *(TCAA),* Mamlaka ya Hali ya Hewa *(TMA),* Tume ya Mawasiliano Tanzania *(TCC),* Mamlaka ya Bandari Tanzania *(THA),* Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* na Mamlaka ya Reli ya

Tanzania na Zambia *(TAZARA)*. Ushauri pamoja na maelekezo yao yatazingatiwa katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya sekta za mawasiliano na uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, utendaji katika sekta ya mawasiliano na uchukuzi umeendelea kuongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Sera ya Kuondoa Umaskini, Usimamizi wa Mazingira pamoja na sera mbalimbali za sekta za Mawasiliano na Uchukuzi na zile za sekta nyingine ambazo zinahusiana na sekta zetu. Katika kutekeleza sera hizo, Wizara imeendelea kushirikiana na wadau hususan katika kutekeleza jukumu la kurekebisha mifumo ya uendeshaji wa sekta ili kuongeza ufanisi na kuondoa kero zinazowakabili wananchi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002 wakati kama huu nilifahamisha Bunge lako Tukufu kuhusu maendeleo yaliyofikiwa katika ukamilisha Sera za Sekta za Mawasiliano na Uchukuzi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Sera ya Taifa ya Uchukuzi sasa imekamilika na kuidhinishwa na Serikali. Aidha, mikakati ya utekelezaji wa sera hii imeandaliwa na ipo katika hatua za kuidhinishwa. Kukamilika kwa sera hii ni jambo la faraja kwani sasa sekta ina mwongozo na mwelekeo uliowekwa bayana kwa kushirikiana na wadau wote muhimu.

Mheshimiwa Spika, uzinduzi rasmi wa Sera ya Taifa ya Uchukuzi unatarajiwa kufanyika baadaye mwaka 2003 ambapo Wizara inatarajia kuanzisha Wiki ya Uchukuzi *(Transport Week)*. Katika wiki hii wananchi watapata fursa ya kuitafakari Sera yenyewe, mikakati na utekelezaji wake. Tunatarajia kupata ushiriki wao katika kuitekeleza sera na pia kuchangia maoni na ushauri katika masuala ya jumla katika sekta hii ya uchukuzi. Wiki ya Uchukuzi itasheherekewa kila mwaka kuanzia mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeidhinisha Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Mawasiliano na Habari *(ICT)*. Wizara inaendelea na maadalizi ya Programu ya utekelezaji wa Sera hiyo, kuandaa mazingira mazuri ya usimamizi, utendaji na uratibu wa asasi na taasisi mbalimbali zinazoshughulikia masuala yote yanayohusiana na huduma za *ICT*. Tutashirikiana na wadau husika katika kutekeleza miradi inayohusiana na kuweka mitandao ya mawasiliano ya Serikalini *(e-government),* kilimo *(e-egriculture),* biashara *(e-commerce),* elimu *(e-education or schoolnet),* afya *(e-medicine)* na ya utalii *(e-tourism)*.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Huduma za Posta, matayarisho yake yamekamilika na itaidhinishwa rasmi na Serikali baada ya muda mfupi. Ni matarajio yangu kwamba Sera hii ya Posta pamoja na mikakati yake ya utekelezaji itakuwa tayari imeidhinishwa na kuanza kutumika rasmi kabla ya mwisho wa nusu ya kwanza ya mwaka huu wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Wizara ilikamilisha kuandaa Mpango Kamambe wa Uendelezaji Miundo mbinu ya Uchukuzi *(Transport Infrastructure Master Plan)*. Aidha, katika kutekeleza mpango huo, Wizara imeandaa programu ya muda mrefu (miaka 20) ya uendelezaji wa sekta ya uchukuzi *(Transport Sector Development Program)*. Programu hii itatekelezwa kwa awamu. Hivi sasa, Wizara

ipo kwenye hatua za awali za kumpata mtaalamu mwelekezi *(Cunsultant)* wa kushauri katika maandalizi ya programu ya miaka mitano ya awali ya utekelezaji *(5 year Plan for Implementation of Transport Sector Development Program).*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC),* iliendelea na zoezi la kurekebisha mifumo ya umilikaji, uendeshaji na utoaji huduma kwa asasi zilizopo chini yake. Asasi ambazo zipo kwenye hatua mbalimbali za ubinafsishaji ni pamoja na Shirika la Reli *(TRC),* Mamlaka ya Bandari *(THA)* na Kampuni ya Huduma za Meli *(Marine Services Company Limited).*

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikamilisha rasmi zoezi la kubinafsisha Shirika la Ndege Tanzania *(ATC)* mwezi Desemba 2002. Shirika la Ndege la Afrika Kusini *(SAA)* lilishinda zabuni ya kununua hisa za Serikali asilimia 49 kwa Dola za Kimarekani milioni 20. Kampuni mpya ya Ndege, *Air Tanzania Company Limited (ATCL)* ambayo bado Serikali ina hisa asilimia 51 imekwishaanza kufanya kazi ya usafiri wa anga ndani na nje ya nchi. Aidha, limeundwa Shirika Mama *Air Tanzania Holding Corporation (ATHCO)* ambalo litasimamia madeni, mali na raslimali ambazo hazikuchukuliwa na *ATCL.*

Mheshimiwa Spika, baada ya mwekezaji kupatikana, hali ya utendaji wa Kampuni inategemewa kuimarika zaidi kwa kuongeza masoko ya hapa nchini na nje ya nchi. Mbali na ndege moja iliyorithiwa aina ya *Boeing 737,* Kampuni imeongeza ndege mbili aina ya *B737-200* na ndege mbili aina ya *Dash-8.* Kuna matarajio ya kuanzisha safari za Ghuba hivi karibuni. Kuanzia mwezi Aprili, 2003, Kampuni imeongeza idadi ya safari katika vituo vya Dar es Salaam; Mwanza, Mtwara, Kilimanjaro, Arusha na Zanzibar kwa hapa nchini na Nairobi, Johnnesburg, Mombasa na Entebbe kwa safari za nje ya nchi. Safari za kwenda, Mbuji Mayi na Kinshasa zinatarajiwa kuanza hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kasoro za hapa na pale za kipindi cha mpito, haya ni mafanikio makubwa hasa ikiwekwa maanani hali mbaya ambayo *ATC* ilikuwa imefikia kabla ya kumpata mbia. Pamoja na Shirika hili kubinafsishwa, chapa za kibiashara ambayo ni alama za Kitaifa hususani picha ya Twiga itaendelea kuonekana kwenye ndege za *ATCL.* Marejeo ya kiufundi ya jinsi picha hiyo itakavyoonekana tena kwenye ndege za *ATCL* pamoja na rangi za bendera ya Taifa yamekamilika.

Mheshimiwa Spika, Serikali na mwekezaji katika *TTCL* bado hatujakubaliana kuhusu taarifa inayotoa hali halisi ya kifedha ya *TTCL* kwa kipindi cha 2000. Baada ya *MSI* mwekezaji katika *TTCL* kufungua kesi Mahakama Kuu, London na Serikali kufungua kesi Mahakama Kuu, Dar es Salaam pande zote zinazohusika yaani Serikali na Mwekezaji *(MSI/DETECON),* tarehe 20 Februari 2003, zilikubaliana kusimamisha kesi hizo kwa muda na kumteua Mtaalamu Huru wa Kimataifa ili kuangalia upya taarifa hiyo ya mahesabu ya *TTCL* ya mwaka 2000 na kushauri ipasavyo. Mtaalam huyo ameteuliwa na Rais wa Taasisi ya Mahesabu yenye Makao yake Makuu Uingereza inayoitwa *The Institute of Chartered Accountants - ICA London - UK.*

Timu ya Serikali katika kushughulikia suala hili, inaongozwa na Katibu Mkuu Kingozi. Mtaalam huyo atapaswa kufanya kazi yake kulingana na Hadidu za Rejea alizopewa na atamaliza kazi yake ndani ya miezi mitatu baada ya kila upande kukamilisha mahitaji yote ya maelezo yatakayohitajiwa na mtaalam huyo. Pande zote zimeahidi kuheshimu maoni ya mtaalam huyo kama uamuzi wa mwisho ili kuendelea na utekelezaji wa mpango wa uwekezaji katika *TTCL.*

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuboresha huduma za mawasiliano vijiji, Serikali inafanya utafiti wa kuangalia uwezekano wa kuanzisha Mfuko maalum wa Kusaidia Mawasiliano Vijijini *(Rural Telecommunications Fund).* Utafiti huo utatupatia mwongozo wa jinsi ambavyo mfuko huu utachangiwa, kuendeshwa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Simu 2000* ilisajiliwa mwaka 2000 kushughulikia mali zote za *TTCL* ambazo sio za msingi katika kutoa huduma za simu *(non core assets).* Majukumu ya kampuni hii ni kukusanya fedha na kulipa pensheni kwa wastaafu wa lililokuwa Shirika la Posta na Simu la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Fedha hizo zinakusanywa kwa kuuza hizo mali ambazo si za msingi katika huduma za simu.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Juni 2002, Kampuni ya *Simu 2000* ilikuwa imeuza nyumba 17 na kufanikiwa kulipa kiasi cha shilingi bilioni 1.4 kwa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* ambazo ni pensheni na kamisheni.

Aidha, nyumba 22 ziliuzwa katika kipindi cha kuanzia Julai, 2002 hadi Julai, 2003 na malipo ya shilingi bilioni 2 zililipwa tena *NSSF.* Malipo hayo yalijumuisha pensheni na kamisheni. Pamoja na hatua hizo, Kampuni ilikabiliwa na matatizo mawili makubwa. Tatizo la kwanza lilihusu ulipaji wa kodi *(capital gain tax)* kila inapouza nyumba. Juhudi zinafanywa kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha ili kupata ufumbuzi wa tatizo hili ambalo linaweza likaathiri ulipaji wa pensheni.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine linahusu kushitakiwa na wapangaji waliokuwa wakiishi kwenye nyumba zilizomilikishwa kwa kampuni. Kesi hii iliisababishia kampuni kuwa na ufanisi mdogo katika kukamilisha malengo yake. Hata hivyo, kesi hii sasa imefutwa na Mahakama Kuu tarehe 18 Machi, 2003 na sasa Kampuni inaendelea kuuza nyumba zilizobakia na kukusanya madeni ili kufanikisha malipo ya pensheni.

Mheshimiwa Spika, juhudi na matarajio ya kumpata mbia mwenye nia, uwezo na utaalam wa kuendesha Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* bado zinaendelea. Kama ambavyo nililitaarifa Bunge lako Tukufu mwaka 2002, Wizara kwa kushirikiana na *PSRC* iliendelea na taratibu za *tender* na hatimaye makampuni saba yalionyesha nia ya kutaka kuendesha Shirika. Hadi kufikia hatua ya kukamilisha maandalizi ya zabuni makampuni sita yalijitoa na kubakia moja. Serikali baada ya kutafakari faida na athari za kubakia na mzabuni mmoja hasa kwa kuzingatia kuwa muundombinu wa reli ni mkubwa na ukodishaji ni wa muda mrefu yaani miaka 25 hivyo ikaona ni vema zoezi hili lisitishwe na tenda itangazwe upya. Hivi sasa, *PSRC* kwa kushirikiana na wadau husika wameanza maandalizi ya kutangaza upya *tender* hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia *(TAZARA),* taratibu za kurekebisha Mamlaka hii zimeanza kwa pamoja na wenzetu wa Zambia. Serikali zetu zinaendelea kuwasiliana kwa lengo la kuwa na maamuzi ya pamoja katika urekebishaji wa mamlaka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa ukodishaji wa Kitengo cha Kontena mwaka 2000, Wizara kwa kushirikiana na *PSRC* iliendelea na jukumu la kutafuta mikakati bora ya kubinafsisha vitengo vilivyobakia vya Mamlaka ya Bandari *(THA)*.

Katika kipindi cha mwaka 2002/2003 mtaalam mwelekezi alikamilisha zoezi la kufanya uchambuzi wa mikakati inayofaa kubinafsisha vitengo hivyo. Mkakati huu umewasilishwa Serikalini kwa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa zoezi la ubinafsishaji wa Kampuni ya *Marine Services Company Limited (MSC)* ambayo inatoa huduma za usafiri kwenye Maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa bado unaendelea baada ya Serikali kuidhinisha mkakati wa ubinafsishaji. Kwa kuzingatia uwezo tofauti wa kibiashara kwa Maziwa yote matatu, Serikali imeamua kwa kampuni ya *MSC* itabinafsishwa kama vitengo tofauti kwa kuzingatia maziwa yalivyo. Utaratibu huu utatoa fursa kwa mwekezaji mwenye nia kuchagua Ziwa moja au zaidi kufanya hivyo. Utaratibu huu utaiwezesha Serikali kuendelea kusaidia usafiri katika Ziwa au Maziwa ambayo hayatakuwa na mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002, nililieleza Bunge lako Tukufu kwamba Shirika la Usafiri Dar es Salaam *(UDA)* limeendelea kuimarika. Mshauri mwelekezaji amekamilisha ripoti ya kupata mkakati bora wa kubinafsisha *UDA*. Serikali inayatafakari mapendekezo yaliyotolewa ili kuyatolea maamuzi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Wizara iliendelea na jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli za utoaji huduma za Mamlaka ya Usalama na Usafiri wa Anga *(TCAA),* Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA),* Wakala wa Hali ya Hewa *(TMA)* na Wakala wa Ndege za Serikali. Kwa ujumla, huduma za taasisi hizi zimeendelea kukua kwa ufanisi mzuri.

Aidha, katika kipindi hicho, Tume ya Mawasiliano *(TCC)* iliendelea na majukumu yake ya udhibiti wa shughuli za Mawasiliano nchini. Umuhimu uliwekwa kwenye kuongeza na kuboresha kiwango cha huduma za mawasiliano ya simu kwa kuyawezesha makampuni yote ya simu nchini kuendelea kupanua ushirikiano wa kibiashara.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuboresha shughuli za udhibiti nchini, Serikali imeazimia kutekeleza uamuzi wa Kitaifa wa kuanzisha Vyombo huru vya udhibiti na kuvipa nguvu zaidi ya kisheria ili kuruhusu nguvu za soko na ushindani zisimamie ukuaji wa shughuli za kibiashara katika jamii. Kwa misingi hiyo, mwezi Aprili, 2003 Bunge lako Tukufu lilipitisha Miswada ya Sheria ya kuanzisha upya Mamlaka ya Udhibiti wa sekta ya Usafiri wa Anga na kuunganisha Tume ya

Mawasiliano na Tume ya Utangazaji. Mamlaka ya Udhibiti wa Anga itakuwa na jukumu la kudhibiti Taasisi au Mashirika yanayoendesha viwanja vya ndege, yanayotoa huduma za kibiashara katika viwanja vya ndege, yanayotoa huduma za chakula kwenye ndege, huduma za maegesho na matengenezo ya ndege, usalama *(Airport Security)* na mafuta ya ndege katika viwanja. Aidha, mamlaka itakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa huduma za usafiri wa anga hapa nchini zinatolewa kwa mujibu wa viwango na taratibu zinazowekwa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga *(ICAO).*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Udhibiti katika Sekta ya Mawasiliano itahusisha huduma za posta, simu, ugawaji na udhibiti wa masafa ya matangazo ya redio, utangazaji kupitia redio na televisheni na teknolojia ya mawasiliano ya habari.

Aidha, Mamlaka itakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa huduma za mawasiliano ya simu nchini zinatolewa kwa mujibu wa viwango na taratibu zilizowekwa na Umoja wa Simu Duniani *(ITU).* Mwaka 2003/2004, Wizara itashirikiana na Wizara nyingine husika ili Mamlaka hizi zianzishwe rasmi mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia iliendelea na hatua ya kuzipitia Sheria mbalimbali za Mawasiliano na Uchukuzi ili kuziwezesha kuwa na uwiano na sera za jumla za uchumi zenye mwelekeo wa soko huria na ushirikishwaji wa sekta binafsi. Sheria zilizofanyiwa marekebisho ni pamoja na Sheria ya Shirika la Reli Tanzania *(Tanzania Railways Corporation Act, 1977)* na Sheria ya Mawasiliano *(Tanzania Communications Act, 1993).*

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na *PSRC* inaendelea na taratibu za kuwezesha kuanza rasmi kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Sekta za Usafirishaji wa Nchi Kavu na Majini ijulikanayo kama *Surface and Maritime Transport Regulatory Authority (SUMATRA).* Ni matarajio yetu kwamba Mamlaka hii itaanza shughuli zake kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2003/2004 na hivyo kuboresha udhibiti katika uendeshaji wa huduma za sekta ndogo za nchi kavu na majini.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia imeendelea kusimamia shughuli za Mikataba ya Utendaji *(Performance Contracts)* kati ya Serikali na Mashirika yaliyo chini yake. Mashirika yanayoendelea kuwa na Mkataba wa utendaji na Serikali ni pamoja na Mamlaka ya Bandari *(THA),* Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* na Shirika la Posta *(TPC).* Kuwepo kwa Mikataba hii kumesaidia sana Mashirika yetu kuweza kufikia malengo mbalimbali ya kiutendaji yaliyojiwekea na hatimaye kuboresha tija.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imeendelea kushiriki kwenye Jumuiya mbalimbali za Kimataifa zikiwemo Jumuiya za Afrika Mashariki *(EAC)* na ile ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC).* Miradi mbalimbali iliyoainishwa katika nchi wanachama wa Afrika Mashariki imeendelea kutekelezwa. Miradi hiyo ni pamoja na ile ya sekta za utabiri wa hali ya hewa, mawasiliano na uchukuzi, uboreshaji wa huduma za posta, simu, usalama wa usafiri wa anga na usafiri kwa njia ya maji hususan eneo la Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kuboresha hali ya miundombinu na huduma za reli, barabara, mawasiliano na usalama wa usafiri wa anga, Jumuiya ya Afrika Mashariki iliandaa mkutano wa wafadhili mwezi Aprili, 2003 ili kutafuta fedha za kuanza kazi za miradi mbalimbali. Katika mkutano huo, wafadhili walionyesha nia ya kutaka kusaidia. Mwelekeo huu ni changamoto kwetu katika kukuza uchumi wa nchi zetu. Miradi iliyowasilishwa kwa wahisani ni pamoja na ile ya barabara, reli ya Tanga - Arusha - Musoma pamoja na uchunguzi wa hali ya uendeshaji wa huduma za usafiri kwa njia ya reli katika nchi za Jumuiya, huduma za simu *(cross border connectively project),* usalama wa usafiri wa anga, usalama wa usafiri katika Ziwa Victoria, huduma za posta na mpango wa maendeleo ya uendelezaji wa miundombinu ya hali ya hewa katika nchi za Jumuiya.

Mheshimiwa Spika, *New Partnership for African Development (NEPAD)* ni mpango mpya wa ushirikiano na maendeleo ya umoja wa Afrika. Madhumuni ni kuondoa umaskini na kuleta ushirikiano wa pamoja na Serikali imeamua kutekeleza masuala ya *NEPAD* kisekta. Sekta mojawapo ni ya miundombinu ambayo inajumuisha nyanja za uchukuzi, mawasiliano, hali ya hewa, nishati na madini, elimu ya juu, ujenzi na ardhi. Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine itajitahidi kutekeleza jukumu hili na hasa sekta hii ya miundombinu isibakie kuwa kikwazo katika maendeleo ya uchumi wetu na ule wa Jumuiya ambazo Tanzania ni mwanachama mfano *SADC* na *EAC* na Afrika kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza kwa ujumla hali ya utendaji wa sekta ya mawasiliano na uchukuzi katika kipindi cha mwaka 2002/2003 na kutoa mwelekeo wa jumla wa mpango wa mwaka 2003/2004, napenda kuchukua nafasi hii kueleza kwa undani zaidi mwelekeo, mipango, mikakati na utendaji wa maeneo mbalimbali ya Wizara ambayo tumepewa dhamana ya kuyasimamia.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, sekta ya usafiri na uchukuzi kwa njia ya barabara imeendelea kuimarika katika kufanikisha shughuli za kiuchumi na kimaendeleo ya jamii katika nchi yetu. Imekua kwa 7.9% mwaka 2002/2003 na inarajiwa kukua kwa 9% mwaka 2003/2004. Hii inatokana na ukweli kwamba sekta hii inabeba karibu asilimia 70 ya mizigo yote inayosafirishwa nchini.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tayari tumeelezwa na Waziri wa Ujenzi jitihada kubwa zinaendelea kufanywa na Serikali kuendeleza na kuimarisha barabara nchini. Kuendelea kuimarika kwa hali ya barabara kuu kumeongeza ushindani katika utoaji wa huduma za magari ya abiria na mizigo. Hali hii imeleta ushindani katika utoaji wa huduma za uchukuzi na kulinda upandishaji holela wa viwango vya nauli. Hivi sasa wasafiri hasa kwenye sehemu za miji mikubwa au barabara kuu wameendelea kuwa na uhuru wa kuchagua usafiri wanaoutaka kwa kuzingatia ubora wa huduma, nauli au muda wa safari.

Mheshimiwa Spika, bado gharama za uchukuzi na usafirishaji Vijijini zimeendelea kuwa kubwa na zisizokidhi mahitaji kutokana na ubovu wa barabara. Kama Sera ya Taifa ya Uchukuzi inavyoelekeza, Wizara inaendelea kushirikiana na Wizara ya

Ujenzi na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kubuni mikakati mbalimbali itakayowezesha upatikanaji wa fedha za matengenezo ya barabara hizo.

Aidha, Wizara inaendelea kushirikiana na wadau wengine ikiwa ni pamoja na muungano wa wasafirishaji wa abiria na mizigo kupitia vyombo vyao. Vyombo hivyo ni pamoja na Muungano wa wenye Kumiliki Mabasi *(Tanzania Bus Owners Association),* Muungano wa wenye Kumiliki Magari ya Kusafirisha Mafuta *(Tanzania Tankers Association)* na wale wenye Kumiliki Malori *(Tanzania Truck Owners Association).* Wizara itaendelea kutoa ushirikiano wa pamoja na vyombo hivi pale inapowezekana kwa lengo la kuboresha hali ya usafiri Mikoani na Vijijini.

Mheshimiwa Spika, usafiri katika miji yetu hapa nchini unaendelea kutolewa katika mazingira ya ushindani mkubwa. Sekta binafsi inaendelea kutoa mchango mkubwa katika huduma hii. Kiwango kizuri cha ushindani kiliendelea kuleta unafuu wa nauli kwa Wananchi kwa baadhi ya njia. Hata hivyo, katika miezi ya hivi karibuni utoaji wa huduma hizi ulikabiliwa na tatizo la kupanda mara kwa mara kwa bei ya mafuta na vipuri kunakotokana na kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania ikilinganishwa na Dola ya Kimarekani, jambo ambalo lilileta changamoto kubwa kwa watoa huduma. Matatizo mengine ni uchache wa mabasi makubwa yenye nafasi za kukaa abiria badala ya kukaa kwenye viti vilivyosongamana na kubanana na hivyo kuwafanya washindwe kusafiri kwa raha na amani. Hali hii pia huhatarisha usalama wa abiria pindi ajali inapotokea.

Hata hvyo, Serikali iliendelea kusimamia usalama wa magari hayo pamoja abiria kupitia Mamlaka za Leseni za Usafirishaji za Mikoa na hasa ile ya Mkoa wa Dar es Salaam. Aidha, kazi imefanyika kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani, ili kuhakikisha kwamba magari yanayotoa huduma ni yale yanayokubalika kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa.

Mheshimiwa Spika, utendaji wa Shirika la Usafiri Dar es Salaam *(UDA)* kwa kipindi cha mwaka 2002/2003 uliendelea kuonyesha ufanisi ikilinganishwa na utendaji wa kipindi kilichopita. Katika kipindi hiki mabasi ya Shirika yalikuwa 40 ikilinganishwa na mabasi 32 mwaka uliopita. Ongezeko hili lilitokana na Shirika kuweza kununua mabasi 10 mapya. Katika kipindi cha mwaka 2002/2003 Shirika la *UDA* lilipata mapato ya shilingi milioni 684.9 kutokana na shughuli za usafirishaji ikilinganishwa na shilingi milioni 561.4 zilizopatikana mwaka 2001/2002. Hili ni ongezeko la asilimia 22%. Hata hivyo mchango wa Shirika hili bado ni mdogo sana ikilinganishwa na mabasi zaidi ya elfu tatu yanayotoa huduma katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar es Salaam lina mpango wa kuanzisha mradi wa mabasi yaendayo haraka *(Bus Rapid Transit - BRT)*. Mradi unaitwa wa mabasi yaendayo haraka kwa sababu yanatumia njia maalum bila kuzuiwa na magari mengine. Lengo la mradi wa mabasi yaendayo haraka ni kuboresha usafi wa hewa kwa kuwa na mpango wa usafiri Jijini unaozingatia yafuatayo: mabasi ya kisasa yatoayo moshi wa viwango vinavyotakiwa ili kutoharibu mazingira na kukuza na kuboresha usafiri usiotumia vyombo vya moto (baiskeli na watembea kwa miguu).

Mheshimiwa Spika, mradi utakuwa na mabasi makubwa ambayo yatamilikiwa na Makampuni au Mashirika binafsi. Watu wanaomiliki mabasi ya daladala watashauriwa na kuwezeshwa waungane na kuunda Kampuni zitakazopewa Mikataba ya kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, mradi utatekelezwa kwa awamu. Awamu ya kwanza itahusisha barabara kuu tatu ambazo ni barabara za Morogoro, Mandela na Nyerere. Awamu hii itagharimu shilingi bilioni 1.2. Awamu ya kwanza inatarajiwa kukamilika Oktoba/Novemba 2005. Serikali kupitia Halmashauri ya Jiji pamoja na wafadhili watagharamia mradi huu.

Mheshimiwa Spika, mradi utaanza Agosti 2003 kwa maandalizi yatakayohusisha utafiti wa awali, gharama, nyenzo na wafanyakazi watakaohusika kwenye mradi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, udhibiti wa huduma za usafirishaji kwa njia ya barabara umeendelea kufanywa na Mamlaka Kuu ya Leseni za Usafirishaji *(CTLA)* na Mamlaka Kuu ya Leseni za Mikoa *(RTLAs).* Leseni zilizotolewa zilihusu magari yanayotoa huduma ndani na nje ya Mikoa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2002 hadi Machi 2003 Mamlaka Kuu ya Leseni za Usafirishaji ilitoa jumla ya leseni 11,103 kwa magari ya abiria na mizigo ikilinganishwa na kipindi kama hiki cha mwaka uliotangulia ambapo jumla ya leseni 8,376 zilitolewa. Leseni za magari ya abiria ni 1,599 na zile za magari ya mizigo ni 9,504. Kiasi cha fedha zilizokusanywa kama maduhuli kutokana na ada za leseni hizo ni shilingi bilioni 1.068 ikilinganishwa na shilingi milioni 897.838 zilizokusanywa kipindi kama hicho mwaka 2001/2002.

Mheshimiwa Spika, mafanikio hayo yametokana na jitihada za kuitangaza Mamlaka kwenye Vyombo vya habari na ufanisi katika ukaguzi unaofanywa wa kuwasaka wanaotoa huduma bila leseni. Mamlaka imeweka utaratibu wa kufanya ziara za kikazi Mikoani mara kwa mara kwa madhumuni ya kutoa leseni na hivyo kuongeza mapato. Aidha, Mamlaka iliendelea na utaratibu wa kuimarisha ofisi zake za kanda kwa kupeleka vitendea kazi ikiwa ni pamoja na magari.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Mamlaka imeazimia kufungua *Expenditure Accounts* kwenye maeneo yenye makusanyo makubwa ya fedha zitokanazo na ada za leseni ili kurahisisha uwasilishaji wa fedha mara tu baada ya kukusanywa. Aidha, Mamlaka inatarajia, kuimarisha matumizi ya kompyuta katika kutunza kumbukumbu na kufanya mawasiliano. Hii itarahisisha mawasiliano na kupunguza muda wa uandaaji na utoaji wa leseni kutoka saa 8 hadi saa 3. Mamlaka pia, inakusudia kuendeleza uhusiano wake na Vyama vya wasafirishaji wa abiria na mizigo kwa nia ya kuwahamasisha wananchama wake waone umuhimu wa kukata leseni za usafirishaji kwa magari yao.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002, sekta ya usafiri kwa njia ya reli hapa nchini imeendelea kuhudumiwa na Mashirika mawili ambayo ni Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia *(TAZARA)*.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa 2002/2003, Shirika la Reli Tanzania lilipata mafanikio mazuri ikilinganishwa na miaka iliyopita. Katika kipindi hicho Shirika lilisafirisha jumla ya tani milioni 1.45 ikilinganishwa na tani milioni 1.35 zilizosafirishwa mwaka 2001. Lengo la Shirika lilikuwa ni kusafirisha tani milioni 1.35.

Aidha, mafanikio hayo ni asilimia 7 zaidi ya yaliyopatikana mwaka 2001 na asilimia 7.1 zaidi ya lengo. Katika mwaka 2002, Shirika pia lilisafirisha jumla ya abiria 684,796 ikilinganishwa na abiria 727,851 waliosafirishwa katika kipindi cha mwaka 2001. Lengo la Shirika lilikuwa kusafirisha abiria 725,000. Utendaji huu ni asilimia 5.9 chini ya ule wa mwaka uliopita wa asilimia 5.5 chini ya lengo. Kupungua kwa abiria waliosafirishwa kunatokana na ajali mbaya ya treni ya abiria iliyotokea kati ya stesheni ya Msagali na Igandu mwezi Juni, 2002 ambapo maisha ya abiria wengi yalipotea na mabehewa kubaribika.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitangazia Bunge lako Tukufu kwamba Ujerumani, imetupa msaada wa shilingi milioni 800 ili Shirika likarabati mabehewa 11 yaliyoharibika wakati wa ajali ya treni iliyotokea kati ya Igandu na Msagali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato, Shirika lilikusanya shilingi bilioni 59.915 katika mwaka 2002 ikilinganishwa na shilingi bilioni 56.609 zilizokusanywa katika kipindi cha mwaka 2001. Lengo lilikuwa kukusanya shilingi bilioni 59.562. Hivyo, mapato yalikuwa juu ya lengo kwa asilimia 0.6, ikiwa ni sawa na ziada ya shilingi milioni 353. Aidha, Shirika limekabili kadri ya uwezo wake tatizo la mabehewa na injini uliosababishwa na ukosekanaji wa vipuri na uchakavu wa injini zenyewe. Changamoto nyingine imekuwa ni kukabiliana na wizi wa vifaa vya mawasiliano na mafuta.

Mheshimiwa Spika, ili kuyakabili matatizo yanayojitokeza, Shirika la Reli *(TRC)* katika kipindi cha 2003/2004, linakusudia kutekeleza mradi 59 ambayo inajumuisha miradi 20 ya njia ya reli kwa gharama ya shilingi bilioni 4.98, miradi 18 ya madaraja na makalavati kwa gharama ya shilingi milioni 327, miradi 6 ya mawasiliano ya simu kwa gharama ya shilingi bilioni 10.603. Shirika litaendeleza uwekaji nyaya za mawasiliano kati ya Dodoma na Tabora zijulikanazokama *Optic fibre.* Miradi mingine itakayotekelezwa ni 10 ya majengo kwa gharama za shilingi milioni 413 na miradi 5 ya kukarabati mabehewa na injini kwa gharama ya shilingi bilioni 2.574 jumla ni shilingi 18.899. Aidha, mradi wa awali wa uimarishaji wa reli ya Singida - Manyoni na Kaliua - Mpanda unatarajiwa kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Shirika litaendelea kununua vipuri kwa kutumia uwezo wake na kuimarisha viwango vya ulinzi sehemu zote za Shirika ili kupunguza wizi wa nguzo na nyaya za mawasiliano. Pamoja na miradi iliyotajwa Shirika pia litatekeleza miradi ya kuweka kokoto na kubadilisha na kuweka reli zenye uzito zaidi kwenye baadhi ya

sehemu. Katika kipindi cha mwaka 2003, Shirika la Reli Tanzania limejiwekea lengo la kusafirisha jumla ya abiria 558,820 na shehena zenye uzito wa tani milioni 1.4.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Mamlaka ya reli ya Tanzania na Zambia iliweka lengo la kusafirisha tani 650,000 za mizigo na abiria 1,000,000. Hadi kufikia kipindi cha robo tatu ya mwaka 2002/2003, Mamlaka ilikuwa imesafirisha tani 470,141 za mizigo na abiria 779,484. Mamlaka ilipata jumla ya shilingi bilioni 19.1 ikilinganishwa na shilingi bilioni 22.65 zilizokadiriwa kupatikana kwa kipindi hicho. Kiwango hiki ni pungufu kwa asilimia 15.67 ikilinganishwa na makadirio.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, changamoto zilizoikabili Mamlaka ni pamoja na kutafuta fedha za uendeshaji. Uhaba wa fedha umeathiri pamoja na mambo mengine ukarabati wa miundombinu, ucheleweshaji wa malipo ya wafanyakazi na uchakavu wa vifaa. Aidha, uhaba huo wa fedha umeathiri kwa kiasi kikubwa ukarabati wa muundombinu wa reli hasa upande wa Tanzania ambako hali ya njia ya reli si nzuri hivyo kusababisha kuwekwa kwa vidhibiti mwendo *(Speed Restrictions)* katika sehemu nyingi. Mmomonyoko wa udongo katika Wilaya ya Mlimba katika eneo la kilometa 555 umeathiri kwa kiasi kikubwa ubora wa njia ya reli.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto zilizojitokeza, mikakati imeandaliwa ili kukabiliana nazo ambayo ni pamoja na kutayarisha mipango ya muda mfupi na kati ya kukarabati reli, injini za treni na mabehewa ya abiria kwa msaada kutoka Serikali ya watu wa China.

Aidha, uboreshaji wa mawasiliano ya simu ulifanywa kwa kutumia *Microwave* na *Optic Fibre.* Ili kukabiliana na upungufu wa injini za treni, pamoja na jitihada za kukarabati injini za zamani zinazoendelea kufanywa, Mamlaka ilichukua hatua ya kukodi injini 2 kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kila ilipobidi kufanya hivyo. Vile vile, *TAZARA* imekubaliana na Shirika la Reli la Kongo kuleta idadi ya mabehewa 150 ya mpango wa kubadilishana mabehewa ili kubeba shehena ya Kongo kutoka bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, lengo la Mamlaka ni kusafirisha mizigo ya tani 650,000 na abiria 1,000,000. Mamlaka inatarajia kuingiza jumla ya shilingi bilioni 38.0. Ongezeko hilo la mapato litatokana na Mamlaka kujiwekea mkakati wa makusudi wa kulenga kusafirisha shehena zinazokwenda na kutoka umbali mrefu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002, bado ajali katika njia za reli zinazomilikiwa na mashirika yote mawili, *TRC* na *TAZARA,* ziliendelea kuwa mojawapo ya kikwazo cha mafanikio. Katika kipindi hicho ajali 215 zilitokea katika Shirika la Reli Tanzania ikilinganishwa na ajali 237 zilizotokea mwaka 2001. Idadi hii ilikuwa ni pungufu kwa asilimia 9.3. Kupungua kwa ajali za treni katika Shirika hili kulitokana na uimarishaji wa matengenezo ya njia katika sehemu mbalimbali. Hata hivyo itakumbukwa kwamba tarehe 24, Juni, 2002 ilitokea ajali mbaya ya treni ya abiria iliyosababisha vifo

vya abiria 288 na majeruhi 400. Tahadhari zote zinaendelea kuchukuliwa na Shirika kuzuia matukio kama hayo kujirudia.

Mheshimiwa Spika, hadi robo ya tatu ya mwaka 2002/2003 ajali katika Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia zilifikia 143 ikilinganishwa na ajali 166 zilizotokea katika kipindi kama hicho mwaka 2001/2002, zikiwa ni pungufu kwa asilimia 13.9. Ajali hizi ziliigharimu Mamlaka shilingi milioni 478 ikilinganishwa na shilingi milioni 564.9 kwa kipindi kama hicho mwaka 2001/2002. Upungufu huo ni wa asilimia 15.4. Kiwango kikubwa cha ajali katika mamlaka kilisababishwa na ubovu wa njia hasa katika maeneo yenye mmomonyoko wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2002/2003, huduma za usafiri na uchukuzi kwa njia ya maji ziliendelea kuathiriwa na kuzorota. Hali ya uchumi na kisiasa katika nchi zinazotumia bandari zetu pamoja na uwezo mdogo wa vyombo vya usafirishaji wa nchi kavu ambao unaathiri uchukuzi wa bidhaa zinazopitia bandarini. Aidha kuongezeka kwa ushindani wa kibiashara katika bandari za ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika kumeendelea kuleta changamoto kubwa katika sekta hii. Pamoja na changamoto zilizojitokeza utendaji wa sekta kwa ujumla ulikuwa wa kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003 Mamlaka ya Bandari Tanzania iliendelea kutekeleza jukumu lake la kuendeleza na kuendesha bandari zetu. Hali ya utendaji kazi katika bandari kuu za mamlaka kwa miezi sita ya mwanzo ya kipindi cha 2002/2003 ilikuwa ya mafanikio. Kwa mwaka mzima wa 2002/2003, Mamlaka ilitarajia kuhudumia jumla ya tani 4,257,660 katika bandari zake kuu. Kitengo cha Kontena kinachoendeshwa na kampuni iitwayo *Tanzania International Container Terminal Services (TICTS),* kinatarajia kuhudumia makontena 146,200. Hadi kufikia Desemba 2002 shehena iliyohudumiwa na Mamlaka ilikuwa tani 2,338,800. Hii ni ongezeko la tani 211,300 au asilimia 9.0. Katika kipindi hicho *TICTS* walihudumia makontena 83,572 sawa na asilimia 57.2 ya lengo la mwaka mzima. Aidha utekelezaji wa viwango vya tija ukilinganishwa na malengo katika kipindi hicho ulikuwa wa kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, mamlaka iliendelea kutekeleza miradi ya maendeleo na ununuzi wa vifaa vya kufanyia kazi. Miradi hiyo ni pamoja na uboreshaji wa lango la Bandari, ujenzi wa eneo la kuhudumia makontena, ununuzi wa vifaa vya kuhudumia mizigo kwa bandari zote, upanuzi wa eneo la bandari ya Mtwara, ujenzi wa kituo cha kuongozea meli - Dar es Salaam na uboreshaji wa eneo la matishari katika Bandari ya Tanga.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mamlaka ya Bandari, Serikali imekubali pendekezo la kujenga gati, Kilindoni, Mafia kwa gharama ya shilingi bilioni 3.5. Tayari Mamlaka imetenga kiasi cha shilingi bilioni 1.96 kwa shughuli hiyo. Katika mwaka 2003/2004 Mamlaka itakamilisha usanifu na kuanza taratibu za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imeamua kuweka usimamizi na uendeshaji wa bandari na magati katika mwambao na maziwa makuu chini ya chombo kimoja. Uamuzi huu utasaidia sana uendelezaji wa

uchukuzi katika mwambao na maziwa makuu. Chombo hicho ni Mamlaka ya Bandari Tanzania.

Mheshimiwa Spika, utendaji kazi wa kitengo cha kontena katika bandari ya Dar es Salaam ambacho kilibinafsishwa septemba, 2000 kwa *TICTS* umekuwa wa mafanikio. Shehena imeongezeka na kiwango cha tija kimepanda. Kitengo hicho kimekuwa cha kwanza kwa ufanisi katika Afrika ya Mashariki na Kusini mwa Afrika. Kinahudumia kontena 20 kwa saa ukilinganisha na kontena 16 kwa saa bandari ya Durban na 10 kwa saa bandari ya Mombasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2002/2003, Mamlaka iliendelea kukabiliana na changamoto mbalimbali ili kuwezesha kufanikisha malengo ya utendaji. Changamoto hizo ni pamoja na kukubali hali mbaya ya uchumi na kisiasa katika nchi zinazotumia bandari za mamlaka na uwezo mdogo wa vyombo vya usafirishaji wa nchi kavu ambao unaathiri uchukuzi wa bidhaa zinazopitia bandarini. Aidha, kuongezeka kwa ushindani wa kibiashara katika bandari za ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika ni changamoto ambayo mamlaka na nchi tutaendelea kuikabili.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hizi, Mamlaka imeendelea kushirikiana na wadau wengine ikiwa ni pamoja na Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* *Tanzania International Container Terminal Services, TAZARA,* Shirika la Reli la Uganda *(URC),* Mamlaka ya Mapato Tanzania na Kampuni za Wakala *(Clearing and Forwarding Companies)* ili kuongeza ufanisi.

Aidha, Mamlaka ina mpango wa kushiriki katika kuanzisha maeneo huru *(EPZ)* ili kuchochea maendeleo ya shughuli zenye maslahi *(Value Added Activities)* sambamba na uanzishaji wa bandari nchi kavu ili kuzidi kuwavutia wateja *(Potential Customers)* pamoja na kupanua na kushikilia masoko.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha 2003/2004, Mamlaka imejiwekea lengo la kuhudumia jumla ya tani 4,345,560 kupitia katika bandari zake zote nchini. Ikilinganishwa na lengo la mwaka jana, lengo la mwaka huu ni zaidi kwa tani 148,330 au asilimia 3.7. Kitengo cha Kontena *(TICTS)* kimeweka lengo la kuhudumia makontena 168,985. Aidha, Mamlaka inatarajia kuingiza pato la shilingi bilioni 75.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Chinese Tanzanian Joint Shipping Company (SINOTASHIP)* inayomilikiwa na Serikali za China na Tanzania imeendelea na shughuli zake za kutoa huduma za uchukuzi wa shehena wa masafa marefu bandarini. Kampuni ya *SINOTASHIP* ina meli nne zenye uwezo wa kubeba tani 61,860 kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa 2002 meli za *SINOTASHIP* zilifanya safari 41 ikilinganishwa na safari 40 za mwaka uliotangulia. Shehena zilizosafirishwa katika safari hizo zilifikia tani 497,979 na hivyo kuiingizia kampuni mapato ya dola za Kimarekani milioni 9.25. Baada ya kutoa gharama za uendeshaji kampuni ilipata faida ya dola

198,911. Kampuni ilikabiliwa na ushindani mkali ndani ya soko la shehena na ulimwenguni kote ambao ulifanya mizigo kuwa adimu na nauli zake kuwa za chini mno.

Kupanda kwa gharama za endeshaji hususani bei za mafuta na vipuri pamoja na hali mbaya ya uchumi katika nchi za Afrika Mashariki na kati ambazo ni chanzo kikubwa cha shehena na tegemeo la biashara ya kampuni ni baadhi ya changamoto zilizoikabili kampuni.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hali halisi ndani ya soko la shehena, kampuni imedhamiria kutekeleza mkakati wa kuongeza kwa kiwango kikubwa jitihada za kutafuta aina za shehena zinazotozwa nauli kubwa hivyo kujiongezea mapato na faida. Eneo jingine lililolengwa na kampuni ni kupunguza matumizi kwa kuongeza tija katika upakuaji wa mizigo melini na pia kusimamia kwa makini gharama za matengenezo ya meli. Hivyo katika mwaka 2003, kufuatia kuuzwa kwa meli yake moja mwishoni mwa mwaka jana na kubaki na meli tatu, kampuni imepanga kufanya safari 23 na kusafirisha shehena za tani 250,000.

Mheshimiwa Spika, msingi muhimu wa mafanikio ya *SINOTASHIP* mwaka hadi mwaka unatokana na kampuni kuzingatia kikamilifu kanuni na taratibu za Kimataifa za usalama wa meli na shehena. Tangu mwaka wa 2000, kampuni imekuwa ikitekeleza kanuni za *International Ship Management (ISM) Code* na imetunukiwa hati maalum iitwayo *Document of Compliance* iliyotolewa na *China Marine Safety Administration (CMSA).*

Aidha, kila meli ya Kampuni imekaguliwa na baada ya kupasishwa, imepewa hati ya *Safety Management Certificate (SMC).* Ukaguzi hufanywa na *CMSA* kila mwaka kuhuisha hati ya kampuni na kila miaka miwili na nusu kuhuisha *SMC* ya kila meli. Kanuni na taratibu hizi zinahusu menejimenti ya usalama wa meli na kampuni kwa ujumla. Kuhusu hali ya meli zenyewe ki-mitambo na uwezo wake kusafiri baharini *(Seaworthiness)* bado ukaguzi wa kila mwaka *(Annual Survey)* hufanywa na *Lloyds Register of Shipping* au *China Classification Society (CCS)* na hati zote zinazotakiwa hutolewa kwa kila meli ya kampuni.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2000 Sheria Na. 3 ya mwaka 1981 iliyoanzisha Shirika la Kudhibiti Shehena ilifanyiwa marekebisho na kulipa Shirika jukumu la kusimamia mwenendo wa soko huria la usafirishaji kwa njia ya maji. Hivyo mwaka 2002/2003, ulikuwa ni mwaka wa pili tangu shirika lianze kutekeleza majukumu hayo mapya.

Katika kipindi hicho, Shirika liliendelea na uratibu, usimamizi na udhibiti wa gharama na mwenendo wa masoko huria ya usafirishaji majini pia kuweka mazingira mazuri ya kuwavutia wafanyabiashara ya usafirishaji wa majini ikiwa ni pamoja na kufuatilia kwa karibu taratibu na uharaka wa uondoaji shehena kutoka bandari zetu za Zanzibar na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Bandari ya Dar es Salaam, Shirika lilibaini kwamba ufanisi katika uondoaji wa shehena kutoka bandarini umepunga na kufanya kiwango cha utendaji kushuka. Shirika lilifanya mkutano wa wadau na kukubaliana kuzingatia kiwango cha kuondoa mizigo bandarini cha siku tano. Kwa upande wa Zanzibar makampuni ya meli yanayofanya safari kati ya Zanzibar na bandari nyingine duniani yamekuwa yakiongezeka. Mwaka 1998 yalikuwa makampuni 3 na yamefikia 8 mwaka huu. Aidha, kuja kwa meli za makampuni hayo kunategemea upatikanaji wa shehena inayokuja na kutoka Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, mapato ya Shirika yanatarajiwa kuwa shilingi bilioni 1.931 ikilinganishwana shilingi bilioni 1.763 zilizopatikana mwaka 2001/2002. Faida kabla ya kodi kwa mwaka 2002/2003, inatarajiwa kuwa shilingi 478.383 ikilinganishwa na shilingi milioni 486.749 mwaka uliotangulia. Mapato kwa mwaka 2003/2004 yanatarajiwa kuwa shilingi bilioni 2.083. Aidha, baada ya kuundwa kwa *SUMATRA* shughuli za udhibiti zinazofanywa na Shirika hili zitahamishwiwa katika chombo hiki kipya.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa mwambao hususan kati ya Dar es Salaam na Mtwara umeimarika kwa kiwango kikubwa tangu ilipowasili meli kubwa na ya kisasa ya *F.B. SANTORINI 3* tarehe 17 Julai, 2002. Meli hii aina ya *Roll On Roll Out (RORO),* ina uwezo wa kubeba abiria 1255 na tani 3427 za mizigo kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, meli hii ilipowasili ilikabiliwa na tatizo la mahali pa kuegesha. Baada ya majadiliano na Mamlaka ya Mandari Tanzania *(THA)* makubaliano yamefikiwa kuwa meli hii itakuwa ikiegeshwa gati namba moja Dar es Salaam. Matatizo mengine yameendelea kushughulikiwa kati ya Wizara yangu, wenye meli na vyombo vingine. Kwa kiwango kikubwa yamepatiwa ufumbuzi na meli inaendelea na ratiba zake kama kawaida. Hata hivyo ili meli hii iweze kuendelea kutoa huduma, itahitaji ipate shehena ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, tangu meli iingie nchini mwezi Julai, 2002 hadi sasa imeweza kusafirisha mizigo tani 21,902 na abiria 45,226 kati ya Dar es Salaam - Mtwara na Dar es Salaam. Serikali imeamua kutekeleza sera yake ya kufikisha huduma katika maeneo ambayo kwa kawaida na kibiashara, yasingeweza kufikika, hasa na sekta binafsi *(Public Service Obligation - PSO).* Tumetumia dhana ya *PSO* kuiwezesha *F.B. Santorini 3* na meli nyingine ziendelee kuhudumia Mikoa ya kusini.

Mheshimiwa Spika, kampuni inayotoa huduma za usafiri katika Maziwa, *Marine Services Company Limited (MSCL)* imeendelea kutoa huduma za uchukuzi katika Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa. Aidha, wamiliki binafsi wa vyombo vya majini wameendelea kushiriki katika kutoa huduma ya uchukuzi kwenye Maziwa yetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea na mpango wake wa kuendeleza magati baharini na kwenye maziwa. Lengo ni kuimarisha usalama wa vyombo vya majini katika maeneo hayo na kuwawezesha wananchi wa maeneo hayo kuwa na huduma za kuaminika. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika kipindi cha mwaka

2002/2003, Serikali imetoa jumla ya shilingi milioni 120 kwa mradi wa ukarabati wa magati ambao uliendelea kutekelezwa chini ya usimamizi wa kampuni ya huduma za meli. Magati yaliyohusika ni pamoja na Bukondo, Shirati na Kinesi ambayo yote yako katika Ziwa Victoria. Kazi ya ukarabati wa gati la Bukondo imekamilika kwa asilimia 75. Kuhusu gati la Kinesi, kazi imeanza Mei 2003 na tayari mawe na mbao zimepelekwa kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Serikali ina mpango wa kukamilisha ujenzi wa magati ya Kinesi, Bukondo na Shirati na pia kuanza ukarabati wa gati ya Nansio (Ukerewe), gati ya Kasanga katika ziwa Tanganyika na maandalizi ya ujenzi wa gati ya *Mbamba Bay,* katika Ziwa Nyasa na gati ya Mafia. Jumla ya shilingi milioni 250 zimetengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002 kampuni inayotoa huduma za usafiri katika Maziwa Makuu *Marine Services Company Limited* iliendelea kutoa huduma za uchukuzi wa mizigo na abiria katika Ziwa la Victoria, Tanganyika na Nyasa.

Katika kipindi hicho, kampuni iliweka lengo la kusafirisha tani 150,431 za mizigo na abira 402,204. Jumla ya tani 141,022 zilisafirishwa na abiria 363,981 zilizosafirishwa mwaka 2001 na abiria 362,575. Malengo ya kampuni hayakufikiwa kwa asilimia 6 kwa upande wa mizigo na asilimia 10 kwa upande wa abiria. Aidha, kwa upande wa mapato kampuni ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 4.014 ikilinganishwa na shilingi bilioni 4.518 zilizokusanywa mwaka 2001. Lengo lilikuwa ni kukusanya shilingi bilioni 4.237, hivyo halikufikiwa kwa asilimia 5.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003 Wizara iliendelea kusimamia usalama wa vyombo vya majini abiria na mizigo yao. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wenye vyombo vya abiria na mizigo wanaozingatia maelekezo ya Serikali kuhusu usalama wa safari za vyombo baharini na katika maziwa yote.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuchukua fursa hii kuwakumbusha wenye vyombo wote kufuata sheria na taratibu zote za usalama vya vyombo vyao. Pia ni muhimu kuhakikisha kuwa vyombo hivyo vinakaguliwa katika muda unaotakiwa na wana vifaa vya kutosha vya usalama na kuzingatia umuhimu wa kutoa mafunzo kwa abiria jinsi ya kutumia vifaa hivyo kila wanapobeba abiria katika vyombo vyao. Wizara yangu inaendelea na maandalizi ya kuanzisha mamlaka ya kusimamia usalama wa vyombo vya majini.

Aidha, Wizara itaendelea kuwatumia wakaguzi usalama wa vyombo ambao watafanya kazi hii hadi hapo itakapoundwa Mamlaka ya usimamizi wa jukumu hili. Serikali inaendelea na juhudi za kuhamasisha na kuweka mazingira mazuri kwa sekta binafsi kuendelea kutoa huduma hii ya usafiri kwa njia ya maji.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kuweka usimamizi na uendelezaji wa Bandari na magati katika mwambao na Maziwa Makuu chini ya Mamlaka moja na

mamlaka hiyo ni Mamlaka ya Bandari Tanzania. Uamuzi huu utasaidia sana uendelezaji wa uchukuzi katika mwambao na Maziwa Makuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa usafiri wa majini unahitaji kufuatwa kwa kanuni na sheria, Wizara yangu imeandali mapendekezo ya marekebisho ya sheria mama inayosimamia usafiri majini. Aidha, marekebisho hayo yanalenga kuboresha usalama wa safari za meli, uhifadhi wa mazingira na taratibu za kiusalama bandarini na ndani ya meli.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002 kipindi kama hiki nililifahamisha Bunge lako Tukufu kuhusu maendeleo yanayoweza kupatika kwa kuangalia usafiri katika Kanda *(corridors)* hususan usafiri na uchukuzi katika ukanda wa Magharibi *(Western Transport Corridor)* unaounganisha Mikoa ya Mbeya, Rukwa, Kigoma, Kagera, Mwanza na Shinyanga.

Aidha, Kanda hii inaungana na ile ya Mtwara ambayo hujulikana kama *Mtwara Corridor* ambayo hujumuisha Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Mbeya, Rukwa na Iringa. Kama Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi alivyoliarifu Bunge lako Tukufu Meneja wa Kuratibu Miradi ya *Mtwara Corridor* ameshateuliwa na tayari ameshaanza kazi. Kuteuliwa kwa Meneja huyu kutasaidia kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ambayo ilikuwa bado haijaanza kutelekezwa. Taratibu za kuteua Mameneja wa kanda nyingine zinaendelea. Wizara ina imani utaratibu huu ni moja ya njia zitakazotumika kutatua matatizo ya usafiri katika maeneo ambayo hivi sasa hayafikiki kirahisi.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa anga duniani bado umeathirika kutokana na shambulio la kigaidi lililofanywa mwezi Septemba, 2001 huko Marekani na vitisho vya kigaidi vya mara kwa mara. Itachukua muda kurejesha mwelekeo wa kukua kwa sekta. Masharika mengi duniani yamefilisika au yamepunguza huduma.

Hata hivyo Tanzania imeendelea kuonyesha ukuaji katika safari za nje ya nchi hasa kutokana na hatua ya mashirika yetu ya *Air Tanzania Company Limited* na *Precision Air Services* kuongeza safari za ndani na nje ya nchi. Aidha, leseni mpya 27 za makampuni ya ndege zilitolewa. Jumla ya leseni zilizotolewa mpaka sasa ni 61.

Mheshimiwa Spika, huduma za usalama wa usafiri wa anga katika kipindi cha 2002/2003 ziliendelea kutolewa katika kiwango cha kuridhisha. Hata hivyo idadi ya abiria waliosafiri ndani na nje ya nchi iliongezeka kutoka abiria 1,263,594 mwaka 2001/2002 hadi kufikia abiria 1,497,996 mwaka 2002/2003 ambalo ni ongezeko la asilimia 18.6.

Aidha, idadi ya abiria waliosafiri ndani na nje ya nchi kupitia kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Dar es Salaam iliongezeka kutoka abiria 612,352 mwaka 2001/2002 hadi kufikia abiria 707,997 mwaka 2002/2003. Hii ni ongezeko la asilimia 15.5 vile vile idadi ya abiria waliosafiri humu nchini katika kipindi cha mwaka 2002/2003 iliongezeka kwa asilimia 19.8 Safari za ndege za Kimataifa kupitia viwanja vyetu ziliongezeka kwa asilimia 3.7 kutoka ndege 19,612 mwaka 2001/2002 hadi kufikia ndege 20,314 mwaka 2002/2003.

Katika kipindi cha mwaka 2002/2003 idadi ya makampuni yaliyopewa leseni ni 27 ikilinganishwa na makampuni 28 yamwaka 2001/2002. Aidha, safari za ndege za Kimataifa na za ndani ziliongezeka kutoka ndege 130,209 mwaka 2001/2002 hadi kufikia 136,975 mwaka 2002/2003 sawa na ongezeko la asilimia 5.2.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002 katika kikao kama hiki nililieleza Bunge lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa miradi ambayo sasa utekelezaji wake umekamilika. Miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Huduma za Usafiri wa Anga *(Air Traffic Service*s). Mradi huu umejumuisha ubadilishaji wa mitambo yote michakavu na ufungaji wa mitambo mipya inayotumia teknolijia ya kisasa kwa ajili ya kutoa huduma za uongozaji ndege katika kituo kikuu kilichopo uwanja wa Dar es Salaam. Mradi huu umegharimu *Euro* milioni 4.65 ukiwa ni mkopo nafuu kutoka Benki ya mitaji ya nchi za Ulaya *(European Investment Bank).* Aidha, mamlaka ilipokea msaada wa vifaa vya kuimarisha usalama vilivyogharimu Dola za Kimarekani milioni 2.0 kutoka Serikali ya Marekani. Vifaa hivi tayari vimekwishafungwa katika viwanja vyetu vya Kimataifa vya Dar es Salaam, Kilimanjaro na Zanzibar na vinafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, aidha, mradi wa ufungaji Rada mpya katika kiwanja cha Kimataifa cha Dar es Salaam ulikamilika mwezi wa Desemba, 2002. Hata hivyo kutokana na matatizo ya umeme, ilibidi mtambo uzimwe hadi mwezi wa Februari 2003 ili kifaa cha kudhibiti umeme kilichogharimu shilingi milioni 54 kinunuliwe na kufungwa. Kifaa hicho sasa kimefungwa na Rada inafanya kazi tangu mwezi Aprili, 2003 baada ya mafunzo ya wataalam kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi itakayoendelea kutekelezwa katika kipindi cha 2003/2004 ni pamoja na mradi wa kituo cha udhibiti wa kuongoza ndege katika anga la eneo la nchi za *SADC (SADC Upper Air Space Control Centre).* Mradi huu bado unaendelea kufanyiwa upenguzi yakinifu kabla ya kutolewa maamuzi ya kuanza utekelezaji wake. Ripoti ya utafiti iliwasilishwa katika Baraza la Mawaziri wa nchi ya *SADC* na kuonekana kuwa bado unahitaji utafiti zaidi kabla ya kutoa maamuzi ya kuanzishwa kwa kituo hicho. Serikali ya Marekani tayari imetoa dola za Kimarekani laki 6 kwa ajili ya kuendeleza utafiti huo.

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine unaotarajiwa kutekelezwa na Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga katika kipindi cha 2003/2004 ni ule wa kuanzishwa kwa kituo cha pamoja cha kuongozea ndege, utafutaji wa ndege zilizopata ajali *(search and rescue co-ordination services)* ramani *(AIS MAP facilities and services)* na matumizi ya pamoja ya vyuo vya mafunzo katika eneo la Afrika Mashariki *(East Africa Civil Aviation Safety Project).*

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ni pamoja na ununuzi na ufungaji wa meza za kisasa kwa waongoza ndege *(ATC Consoles)* na vifaa vya redio na mawasiliano katika uongozaji wa ndege katika viwanja vya Mwanza, Arusha na Zanzibar. Katika mwaka 2003/2004 mamlaka itanunua jenerata za umeme za akiba kwa viwanja vya Zanzibar na Mtwara na itafunga mitambo ya nguvu ya miozi ya jua katika kiwanja cha Songea.

Mamlaka itanunua na kufunga mtambo wa usambazaji wa mawimbi ya redio Mkoani Ruvuna utakaogharimu shilingi milioni 86 ili kusaidiana na mtambo ulioko Mtwara katika Ukanda wa Kusini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za kuboresha na kuweka mitambo mipya ya usalama na uongozaji wa ndege, Wizara inatekeleza awamu ya kwanza ya kukibadilisha chuo chetu cha Anga *(Civil Aviation Training Centre)* kilichopo Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Dar es Salaam kuwa Wakala wa Serikali *(Executive Agency).* Lengo ni kuinua kiwango cha ufundishaji na kuongeza ufanisi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003 Mamlaka ya Viwanja wa Ndege Tanzania iliendelea kuhudumia viwanja vya ndege kuzingatia sera na mwelekeo wa sasa wa kuwezesha viwanja vya ndege vinavyoweza vijiendeshe kibiashara ili kujitosheleza na kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania iliendelea na matengenezo madogo madogo ya viwanja ili kuwezesha ndege kutua na kuruka kwa usalama. Matengenezo makubwa ya miundombini na uboreshaji wa mitambo ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Dar es Salaam na viwanja vingine. Mamlaka ilikamilisha kujenga sehemu ya uzio wa ukuta wa matofali iliyokuwa imesalia yenye urefu wa kilometa 2. Kukamilika kwa ukuta huo kumeongeza usalama katika kiwanja hicho na hivyo kupunguza malalamiko kutoka Mashirika ya ndege hasa ikichukuliwa usalama thabiti unaotakiwa kutokana na vitendo vya ugaidi.

Mheshimiwa Spika, matengenezo mengine yaliyofanywa kwenye kiwanda cha Kimataifa cha Dar es Salaam ni katika barabara ya kuruka na kutua ndege pamoja na viungio vyake na sehemu za maegesho na vivuko vine vya abiria kutoka kwenye ndege hadi jengoni. Vile vile, Mamlaka inaendelea na ukarabati mkubwa wa mitambo ya viyoyozi pamoja na umeme *(Power supply).* Mamlaka imenunua mashine za ukaguzi wa mizigo *(X- rays)* na vifaa vingine vya usalama. Taratibu zinafanywa za ununuzi na usimikaji wa mitambo ya uhakiki wa mizigo ya abiria ili kwenda sambamba na mifumo ya kisasa iliyopo kwenye viwanja vingine vya Kimataifa.

Mamlaka iliendelea na ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza ambao ulihusu uwekaji taa kwenye barabara za kurukia na kutua ndege na kuelekea kwenye maegesho ya ndege kwa ajili ya usalama wa ndege wakati wa usiku. Mamlaka ilikamilisha usanifu wa jengo jipya la abiria na mizigo pamoja na *Hanger* ya kufanyia matengenezo ya ndege.

Mheshimiwa Spika, Kiwanja cha Ndege cha Arusha kilifungwa taa kwenye maegesho. Zinasaidia kuongeza usalama wa ndege zinazoegeshwa hapo kiwanjani wakati wa usiku. Ujenzi wa ukuta kuzunguka uwanja kwa ajili ya kuimarisha usalama umeanza Aprili, 2003. Matengenezo mengine kwenye kiwanja hicho yamehusu ukarabati na uimarishaji wa njia ya kurukia na kutua ndege. Mamlaka pia imekamilisha usanifu mkubwa wa mpango wa Kiwanda cha Arusha *(Master Plan).* Mazungumzo

yanaendelea kati ya Wizara yangu na Wizara ya Kilimo na Chakula na Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu upatikanaji wa eneo kubwa zaidi kwa ajili ya uwanja wa ndege wa Arusha.

Mheshimiwa Spika, kazi mbalimbali zilifanywa kukiendeleza kiwanja cha Mtwara. Kazi hizi zilihusu matayarisho ya ramani *(Master Plan)* ya usanifu wa Jengo la kuongozea ndege na ukumbi wa watu mashuhurri, usanifu wa ukumbi wa kuondokea abiria na kuendelea na matengenezo ya njia ya kurukia na kutua ndege.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kiwanja kipya cha Ndege Mbeya (Songwe) umeendelea vizuri. Karibu wote waliokuwa kwenye eneo la kiwanja wamefidiwa nyumba pamoja na mashamba yao. Kazi ya kusawazisha eneo la kiwanja imekamilika. Ujenzi wa jengo la abiria unaendelea. Mwaka 2002/2003, Serikali imetenga shilingi bilioni moja kwa kazi hizo, hiki ni kiwanja cha kwanza ambacho Mamlaka itakijenga yenyewe.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003 matengenezo yalifanywa kwenye viwanja vya ndege vya Musoma, Tabora, Sumbawanga, Bukoba, Lake Manyara, Shinyanga na Dodoma. Aidha, katika kuimarisha usalama wa viwanja vyetu, juhudi zinaendelea za kuinua viwango vya usalama hasa katika viwanja vya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Arusha, Mtwara, Mwanza na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, hatua zinazochukuliwa ni pamoja na ununuzi wa mitambo ya kutambua mabomu, ununuzi wa mitambo ya ukaguzi wa mizigo, ujenzi wa uzio kuzunguka viwanja, ununuzi wa milango maalum ya kupitia abiria na mashine maalumu za mkono za kutambua vyuma. Aidha, mtambo maalumu wa kuona kwa njia ya *Television* utawekwa katika kiwanja cha Dar es Salaam. Magari na pikipiki za doria zitanunuliwa kwa ajili ya viwanja hivyo. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege pia itaimarisha huduma za Zimamoto kwa kununua magari ya Zimamoto na vipuri vyake.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004 Mamlaka imepanga kutekeleza mpango wake wa maendeleo kwa kuendeleza Kiwanja cha Ndege cha Songwe kwa kusimamia ujenzi wa jengo la abiria, kuanza kujenga barabara ya kutua na kuondokea ndege pamoja na viungio na maegesho yake.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004 Mamlaka itaendelea kufanya matengenezo ya barabara ya kurukia na kutua ndege na ujenzi wa uzio kwa ajili ya usalama wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara na upanuzi wa ukumbi wa watu mashuhuri na magari ya Zimamoto. Kiwanda cha Ndege cha Mwanza kitafanyiwa ukarabati kwenye sehemu za maegesho kwa ajili ya ndege za mizigo na viungio vyake pamoja na sehemu ya kugeuzia ndege. Aidha, ujenzi wa jengo la abiria na uzio utaanza katika mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka itaendelea kutoa huduma za matengenezo na uendeshaji wa viwanja vya ndege vilivyobaki kulingana na upatikanaji wa fedha. Huduma za matengenezo zitaelekezwa zaidi kwenye viwanja vya Tabora, Kigoma, Musoma, Singida, Mafia, Bukoba, Dodoma, Mbeya, Ziwa Manyara, Mafia, Shinyanga,

na Sumbawanga. Aidha, Mamlaka itajenga vituo vidogo vya abiria na huduma katika viwanja vya ndege vya Biharamulo (Katoke) na Mpanda.

Mheshimiwa Spika, kati ya Julai, na Desemba, mwaka 2002, Shirika la Ndege Tanzania *(ATC)* lilikuwa kwenye hatua za kubinafsishwa. Shirika liliendelea kutoa huduma za usafiri wa anga. Katika kipindi hicho Shirika liliweza kusafirisha jumla ya abiria 67,340 katika safari za ndani ya nchi na abiria 67,130 katika safari za nje. Mizigo iliyobebwa kwa safari za ndani ni tani 1,507 na kwa safari za nje ni tani 726.

Aidha, katika kipindi hiki Shirika lilikabiliwa na matatizo ya kibiashara na kiuendeshaji ambayo yalilisababishia Shirika kufanya kazi kwa hasara. Matatizo hayo yalikuwa ni pamoja na mtaji mdogo, madeni mengi yaliyosababishwa na gharama kubwa za uendeshaji na ndege za zamani. Hata hivyo, baada ya kumpata mwekezaji na kulibadilisha Shirika kuwa Kampuni, hali ya utendaji imeanza kuimarika na hatimaye kuongeza masoko ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Wakala wa Ndege za Serikali ulianzishwa na uliendelea kutoa huduma zake za kuwasafirisha viongozi wa Serikali pamoja na kutoa huduma za kibiashara pale ilipowezekana. Katika kutekeleza majukumu yake Wakala uliendelea kukabiliwa na changamoto ya kutoa huduma pamoja na uhaba wa ndege. Katika jitihada za kuboresha huduma zake, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wakala unatarajia kupata ndege mpya inayokwenda masafa marefu na hivyo kuongeza idadi ya ndege zake kufikia nne. Uwezo wa kwenda masafa marefu wa ndege hiyo mpya utaongeza biashara na mapato kwa kuwa safari nyingi za aina hiyo zilikuwa hazifanywi na Wakala. Kupatikana kwa ndege hiyo pia kutaongeza kwa kiwango kikubwa usalama wa usafiri wa viongozi wa juu na kupunguza bugudha wanazozipata hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kukuza biashara na mapato, Wakala wa Ndege za Serikali ulijitangaza kibiashara katika majarida mbalimbali. Jambo hili liliongeza biashara na kudhihirisha kwamba kuna haja ya Wakala kuwa na ndege za kutosha ili kuweza kukidhi mahitaji ya usafiri wa viongozi na mahitaji ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, huduma za mawasiliano ziliendelea kupanuka hasa kutokana na kuongezeka kwa wawekezaji katika sekta hii nchini. Aidha, sekta hii inajumuisha huduma za simu za msingi na zile zisizo za msingi pamoja na huduma za mawasiliano kwa njia ya posta. Tume ya Mawasiliano Tanzania *(TCC)* imeendelea kusimamia shughuli za mawasiliano nchini kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, ili kujiimarisha kiutendaji, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Tume ya Mawasiliano ilianza ujenzi wa Kituo ambacho kitafungwa mtambo wa kisasa wa kufuatilia matumizi ya masafa yanayotolewa kwa ajili ya matumizi ya mawasiliano ya simu na redio *(Fixed frequency monitoring equipment).* Ujenzi huo unatarajiwa kukamilika na kituo kuanza kufanya kazi ifikapo Desemba, 2003. Kituo hicho kitasaidiana na mtambo mwingine uliofungwa kwenye gari *(mobile*

*frequency monitoring unit)* na ambao unatumika hivi sasa katika kufuatilia matumizi ya masafa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa pamoja, mitambo hiyo itasaidia kutatua tatizo la maingiliano ya masafa na hivyo kuleta ufanisi katika matumizi ya masafa. Vile vile mitambo hiyo inao uwezo wa kuwatambua watumiaji ambao hawana leseni.

Mheshimiwa Spika, katika utoaji wa leseni, Tume ilitoa leseni 18 za makandarasi wa kufunga na ukarabati mitambo ya redio na simu na kufanya idadi yao kuwa 59. Leseni 2 za watoa huduma za *Internet* zilitolewa na kufanya idadi yao kuwa 21. Leseni 2 za wasambazaji takwimu *(Public Data Communication)* zilitolewa na kufanya idadi yao kuwa 11. Leseni 6 za Takwimu kwa matumizi ya ndani *(Closed User Group)* zilitolewa na kufanya idadi yao kuwa 9. Mamlaka ilitoa leseni 3 za huduma za Posta kwenye huduma ya uchumuzi wa vifurushi *(Courier Services)* na kufanya idadi kuwa 15.

Aidha, katika kufuatilia utekelezaji wa masharti ya leseni na sheria za Tume ya Mawasiliano, ukaguzi ulifanyika nchi nzima na makampuni 42 yasiyokuwa na leseni halali kufanya shughuli za mawasiliano yaligundulika na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, mwezi Januari, 2003, Tume ilifuata leseni ya Kampuni ya Simu za Mkononi ya *Tritel* kwa kushindwa kutimiza masharti ya leseni yake. Hatua za kisheria za kufilisi kampuni hiyo zimechukuliwa.

Mheshimiwa Spika, Tume ilifanya ukaguzi wa mitandao yote ya makampuni ya simu za mkononi nchini. Ukaguzi huo uliweza kubaini kuwa gharama za usambazaji wa huduma hizo zinatofautiana. Hiki ndicho chanzo cha tofauti katika kulipia gharama za simu za mkononi. Hata hivyo, kwa kudhibiti hali hii, Tume iliweka kiwango cha juu ambacho kampuni moja inaweza kuilipa kampuni nyingine.

Mheshimiwa Spika, ili kujua gharama za kulipia simu kutoka mtandao wa kampuni moja kwenda kampuni nyingine, Tume imeamua kushirikiana na Kampuni iitwayo *ANALYSIS* ya Uingereza kufanya utafiti wa kujua gharama halisi za kuunganisha mawasiliano ya simu *(interconnection rates).* Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2003.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2003/2004, Tume inatarajia kupokea na kushughulikia maombi ya leseni za huduma ya posta, simu na utangazaji.

Aidha, Tume itahakikisha kwamba nchi yetu inapokea na kutumia teknolojia mpya ya mawasiliano, kupata nguvu kazi na vitendea kazi vya kutosha ili kuweza kudhibiti sekta hii ambayo ina ushindani mkubwa wa kibiashara na teknolojia. Vile vile, Tume itahakikisha kuwa huduma za mawasiliano zinasambaa nchini kote katika kiwango kinachotakiwa na gharama nafuu. Tume itaandaa mpango kabambe wa masafa yote ambayo yanatarajiwa kutumika Kitaifa na Kimataifa na kusimamia utayarishaji wa Anuani za Posta Kitafa *(National Address System)* ili kuboresha utambulisho wa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Tume itajihusisha katika maandalizi ya kuunganisha udhibiti wa mawasiliano na utangazaji na kuanzisha chombo kipya cha udhibiti.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002 Kampuni ya Simu Tanzania ilifanikiwa kujenga mitambo mipya ya kuuganisha mawasiliano ya simu *(Digital Exchanges)* katika maeneo ya Maswa (njia 1500), Bariadi (512), Meatu (512), Lalago, Chunya (512) na Ileje (512). Aidha, upanuzi wa mitambo iliyopo ulifanyika *Oysterbay* (njia 1,032), *Nyerere Road* (1,584), Wageni (1,304), Mwanza (440), Dodoma (1021), Moshi (596) na Tanga (852). Jumla ya njia mpya 9,927 zimeongezwa kwenye mtandao na njia 8,000 zimebadilishwa kutoka *Analogue* kuwa *Digital.*

Mheshimiwa Spika, miradi mingine iliyotekelezwa ni pamoja na kuboresha mtambo wa kurusha mawasiliano ya simu *(Transmission System)* kwenye njia ya mawasiliano ya Dar es Salaam - Lindi - Mtwara. Mtambo huu ambao ni wa teknolojia ya *digital* umeboresha huduma za mawasiliano ya simu mkononi Lindi na umeiwezesha *TTCL* kukodisha njia zake kwa kampuni za Simu za Mkononi katika Mikoa ya Mtwara na Lindi. Njia za mawasiliano za Dar es Salaam - Bukoba na Dar es Salaam- Kigoma zimeboreshwa kwa kutumia teknolojia ya *V-SAT.*

Mradi huu umeiwezesha *TTCL* kukodisha njia zake za simu kwa kampuni za simu za mkononi ili itoe huduma zao katika mji ya Bukoba na Kigoma. Pia mradi huu imewezesha kuwa na njia nyingine mbadala *(direct alternative link)* inayounganisha miji hiyo na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, njia ya mawasiliano katika Wilaya za Shinyanga, Maswa, Meatu na Bariadi imeboreshwa kwa kuweka mitambo inayojiendesha yenyewe *(Automation and Digitalizatio).* Uboreshaji huu umefanyika pia kwa mji mdogo wa Lalago. Miradi mingine iliyotekelezwa ni kuunganisha njia ya mawasiliano kwa miji ya Songea na Mbinga, kufunga mitambo ya digital kwenye njia ya mawasiliano ya Makambako - Ilembula, kuhamisha mitambo *(Re-deployment)* iliyokuwa iantumika kati ya Arusha na Ngorongoro, kwenda kuhudumia njia kati ya Ileje na Mbeya. Aidha, mtambo mwingine uliokuwa unatoa huduma kati ya Kurasini na katikati ya Dar es Salaam ulihamishwa ili utoe huduma kati ya Kiwanja cha Ndege cha Dar es Salaam na katikati ya mji.

Mheshimwia Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Kampuni ya Simu *(TTCL)* imepanga kutumia shilingi bilioni 17 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kuboresha mtandao na ubora wa huduma za kampuni hiyo. Miradi iliypangwa kutekelezwa ni pamoja na kuanzisha mtandao wa kisasa wa *Intelligent Network Platform (IN)* ili kuwezesha kuwapo mfumo wa kulipia kwanza kabla ya kutumia huduma.

Aidha, *TTCL* itafanya upanuzi wa huduma kufikia maeneo muhimu ya uchumi yakijumuisha migodi ya dhahabu ya Kahama na Buhemba, Kiwanda cha Saruji Tanga,

Kiwanda cha Sukari Kagera,mashamba ya Chai ya Kibena na Mfundi, eneo la Hoteli za Kitalii Bagamoyo na Pwani ya Mashariki Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine iliyopangwa kutekelezwa ni ya kubadilisha mitambo ya zamani ya aina ya analogue ambayo ina zaidi ya miaka 20 sasa na kuweka mitambo ya kisasa ya *digital* kwa njia za Mbeya - Kaluwe - Sumbawanga, Nyololo - Songea, Mwanza - Geita-Bukoba, Njombe - Makete, Njombe - Ludewa, Kaluwe - Tunduma, Kaluwe - Mbozi, Kaluwe - Ileje, Sumbawanga - Namanyere.

Kampuni itaweka mitambo mipya ya kurusha mawasiliano Igunga, Nzega, Isaka na Babati. Kampuni itaondoa mitambo ya zamani ya simu ili kuboresha huduma za mawasiliano katika miji ya Bukoba, Kigoma, Singida na Mtwara. *TTCL* itabadilisha mitambo ya zamani aina ya analogue ya Karanga (Moshi) na Miji ya Tabora na Mwanza na kuweka ya kisasa aina ya *digital.*

Kampuni itaondoa mitambo ya zamani ya kukoroga *Magneto Switches* ya Mafia, Tunduma, Kibosho, Kondoa na Namanyere na kuweka mitambo inayojiendesha yenyewe. Mitambo inayohusu awamu hii ya utekelezaji tayari imeshaagizwa. Katika mpango huu ambao fedha zake zimeidhinishwa, *TTCL* itabadilisha mitambo yote ya kizamani ya analogue kuwa *digital.*

Mheshimiwa Spika, inatazamiwa kuwa mafanikio ya utekelezaji wa miradi hii yataboresha kwa kiasi kikubwa ubora wa mtandao na huduma za simu pote nchini. Hii itaifanya *TTCL* iweze kujizatiti katika nafasi yake ya kuwa uti wa mgongo wa mawasiliano ya simu nchini na hivyo kutoa mchango unaostahili katika jitihada za Taifa za kuboresha uchumi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kampuni za simu za mkononi zimeendelea kupanua mitandao yao ya simu katika sehemu mbalimbali nchini. Makampuni hayo ni *Vodacom, Celtel, Mobitel* na *Zantel.*

Mheshimiwa Spika, kampuni ya *Vodacom* imepanua mtandao wao kufikia Mikoa yote ya Tanzania na Wilaya 75 ambazo ni Dar es Salaam: Jiji la Dar es Saalam, Pwani: Bagamoyo, Kibaha na Chalinze; Zanzibar na Pemba; Tanga: Tanga Mjini, Segera na Korogwe; Morogoro Mjini; Dodoma Mjini, Singida Mjini, Arusha Mjini, Monduli, Makuyuni, Ngorongoro na Namanga; Kilimanjaro: Moshi Mjini, Rombo, Marangu, Mwanga na *Kilimanjaro Airport;* Manyara: Ngorongoro: Mara: Musoma Mjini; Mwanza: Mwanza Mjini, Magu, Misungwi, Sengerema na Geita; Kagera: Bukoba Mjini, Muleba na Karagwe; Shinyanga: Shinyanga Mjini, Mwadui, Isaka na Kahama; Tabora: Tabora Mjini na Nzega; Kigoma: Kigoma Mjini; Rukwa: Sumbawanga; Lindi Mjini na Mtwara Mjini; Ruvuma: Songea Mjini, Mbeya: Mbeya Mjini, Mbalizi, Vwawa, Tunduma, Uyole, Igurusi, Tukuyu na Kyela; Iringa: Iringa Mjini, Tanangozi, Ifunda, Mafinga, Makambako, Njombe.

Aidha, mtandao wa *Vodacom* uko katika barabara kuu zifuatazo:- Dar es Salaam - Kibaha - Chalinze - Morogoro-Ifakara; Chalinze - Segera-Tanga; Segera-Same-Moshi-Mwika-Marangu; Moshi-Arusha-Namanga; Arusha-Makuyuni-Monduli-Ngorongoro;

Iringa-Makambako-Njombe; Makambako-Mbeya-Tunduka; Mbeya-Tukuyu-Kyela; Nzega-Shinyanga-Mwadui; Shinyanga-Isaka-Kahama-Sengerema; Mwanza-Sengerema-Geita-Muleba-Bukoba. Hadi sasa *Vodacom* imefikisha wateja 500,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Celtel* imeeneza huduma zake Mikoa yote ya Tanzania na Wilaya 64 kama ifuatavyo:- Arusha: Arusha Mjini, Tengeru, *Usa-River, KIA,* Mererani, Babati, Makuyuni, *Lake Manyara,* Karatu, Ngorongoro, Namanga na Lengijave; Kilimanjaro: Moshi Mjini, Hai, Machame, Arusha-*Moshi Road, TPC,* Marangu, Moshi-*Tanga Road,* Himo, Mwika, Rombo, Mwanga na Same; Tanga: Tanga Mjini, Pongwe, Muheza, Pangani, Mombo, Lushoto, Handeni, Tanga-*Segera Road* na Segera-*Chalinze Road;* Pwani: Kibaha, Chalinze, Mlandizi, Bagamoyo, Dar es Saalm - Chalinze-*Segera Road* na Dar es Salaam - *Morogoro Road;* Dar es Salaam Mji wa Dar es Salaam; Morogoro: Morogoro Mjini, Turiani, *IDM - Mzumbe,* Mikumi, Dar es Salaam - *Mikumi Road (Mikumi National Park)* Kilombero na Ifakara; Iringa: Iringa Mjini, Mafinga, Makambako na Njombe; Ruvuma: Songea Mjini na Mbinga; Mbeya; Mbeya Mjini, Mlowo, Tunduma, Tukuyu na Kyela; Rukwa: Sumbawanga Mjini; Kigoma: Kigoma Mjini, Tabora: Tabora Mjini na Nzega; Singida: Singida Mjini na Manyoni; Dodoma: Dodoma Mjini na Mpwapwa; Shinyanga Shinyanga Mjini, Bariadi, Isaka, Kahama Mjini na *Kahama Mining;* Mwanza: Mwanza Mjini, Magu, Sengerema na Geita; Kagera: Bukoba na Ngara; Mara: Musoma, Bunda, Tarime, Sirari na Bunda-*Musoma Road;* Lindi: Lindi Mjini; Mtwara: Mtwara Mjini na Masasi; Zanzibar na Pemba: Mjini Magharibi, Unguja Kusini, Unguja Kaskazini, Wete, Mkoani, Chakechake. Hadi Juni, 2003 Kampuni ya *Celtel* ilikuwa na wateja 170,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kampuni ya *Mobitel* imepanua mtandao na sasa imefika Mikoa yote isipokuwa Tabora, Singida na Lindi na imefika Wilaya 70 kama ifuatavyo:- Dar es Salaam: Kinondoni, Temeke na Ilala; Pwani: Kibaha, Kisarawe, Bagamoyo na Mkuranga; Morogoro: Morogoro Mjini; Tanga: Tanga Mjini; Dodoma: Dodoma Mjini; Arusha: Arusha Mjini; Kilimanjaro: Moshi Mjini, Moshi Vijijini, Rombo na Hai; Iringa: Iringa Mjini, Makambako na Njombe; Mbeya; Mbeya Mjini; Mwanza: Nyamagana na Ilemela; Shinyanga: Shinyanga Mjini, Kahama na Mwadui; Mara: Musoma, Tarime na Sirari; Kigoma: Kigoma Mjini na Kasulu; Ruvuma: Songea Mjini; Mtwara: Mtwara Mjini; Rukwa: Sumbawanga; Kagera: Bukoba; Mjini Magharibi: Mjini Magharibi; Magharibi; Magharibi, Kaskazini A: Kaskazini A; Kaskazini B: Kaskazini B; Kusini: Kusini; Chakechake: Chakechake; Hadi Juni 2003, kampuni ya *Mobitel* ilikuwa na wateja 165,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Zantel* imefika Mikoa yote ya Unguja na Pemba kama ifuatavyo:- Kazimkazi, Makunduchi, Paji na Jambiani; Mjini Zanzibar, Tunguu; Chwaka, Kiwengwa, Nungwi, Bububu, Mahonda. Pemba: Mkoani, Tambile, Kengeja, Chakechake, sehemu ya Ziwani na Wete. Hadi sasa *Zantel* ina wateja 42,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ilipofika Juni, 2002, wateja wa simu za mkononi walikuwa 490,000. Idadi hiyo sasa katika kipindi cha mwaka mmoja tu imepanda kufikia 877,000. Haya ni mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukichukulia kwamba idadi ya wateja wa *TTCL* ambao wameunganishwa na mtandao ni 160,000 maana yake idadi ya Watanzania waliounganishwa na simu sasa imefikia 1,037,000. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa mara ya kwanza katika historia ya mawasiliano nchini idadi ya wenye simu ni zaidi ya wateja 1,000,000 ikilinganishwa na idadi ya wateja 100,000 mwaka 1995. Mafanikio haya si haba, yanatokana na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002, barua zilizotumwa na kusambazwa kupitia mtandao wa Posta ndani ya nchi zilikuwa milioni 19.0 zikiwa pungufu kwa asilimia 0.5 ikilinganishwa na milioni 19.0 zilizotumwa mwaka 2001. Barua zilizotumwa nje ya nchi zilikuwa milioni 6.1 ambazo ni ongezeko la asilimia 5.2 ikilinganishwa na barua milioni 5.8 zilizotumwa mwaka 2001. Vifurushi vilivyotumwa katika soko la ndani vimeongezeka kwa asilimia 12.6 kutoka vifurushi 28,309 mwaka 2001 hadi kufikia vifurushi 31,862 mwaka 2002.

Wakati huo huo vifurushi vilivyotumwa nje ya nchi vimeongezeka kwa asilimia 5.5 kutoka vifurushi 5,488 mwaka 2002 hadi kufikia vifurushi 5,789 mwaka 2002. Barua zilizosajiliwa posta (rejista) zilizotumwa katika soko la ndani katika kipindi cha mwaka 2002 zilikuwa 324,214 ambalo ni ongezeko la asilimia 1.2 ikilinganishwa na rejista 320,425 za mwaka 2001. Pia rejista zilizotumwa katika soko la nje zilikuwa 31,814 ikiwa ni ongezeko la asilimia 11.7 ikilinganishwa na rejista 28,486 za mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, aidha, idadi ya Hawala za Posta *(Express Money Orders)* zilizotumwa iliongezeka kwa asilimia 0.9 kutoka 278,068 mwaka 2001 hadi 280,798 mwaka 2002. Hata hivyo kwa upande wa utumaji fedha katika nchi za Afrika mashariki, idadi ilipungua kwa asilimia 38.8 kutoka 3,794 mwaka 2001 mpaka 2,320 mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, huduma ya *EMS* ambayo inahusisha ukusanyaji na usambazaji wa nyaraka na vipeto iliendelea kutolewa kwa ufanisi. Nyaraka na vipeto vya haraka vilivyosambazwa ndani ya nchi viliongezeka kwa asilimia 8.1 ambapo vya Kimataifa viliongezeka kwa asilimia 33.4. Kadhalika utumaji fedha kwa njia ya haraka *(Money Fax)* uliongezeka kwa asilimia 18 kutoka 157,661 kwa mwaka 2001 hadi kufikia 186,360 kwa mwaka 2002. Vile vile utumaji wa taarifa za haraka *(EMS Fax Messages)* uliongezeka kwa asilimia 5 kutoka 9,427 kwa mwaka 2001 hadi kufikia 9,904 kwa mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002 Shirika limeendelea kuimarisha na kuendeleza huduma mpya za uwakala wa kukusanya na kufanya malipo ya fedha *(post Giro),* usambazaji wa mizigo *(Post Cargo),* usambazaji wa barua za matangazo *(Adversing Mail)* na vituo vya huduma ya barua pepe *(Internet Café).*

Aidha, Shirika limeendelea kuboresha huduma ya matumizi ya teknolojia mpya kwa kufunga kompyuta zitakazotumika katika mtandao wa mawasiliano na upashanaji habari katika Posta Kuu za Mikoa ili kusogeza huduma za Posta karibu na wananchi,

Shirika limebuni mradi wa masanduku maalum ya kupokea barua *(cluster boxes)* ambayo yamefungwa kwa majaribio katika maeneo mbalimbali katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002, Shirika lilikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na ufanisi mdogo wa kusambaza barua kwa wateja katika maeneo ya vijijini. Hii ni kutokana na ubovu wa miundo mbinu ya mawasiliano na usafishaji kwa baadhi ya njia, mtaji mdogo, kuwa na madeni makubwa na kuongezeka kwa ushindani usiozingatia sheria na taratibu zilizowekwa. Pamoja na changamoto hizo, shirika liliendelea kupanga mikakati na mbinu mbalimbali za kuliwezesha kuimarisha utendaji wake.

Katika kipindi cha 2003/2004, Shirika limepanga kujenga ofisi mpya za kisasa za Posta katika miji ya Isaka, Mpanda, Katesh, Olkesumet na Namanyere. Pia litafanya ukarabati wa majengo na vifaa, kufanya ununuzi wa magari na pikipiki ili kuongeza na kuboresha kasi ya usafirishaji na usambazaji wa barua na vifurushi. Shirika litaongeza huduma ya utumaji fedha kwa njia ya haraka *(electronic money transfer).* Lengo ni kuhakikisha huduma hii inapatikana katika makao makuu ya Wilaya zote nchini.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003 nililifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu ilipewa jukumu la kuratibu shughuli zote zinazohusiana na huduma za *ICT*. Manufaa ya huduma za *ICT* ni makubwa ikizingatiwa kuwa *ICT* inahudumia sekta zote za uchumi nchini na kuwezesha jamii kupokea na kubadilishana taarifa na habari miongoni mwao. Teknolojia hii pia ni nyenzo muhimu sana katika kupunguza pengo lilopo kati ya nchi zinazoendelea na zile zilizoendelea na kati ya wananchi wanaoishi mijini na wale walio vijijini, katika nchi kama Tanzania *(Digital divide).*

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu ilikamilisha maandalizi ya Sera ya Teknolojia ya Mawasiliano na Habari. Serikali iliidhinisha Sera hiyo mwezi Machi, 2003. Matayarisho ya mkakati wa utekelezaji wa sera yanaendelea chini ya Kamati maalum ya wataalam waliosaidia katika maandalizi ya awali ya sera hiyo. Utekelezaji wa programu ya *ICT* utahitaji misingi imara ya kisheria. Wizara itashirikiana na wadau wengine katika kuandaa sheria husika. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa mchango wao mkubwa katika maandalizi ya Sera kupitia Semina ya Wabunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Desemba, 2003 utafanyika mkutano wa Wakuu wa nchi zote duniani kuhusu matumizi ya huduma za *ICT* kwa jamii *(The World Summit on Information Society (WSIS).* Madhumuni ya *WSIS* ni kuweka msimamo wa pamoja na kujadili mikakati ya namna ya kujenga jamii duniani yenye uwezo na maarifa ya kutumia teknolojia ya mawasiliano na habari kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za uzalishaji kwa lengo la kuharakisha maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nchi zote ikiwemo Tanzania zinashiriki katika mikutano ya matayarisho ya mkutano huo. Tayari mikutano miwili ya matayarisho imekwishafanyika

huko Geneva. Kikanda, kumekuwepo mikutano na mijadala mbalimbali katika Bara la Afrika. Tanzania imekuwa ikishiriki kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ilikuwa mwenyeji wa mkutano wa Umoja wa Simu Duniani *(ITU)* uliozungumzia matumizi ya huduma za *ICT* katika kutekeleza ushirikiano mpya wa maendeleo Barani Afrika *(New Partenrship for African Development (NEPAD).* Mkutano huo uliofanyika Arusha, mwezi Machi, 2003.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wa Mawasiliano wa Afrika walikutana Mauritius, Aprili, 2003 kujadili na kupata msimamo wa pamoja juu ya *WSIS.* Mkutano wa hivi karibuni umefanyika Cairo, Misri tarehe 16-18 Juni, 2003, kwa shabaha ya kuainisha misimamo ya Bara la Afrika na nchi za kiarabu.

Mheshimiwa Spika, *Simunet* ni Kampuni tanzu ya Kampuni yaSimu Tanzania *(TTCL)* ambayo inashughulikia mawasiliano ya takwimu na tovuti. Hivi sasa kuna jumla ya makampuni 16 yanayotoa huduma za mawasiliano ya takwimu *(Data Communications Service Providers (DSPs).*

Aidha, kuna jumla ya makampuni 23 yanayotoa huduma za tovuti na barua pepe *(Internet Service Providers - ISPs, E-mail).* Huduma hizi kwa pamoja hadi sasa zinaifanya Tanzania kuwa na huduma ya msingi ya mawasiliano ya kisasa *(IP - Backbone)* wenye jumla ya njia 10 za lango la Kimataifa *(International Gateway).* Vituo 50 vya mawasiliano ya tovuti *(50 Points of Presence - POPs)* vimesambazwa nchini. Vituo hivi viko karibu Mikoa yote nchini. *POPs* zinasaidia sana kupunguza gharama za mawasiliano ya tovuti Mikoani na Wilayani.

Mhehimiwa Spika, sekta binafsi katika *ICT* imeshawishiwa na imekubali kuanzisha *Internet Exchange Point (IXP)* nchini. *IXP* itawezesha kuwa na huduma ya mawasiliano ya kisasa ya haraka na salama. Mawasiliano haya yatafanyika nchini ambapo hivi sasa inabidi tutumie *IXP* za nje ya nchi. Mradi huu utachangiwa na *UNDP* na unatarajiwa kuanza Dar es Salaam Agosti, 2003. Makampuni ambayo yanatoa huduma ya tovuti chini ya chama chao cha *Tanzania ISP Association* nayo yatachangia katika kuanzisha huduma ya *IXP.*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya kieletroniki sasa hivi ni changamoto kwa Serikali nyingi duniani zinazoongozwa kwa ufanisi na kwa misingi ya demokrasia na utawala bora wenye uwazi na haki. Serikali ya kieletroniki huongeza tija katika taasisi zote za umma kutokana na kuwepo kwa mawasiliano rahisi kupitia mtandao imara unaounganisha huduma zote muhimu za Serikali na Serikali na wananchi.

Kwa ujumla, Serikali ya kielektroniki ni njia ya kufanikisha maendeleo ya wananchi kwa haraka na kwa gharama nafuu, kwa kutumia *ICT.* Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi itashirikiana kwa karibu sana na Idara Kuu ya Utumishi katika kutekeleza azma ya Serikali ya kuwa na Serikali ya kieletroniki.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/03, Mamlaka ya Hali ya hewa iliendelea kuboresha huduma zake katika maeneo mbalimbali. Maeneo hayo ni pamoja na kuongeza vifaa, kujenga vituo vikuu viwili vya kupimia hali ya hewa *(synoptic stations)* Handeni na Singida. Vile vile Mamlaka imefunga mitambo inayojiendesha yenyewe ya kupima hali ya hewa *(Automatic Weather Stations)* kwenye vituo vya Zanzibar, Tanga, Mwanza, Dodoma na Arusha. Mamlaka pia imefanikiwa kuboresha maslahi na mafunzo ya wafanyakazi. Aidha, Mamlaka iliweza kuwatembelea na kuwa na mahojiano na wateja wake sehemu mbalimbali nchini kwa madhumuni ya kuweza kujua mahitaji yao na jinsi ya kuboresha utoaji huduma.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Dr. Mohamed Mhita, amechaguliwa kwa mara ya pili kuwa Rais wa Kanda ya Afrika kwenye Shirika la Hali ya Hewa Duniani. Nafasi hii inatoa fursa nzuri kwa Mamlaka kuweza kushiriki katika mipango ya maendeleo ya huduma za hali ya hewa katika Bara la Afrika na Dunia kwa ujumla na hatimaye kuweza kutoa mchango mzuri katika mahitaji ya huduma hii muhimu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/04, Mamlaka imeazimia kuongeza ubora wa huduma kuzingatia matakwa ya wateja. Mamlaka pia itaongeza vifaa, mafunzo kwa wafanyakazi na vituo vya kupimia hali ya hewa *(surface* na *automatic stations)* kwa nia ya kuboresha upatikanaji wa takwimu na utabiri na kuwa karibu na wateja. Mamlaka katika jitihada za kuondoa tatizo la uhaba wa ofisi, inatarajia kuanza ujenzi wa jengo la Makao Makuu. Tayari Serikali imeipatia Mamlaka kiwanja kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kupata ushirika au kufanikisha ushiriki wa wanawake katika shughuli mbalimbali za sekta. Wanawake wameendelea kujitokeza katika ujenzi wa miundombinu na utoaji wa huduma za sekta. Ni nia ya Wizara yangu kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ili kuhakikisha kwamba utekelezaji wa sera ya teknolojia ya mawasiliano na habari unazingatia umuhimu wa kutumia teknolojia ya kisasa kupunguza tofauti za kijinsia katika maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kushirikiana na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuandaa mikakati na kutayarisha programu ya utekelezaji katika kuboresha usafiri Vijijini ikiwa ni pamoja na upatikanaji na utumiaji wa *Non-Motorized Transport* kwa wanawake nchini. Programu hizi zinalenga kuwapunguzia wanawake matatizo ya kutembea umbali mrefu huku wakiwa wamebeba mizigo kichwani, badala yake watapata fursa ya kushiriki kwenye shughuli nyingine za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, aidha, pamoja na mikakati hiyo, Wizara imepokea maelekezo ya Serikali ya kuwepo na kitengo cha jinsia kwa kila Wizara ili kufuta tofauti zilizopo na kuwa na haki sawa. Hivi sasa Wizara imeanza maandalizi ya kuunda kitengo hicho.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Wizara iliendelea na jitihada za kuwapatia taaluma muhimu za kuwaongezea ujuzi watumishi wake. Taaluma hizo

zilihusu utunzaji wa kumbukumbu, uhasibu na biashara. Katika kipindi hicho, watumishi tisa walihudhuria mafunzo ya muda mrefu katika fani za uhasibu na biashara.

Aidha, watumishi (makarani) 14 wanaendelea kupata mafunzo katika utunzaji wa kumbukumbu. Kati yao saba wanasoma ngazi ya *Certificate* na saba waliobaki wanasoma ngazi ya *Diploma.* Wizara inaendelea kuanda programu ya mafunzo kwa lengo la kuwa na mpango endelevu wa utoaji wa mafunzo mbalimbali kwa wataalam wa sekta kwa kutumia vyuo na taasisi za sekta.

Katika kutekeleza sera ya Serikali kuhusu mabadiliko ya mfumo wa utendaji wa Serikali, Wizara kwa kushirikiana na Idara Kuu ya Utumishi imeanza kutoa mafunzo ya *Performance Management System.* Kutokana na mafunzo haya, Wizara iko kwenye hatua ya kuandaa Mkataba wa Huduma kwa Wateja *(Client Service Charter).*

Mheshimiwa Spika, jukumu la kupiga vita Ukimwi bado limepewa umuhimu mkubwa hususan katika kipindi hiki ambacho maambukizi hayajali umri. Katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Wizara yangu iliendelea na jukumu la kutoa mafunzo mbalimbali kwa wafanyakazi kwa nia ya kuwaelimisha namna ugonjwa wenyewe unavyosambaa.

Sambamba na jukumu hilo, Wizara katika kipindi hicho iliandaa mpango wa sekta kuhusu Ukimwi ambao utatekelezwa katika kipindi cha miaka miwili. Pia imetenga fungu katika bajeti ya mwaka 2003/2004 ambalo litasaidia utekelezaji wa mpango huo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji kimeendelea kuboresha miundombinu na mazingira yake ili kuweza kuendelea na jukumu lake la kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri katika sekta ya usafirishaji na uchukuzi nchini. Idadi ya wanafunzi wanaochukua masomo ya Stashahada ya Juu ya Uongozi katika Usafirishaji na wale wa Stashahada ya Ufundi wa magari imeongezeka kutokana na idadi ya wanafunzi 149 mwaka jana hadi kufikia wanafunzi 229 mwaka huu. Idadi hiyo ni pamoja na ongezeko kubwa la wanafunzi wanawake, kutoka wanafunzi sita mwaka jana hadi kufikia wanafunzi 26 mwaka huu. Halikadhalika, wamiliki wa magari ya abiria na mizigo, Wizara na idara mbalimbali za Serikali pamoja na asasi za umma na za watu binafsi nchini zimeendelea kufaidika na mafunzo ya kozi fupi yanayoandaliwa na Chuo hicho. Washiriki wapatao 587 wamefaidika na kozi za namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji kinaandaa mpango wa maendeleo ambao unaendana na Dira ya Taifa ya 2025. Nia ni kukifanya Chuo kiende na wakati na kitoe mchango wake katika taaluma ya usafirishaji nchini na katika Kanda ya Afrika ya Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003 Chuo cha Mabaharia cha Dar es Salaam kiliendelea na jukumu lake ka kutoa elimu ya ubaharia. Chuo kwa kushirikiana na *International Maritime Organization* kiliendesha kozi ya taaluma ya ufundishaji kwa Walimu wa Chuo cha Mabaharia Dar e Salaam, vyuo vingine vya hapa nchini pia vilivyofaidika na mafunzo hayo ni *Bandari College, Mbegani FDC, Dar es Salaam Institute of Techonolgy* na Chuo cha Uvuvi Nyegezi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Chuo kwa kushirikiana na *IMO* na Wizara pamoja na vyuo vingine kilifanya Warsha ya Mkataba mpya wa Kimataifa juu ya mafunzo ya mabaharia wa meli za uvuvi *(STCW Fishing Vessels)* na nchi 19 zilihudhuria warsha hii. Mkataba huu utaanza kutumika mara tu nchi zenye meli za uvuvi zitakapouridhia.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba baada ya Serikali kukamilisha utekelezaji wa masharti ya Mkataba wa Kimataifa wa mafunzo kwa Mabaharia *(STCW-95)* nchi sasa imekubalika kwamba inatekeleza Mkataba huo na hivyo kujumlishwa katika idadi ya nchi zinazokidhi masharti haya *(White List).* Jambo hili limetoa nafasi ya kutambuliwa Kimataifa wahitimu wa Chuo pamoja na Chuo chenyewe. Kitendo hiki cha kutambuliwa Kimataifa Chuo pamoja na wahitimu wake kimepanua wigo wa vijana wetu kupata ajira katika meli za Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa maelezo niliyotoa yanatosha katika kuliarifu Bunge lako Tukufu pamoja na wananchi kwa ujumla kuhusu utendaji wa sekta ya mawasiliano na uchukuzi kwa kipindi kilichopita. Napenda kueleza kwamba, juhudi zinafanywa za kuendelea kuyatatua matatizo yaliyopo. Tutaendelea kujitahidi kuboresha huduma zetu kama mwelekeo wa shughuli za sekta unavyoelekeza. Lengo la Serikali ni kuona kwamba sekta hii inaimarika na hivyo kuleta maendeleo tuliyokusudia na kuwajengea wananchi imani ya utekelezaji wa majukumu yetu na dhamana tuliyopewa ya kuongoza vyombo vya umma kama Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ilivyoainisha.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yangu kuwa Waheshimiwa Wabunge watakuwa tayari kutukosoa pale tulipokosea, kutuweka sawa pale tulipoteleza na vile vile kuwapongeza wafanyakazi wa sekta hii pale walipofanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijamalizia hotuba yangu sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshirikiana nasi katika kufanikisha malengo tuliyojiwekea. Hawa ni pamoja na wahisani mbalimbali waliotusaidia katika kukamilisha progamu na mipango yetu ya sekta ya mawasiliano na uchukuzi katika kipindi kilichopita.

Aidha, napenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa Mashirika na taasisi za Kimataifa zilizochangia katika kuboresha huduma mbalimbali na miumndombinu ya sekta hii. Nchi na Mashirika hayo ni pamoja na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP),* Shirika la Kimataifa linalosimamiaUsafiri wa Majini *(IMO),* Shirika la Umoja wa Kimataifa linalosimamia Usalama wa Usafiri wa Anga *(ICAO),* Shirika la Kimataifa linalosimamia Masuala ya Simu *(ITU),* Jumuiya ya Kimataifa inayosimamia masuala ya Huduma za Posta *(IPU),* Shirika la Hali ya Hewa Duniani *(WMO),* Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB),* Uholanzi, Sweden, Kuwait, Umoja wa Nchi za Ulaya, Finland, Denmark, Ujerumani, Uingereza, Japan, China, Ubelgiji, Ufaransa, Italia, Benki ya Dunia, Benki ya Raslimali ya Ulaya, Urusi na wengine wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kutoa shukrani zangu kwa viongozi wenzangu katika Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi nikianza na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr.

Maua Daftari, Katibu Mkuu Ndugu Salim Himid Msoma, Wakuu wa Idara, Viongozi wa Asasi na Taasisi tunazozisimamia, pamoja na watendaji wote wa Wizara yangu. Ushirikiano wao mkubwa walionipa umenisaidia sana katika kutekeleza majukumu ya Serikali na hasa lile la kuendeleza sekta za mawasiliano na uchukuzi. Ni wazi kwamba bila mchango wao ingeniwia vigumu sana na hata kutowezekana kufikia mafanikio yote haya katika kuendeleza sekta hii. Nawashukuru sana. Pia nawashukuru sana wananchi wa Rungwe Mashariki kwa ushirikiano wao, mshikamano na imani yao kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ipasavyo katika kipindi cha mwaka 2003/04, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 45,264,572,400/=. Kati ya fedha hizo shilingi 20,972,699,100/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, shilingi 332,060,300/= kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na shilingi 23,959,813,000/= ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 23,959,813,000/= za miradi ya maendeleo, shilingi 1,850,000,000/= ni za hapa nchini na shilingi 22,109,813,000/= ni fedha za kigeni toka kwa wahisani mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza wakati nikiwasilisha hotuba yangu. Hotuba hii inaweza kupatikana vile vile katika tovuti ya Wizara na tovuti ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Msemaji wa Kamati ya Miundombinu kutoa maoni yake. Waheshimiwa wafuatao ndiyo watakuwa wasemaji wa kwanza. Mheshimiwa Ismail Ivwatta atafuatiwa na Mheshimiwa Haroub Masoub, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni na wa nne ni Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, wajiandae baada ya Msemaji wa Upinzani.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU (k.n.y. MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO - MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Na. 81(1) ya mwaka 2003, napenda nitumie fursa hii kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, taarifa ya Kamati ya Miundombinu inayohusu Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi juu ya Mipango na makadirio ya bajeti ya mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua mpango wa makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2003/2004, Kamati yangu ilipata maelezo mbalimbali kuhusu dira *(vision),* majukumu ya Wizara pamoja na taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Miundombinu ya mwaka 2002/03. Kamati pia ilipata taarifa ya mapato na matumizi ya Wizara kwa kipindi cha mwaka 2002/03, pamoja na mafanikio na matatizo yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa mpango wa kipindi kilichopita. Aidha, Kamati ilipata maelezo kuhusu kazi zilizopangwa kufanywa na

Wizara katika kipindi cha mwaka wa fedha cha 2003/04 na maombi ya fedha kwa kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Wanakamati wenzangu kwa mchango wao mkubwa wa kupitia na kuchambua mpango na makadirio ya bajeti ya Wizara hii kwa kina na ufasaha mkubwa. Mawazo yao na ushauri wao ndio uliowezesha kukamilika kwa taarifa hii. Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu 103B(1) Toleo la 2003, napenda niwatambue kwa majina wajumbe wa Kamati ya Miundombinu walioshiriki katika zoezi hili ambao ni, Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, Mwenyekiti, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe ambao ni Mheshimiwa Lydia Boma, Mheshimiwa Zamda Bozzen, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mheshimiwa Robert Buzuka, Mheshimiwa Abdallah Feruzi, Mheshimiwa Ally Karavina, Mheshimwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, Mheshimiwa Mohammed Missanga, Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Sijamini Shaame na Mheshimiwa Maria Watondoha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati iliridhishwa na maandalizi na mawasilisho yaliyofanywa na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kuhusu mpango na Makadirio ya Bajeti ya mwaka 2003/2004.

Napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara Ndugu Salim Msoma, kwa kazi nzuri waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii, kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati yangu imeridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Wizara katika kutekeleza maelekezo yote ya Kamati kwa kadri ilivyoweza. Nachukua tena fursa kuipongeza Wizara kwa juhudi zilizofanywa katika utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi katika taarifa yake kwa Kamati juu ya utekelezaji wa malengo ya Wizara kwa mwaka 2002/2003 aliainisha mafanikio na matatizo kwa kipindi hicho kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafanikio ni kuwa Serikali ilipitisha sera mbalimbali na utekelezaji wake umeshaanza, Wakala wa Ndege za Serikali imefanya matengenezo makubwa ya ndege moja ya Serikali, Wizara kwa kushirikiana na Idara Kuu ya Utumishi *(CSD)* imefanya mapitio katika muundo wa kada zilizopo katika Wizara, ubinafsishaji wa *ATC* ulikamilika ambapo asilimia 49 ya hisa zimeuzwa kwa Shirika la Ndege la Afrika ya Kusini *(SAA)* na Serikali imebaki na asilimia 51, Wizara imepewa jukumu la kuratibu utayarishaji wa mipango ya maendeleo ya miundombinu kwenye Taasisi ya Ushirikiano wa Nchi za Afrika *(NEPAD)* na Wizara imeshiriki katika vikao mbalimbali vya Kitaifa na Kimataifa vinavyohusika na masuala ya mawasiliano, uchukuzi na hali ya hewa.

Pia Wizara kwa mwaka wa fedha 2003/04 hadi kufikia Mwezi Machi ilikusanya mapato ya shilingi bilioni 2.526 na kufikia Juni, 2003 inatarajiwa kufikia shilingi bilioni 3.6 na Wizara imeendelea na utekelezaji wake wa programu za maendeleo katika ukarabati wa taasisi zake zikiwemo Shirika la Reli, Viwanja vya Ndege na Kampuni ya Meli *(MSC)* na ujenzi wa magati.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mpango wa mwaka 2002/2003 matatizo mbalimbali yalijitokeza na kusababisha baadhi ya majukumu yasikamilike kwa ufanisi kama ilivyotarajiwa. Changamoto hizo kwa muhtasari ni hizi zifuatazo:-

- Ndege moja ya Wakala wa Ndege za Serikali iliharibika kwa miezi minne kuanzia Septemba, 2002 hadi Machi, 2003.

- Kuchelewa kulipa madeni kwa baadhi ya taasisi ambazo hutumia ndege za Serikali.

- Upungufu wa wakaguzi wa vyombo vya majini.

- Ukosefu wa fedha za kutosha kuendeshea shughuli zilizopangwa na Wizara kutoka Serikalini.

- Uhaba wa vitendea kazi katika Mamlaka mbalimbali.

- Wizara haikuweza kutekeleza kikamilifu mikakati iliyopangwa kwa nia ya kupunguza kasi ya kuenea kwa maambukizi ya Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, mwelekeo na malengo ya Wizara kwa mwaka 2003/2004 yalielezwa vizuri na napenda kusema kwamba wajumbe walikubaliana na mpango huo. Sasa nikija katika maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa tathmini ya mawasilisho ya mpango na bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2003/2004, naomba sasa nitoe maoni, ushauri na maelekezo ya Kamati kwa Wizara na Serikali kwa ujumla.

Kamati inashauri kuwa Wizara iandae programu ya utekelezaji *(Action Plan)* kwa kila sera ili mipango itakayotekelezwa ijulikane. Aidha, sera na mikakati ya Wizara viwiane ili kuwezesha tathmini ya utekelezaji *(performance appraisal).*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubinafsishaji wa mashirika yaliyoko chini ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na kwa kuzingatia unyeti wa mashirika hayo, Kamati inaendelea kusisitiza tahadhari iliyotolewa mwaka jana ya kuitaka Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na Serikali kwa ujumla kuwa waangalifu katika zoezi la ubinafsishaji wa mashirika ili maslahi ya Taifa yaweze kulindwa na kuepuka migogoro inayoweza kujitokeza kwa vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imekuwa na wasiwasi juu ya kasi ya zoezi la ubinafsishaji au ukodishaji wa Mashirika ya sekta ya uchukuzi kama vile Shirika la Reli

*(TRC), TAZARA* na kadhalika. Mashirika haya yanakabiliwa na matatizo ya uchakavu wa vifaa, miundombinu pamoja na raslimali, hivyo kufanya zoezi la kupata wawekezaji au wakodishaji kuwa gumu. Kamati inashauri kuwa Serikali iweka utaratibu mzuri wa kuyasaidia mashirika hayo hasa wakati wa kipindi hiki cha mpito ili yaendelee kutoa huduma ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu. Iwapo mashirika haya hayatasaidiwa ipo hatari ya kuyumbisha mwelekeo wa Taifa na biashara ya usafirishaji iliyopo sasa toka nchi jirani kama vile Rwanda, Kongo *(DRC),* Zambia, Malawi na kwingineko kwa kukimbilia nchi nyingine.

Kamati ilipokea taarifa ya maendeleo ya ujenzi wa uwanja wa ndege wa Songwe na inaishauri Serikali itenge fedha za kutosha kukamilisha ujenzi wa uwanja huo. Aidha, Kamati inashauri Serikali itafute uwezekano wa kutatua tatizo sugu la maji katika uwanja huo, kwa mfano kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya utafutwe uwezekano wa kuvuta maji kutoka Mto Mbalizi ambayo yatawanufaisha wananchi wengi wanaoishi katika maeneo yanayozunguka uwanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hali ya Hewa haina ofisi za kuridhisha. Kamati inaishauri Serikali isaidie kuiwezesha Mamlaka hii kujenga jengo la kisasa ili kufanya kazi kwa ufanisi na kutunza kumbukumbu na takwimu kwa uhakika na usalama.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imebaini kuwa katika mashirika yaliyo chini ya Wizara hii kuna wafanyakazi wengi ambao wamefikia umri wa kustaafu. Tatizo hili lilijidhihirisha zaidi katika Mamlaka ya Hali ya Hewa. Kamati inashauri uwekwe mpango wa makusudi wa mafunzo kwa ajili ya kujaza nafasi kwa wanaokaribia kustaafu hasa kwa kuzingatia kwamba utaalam huu ni adimu na nyeti..

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba mpango wa kupeleka mitambo ya simu ya kisasa katika maeneo yaliyokwishaahidiwa kupata mitambo hiyo kama vile Mafia, Liwale, Kilwa, Sikonge, Urambo na kadhalika umekuwa wa kusuasua. Kamati inashauri ahadi zilizotolewa zitekelezwe (hususan Makao Makuu yote ya Wilaya yapatiwe huduma ya simu) kwa wakati ili wananchi wajenge imani zaidi kwa Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa na utendaji hafifu wa Kampuni ya *TTCL* katika kukamilisha Mkataba wa uwekezaji na masharti ya leseni yake. Kamati ilipata taarifa kuwa, utekelezaji wa Mkataba huo wa *TTCL* haukwenda kufuatana na makubaliano yaliyokuwa kwenye Mkataba, jambo lililosababisha Tume ya Mawasiliano kuwatoza faini, ambayo hadi sasa bado hawajailipa. Kamati inashauri kwamba hatua za haraka zichukuliwe katika kutekeleza masharti ya Mkataba. Aidha, Serikali iangalie uwezekano wa kuwafutia *TTCL exclusivity* yao kwa vile wamekiuka masharti ya uwekezaji na leseni yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine la ushauri, Kamati inashauri kuwa Serikali ifanye kila jitihada katika kuharakisha ulipaji wa madeni yake sugu kwa taasisi na mashirika yanayotoa huduma kama vile Mamlaka ya Ndege za Serikali, *TRC, TAZARA* na mengineyo yaliyo chini ya Wizara. Hii itatoa fursa kwa mashirika hayo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingine ni kwamba suala la *fuel levy* limeendelea kujitokeza tena kama suala linalohitaji kuangaliwa kwa undani zaidi. Bunge lako Tukufu lilipitisha Muswada wa Sheria ya Ushuru wa Mafuta *(fuel levy),* ambayo inachangiwa na watumiaji wa mafuta wote nchini ikiwa ni pamoja na meli, reli na ndege. Hata hivyo matumizi ya *levy* hii yameelekezwa kwenye matengenezo ya ujenzi wa barabara na madaraja tu. Kamati inaishauri Serikali ifikirie utaratibu ambao meli, reli na viwanja vya ndege zetu zitafaidika na levy hii kama sekta muhimu katika maendeleo ya miundombinu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inashauri Wizara kuratibu upya gharama za simu za mikononi kwani ni ghali mno zinazowafanya wananchi hususan wa Vijijini kushindwa kumudu matumizi ya simu hizo. Aidha, Serikali iharakishe uundwaji wa Mfuko wa kupeleka simu Vijijini *(Rural Telecom Fund)* ambao utakuwa ni mkombozi wa wananchi walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu nembo ya Taifa kwenye ndege za *ATCL,* Kamati inashauri Serikali ihakikishe kuwa nembo ya Twiga inawekwa kwenye ndege zote za Kampuni iliyobinafisshwa ya *ATCL* ili kulitambulisha Taifa. Hii pia ikizingatiwa kwamba Serikali ina hisa nyingi katika Kampuni hii. Kwa hiyo ni haki kabisa kuonyesha nembo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tanzania ina bahati ya kuzungukwa na nchi za Maziwa Makuu zaidi ya nane na ambazo hazina matoleo ya bandari *(Landlocked)* na zingeweza kutumia bandari zetu, Serikali iimarishe miundombinu iliyopo ili kujenga uchumi wake kwa kutumia nafasi yetu kijiografia *(geographical position)* kwa kuboresha miundombinu ya reli, bandari, viwanja vya ndege kwa uwiano sawia ili vyote vichangie katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu limeshapitisha sheria ya kuanzisha Mamlaka ya kusimamia usafiri wa nchi kavu na majini yaani *SUMATRA* lakini mpaka hivi sasa mamlaka hii haijaanza kufanya kazi. Kamati inaishauri Serikali kuanzisha mamlaka hii mara moja ili makusudi na malengo ya kuundwa kwake yakamilishwe.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati yangu kupitia na kujadili kwa kina Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi iliombwa kuidhinisha kiasi cha shilingi bilioni 39.462. Kati ya hizo shilingi milioni 332 ni mishahara ya watumishi, bilioni 20.97 ni fedha za matumizi mengineyo na shilingi bilioni 18.157 zikiwa ni fedha za miradi ya maendeleo. Kamati ilikubali kwa niaba yenu Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu iliridhishwa na maandalizi na mawasilisho yaliyofanywa na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kuhusu mpango na makadirio ya Bajeti ya mwaka 2003/04. Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Naibu wake Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Katibu Mkuu ndugu Salim Msoma, pamoja na wataalam wa Wizara kwa kazi nzuri waliyoifanya ya matayarisho ya bajeti pamoja na ushirikiano wao na Kamati ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inaishukuru Wizara kwa maandalizi ya ziara za Wabunge kabla ya kuanza vikao hivi vya Bajeti. Hii imewapa fursa Wanakamati kujielimisha na kuzifahamu vema shughuli za Mashirika, Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara hii na hatimaye kufanya uchambuzi wa bajeti kuwa rahisi kwa kutambua na kubaini changamoto kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena napenda kukushukuru wewe binafsi na Ofisi yako, Waheshimiwa Wabunge na hasa wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Katibu wa Bunge Ndugu Kipenka Mussa, Katibu wa Kamati hii Bibi Justina Shauri, kwa kuwezesha kukamilika kwa zoezi la kuchambua mpango na makadirio ya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2003/04 kwa ufanisi na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu sasa naomba kuwasilisha na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2003/2004 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43 (5) (b) (c) toleo la 2003.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuingia katika Bunge la Tanzania kama Mbunge. Ninawashukuru sana wenzangu katika Chama Cha Wananchi *(CUF)* kwa kunisimamisha kama mgombea wao wa Kiti cha Ubunge Jimbo la Ole na nawashukuru na kuwapongeza sana wapiga kura wa Jimbo hilo kwa kunitwisha kura nyingi kabisa na kwa hali hiyo kuwabwaga wenzetu wa CCM na wengineo kwa kishindo kikubwa. Nawapongeza waheshimiwa wenzangu kutoka *CUF* kwa kuzoa kura kibao na kupata ushindi mkubwa katika Majimbo yao. Pia nachukua nafasi hii kuwapongeza Wabunge wa CCM walioshinda katika Majimbo katika uchaguzi mdogo wa hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nawashukuru wenzangu katika Kambi ya Serikali mbadala kwa kunipa utumishi katika nafasi ya Waziri mbadala au Waziri anayesubiri katika Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Pia namshukuru Profesa Mark Mwandosya kwa kunipatia kitabu chake cha hotuba yake hivi leo Ijumaa tarehe 4 Julai, 2003, mwendo wa saa 3.15 asubuhi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, maisha ya kisasa hayawezekani bila ya kusaidiwa na mawasiliano na uchukuzi. Uchumi wa kisasa unahitaji bidhaa kuhamishwa kutoka kwa aliyezizalisha kwa ziada kwenda kwa anayezihitaji au zinakohitajika na anao upungufu utakaokidhiwa na bidhaa hizo kwa wakati sahihi, hali njema na bei sahihi. Upashanaji habari wa kisasa ni ule unaozingatia uharaka, usahihi na pia sababu za kiuchumi.

Sasa hivi gumzo kubwa duniani ni upashanaji habari. Shinikizo dhidi ya vijiuchumi tegemezi vya nchi zetu changa linalofanywa na wakubwa wa dunia chini ya uongozi wa Marekani hasahasa kwa kutumia aina mpya ya ukoloni na ubeberu uitwao utandawazi.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi duniani kinachozungumziwa ni *Connectivity and interactivity* yaani ni kwa vipi mtu ataunganishwa na mifumo ya kisasa ya kimawasiliano na kihabari na ni kwa vipi mtu anaingiliana na kubadilishana habari na wengine, kwa uharaka na ufanisi wa hali ya juu. Teknolojia za habari na mawasiliano ni muhimu mno katika kuifanya dunia iwe kama kijiji kidogo yaani *global village.*

Mheshimiwa Spika, mifumo na mitandao bora ya uchukuzi kwa mfano reli, barabara, bandari, viwanja vya ndege, vituo vya mabasi na kadhalika pamoja na ubora wa vyombo husika kama magari, treni, ndege, meli na boti ni hitaji muhimu la kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa mitandao makini ya kimawasiliano na kihabari, kwa mfano simu za aina mbalimbali, mifumo ya posta, mifumo na mitandao ya Kimataifa ya mawasiliano ya kikompyuta, huduma za usafirishaji wa vipeto nje ya mfumo wa posta, huduma za redio, *Television* na magazeti ya aina mbalimbali ni kiungo muhimu mno katika ufanisi wa shughuli za uchumi wa kisasa, biashara za kisasa, uendeshaji Serikali wa kisasa na kwa ujumla maendeleo ya kisasa. Serikali iwe na mipango madhubuti ya kuhakikisha kuwa haya yote yanapatikana Vijijini na nchi zima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jambo lililo wazi kwamba bado Serikali inafanya juhudi za kubinafsisha *TRC.* Inasisitizwa tena kwamba pamoja na Serikali kung'ang'aniza ubinafsishaji wa *TRC* ni lazima tahadhari kubwa zichukuliwe, hasa kutokana na unyeti wa Shirika hilo kwa uchumi wa Taifa. Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC)* ni lazima iweke mbele maslahi ya Taifa na siyo kujichimbia kwenye mambo ya kiufundi tu. Ubinafsishaji wa *TRC* ni jambo zito kiuchumi na kisiasa na halitakiwi kukurupukiwa tu. Kwa mwaka 2002 mapato ya *TRC* yalikuwa shilingi bilioni 58.3 ikilinganishwa na shilingi bilioni 59.6 mwaka 2001, sawa na upungufu wa asilimia 2.1.

Mwaka 2002, Shirika la Reli lilisafirisha jumla ya abiria 684,799 ikilinganishwa na abiria 727,851 mwaka 2001, sawa na upungufu wa asilimia 5.9.

Mheshimiwa Spika, ubinafsishaji wa *TRC* utakuwa ni jambo linalozungumzika kama upo uhakika kwamba ubinafsishaji huo:-

(i) Utaleta injini mpya za kutosha na mabehewa ya kisasa.

(ii) Utaleta mifumo ya kisasa ya mawasiliano na uongozaji treni. *(Makofi)*

(iii) Utaleta mabadiliko makubwa katika njia zenyewe za reli kwa maana ya kuziboresha au hata kujenga reli mpya. *(Makofi)*

(iv) Utaongeza idadi ya abiria wanaosafirishwa na mizigo itakayosafirishwa. *(Makofi)*

(v) Utaongeza morali ya kazi ya wafanyakazi kutokana na mafunzo bora na vipato safi na utafutilia mbali ajali nyingi za kizembe zinazoikabili *TRC* sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, ubinafsishaji wa kiholela unaoambatana na kupunguza wafanyakazi wengi na bila ya kupata mafao stahili na kwa wakati, husababisha manung'uniko yasiyoisha, hasira, na hata vitendo vya hujuma. Serikali ituambie inabinafsisha *TRC* au huduma au vyote? Maana Watanzania wangependa wabaki na *TRC* kama mali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado ubinafsishaji wa *TTCL* unaonekana kuzua maswali mengi kuliko majibu yanayopatikana. Wananchi wengi hawapingi ubinafsishaji wa Shirika hilo muhimu ila wanaamini ubinafsishaji huo haujakaa kisawasawa na una dalili za kupuuza maslahi ya msingi ya Taifa, na pia kumdekeza mno mwekezaji husika. Serikali inawajibika kutoa maelezo ya kina kuhusu namna maslahi ya kiuchumi ya Taifa yanavyolindwa katika ubinafsishaji huo. Mambo ndani ya *TTCL* yasifunikwe na maelezo ya kijuujuu tu. Wananchi wanayo haki ya kujua kile hasa kilicho ndani kabisa ya ubinafsishaji huo, ambacho kinalinda na kunenepesha maslahi ya kiuchumi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwaka 2002, kwa upande wa simu wa *TTCL,* idadi ya simu kwa kila watu 1000 ilikuwa 0.51, na ukijumlisha mchango wa Kampuni nyingine za simu za mikononi, *teledensity* au idadi ya wenye huduma ya simu kwa kila watu 1000, sasa ndiyo imefikia 1.3. Hali ya mawasiliano ya simu bado ni ya chini sana kwa nchi nzima, lakini hali ni mbaya zaidi katika maeneo ya vijijini. *TTCL* lazima iwe tayari kufanya uwekezaji mkubwa na wa kisasa katika mawasiliano ya simu vijijini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na unyeti wa sekta ya simu kwa uchumi na usalama wa Taifa, ni busara kuhakikisha hao wanaodaiwa kuwa ni wawekezaji mahiri katika *TTCL* wakadhibitiwa kwa umakini wa hali ya juu. Isiwe kila wanaloamua na kwa namna wanavyoamua, na katika wakati walivyoamua ndiyo inakuwa hivyo hivyo tu. Ni lazima wenye nchi yao wajue muda wote kinachoendelea ndani ya *TTCL* na siyo kuburutwa tu na ngoma ya mdundiko ya uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kurahisisha mawasiliano siyo tu ni muhimu kwa maisha ya jamii, bali pia huchangia uchumi wa Taifa. Usajili wa simu za mkononi umetusaidia sana kuboresha mawasiliano hapa nchini. Lakini jambo la kushangaza ni kuwa baadhi ya Kampuni zinafanya kazi katika sehemu kubwa ya nchi na nyingine zimebanwa sehemu moja tu.

Mheshimiwa Spika, tunategemea Mheshimiwa Waziri wakati atakapofanya majumuisho atatupatia sababu za msingi ni kwa nini Kampuni ya *ZANTEL* inafanya shughuli zake kule Zanzibar tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufikia mwezi Desemba 2002, *ATC* ilikuwa imebinafsishwa kwa kuunda ubia na *SAA* ya Afrika ya Kusini na kuanza kuitwa *Air Tanzania Company Limited (ATCL).* Inashauriwa Serikali isiziachie hisa zake katika *ATCL* zinazofikia asilimia 51. Bado ipo hatari ya kuiweka kila Taasisi nyeti kiuchumi na kimikakati kwenye mikono ya wageni, hata kama ni kwa hiyo asilimia 49. Hisa za Serikali katika Mashirika nyeti yanayobinafsishwa ni muhimu ziendelee kuwepo na kulindwa kwa sababu kubwa ya kulinda maslahi ya Taifa.

Bado Watanzania tunajiuliza kwamba pamoja na kuwa na hisa nyingi kuliko *SAA* iweje sasa wawe na mamlaka makubwa kiasi cha kuondosha Nembo ya Taifa la Tanzania na kuweka chini, Bendera na Twiga kama alama ya nchi yetu na Nembo ya kwao kuwekwa juu. Hii ni kulidhalilisha Taifa. Kwa hiyo, tunaomba maelezo ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia Wakala wa Ndege za Serikali *(TGF)* ndege za Serikali zimekuwa zikifanya safari kibiashara mpaka nje ya nchi. Si jambo baya ndege hizo kufanya shughuli zake kibiashara, lakini zipo kila sababu za Watanzania kutaka zoezi hilo liendeshwe kwa tahadhari ya hali ya juu. *Air Tanzania Corporation* pamoja na kuwa na malengo ya kibiashara tangu mwanzo, imeishia kubinafsishwa baada ya utendaji ulioambatana na matatizo mengi, ikiwa ni pamoja na hasara kubwa. Watanzania wangelipenda kujua ni kwa vipi Wakala wa Ndege za Serikali *(TGF)* atafanya safari zake kibiashara na kwa faida, mahali ambapo hata Mashirika ya Umma ya siku hizo kama *ATC* yaliishia kupata hasara.

Mheshimiwa Spika, bado wananchi wa Tanzania wanataka kujua suala la ununuzi wa ndege rasmi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limefikia hatua ipi baada ya kudokezwa wakati fulani huko nyuma. Tatizo si kama ndege inunuliwe au isinunuliwe, na ni wazi kwamba shughuli za Rais wetu zinahitaji matumizi ya ndege nzuri ya kawaida. Tatizo kama ukarabati wa Ikulu Dar es Salaam na ujenzi wa ukuta mzito na mkubwa kuzunguka Ikulu, ni tabia ya Serikali yetu ya kujiingiza katika vitu vinavyonunuliwa kwa mabilioni mengi ya fedha za Watanzania, kama vile Watanzania hawana matatizo mengine ya kuyashughulikia, kwa mfano afya ya msingi na elimu ya msingi. Ndege inaweza kununuliwa lakini basi angalau ifananefanane na umaskini uliokithiri wa Watanzania. Ni lazima iwe ni ndege ya kawaida inayoweza kutumiwa na kiongozi wa watu maskini na asiyetaka makuu wala ufahari. Serikali isinunue ndege ambayo inawakera hata wale wote wanaotoa misaada kuisaidia Tanzania ijitegemee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mrundikano mkubwa wa magari yasiyo salama katika miji mingi ya Tanzania, hasa ile mikubwa, yanayofanya biashara ya kubeba abiria, na hasa *mini-buses* na hata *micro-buses.* Pamoja na kujaza watu kupita kiasi, mabasi hayo, na hasa yale yanayoitwa vipanya, hukiuka kanuni za usalama barabarani mara kadhaa na hayana matengenezo ya kutosha. Yafuatayo yanapendekezwa kuhusu namna ya kuboresha usafiri mijini:-

(a) Kuwe na mabasi ya aina maalum na yenye sifa maalum kwa ajili ya matumizi ya mijini na yanayomhakikishia abiria usalama na utulivu;

(b) Magari mabovu na yote yaliyochakaa yaondolewe katika barabara za mijini haraka iwezekanavyo;

(c) Askari wa usalama barabarani wawajibike kufanya kazi yao kama inavyotakiwa iwe. Rushwa miongoni mwa Askari Polisi walioko barabarani zinamaliza maisha ya Watanzania, kwa kudekeza madreva wazembe na kuchochea ajali; na

(d) Utoaji wa leseni za udreva ufanywe kiumakini sana na mamlaka husika zijiepushe na tatizo sugu la rushwa katika utoaji wa leseni. Utaratibu wa kuziwajibisha mamlaka za leseni zinazonuka rushwa ni lazima uanzishwe na uwe wazi.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa mabasi ya Mikoani unatumiwa na Watanzania wengi kwa sasa. Serikali iimarishe usafiri huo kwa manufaa ya Watanzania wengi kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Ihakikishe mabodi ya mabasi yamejengwa kwa kufuata viwango vinavyokubalika Kitaifa na Kimataifa;

(b) Ihakikihe mabasi yote yapo katika hali bora kiufundi kuweza kufanya safari za mbali;

(c) Ihakikishe hakuna abiria wanaozidi katika uwezo wa basi unaotambulika rasmi;

(d) Ihakikishe mabasi hayazidishi uzito wa mizigo unaokubalika kisheria. Sasa hivi mabasi mengi yamekuwa malori ya mizigo ya kimyakimya na yanabeba mizigo kupita kiasi;

(e) Ihakikishe mabasi yanazingatia kanuni za mwendo salama ili kulinda maisha ya abiria na watumiaji wengine wa barabara; na

(f) Ihakikishe leseni zinazoruhusu mtu kuendesha basi la abiria hazipatikani kirahisi na zisiwakute wasio na sifa sahihi. Leseni hizo ziwe na masharti maalum ili kupata madereva bora badala ya bora madreva.

Mheshimiwa Spika, ni matazamio ya kila Mtanzania kwamba baada ya lile janga baya la *MV Bukoba* kule Ziwa Victoria, sasa Serikali iko makini na matengenezo pia ukaguzi wa mara kwa mara wa vyombo vya majini. Watanzania hawapo tayari kusikia janga jingine linalofanana na lile la *MV Bukoba* na litakalotokana na uzembe wa ukaguzi na matengenezo ya mara kwa mara ya vifaa mbalimbali na vyombo mbalimbali vya majini. Watanzania wote wamechoshwa na majanga yenye asili ya uzembe wa watendaji katika maeneo husika. Serikali bado inazo dalili za kuzembea katika suala zima la *maintenance* ya vitu vyenye mwelekeo wa kimitambo, na ndiyo maana juzi juzi tu Taifa lilijikuta katika janga baya la ajali ya treni mkoani Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kiufundi, huwa upo uwezekano wa chombo kilichozama majini, kwa mfano meli au boti, kuibuliwa na kufanyiwa matengenezo ambayo huweza kukirudisha chombo husika katika matumizi ya kiuchumi. Pamoja na matatizo mengi ya kisiasa na kiuchumi kwa sasa, Taifa la Russia chini ya Rais Putin limekwisha iibua nyambizi yake iitwayo *Kursk* iliyozama katika bahari ya *Barents* miaka michache iliyopita. Zipo kila sababu za Serikali na Shirika la Reli la Tanzania kufanya juhudi za kuiibua *MV Bukoba* ambayo kwanza mahali ilipozamia ni jirani sana na bandari ya Jiji kubwa la Mwanza, ili ifanyiwe matengenezo ya hali ya juu, na baadaye ipate kamisheni mpya na iendelee kutumika kwa faida ya uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, ukiondoa viwanja vya Kimataifa vya ndege vya Dar es Salaam na Kilimanjaro na ukiondoa viwanja vya Mwanza na Zanzibar, viwanja karibu vyote nchini havina taa maalum kwa ajili ya ndege kutua usiku, ikiwa ni pamoja na uwanja wa ndege uliopo Manispaa ya Dodoma ambapo Serikali inashinda kila siku. Hata kama ni kwa awamu, ni jambo la busara kwa Serikali kuanza kuviboresha viwanja vya ndege Mikoani, ili hata penye mazingira ya dharura ndege zitue usiku na pia Serikali ipate mapato zaidi. Uwanja wa ndege wa Dodoma umeanza kuwa na shughuli na harakati nyingi za Kitaifa na Kimataifa, na sasa ni wakati muafaka wa kufikiria namna ya kuuimarisha, ikiwa ni pamoja na kuuwekea taa.

Mheshimiwa Spika, kuwasiliana kwa kutumia simu za mikononi ni gharama kubwa sana katika Tanzania. Ni lazima sasa, ili kulinda maslahi ya mtu wa kawaida, kwa Serikali kutengeneza mazingira, kimakusudi kabisa, ambayo yatampunguza gharama za miito ya simu hizo kwa mteja wa hali ya kawaida kabisa. Simu si anasa katika karne ya 21 inayohitaji sana uhangaikaji na uchakarikaji kujitafutia maisha, simu ni hitaji la lazima. Serikali ipitie upya sera zake mbalimbali, kwa mfano kodi, na kadhalika kwa lengo la kuyaangalia upya Makampuni hayo, na hatimaye kupunguza makali kwa mwananchi wa kawaida.

Tunalipongeza Shirika la *Vodacom* kwa kupunguza gharama kwa wateja wake, tunayataka Mashirika mengine yafanye hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kubinafsisha vitengo fulani fulani vya Mamlaka ya Bandari Tanzania *(THA),* bado yapo matukio mengi ya wizi katika bandari ya Dar es Salaam, na hasa wizi wa vifaa kama redio na kadhalika kutoka kwenye magari yanayoingizwa nchini. Kwa miaka mingi sasa wizi huo umeendelea kushamiri kama vile bandari hiyo haina mwenyewe, na Serikali haipo. Wizi bandarini unawavunja moyo wawekezaji wa ndani na wa nje na ni lazima sasa ukomeshwe kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu *TAZARA* inakabiliwa na uhaba wa fedha za uendeshaji kutokana na upungufu wa mizigo, kutokana na kutokuwepo mzigo wa kutosha wa shaba kutoka Zambia, pamoja na ushindani wa njia nyingine za usafiri, hasa baada ya Afrika ya Kusini kulazimika kuachana na sera za ubaguzi wa rangi, ni lazima sasa *TAZARA* yenyewe, na pia Serikali za Tanzania na Zambia zibuni na kutafuta njia mbadala za kuhakikisha reli ya *TAZARA* inaendelea kuwa ni mradi wa kiuchumi badala ya mradi wa kisiasa na kialama *(symbolical)* tu.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya njia mbadala zinazopendekezwa ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha shughuli za uzalishaji wa kilimo na mali za misitu katika maeneo ya Ifakara, Makambako, Njombe, na kadhalika;

(ii) Kukifufua kwa haraka kiwanda kikubwa cha karatasi kule Mgololo - Mufindi, Iringa;

(iii) Kuendeleza mradi wa Chuma wa Liganga kule maeneo ya Madaba, Njombe kuelekea Songea;

(iv) Kuimarisha mradi wa Makaa ya Mawe kule Kiteweka - Mchuchuma; na

(v) Kuimarisha kilimo cha mazao ya chakula mkoani Mbeya.

Hayo yote yamependekezwa kwa upande wa Tanzania tu, yako mambo mengi yanayoweza yakafanywa na Zambia, ikiwa ni pamoja na kuangalia upya sera yake nzima ya kuacha kupitishia bidhaa zake nyingi kwenye bandari ya Afrika ya Kusini na wakati fulani Msumbiji. Kwa lengo la kupunguza msongamano wa magari Jijini Dar es Salaam ambao unasababisha ajali nyingi, unapoteza muda, unachangia sana kuchafuka kwa hewa na unaongeza kelele na kero, inashauriwa Wizara isaidiane na *think tanks* kama Chuo cha Usafirishaji *(NIT)* na Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi cha Dar es Salaam pia Wizara ya Ujenzi ili yafuatayo yafanyiwe kazi:-

(a) Uwezekano wa kuwa na reli za mijini na pia treni za mijini;

(b) Uwezekano wa kutumia usafiri wa boti au meli kwa shughuli za Jijini;

(c) Kupanua zaidi barabara;

(d) Kuanzisha barabara mpya kabisa;

(e) Kuwa na barabara zipitazo juu *(fly overs)* kwenye angalau makutano ya barabara kubwa;

(f) Kuyaondoa kabisa barabarani magari kuukuu sana na yanayozimikazimika ovyo; na

(g) Kuwa na sera za makusudi za kupunguza idadi ya magari ya aina fulani kwa malengo maalum.

Mheshimiwa Spika, wawekezaji watamiminika Tanzania bila ya gharama kubwa ya kupiga debe kama sekta nzima ya mawasiliano na uchukuzi itaboreshwa na kuendelezwa.

Mheshimiwa Spika, dunia ya sasa ni biashara na uwekezaji ndani ya sheria zinazoongozwa na utandawazi. Yote hayo yanategemea mno maendeleo ya kimawasiliano na kihabari na ndiyo maana sasa dunia inazungumzia *electronic commerce electronic business, electronic governments, electronic administration* na siyo hayo tu bali hata *electronic democracy.* Dawa ni kushiriki katika dunia ya kuwasiliana na kuhabarishana kielektroniki na siyo kujitenga.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza mjadala nikumbushe tu kwamba hii Wizara imepangiwa siku moja sawa na Wizara nyingine nyingi zitakazofuata baadaye. Kwa hiyo, mjadala ukiisha saa saba tu watakuwa wamesema wachache mno. Kwa hiyo, kwenye Wizara hizi zenye siku moja tu, tutaendelea na mjadala jioni mpaka labda kwenye saa 12.00 hivi. Halafu ndiyo wenye kujibu hoja wanashika nafasi yao. Baada ya maelezo hayo sasa namwita Mheshimiwa Ismail Iwvata.

**MHE. ISMAIL J.R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya awali ili niweze kuchangia katika hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi. Kwa sababu na mimi ni mara yangu ya kwanza kuzungumza naomba niungane na wenzangu waliotangulia kwanza kwa kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioweza kuchaguliwa katika chaguzi ndogo za hivi karibuni. Nawapongeza sana na tunawakaribisha Bungeni pamoja na michango yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuendelea naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, watumishi wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi pamoja na watumishi wa Mashirika yote yaliyo chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili nisije nikajikuta nimesahau au nimepitiwa basi naomba nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitazungumzia mambo mengi, mimi nitazungumzia kitu kimoja tu katika hotuba yangu. Lakini kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa *commitment* ambayo Wizara imeweka kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja cha ndege pale Singida. Kitu ambacho kitafanya na sisi katika Mkoa wetu wa Singida tuweze kuwa na huduma ya usafiri wa ndege kitu ambacho kilikuwa hakipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa hatua ya kuimarisha reli ya Singida, Manyoni itasaidia kufanya abiria wetu waweze kusafiri kwa uhakika zaidi na bila ya wasiwasi. Kwa hiyo tunamtakia kila la kheri katika kuweza kufanikisha mambo yake.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mimi sikusudii kuzungumzia mambo mengi. Lakini kubwa ambalo wapiga kura wangu hususan katika Jimbo la Manyoni

Magharibi wamenituma nizungumze katika Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kuhusu suala la mawasiliano ya simu katika Mji wa Itigi. Mji wa Itigi kwa walio wengi na ambao pengine hawasafiri safiri sana Mikoani wanaweza wakawa wanajiuliza huyu bwana anazungumzia habari ya kijiji, kweli ni mji wa kijijini. Lakini ni mji mdogo ingawa bahati mbaya haupo katika orodha ya Miji midogo ambayo imetangazwa hivi karibuni na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa alipokuwa anajaribu kutoa vigezo vya sehemu ili uwe Mji mdogo alijaribu kutoa vigezo. Kimojawapo alichotoa ilikuwa ni idadi ya watu, kwa kweli pale Itigi idadi ya watu ipo ya kutosha tu. Akazungumzia kigezo kingine kwamba lazima kuwe na huduma za jamii na pale huduma za jamii tunazo. Kwanza, tuna shule za msingi 3 na hizo shule za msingi ninazozizungumzia ni za pale pale mji katika umbali wa *radius* ya kilomita 2 na kuna shule ya msingi nyingine tena tunaijenga ya nne.

Lakini vilevile tuna shule ya sekondari. Lakini vilevile tuna kituo cha Afya kiko pale, sizungumzii huduma nyingine zilizo katika vijiji vingine ambavyo kwa pamoja na Itigi vinafanya Kata, mimi nazungumzia kwa Itigi peke yake. Tuna hospitali ya *Mission* inaitwa *St. Gasper Hospital* na hii hospitali ni ya kawaida. Lakini kwa walio wengi wanaitumia kama ni hospitali ya rufaa, kuna watu wanatoka Mpanda, Mkoa Rukwa, watu wanatoka Tabora, watu wanatoka Kigoma na watu wanatoka Shinyanga wengi wanakuja kutibiwa pale na hiyo hospitali ina vitanda karibu 150 vya kulaza wagonjwa, na hivi sasa wanajenga wodi ya kulaza watoto kama 200.

Kwa hiyo, unaweza ukaona ni hospitali kubwa na hao watu wanaokuja kwa ajili ya kutibiwa pale mara nyingi wanahitaji kufanya mawasiliano na ndugu zao.

Mheshimiwa Spika, lakini si hivyo tu, kigezo kingine alisema kwamba ni lazima kuwe na njia zinazokutana pale. Njia moja tuna reli ya kati inayotoka Dar es Salaam inapitia pale Itigi kwenda mpaka Tabora, kwenda mpaka Kigoma na mpaka kwenda Mwanza. Lakini vilevile tuna barabara ya kutoka Arusha-Babati-Singida-Itigi-Rungwa mpaka Mbeya, na tuna barabara ya kutoka Manyoni-Itigi-Tabora na kila siku kuna basi la kutoka Tabora kuja Dodoma na kutoka Dodoma kwenda Tabora.

Kwa hiyo, unaweza ukaona ni mahali pa namna gani jinsi palivyo. Lakini si hivyo tu, tuna kiwanja cha ndege kizuri sana na hiki kiwanja siyo cha mapambo maana yake katika viwanja vya ndege vilivyopo katika miji mingi ya Wilaya unakuta vinakaa tu havitumiki. Kile kiwanja kinatumika na mara nyingi kinatumiwa na *flying Doctors* kutoka *KCMC,* Moshi kuja kutibu wagonjwa wale waliolazwa katika hospitali ya *St. Gasper.* Kwa hiyo, ni mahali ambapo panahitaji mawasiliano.

Lakini vile vile tuna *station* kubwa tu inayounganisha wasafiri wanaosafiri katika hii reli ya kati kwenda kama sehemu za Singida na mahali pengine. Lakini vile vile tuna kituo cha polisi. Kwa shughuli za uchumi tuna shughuli za kilimo na mifugo pale wananchi wake ni wafugaji wengi tu. Lakini si hivyo tu, kuna machimbo ya *gypsum* ambayo *gypsum* yake ndiyo inayotumika katika Kiwanda cha Saruji cha *Wazo Hill* na

wakati sisi Kamati yetu tulivyotembelea *Wazo Hill* walisema kwamba wao *Gypsum* yao wameamua wawe wanaichukua toka Itigi na haiendi *Wazo Hill* tu, hata watu wa Rwanda pia wanakuja kuchukua *Gypsum* kutoka pale Itigi.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile tuna kiwanda cha kutengeneza chaki kipo pale. Watu wengine mnahangaika kwenda kutafuta chaki Dar es Salaam pengine mnakwenda kununua chaki ambazo zimetoka Itigi - Dar es Salaam.

Sasa mimi ningetoa wito kwa majirani zetu wa kutoka Mbeya, Tabora, Shinyanga, Kigoma badala ya kufanya masafa marefu kwenda kufuata chaki Dar es Salaam waje pale Itigi watapata chaki nzuri tu. Kwa maelezo haya ya shughuli za kiuchumi nafikiri Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi atakubaliana na mimi kwamba tunahitaji kupatiwa huduma bora za simu.

Hivi sasa tuna *exchange* ama *switch board* yenye njia mbili tu, na hivi juzi nilipokuwa napiga simu niliambiwa njia moja haifanyi kazi. Sasa unaweza ukafikiria kwa shughuli kama hizi nilizozitaja kwa njia moja tunawasiliana namna gani. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri atufikirie kutuweka Mtambo wa kisasa wa simu wenye kuweza kuwa na mawasiliano mazuri.

Mheshimiwa Spika, mimi sina wasiwasi na Mheshimiwa Waziri kwa sababu Wilayani pale Manyoni tuliwahi kuahidiwa mtambo wa kisasa kutoka India ulikuja lakini ukawa na matatizo. Alipokuja Mheshimiwa Waziri mwezi Januari 2001 alisema hilo tatizo mimi nitalimaliza na kweli akalimaliza. Mtambo ukaanza kufanya kazi, bahati mbaya ukapigwa radi mwezi Desemba. Akasema hakuna wasiwasi tutawapatia mtambo mwingine na huo mtambo mwingine umeishakuja hivi sasa unafanya kazi. Ukitaka kufanya mawasiliano Manyoni unagusa tu mambo yanakuwa mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa naomba kwa huu Mji wa Itigi basi watufikirie. Watu wa *Celtel* wako tayari kutuletea huduma ya simu za mkononi, lakini kikwazo hakuna link ya *TTCL.* Sasa Mheshimiwa Waziri naomba tu nikuarifu kwamba watu wa *Roman Catholic Mission* ambao ndiyo wamiliki wa hiyo hospitali wako tayari kujenga mnara wenye urefu wa mita 60 kwenda juu.

Mheshimiwa Spika, ssa kwa mchango huo nakuomba basi Mheshimiwa Waziri na watumishi wako wote ambao najua ni wachapakazi wazuri tu, na nafikiri kwa maelezo haya nafikiri wamekwishakuwa na huruma ya kutufikiria kutuwekea mawasiliano mazuri. Hebu angalia basi uwezekano wa kutuwekea hiyo link ikiwezekana tuanze kupata huduma.

Mheshimiwa Spika, haya mambo ya Ubunge na wakati mwingine hasa mkiwa Waheshimiwa Wabunge wawili ndani ya Wilaya moja, kuna tabia ya kulinganisha mbona wenzetu huku wanapata hii huduma, sisi mbona hatupati. Wanaweza wakadhani kwamba labda Mheshimiwa Mbunge mwingine hafanyi kazi, lakini kumbe hapana, wakati mwingine ni matatizo ya kiuchumi ndiyo yanayofanya hizi shughuli zisiende.

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi nakumbuka alipokuja pale Manyoni mwezi Januari, 2001, alisema Wilaya ya Manyoni ina Waheshimiwa Wabunge wawili, lakini akasema naye anajiunga kuwa Mbunge wa tatu.

Naomba asisahau hiyo ahadi yake ya kuwa Mheshimiwa Mbunge wa tatu, anajua ni sababu gani yeye ni Mheshimiwa Mbunge wa tatu. Ni kwa sababu mzee wake aliwahi kuwa *Post Master* pale Manyoni. Naomba aendelee kutimiza hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Itigi tulishaahidiwa hii ahadi ipo na naamini itatekelezwa. Lakini sasa tatizo inasemekana huyu mwekezaji aliyechukua hii Kampuni ya Simu uwezo wake kifedha unaonekana ni mdogo na ndiyo maana hata ile ahadi yake ya kujenga njia 800,000 hajaitimiza na hata wenzangu nafikiri wa Kamati ya Miundombinu wamezungumza hapa kwamba kwa kutotimiza ahadi yake amepigwa faini na faini, faini yenyewe hajailipa.

Mheshimiwa Spika, sasa hii ni dalili tosha ya kuonyesha kwamba huyu mwekezaji inaonekana uwezo wake ni mdogo na masharti ya mwekezaji ni kwamba anatakiwa awe na mtaji, awe na teknolojia na awe na ujuzi.

Sasa katika hali kama hii si inatia mashaka kwamba huyu mtu uwezo wake ni mdogo. Sasa sijui Wizara inafanya nini kuona kwamba huyu mtu anatimiza haya masharti ili aweze kupewa hii Kampuni kamilifu.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naomba nikushukuru. Lakini nimwombe Mheshimiwa Waziri afikirie maombi yetu ya kutoboreshea mawasiliano katika Mji wa Itigi.

Baada ya kusema hayo, naomba nirudie kusema kwamba naunga mkono hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuiunga mkono hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa asilimia mia moja na kwa kweli naipongeza sana.

Mheshimiwa Spika, sina sababu hata moja kuibugudhi hotuba hii, kwa sababu mwaka jana Mheshimiwa Waziri mengi aliyoyaeleza katika kitabu chake cha hotuba na vile vile katika majumuisho yake mengi yametekelezwa katika Wizara yake. Kwa hiyo, mimi nitakachokisema nitaboresha baadhi ya sehemu tu. *(Makofi)*

Moja kwa moja niombe tu Mheshimiwa Waziri, anisaidie labda kuboresha kwa mwaka huu yale ambayo ameyasahau. Mheshimiwa Waziri, pamoja na watendaji wake wote, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, watendaji wa Wizara nawapongeza kwa kazi nzuri waliyoifanya kipindi chote cha mwaka jana hadi kufikia leo hii. Mimi naamini wewe upeo wako ni wa juu kabisa. Mwaka jana Wizara hii uliipangia tarehe 5 kutoa hotuba yake na ili itimize mwaka mmoja kamili, ni leo tarehe 4, kwa hiyo, leo ni siku yao ya kuzaliwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, ukweli ni wacheshi, wachangamfu, wachapakazi wapole na mwisho kabisa wana ushirikiano mzuri sana na sisi sote hapa Bungeni. *(Makofi)*

Lakini kabla ya kuendelea na mchango wangu, Msemaji Mkuu wa Upande wa Upinzani anayehusika na Wizara hii, kama alishangazwa kupata kitabu leo saa 3.15, mimi simsaidii Mheshimiwa Waziri, lakini ninachokiamini, Kamati zetu za Kudumu Bungeni tunapokutana Dar es Salaam, Mawaziri wote wanatoa rasimu yao ya hotuba ambayo wangelitoa hivi sasa. Hata kama amepata saa 3.15, mimi nasema amepata mapema sana. Kwa sababu hata sisi Kamati zetu tunapewa wakati ule vinapogawiwa humu ndani. Sasa napenda tu kwa sababu mimi naamini kwamba ni mgeni, nitoe taaluma hii ili asiwe na wasi wasi kwamba labda ameonewa kwa sababu ni Mpinzani, hakuna anayebughudhiwa hapa Bungeni hata mmoja.

Mheshimiwa Spika, sasa ninasema kwamba, jana niliporejea kutoka Bungeni hapa, nilipata simu kutoka Wilaya ya Kati, Jimbo la Koani, ambako ndio Jimbo langu la Uchaguzi. Nilichopigiwa simu ni kwamba baadhi ya mambo ambayo mwaka jana Mheshimiwa Waziri ukweli aliyasimamia kikamilifu kutokana na matatizo ya simu zile ambazo ziko Mwera za *Wireless Local Loop*. Mimi nashukuru sana mara tu baada ya Bajeti kumalizika, inaonyesha Mheshimiwa Waziri, alitoa agizo kwa mambo mawili. Moja la kuzimika simu isifanye kazi *soon* baada ya umeme kuzimika basi simu zilikuwa hazifanyi kazi. Kwa utaratibu wa simu za *Wireless Local Loop,* inachukua saa 6 mpaka 8 baada ya kuzimika umeme zinakuwa zinafanya kazi. Lakini naona kwa mujibu wa taarifa niliyoipata jana, mwezi mzima huu uliopita matatizo yale yamerudia tena. Ningelimwomba Mheshimiwa Waziri, atumie busara yake ambayo ameitumia mwaka jana kuona matatizo yale yako wapi, kwa sababu naona siku hizi nimeambiwa kwamba ukizimika tu umeme na simu zile zote hazifanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri wiki moja iliyopita unajua sisi tukiwa hapa Bungeni kama unavyojua, wengi wetu tunakuja peke yetu. Sasa usingizi hatupati mpaka tupige simu majumbani mwetu kule tunakotoka jimboni. Sasa cha kusikitisha wiki moja iliyopita uliniruka usingizi saa 8 za usiku nikaamka kutaka kumpigia na kuzungumza na Mama Ngina kule simu haifanyi kazi, kumbe vile umeme ulikuwa umezimika. Sasa ningemwomba Mheshimiwa Waziri, atuonee huruma tuko wapweke hapa Bungeni. Kwa hiyo, tunapotaka kuwasiliana na kina Mama Ngina kule kila mmoja tuweze kuwasiliana nao. *(Makofi)*

Lakini la pili kuhusu simu hizo vile vile ningeliomba nakumbuka nilizungumzia kutokana na utoaji wa bili za simu za huo mtambo wa *Wireless Local Loop* za Mwera. Walikuwa na utaratibu ambao niliueleza mwaka jana na Mheshimiwa Waziri inaonyesha vile vile alitoa agizo lile ikawa bili tunaletewa katika mikoa yetu inayohusika. Lakini cha kusikitisha ni kwamba, walifanya agizo lile, wakatimiza yale na *collection* ya wenye mapato wakawa wanapata vizuri kabisa. Lakini utaratibu ule kuanzia mwezi Januari ni kwamba, umekoma na haufanywi tena. Wanatakiwa watu wakitoka Makunduchi kwa Mheshimiwa Abdisalaam kule, wanaotoka Chwaka kwa Mheshimiwa Yahya, wanaotoka Jimbo la Uzini kwa Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, wanaotoka Koani kwa Haroub Said Masoud, waende mjini wakakae foleni kusubiri bili zao. Mimi ningelimwomba Mheshimiwa Waziri, vile vile na hili alisimamie kwa mara nyingine tena.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi nitazungumzia suala la *ZANTEL.* Nashukuru sana mwaka jana wakati nilikuwa nikichangia suala la *ZANTEL* nilizungumza na ukweli nilizungumza kwa uchungu kabisa. Lakini kutokana na hatua mbalimbali ambazo Mheshimiwa Waziri, amechukua, mimi nasema safari hii naomba tu anisaidie pale alipofikia kutokana na agizo lake alilolitoa mwaka jana. Baada ya kuchangia cha kufurahisha Mheshimiwa Waziri na napenda kunukuu yale mambo ambayo ukweli alikuwa akinijibu mimi pamoja na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, waliochangia kuhusu habari ya *ZANTEL* na hapa awali ya kunukuu. Nukuu ile katika majumuisho yake Mheshimiwa Waziri alisema hivi: "Mheshimiwa Mwenyekiti, *ZANTEL* naomba kwa haraka tu niseme tarehe 25 Juni, 2002 *ZANTEL, TTCL, TTC* na Tume ya Mawasiliano, walikutana chini ya Uenyekiti wangu tulizungumza hili suala kwa kina sana. Tulichobaini kuwa wao *ZANTEL* wanasema hawana tatizo na *TTCL* kuwa na ukiritimba. Kwa sababu Ukiritimba hauhusu Zanzibar, ukiritimba wa *TTCL* ni huku lakini sio Zanzibar. Halafu Zanzibar ina leseni ya kuja upande huu wa Muungano, inayo haijanyimwa isipokuwa sasa kutokana na ukiritimba wa *TTCL,* upande huu, basi inabidi wakubaliane namna ya kuendesha biashara ndio hili tu".

"Mimi nakubaliana nalo kabisa kwa sababu waliambiwa kwanza waweke mtambo wao mwingine Dar es Salaam hapana, Mheshimiwa Waziri anasema kwa kweli ni gharama sana ni kama kurudia rudia. Sasa tunajaribu kupata ufumbuzi wa kiufundi kuhusu hili suala la ukiritimba wa *TTCL* na nimeambiwa kwamba, inawezekana bila hata kuathiri makubaliano kati ya Serikali na *TTCL.* Tumeamua kwamba waendeleze mazungumzo ya Kibiashara ambayo yatalenga kuinufaisha *TTCL* na *ZANTEL* katika ile tunayoita *win win situation*. Kila mtu afaidike. Mazungumzo haya yatasimamiwa na Tume ya Mawasiliano na tumepeana miezi sita kufikia Desemba tuwe tumepata suluhu". *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na majumuisho haya mazuri Mheshimiwa Waziri, nina hakika bado alikuwa anayafuatilia masuala. Sasa mimi ningelimwomba tu bado kilio cha Wazanzibar ni kutokana na Kampuni hii ya *ZANTEL* kutopewa kibali cha kutoa huduma Bara. Nasema hayo kwa sababu simu za mkononi za Makampuni yote hayo hazilingani hata kidogo na urahisi wa huduma ambayo tunalipa *ZANTEL,* nina imani Makampuni hayo yanaogopwa na ndiyo maana yanafanya ukiritimba huo kwa sababu

ikiingia *ZANTEL* hapa Bara, naamini hakuna hata mmoja atakayekubali kujiunga na Kampuni yoyote kama si *ZANTEL*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, wengi walizungumza bei kubwa ya huduma za simu na vile vile lazima tumshukuru Mheshimiwa Waziri katika kila *function* ambayo alikuwa akifanya pamoja na Makampuni yote hayo, alikuwa akikemea sana bei za juu za huduma za simu za mkononi. Kwa hiyo, ningelimwomba tu Mheshimiwa Waziri, aendelee na juhudi yake hiyo ya kuyataka Makampuni kupunguza bei na vile vile kuiruhusu hii Kampuni ya *ZANTEL* ku-*operate* hapa Bara.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo labda tu nisaidie kwamba hilo hilo la simu za mkononi. Tuna Wizara hapa au Waziri mzima anayehusika na uondoaji au kupunguza umaskini nchini, nasema hilo ni suala zuri sana. Lakini nina imani kabisa hatua ya kuondosha umaskini katika nchi yetu utakuwa hatupigi hatua wala hatufikii kama wananchi wataendelea kulipa gharama kubwa za simu za mkononi. Tunajishuhudia sisi wenyewe Wabunge hapa kama ipo posho kidogo tunachopewa hapa kile cha kila wiki basi chote kinakwenda katika simu za *MOBITEL, VODACOM, CELTEL,* Majimboni kwetu tunarudi hoi bin taabani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nina imani Mheshimiwa Waziri, kwa ujasiri wake, mambo haya machache niliyozungumza na nazungumza kwa upole kabisa kama alivyokuwa mpole yeye na Naibu wake, naamini atayatekeleza. Lakini la mwisho kabisa kabla ya kuunga mkono ningeliomba baada ya Bunge hili, mimi sitaki kumhangaisha Mheshimiwa Waziri, kwanza yeye ni mkubwa, mtu mrefu, ningeliomba nipewe Naibu wake, nifuatane naye bega kwa bega mpaka Jimbo la Koani. Ahsanteni na naunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hilo unahitaji ruhusa ya Spika na haipatikani. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. FETEH SAAD MGENI:** Kwanza na mimi sina budi kukushukuru kwa kunipa nafasi hii nami nichangie machache katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, sina budi na mimi niungane na wenzangu hasa ilivyokuwa ni mara yangu katika Mkutano huu wa 12, ni mara yangu ya mwanzo kupata nafasi katika mwaka huu kuzungumza katika Bunge lako Tukufu, basi nami sina budi kwanza kuwapongeza ndugu zetu wote wale ambao walivuka kwenye Uchaguzi mdogo uliofanyika hivi karibuni. Lakini kwanza napenda kuwapongeza wale kutoka Chama Tawala cha CCM. Halafu pia naendelea kuwapongeza wale ndugu zangu kutoka Chama cha *CUF*. Nadhani sasa kazi yetu ni moja tu kushirikiana katika kuwatumikia wananchi wetu. Tumemaliza kazi zetu huko vijijini katika Majimbo yetu sasa kilichobakia kushikamana, kukamatana, kushirikiana, kuwatumikia wananchi na kuisaidia Serikali kama iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tuna timu yetu hapa ya *Bunge Sports Club,* tunapokuwa kule katika timu tunakuwa *as a one team*, tunashirikiana kufanya mazoezi na kupambana

na timu yoyote na tunaleta ushindi mzuri, ninyi wenyewe mmekubali katika mechi ya Mabalozi. Sasa mfumo huo huo ndio tunaotaka tushirikiane kwa Vyama vya Upinzani na Chama Tawala cha CCM tufanye kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nichukue nafasi ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri, yeye mwenyewe binafsi, Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wake, ambao kwa kazi nzuri kabisa waliyoifanya na kutuletea hapa na naamini tutaipitisha. Sasa ili nisije nikasahau huko mbele kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Bumbwini, tunaipongeza na kuipitisha moja kwa moja. Mimi nakubali kwamba, kweli Mheshimiwa Waziri, ni mfanyakazi bora, mfanyakazi hodari na kweli Rais aliposema kwamba hawa ni askari wake wa miavuli, basi nakubali kwamba ni askari kweli wa miavuli na mimi namwambia kwamba yeye ni kweli ni *Air Marshal* hasa.

Nasema hivyo kwa sababu katika Wizara hii moja, katika Wizara kubwa ni yake yeye Mheshimiwa Waziri. Wizara ambayo tunasema kwamba, imeenea kote. Asili ya kumwita *Air Marshal* ni kwamba, yeye ni mpiganaji wa anga, anga lote analo yeye. Yeye ni mpiganaji wa baharini, vyombo vyote anavyo yeye. Yeye ni *Field Marshal,* kwa sababu nchi kavu yote anayo yeye. Sasa kwa nini tusimsifu na kwa nini tusimpongeze. Ninachokiomba kwake Mheshimiwa Waziri, ni ushirikiano wake na ushirikiano na Bunge hili, pamoja na wananchi wote katika kuleta maendeleo na Mungu atakusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia kwa upande wa Bandari na Usafiri wa baharini. Nampongeza Waziri kwa kazi nzuri ambayo ametueleza hapa, juhudi zote zilizofanywa mpaka kupatikana mafanikio, kutatua matatizo mengi yaliyoko kule baharini. Baharini kuna matatizo na sisi watu tunaokaa visiwani ndio tuliokuwa tunajua vizuri zaidi. Tatizo la vyombo vyetu ambavyo vinatusaidia katika kutuvusha vingi vimeshakuwa vya muda mrefu, yaani vimeshachakaa na vyombo vya baharini vina utaratibu maalum kila miezi sita na kila mwaka lazima vipandishwe kwa ajili ya kuhakikishwa usalama na uzima wa vile vyombo.

Mheshimiwa Spika, vyombo vyetu vinachelewa kupandishwa na kufuata *route* yake iliyopangwa. Hiyo inaweza ikasababisha maafa kwa sababu kawaida ya chumvi inakula sana vyuma. Kadri unavyokitumia chombo baharini kile chombo kinaliwa na chumvi na kuna wadudu maalum ndani ya bahari wanatafuna kile chuma. Sasa ikiwa vyombo vyetu wataalam wetu hawa hawatakuwa wakali, kuhakikisha chombo hiki kimepandishwa muda fulani na kimefanyiwa *survey* na kinastahili kurejeshwa kwa ajili ya kuchukua abiria tena, basi kuna hatari na itakuwa jukumu hilo bado liko kwa upande wetu Serikali kama hatukusimamia hayo ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninachokiomba ni kwamba, juhudi hiyo iendelezwe. Kuna vyombo vingine havina vifaa kamilifu vya uokoaji wa maisha yaani *life gargets*, *life rings* na *life boats* hamna. Kama vimo havijafanyiwa *checking* kwa muda mrefu, siku wanapohitaji kukitumia inawezekana kikafeli. Sasa hilo namwomba Mheshimiwa Waziri na wataalam, wajitahidi sana katika kuliangalia.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii sitaki nizungumzie mengi, lakini naomba vile vile kumkumbusha Waziri kupitia kwako kwamba, sasa hali tumeshafika miaka 40. Miaka 40 kama ni mtu anaitwa mtu mzima aliyekuwa anaweza hata kuwa Rais wa Nchi. Hiyo ina maana kwamba nchi yetu imepiga hatua kubwa lakini bado kwa upande wa baharini hatujakuangalia sana. Sasa umefika wakati tuwe na vyombo maalum, tulivyojiandaa vya kwenda kuokoa maisha ya watu waliozama na vyombo vinavyozama baharini. Hatuwezi kubaki pale tunaomba kama chombo fulani kiko mahali fulani kinazama tunatafutana cha kwenda kupokelea hakuna. Lazima tuwe na *fast patrol boat* kwa ajili ya *rescue* tukawasaidie watu wetu. Inapigwa *SOS* huko tunaisikiliza hatuna la kufanya. Vyombo vilivyo jirani pengine hata visiende kuwaokoa wenziwao. Lakini bado kama katika *territorial water* yetu lazima sisi tuchukue jukumu la kwenda kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, lingine ninaloomba kumkumbusha Waziri kupitia kwako ni kwamba, hivi sasa kuna ujenzi wa ovyo ovyo ambao unajengwa katika mwambao mwa bahari. Huu unafanya maji ya bahari yasiweze kutembea mpaka pale ambapo yalitakiwa yafike katika fukwe zake. Kwa hiyo, utakuta yale maji yanatafuta mahali pengine pa kutoboa, lakini maji lazima yatachimba mahali pengine, hayawezi kuzuilika. Sasa tatizo ninaloliona kwa upande wangu ni kwamba, kama itakuwa *survey* yetu ya kuiangalia hali ya bahari yetu hasa kuifanyia *chart* katika kuiangalia hali ya bahari inavyokuwa na bahari inavyopungua, basi tutaweza kufanya makosa. Nayo ni kwamba, maboya yetu yale yanaweza yakaondoka katika *position* zake na yakiondoka katika *position* maana yake msafiri anayekuja pale na meli yake anajua mahali fulani pana boya lakini lile boya kumbe halipo lishakuwa *drifted.*

Mheshimiwa Spika, vile vile tuangalie hali ya minara. Nashukuru Mheshimiwa Waziri, kipindi kilichopita amenijibu vizuri tu kwamba, minara imeangaliwa na inachukuliwa juhudi ya kupakwa rangi na kutazamwa mataa ili yamsaidie msafiri aone ile *position* kwamba ndio na ni sahihi na kujua wapi anakoelekea. Kwa hiyo, naomba kuangalia hasa kufanyiwa *survey* katika bahati yetu. Bado tunazo *charts* za zamani na zinaweza kupotosha usafiri. Naomba sana.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuzungumzia hii hali ya *Meteorology,* watu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa. Nashukuru kwamba juhudi kubwa Mheshimiwa Waziri, ametueleza hapa imefanywa, zana za kisasa zimepatikana. Lakini pia naomba tuangalie kwa kutoa taarifa kwa vyombo vilivyomo baharini, hawa watu wa *Meteorology* wanayo haki ya kuweza kuviambia leo hali ya hewa iko kiasi fulani, kwa hiyo, wanataarifiwa watumia bahari leo kwa hali iliyoko wasitembee baharini. Utaratibu huo upo kwa nchi za wenzetu. Sasa tunaelezwa tu hali ya hewa ya mvua, mawingu, lakini hali ya hewa ya bahari na bahari yenyewe, wasafiri pia tunataka tuelezwe nayo. Naomba sana hilo.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumzie chuo chetu cha *DMI.* Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, juhudi aliyoifanya mpaka leo chuo chetu kinatambulika katika ulimwengu. Mimi nimefurahi na juhudi na hasa yule *Principal* wa Chuo ni mtu hodari. Ni mtu mfuatiliaji, ni mtenda kazi kwa hiyo, naomba tuwe pamoja katika kumsaidia ili afanikishe kazi zake. Kile ni chuo kinachowasaidia vijana wetu.

Chuo kile cha Ubaharia ni sehemu ya pili ya kuwapatia vijana wetu kazi na hasa kwa sisi watu wa Mwambao wa Baharini ndiyo maisha yenyewe tu katika bahari. Sasa Chuo kile kikifika hadi kutupwa kikawa kinasahauliwa tunajirudisha nyuma sisi badala ya kupeleka mbele chombo chetu na sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, katika chuo kile tunahitaji mpate vyombo vya kusaidia kazi zake. Tuna tatizo moja amelikuta pale hasa la watu wetu baada ya kupata masomo ya mwaka mmoja au miwili sasa wanapotakiwa kwenda baharini kwa ajili ya *sea time*, mwende baharini mkafanye kazi ili mpate kuwa na uzoefu wa baharini. Matokeo yake tunapowaomba matajiri wanakataa, wenye meli zao wana hiari yao kumpokea mtu. Naomba kitungwe kifungu cha sheria au kipatikane kifungu cha sheria, kitakachombana tajiri wa meli aweze kuwapokea na awalipe posho watu wetu kama wengine wanavyotakiwa kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda wangu uliobakia ni mchache, sasa naomba tu kumkumbusha Mheshimiwa Naibu Waziri, tulizungumza Bumbwini bahati yetu mbaya, hatuna barabara Bumbwini, moja katika mawasiliano. Hatuna hata simu katika Jimbo la Bumbwini. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, sikusudii kutoa shilingi, mimi siwezi kutoa shilingi hata siku moja katika Wizara hii, jinsi ninavyoipenda na jinsi ilivyo karibu na mimi. Lakini niko tayari hata kama kuongezea basi ningeiongezea. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri sasa iwekwe kwenye Hansard kwa maana ya kwamba natumaini sasa atanisaidia zaidi ili na mimi angalau simu moja ipatikane hamna hata moja. Unatoka tangu mjini mpaka shamba hata mahali pa kupiga simu hapana. Sasa nitawasiliana na wewe vipi Mheshimiwa Naibu Waziri, pale litakapotokea jambo. Mheshimiwa Waziri nakuomba sana kupitia kwa Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kumalizia juu ya suala la *ZANTEL*. Sitaki nilizungumzie sana, wenzangu wameshazungumza vya kutosha, ninachokiomba Mheshimiwa Waziri, hebu hili suala tuliondoe. Tutakaa nalo mpaka lini, suala hili ni moja katika kero hizi nazo. Si kero tu linaharibu hali ya hewa nzuri iliyopo baina ya Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, kaeni kitako limalizwe. Ningelipenda Bajeti ijayo tuseme kwamba, sasa hivi suala limemalizika halipo tena.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo kwa heshima zote na kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Bumbwini, tunaiunga mkono kwa mara nyingine tena Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ipite mia kwa mia. Nakushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kwa heshima kubwa, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie hoja ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi. Lakini kabla sijafanya hivyo, naomba niseme mambo mawili. La kwanza, niungane na Wabunge wenzangu, kuwapongeza Mheshimiwa Dr. Malecela na Mheshimiwa Anne Kilango, kwa kufunga ndoa yao. Ilikuwa sherehe ya *millennium*, Mungu abariki maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ninaunga mkono mia kwa mia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Prof. Mwandosya na Naibu wake Dr. Maua Daftari na wasaidizi wake wote, wanafanya kazi nzuri na wanastahili pongezi. Ukiondoa tatizo nitakalolieleza hapa, Wizara hii imefanya mambo mengi mazuri na yenye faida kwa wananchi wetu kwa kadri walivyoweza. Pamoja na kazi nzuri, Wizara hii imefanya Kampuni ya Simu *(TTCL)*, ndio imerudisha nyuma jitihada za Wizara hii kujenga mfumo wa mawasiliano katika uchumi na maendeleo ya kisasa. Kwa mujibu wa kijitabu hiki, Mheshimiwa Spika unakumbuka tuligaiwa hapa kinaitwa *"TTCL Today and into the Future"*. Katika utangulizi wake inaelezea mambo mawili makubwa na ninataka niyaseme. Katika kipindi hiki cha upendeleo hadi 2005, *TTCL* watakuwa wamefanya mambo haya nitakayoyataja: La kwanza, kuongeza mtandao wa simu kufikia wateja 800,100, ukurasa wa 2 wa kitabu hiki. Lakini la pili kuweka simu za kulipia katika kila kijiji au kwenye kila eneo lenye watu 3,000 au zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika mambo haya mawili ambayo kwa kweli yamo katika leseni ya *TTCL,* bado hayajatimizwa kikamilifu. Hawakuweza kutimiza masharti ya leseni yao sio kwa sababu hawana fedha, hapana,*TTCL* ina fedha. Mtu akikwambia *TTCL* haina uwezo wa kifedha anakudanganya. *TTCL* sasa inakusanya mapato ya kutosha. Lakini nataka niseme mambo mawili.

Mheshimiwa Spika, unakumbuka na ni hoja ya Wabunge hapa kwamba, *TTCL* bado haijatulipa Dola 60 milioni, hiyo ni kweli. Tukisema hili jambo liko Mahakamani tunaliacha. Lakini vile vile tunakumbuka kwamba, *TTCL* ilipotulipa 60 milioni za mwanzo tuliwaambia kaeni nazo muimarishe *TTCL*. Wenyewe wakaenda kuanzisha *CELTEL*. Sawa. Kwa hiyo, deni hawajamaliza na uwekezaji haufanywi. Nisingependa kutia shaka juu ya umakini, uwezo wa kifedha na ukweli walionao *TTCL.* Lakini tatu, wamepewa kipindi cha upendeleo hadi mwaka 2005 ili wajiimarishe, lakini hatuoni jinsi gani wanavyojiimarisha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na *TTCL* kupewa kipindi cha upendeleo kama nilivyosema, kwanza hawatimizi masharti ya leseni yao, pili hawalipi salio la thamani ya hisa walizonunua na hata wakipewa adhabu hawalipi faini ya adhabu! Naomba kuwauliza *TTCL* jeuri hii, kichwa ngumu hiki wametoa wapi? Wanafanya haya wakiwa wamenunua asilimia 35 tu, je, wakinunua asilimia 50, jeuri yao itapanda asilimia ngapi? Kwa kweli *TTCL* inaitia doa Serikali yetu inayoaminika katika Utawala Bora unaoheshimu Sheria na taratibu za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kijitabu hiki ukurasa wa 12 inaonyesha kwamba, Kibakwe watapatiwa simu. Katika kufuatilia kwa Waziri, *TTCL* waliahidi kwamba, watapeleka simu mwaka huu wa 2003, unaweza kusema 2003 haijaisha, ninakubali, lakini si ni lazima mtu uone dalili na kama hakuna dalili si ni lazima uanze kuzungumza?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri aliniandikia barua, naomba niisome kwa heshima yako. "Kampuni ya Simu Tanzania wamenitaarifu kwamba, Mji mdogo wa

Kibakwe uko kwenye Mpango wa Kampuni ya Simu *(TTCL)*. Kufuatana na mpango huo, Kibakwe itapatiwa simu mwaka ujao wa 2003 kwa kuweka mtambo wa njia 120. Naomba Wananchi wa Kibakwe, wawe na subira mpaka hapo simu zitakapopatikana mwaka ujao." Hiyo ilikuwa ni mwaka jana, 2002.

Mheshimiwa Spika, kuna sentensi muhimu aliyomalizia Mheshimiwa Waziri hapa kwamba, "naahidi" na Waziri akiahidi maana yake ni Serikali imeahidi, ndiyo utaratibu wa nchi hii. "Naahidi kushirikiana na wewe ili kutimiza azma hiyo." Mheshimiwa Waziri alichokuwa anasema ni kile kilichopo katika mpango wa *TTCL*, alikuwa hasemi jambo jipya na alikuwa haniombei jambo jipya, bali ni jambo ambalo tayari liko kwenye mipango ya *TTCL.*

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba, tangu hapo Mheshimiwa Waziri, amekuwa akitoa ushirikiano wa dhati kabisa na Wananchi wa Kibakwe wanavuta subira. Lakini ukivuta subira sana hukatika. Naomba kuwauliza *TTCL*, Wananchi wa Kibakwe wasubiri mpaka lini kwani wateja zaidi ya 200 wamekwisha jiandikisha.

Mheshimiwa Spika, vile vile, *TTCL* katika mipango yao walisema wataondoa mitambo ya kukoroga na kuweka mitambo ya *digital* katika Kijiji cha Mtera. Hii Mtera ni ile ya Jimboni kwangu. Sasa, *TTCL* haizungumzii tena suala la kuondoa mtambo wa kukoroga na kuweka mtambo wa kisasa kule Mtera. Nafikiri ilikuwa ni lengo lao kuhakikisha kwamba, wanweka mitambo ya kisasa ili kuwe na mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, napenda kuongezea hapo kwamba, pale Mtera kuna minara ya *TTCL* na wateja wako tayari kupata huduma ya simu za mkononi. *Celtel* wanaweza wakatoa huduma na wakapata wateja bila matatizo. Pengine Mheshimiwa Waziri, atakubaliana nami juu ya unyeti wa eneo la Mtera. Wote tunafahamu pale Mtera kuna vinu vya kutoa umeme, lakini hakuna mawasiliano ya uhakika. Ninafahamu *Celtel* ni wepesi siyo kama baba yao *TTCL.* Baba yao huyo amekuwa mzito, lakini kijana *Celtel* amekuwa mwepesi kwani ameitikia maombi ya Wananchi. Naomba niwapongeze *Celtel* kwa dhati, wametuwekea huduma ya simu za mkononi Mpwapwa na ni lazima niwashukuru. Naomba waendelee na juhudi hizo hususan kupeleka huduma ile Mtera, Kibakwe na Pwaga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ndugu zangu wa *TTCL* wasidhani nina chuki binafsi dhidi yao. Mzee Mbowe ni rafiki yangu wa siku nyingi, lakini pengine ni kwa sababu huduma yao inatakiwa kila mahali, ni huduma muhimu. Kwa hiyo, anapoona tunaomba huduma hiyo kwa hali hii lengo ni hilo kwamba, katika karne ya sasa huwezi kufanya biashara wala mawasiliano bila kuwa na simu.

Mheshimiwa Spika, nafikiri wenzangu wa *TTCL* wamenielewa, naomba waniambie, lakini watanisamehe mpaka kipindi chote cha Bunge 2005 tutakapoongea kwa simu kule Kibakwe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja na ninamtakia kila la kheri Waziri katika kufuatilia suala hili la *TTCL*. Ni kazi kubwa, lakini nina imani atakabiliana nayo. *(Makofi)*

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niwe miongoni mwa wazungumzaji wa asubuhi hii katika hotuba ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri, ambayo ina lengo la kuendeleza Wizara hii na kutumikia Wananchi pamoja na kukuza maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina maelezo machache nitakayochangia, ambayo nadhani yanaweza kusaidia au kuboresha hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi. Kwanza ni kuhusu Mamlaka ya Hali ya Hewa, nadhani Taasisi hii ni muhimu sana na ina mchango mkubwa sana. Mbali na Wizara hii ya Mawasiliano na Uchukuzi, Taasisi hii inazigusa Wizara nyingine nyingi sana, mfano Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu katika hotuba zilizopita hasa katika Wizara ya Kilimo wameweka malengo makubwa sana ambayo yanaelekeza kukuza kilimo. Sasa kama ni kukuza kilimo, pamoja na mwelekeo wa Taifa kuelekea kwenye kilimo cha umwagiliaji maji, hiyo bado ni hatua ndefu sana kuifikia. Katika hatua za mwanzo tutaendelea kutegemea mvua na hata huko kwenye umwagiliaji maji bado mvua inategemewa isaidie kudunduliza hayo maji ili yaweze kutosheleza katika huo umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, wanaohusika kuongoza kilimo ili kifanikiwe ni hawa watu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa, lakini bahati mbaya sana tunaposikiliza taarifa za Mamlaka hii inatuambia inatabiri. Kutabiri maana yake ni kwamba, nafasi ya uhakika iko chini ya 50%, kwa sababu kitu kinaweza kitokee au kisitokee. Sasa, ni vizuri tukaondoka huko kwenye kubahatisha bahatisha. Hata ukiangalia Katiba inasema, utafiti wa hali ya hewa, lakini kazi inayofanyika ni utabiri wa hali ya hewa. Kwa maana hiyo, ni kinyume na lengo lililokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si hayo tu, Mwenyekiti wa Kamati inayohusika na Wizara hii alituambia kwamba, hata Ofisi za Mamlaka hii haziridhishi. Kwa hiyo, ofisi inapokuwa hairidhishi, nafasi ya kazi inayofanywa kuridhisha pia inakuwa ni ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaitegemea Serikali iikuze hii Mamlaka ya Hali ya Hewa ili iweze kuwa Kiongozi mzuri sana katika kukuza uchumi wa nchi. Hii inaweza ikatuongoza wakati gani ni wa kilimo na inaweza ikatuelekeza kwamba, mwaka huu tuwahi au tuchelewe kupanda kutegemea na hali ya mvua itakavyokuwa. Au pengine ikatueleza kwa mwaka mzima au mwaka ujao tutakuwa na hali gani.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya mara nyingi tunapokea taarifa za kile kilichotokea. Mfano kati ya tarehe 20 - 23 Juni, 2003 kulitokea mvua kubwa sana katika maeneo ya Pwani, Mamlaka ilizungumza katika Vyombo vya Habari, lakini ilizungumzia ile mvua kwamba ilikuwa hivi na hivi. Haikuzungumza kabla kama itakuja mvua kubwa au vitu kama hivyo. Tunapokosa kitu kama hicho, ule mchango ambao unategemewa

kwenye Taasisi hii unakuwa ni hafifu. Ninaamini kwamba, Taasisi hii inao Wataalam wazuri na ambao wana uwezo mzuri sana, lakini kinachokosekana ni vitendea kazi. Kwa hiyo, ni vema Serikali ikawa na mtazamo maalum ili vifaa vipatikane vitakavyosaidia wafanye kazi ile inayokusudiwa ya Utafiti wa Hali ya Hewa na Wananchi wajulishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, nimejaribu kuangalia vitabu vinavyoonyesha huo mgawanyo wa matumizi kwa mwaka huu wa 2003/2004, sikuona chochote ambacho kinaonyesha ni kwa kiwango gani Mamlaka hii itaongezewa nguvu ili ifikie pale panapokusudiwa. Kwa hiyo, hatari iliyopo ni kwamba, hata ule mpango tunaouzungumza wa kukuza kilimo na mambo mengine bado utakuwa unakwenda katika hali ya kubahatisha. Hivyo, ni vema tatizo hili tulione ili Mamlaka ya Hali ya Hewa iweze kuongoza hata na Wizara nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Profesa Mwaga, amezungumzia vizuri sana kuhusu suala la *TTCL*. Katika suala hilo sitakwenda ndani sana, nitagusia kidogo tu. Mawasiliano ni chombo muhimu sana katika maendeleo, hivyo, kubinafsishwa kwa *TTCL* lengo lilikuwa ni kuongeza ufanisi, lakini kuna tatizo kubwa sana. Kwanza, ndiyo huo ubishi uliopo kwa wawekezaji pamoja na matatizo mengine chungu nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani ni vema Bunge lako Tukufu likaarifiwa ufanisi ambao umefikiwa mpaka hivi sasa ndani ya *TTCL,* ili tujue ni teknolojia gani ambayo imeingizwa tofauti na ilivyokuwa mwanzo. Tukichukulia kigezo cha mapato, tunaweza tusione lengo halisi tulilokuwa tunakusudia pale Kampuni hii ilipokuwa inabinafsishwa. Tukizingatia kwamba, wamepunguza wafanyakazi na wameendelea kubana wateja wao katika malipo, kwa vyovyote vile mapato ya Kampuni yatakua, lakini kinachohitajika ni ufanisi. Sasa, sijui suala hilo liko katika kiwango gani. Ni vema tukaarifiwa na tukaona kama katika kubinafsisha Kampuni hiyo tulikuwa tuko sahihi au tumekosea na huyu tuliyempa ni mtu sahihi au mbabaishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kuzungumzia kuhusu Kampuni za Simu za Mkononi. Kuna haja ya Serikali kuziuliza hizi Kampuni kwa sababu sasa hivi kuna matatizo mengine ya usumbufu mkubwa sana hasa kwa Kampuni ya *Mobitel.* Hivi karibuni kama ukinunua kadi ya simu ya *Mobitel* na kama una dharura unataka kupiga kwa haraka, unaweza ukatumia saa moja au mbili bado kadi haijakubali kuingia ndani ya simu na huko unakopiga japo namba ile una hakika nayo na hukukosea katika kuiandika, utasikia mara simu inakujibu *"Please check the number you have dialed."* Simu hizi zinatusumbua na kututesa. Namba nimeshaangalia kwamba ndiyo sahihi, lakini bado lugha ile ile inarudia tena, sasa sijui...

**MBUNGE FULANI:** Ni maruhani!

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Sijui ndiyo maruhani yamekwishaingizwa kwenye Mobitel! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vizuri kama kuna matatizo ya kitaalam, Kampuni iyatanzue kwa sababu ni usumbufu. Unaweza kudhania labda simu yako ni mbovu, kumbe Kampuni yenyewe ndiyo yenye matatizo. Ni vema Serikali ikawauliza *Mobitel* katika suala hili kwamba, mbona wanatusumbua hivi, ili tuepukane na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, Kampuni za Simu za Mkononi zimeonyesha kukua kwa kiwango cha watumiaji wa simu hizi. Mfano kuna takwimu nzuri tu, *Vodacom* wateja wao wamefikia 500,000, *Celtel* 150,000 na *Mobitel* 160,000. Nadhani *Mobitel* hawakwenda kwa kasi kutokana na tatizo lake nililolitaja, pamoja na kwamba ni Kampuni ya zamani zaidi ukilinganisha na hizo nyingine. Halafu *Zantel* wana wateja 22,000.

Mheshimiwa Spika, napenda nigusie kidogo kuhusu Kampuni hii ya *Zantel.* Mwaka 2001 nilipokuwa nikichangia hapa Mheshimiwa Waziri alikubali kwamba, *Zantel* wana vifaa vya kisasa na napenda nikiri kwamba, zipo nchi za nje ya Tanzania zinazotumia mawasiliano kupitia Kampuni hii, mfano ni Afrika Kusini, Kenya, Malawi na nchi nyingine. Tunaporuhusu Kampuni za nje kuwekeza katika nchi yetu, madhumuni yetu ni kwamba, nchi nayo ifaidike na kadri wateja wanavyoongezeka, maana yake ni kwamba kiwango cha kodi kutoka katika Kampuni hiyo nacho pia kitakua na hivyo Pato la Taifa litaongezeka.

Sasa, tujitahidi kutanzua matatizo yaliyopo kwa sababu tunapoteza fedha nyingi sana kutokana na mambo mengine ambayo si ya lazima, labda kwa kushindikana kuenea kwa Kampuni hii. Kuna masharti ya kuwekeza katika nchi, kama tatizo ni Kampuni yenyewe, basi hakuna haja ya kuendelea nayo, hii ni sawa na kupewa fedha halafu ukaambiwa usizitumie, maana yake nini! Kama tatizo ni *Zantel* yenyewe, basi idhibitiwe au kama tatizo ni urasimu uliopo ndani ya Serikali ni kwa nini tusiuondoe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya matatizo mengine ambayo si ya msingi na wala si ya lazima yanachangia kwa kiwango kikubwa sana kupunguza Pato la Taifa. Kwa hiyo, ni vema matatizo haya ambayo yanaepukika tuyaepuke ili tufikie lengo la kukua kwa Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nimalizie kwa kusema kwamba, ninaunga mkono hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya, Naibu wake, dada yangu mpenzi, Mama Maua Daftari na Maafisa wote waliosaidia maandalizi ya hotuba hii nzuri na makini iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri. Kwa kweli hotuba hiyo ni nzuri na imeonyesha jinsi watakavyoweza kupunguza kero ambazo zilikuwa zinatukabili watu wengi tu katika Wizara yake. Nawapongeza sana, kwa hiyo natanguliza kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nianze kutoa maoni yangu katika vipengele vifuatavyo na vingi vitakuwa ni kumwomba Mheshimiwa Waziri. Jambo la kwanza ambalo napenda kuzungumzia ni kuhusu ombi ambalo niliwahi kulitoa hapa Bungeni, kuhusu upoteaji wa tiketi yangu katika Shirika la *Precision* na ambapo sikulipwa. Napenda kusema kwamba, nimepata faraja kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara hiii kwa kuniandikia barua, nimeipokea juzi tu ikionyesha kweli kuna matumaini ya kurudishiwa fedha zangu kutokana na juhudi zinazofanywa na Wizara hiyo. Namshukuru sana tena sana Katibu Mkuu huyo, nadhani wenyewe wa *Precision* popote walipo watajua kwamba nilishapata taarifa hii na Bajeti yangu naongeza fedha hizo ambazo nategemea kuzipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuhusu simu zetu za mkononi. Wabunge wenzetu wamezungumzia hapa, lakini nami napenda nizungumzie kwa namna nyingine. Ni kweli simu hizi tunazitumia, zinatusaidia sana na tuna uhakika kwamba fedha tunazoweka tunazitumia kwa uhalali, yaani hatupunjwi kutokana na matumizi ya simu hizo. Lakini kuna kitu kimoja cha kushangaza, unapozungumza mara ghafla tu unasikia na mwenzako mahali fulani anazungumza na maneno yake yanaingia kwenye simu yako wakati na wewe unazungumza kwenye simu yako! Sasa unashangaa, kulikoni? Namba hii ni ya kwangu tu au nimeunganishwa na watu wengine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala hili linatupa wasiwasi kwamba hizi fedha tunazoweka yaani Dola 5 au 10 huenda tupo watumiaji wengi na kwa vile hazichelewi kwisha zinayeyuka kama barafu, ukizungumza mara moja/mara mbili Dola 10 zimeisha, ikiingiliana na kitu cha aina hiyo, kwamba unamsikia mwenzako wakati akiongea, kwa kweli unaanza kuwa na mashaka.

Tunaomba Mheshimiwa Waziri, awasiliane na Mashirika haya ya simu za mkononi warekebishe mitambo yao ili kutupa matumaini kwamba hatudhulumiwi fedha ambazo tunazitoa kwa matumizi ya simu zetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba, simu hizi sijui zimekuwa na kasoro gani, kwani hatukawii kuibiwa! Yaani ukiweka kwenye Mfuko, dakika mbili tu unakuta haipo, wala hujui nani kaiba! Ukienda kuripoti katika Shirika husika unaweza ukapewa namba mpya au ukarudia ile ya zamani, hapo ndipo ninapokuwa na wasiwasi na utaratibu huu siupendi ingawa sina uwezo wa kuubadilisha. Nafikiri kama kunakuwa na uwezekano, mtu akiibiwa au kupoteleza simu yake, basi apewe namba mpya siyo kurudia ile ya zamani na kuwe na uhakika kwamba, hakuna uingiliaji wa simu unapozitumia simu hizo. Hilo litatuongezea upenzi kwa Mashirika yanayohusika na simu hizo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo naomba nilizungumzie ni kuhusu malalamiko ya wafanyakazi wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ambao wanapunguzwa. Kuna Watumishi wa Posta ambao walipunguzwa kazi mwaka 1998, katika kupunguzwa kwao hawakuridhika, waliomba vikao vingi tu ili wakae wazungumze na ili warekebishe kutokana na maslahi waliyokadiriwa kulipwa kuwa ni finyu mno. Mfano mtu amefanya kazi miaka mingi na amelizalishia Shirika, lakini

anachokuja kupata ni kidogo sana, mtu mwingine anapata Sh.150,000/=, akipanda sana anapata Sh.300,000/= kwa muda wote pengine amefanya kazi miaka 15, 20 au 30, lakini anachokivuna ni kibaya sana hakiridhishi!

Mheshimiwa Spika, katika hatua za kuwaomba Viongozi wao kuhusu malipo yao linatokea suala la kupuuzwa. Linapotokea suala la kutosikilizwa au kutohurumiwa inabidi wakimbilie Mahakamani bila kujua kwamba huko wanakokwenda ndiko wanakwenda kuumia zaidi kwa sababu hawana uwezo wa kisheria na wakiweka Mawakili, Mawakili wale wanakuwa huku na huko kwa sababu wanatafuta na kutetea watu wengine ndiyo ajira yao na pale panapoonekana kuna mwanya wa kupata pesa zaidi, nadhani wanaegemea zaidi huko.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba wao wameenda Mahakamani, Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, dada yangu Mheshimiwa Maua Daftari, kwa mnavyoonekana ni watu watulivu na Wachamungu sana, yaani mnaopenda kuabudu sana, nadhani kwa tabia zenu hizo mngeonyesha kuwasaidia Watumishi hawa ambao wanapata matatizo mapema kabla hawajaamua kwenda Mahakamani.

Huko Mahakamani hawa waliostaafishwa au kuachishwa kazi mwaka 1998 mpaka leo hii hawajajua hatima yao kwa sababu wanasheria wanawazungusha, kila wanapokwenda Mahakamani Wanasheria wa Wizara yako wanaosimamia kesi hiyo, naomba niitaje hiyo kesi Namba 45 ambayo sasa hivi iko Mahakamani, wanaweka pingamizi, wakienda tena wakizungumza wakishinda watumishi basi wanaweka pingamizi tena na huku wanabadilisha mawakili katika Wizara.

Sasa kwa kweli wanaoteseka pamoja na kwamba wafanyakazi wale wanateseka kimoyo, lakini wanawake na watoto ambao wanategemea baba zao na wazazi wao kuwahudumia kwa njia mbalimbali kama, chakula, mavazi, shule wengine wanarudishwa kwa sababu hali ya kifedha haiwatoshelezi. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri, uwe unajaribu kuyarekebisha masuala yao mapema kabla hawajapotoka kwenda Mahakamani. Hawaendi Mahakamani kwa kupenda kwao ni kwa sababu ya kuchanganyikiwa. *(Makofi)*

Hata sisi hapa Mheshimiwa Waziri, tunapokosa maslahi yetu au tunapokosa nafasi hizi kwenye Majimbo yetu tunachanganyikiwa. Utanikuta labda mimi baada ya mwezi mmoja huwezi kunijua kwamba huyu ndiyo Esha Stima, aliyekuwa anapendeza alipokuwa anakuja Bungeni au ukinikuta barabarani kwa sababu hali yangu ya kifedha inakuwa siyo nzuri ninabadilika. Kwa hiyo, watumishi ambao mnaacha kuwasaidia kwa muda mrefu mpaka wanakimbilia Mahakamani, nao wanapata matatizo ya aina hiyo. Mheshimiwa Waziri nilikuwa naomba na watumishi muwasaidie ili wajue hatima yao. Kama kweli wanastahili kupewa haki hiyo, basi wapewe, la kama hawastahili waambiwe wazi wasizungushwe kwa ujanja wa kisheria ambao watendaji wanafahamu, lakini wao watumishi wadogo hawafahamu kitu chochote. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

La pili, nataka nizungumzie kuhusu haki za watumishi hao wanapokuwa kazini na kwa bahati mbaya wanapopata ajali, wengine wanapata ulemavu wa kudumu na wengine wanaugua magonjwa ya kawaida wakiwa kazini. Kwa uhakika hawalingani maslahi na

viongozi wa juu na wale wa chini katika huduma hizo. Lakini wangejaribu kuona utaratibu wa kibinadamu kwamba wanahitaji kupata misaada, dawa, posho za kuwakimu wanapokuwa kwenye matibabu hayo kuliko ilivyo hivi sasa. Nasema hivyo kwa sababu mimi mwaka 2002 nilipopata ajali nililazwa Hospitali ya Moi. Nilikuwa na watumishi wa Wizara yako. Kwa kweli mambo mengi wanayostahili kupewa ya kibinadamu hawakuyapata sawa sawa.

Sasa sijui Mheshimiwa Waziri mwenyewe na Mheshimiwa Naibu Waziri, kama mnajua kwamba watumishi wanazungushwa kupata haki zao za msingi. Tuelewe kabisa kwamba, magonjwa yanaweza kumpata mtu yeyote. Kwa misingi hiyo naomba uangalie kwa makini kama watumishi wa chini wanapata huduma nzuri kutoka kwa watendaji wako kwa sababu wewe una shughuli nyingi sana, si rahisi mambo madogo madogo kuweza kuyafahamu au kukuletea mezani kwako, wanamaliza wao wenyewe, wakati watu wanateseka na wewe hujui lakini watu wanakutambua wewe kwamba ndiye mkubwa wa watumishi wote katika Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siku hizi Wabunge wana matatizo hapa, ukisema mtu mwingine anachangia maneno anakushauri kitu si kweli. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri, kwa asilimia mia kwa mia. Nashukuru sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. SAMWEL M. CHITALILO:** Mheshimiwa Spika na mimi sina budi kukushukuru kwa kunipa nafasi hii, ili niweze kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kumshukuru Naibu wake, kwa kazi nzuri walizoweza kufanya kipindi chote cha kuwepo kwao kwenye hiyo Wizara. Vile vile sina budi ya kumshukuru Katibu Mkuu wa Wizara hiyo na watendaji wote wa Wizara hii ya Mawasiliano na Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni tabia yetu sisi Wabunge ya kusimama kila mwaka, kila Bunge la Bajeti tukileta vilio mbalimbali kwa ajili ya matatizo na kero mbalimbali za wananchi wetu. Mimi kama Mbunge, nikiwa mwakilishi wa wananchi, siji na mawazo yangu binafsi kichwani, ninapewa mawazo na wananchi wangu, ninaona wazo gani la kupeleka na wazo gani ambalo naweza nikaliacha. Kwa hiyo, tunaposimama hapa tunasimama kwa niaba ya wananchi tuliowaacha huko nyumbani. *(Makofi)*

Mwaka 2002 nilisimama hapa na kuchangia Hotuba ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, nadhani sasa imekuwa mwakajuzi nikasema kwamba, Mheshimiwa Waziri timu yake, Mkuu wa *TTCL* Mkoa wa Mwanza na Msaidizi wake mmoja, walinialika walikuwa na fomu za kujaza kwamba wananchi wataweza kupatiwa simu, baada ya kujaza hizo fomu. Kule kwangu hakuna umeme na hilo walikuwa wanalifahamu kabisa wazi, Jimbo la Buchosa halijapata umeme. Mimi nikajua kwamba hizi fomu wamezileta kwa sababu labda ya kuleta simu za *wireless.* Lakini wakati nachangia hotuba ya Wizara hii, nilimwuliza Waziri nikamwambia mbona majibu hayaeleweki na sijapata jibu lolote kwa sababu hawa wananchi tayari walijiza zile fomu na wakazirejesha Wilayani na

Mkoani, sasa majibu yamekuwa kimya moja kwa moja. Mimi nilifuatana na hawa wataalam je, hii si kwamba kutaka mimi nieleweke kwamba ni mbabaishaji kwa wananchi wangu? Nilisema nijibiwe hapa lakini sikuweza kujibiwa. Sasa ninakuomba na ninakuagiza nipate jibu la kueleweka leo na kuniwekea imani. Nilikwambia kwamba labda Wizara inatayarisha mtu mwingine.... *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Elekeza maneno yako kwa Spika siyo kwa Waziri.

**MHE. SAMWEL M. CHITALILO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nilimwambia mwaka 2002 Mheshimiwa Waziri kwamba, labda Wizara inatayarisha mtu kwenda kugombea kwenye Jimbo langu ndiyo maana walinichukua na wataalam wao na kwenda kugawa hizo fomu halafu baadaye hakuna majibu na mimi nimewapa matumaini wananchi wangu kwamba, watapa simu. Naomba nipate jibu la uhakika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nina maombi mawili. Kwanza, Jimbo langu la Buchosa sehemu kubwa ni visiwa. Nina visiwa zaidi ya kumi. Kata mbili ni visiwani kabisa. Hizi kata zingine 10 ndizo ziko nchi kavu. Jimbo la Buchosa lina watu zaidi ya laki mbili, kwa sensa iliyofanyika siku za karibuni. Watu hawa wote wanaishi bila mawasiliano ya kueleweka. Jimbo hili lina wavuvi wakubwa na wavuvi wadogo. Watu wengi wanajishughulisha na shughuli za uvuvi. Katika ukurasa wa 42 wa hotuba hii naomba kunukuu: "Wizara iliendelea na mpango wake kuendeleza magati baharini na kwenye maziwa, lengo ni kuimarisha usalama wa vyombo vya majini katika maeneo hayo na kuwawezesha wananchi wa maeneo hayo kuwa na huduma za kuaminika".

Mheshimiwa Spika, kuna meli ambayo ni ya Serikali na meli zingine binafsi ambazo zinakuja moja kwa moja kwenye Kisiwa cha Maisome. Kisiwa hiki kina kirefu sana cha maji. Unakuta hata ile meli haifiki moja kwa moja nchi kavu, inabidi itumike mitumbwi ya kawaida ili watu wapande kwenye mitumbwi na baadaye ndiyo wapelekwe nchi kavu kiasi kwamba, inasababisha watu wengine kudondoka kwenye maji na inahatarisha maisha ya watu, wengine wanakufa na wengine wanaumia vibaya sana. Kwa mfano, mwaka 2001 watu walikuwa wanasafiri kwa mitumbwi hiyo hiyo ninayosema kwamba ni hatari kutoka Kaunda kuja Maisome na kwa bahati mbaya watu zaidi ya thelathini na kitu walipoteza maisha. Mimi hili ni ombi langu la peke kwamba, naiomba Wizara iweze kushughulikia Gati la Mwaisome na ikiwezekana namwomba Waziri aje Maisome ili aweze kusaidia kufanya harambee na kuhamasisha watu wengine ili waweze kusaidia kupata fedha ya kutengeneza gati hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu la pili ninamwomba Mheshimiwa Waziri, kutokana na shughuli nilizozitaja hapa kwamba, Jimbo la Buchosa lina zaidi ya visiwa 11, kwa kuwa simu za *Vodacom* na *Celtel* kule kidogo zinafika kando kando ya Geita na Geita si mbali sana kuja Jimboni Buchosa.

Kwa sababu wavuvi hawa wanavamiwa sana kule Ziwani na majambazi na hawana mahali pa kupiga simu au kutoa taarifa zao kwa haraka wanapovamiwa, ninaomba Mheshimiwa Waziri, ajaribu kuangalia uwezekano wa kuweka mnara *either*

kuwaomba hao watu wa makampuni ya *Vodacom* na *Celtel* ili yaweze kuweka minara ya simu katika Kisiwa cha Maisome, Zilagula, Iyozu, Kome, Nyehunge na Nyakalio. Nyaunge na Nyakaulilo ni nchi kavu. Hizi sehemu zingine nilizotaja zote ni visiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na uwingi wa kazi alizonazo Mheshimiwa Waziri, vile vile namwomba kwamba Jimbo lina zaidi ya watu laki mbili na zaidi kama nilivyosema, lakini hata huduma ya posta hakuna. Ninaomba na lenyewe aliangalie kwa umakini na upendeleo wa pekee kwamba, maombi yangu haya ayafanyie kazi vizuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo unajua siku zote mimi huwa sipendi kuzungumza maneno mengi, sitaki kukupotezea muda wako maana naona umekalia kiti muda mrefu hapo, najua unataka kunyanyuka kidogo.

Naomba kuungana na wenzangu wote waliosimama na kuchangia hoja hii na mimi kwa heshima zote ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kuzingatia maneno mazuri ya Mheshimiwa Samwel Chitalilo, sasa nitasitisha shughuli za Bunge. Lakini waliopangiwa kuchangia kipindi cha mchana ni watatu wafuatao, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Faustine Rwilomba na Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi. Baada ya hapo Mawaziri wataanza kujibu hoja zilizotolewa.

Kwa kuwa waliopangwa kusema kipindi cha asubuhi wamemalizika, sasa nashughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.44 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze na mimi kuchangia hoja hii ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Kwanza, natoa pongezi kwa Mawaziri na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri wanayoifanya na kwa Bajeti nzuri ukiacha hili nitakalolizungumzia sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mimi nitazungumzia suala moja tu nalo ni suala zima la uhamishaji wa wananchi wa familia 3,500 zenye watu kama 20,000 katika maeneo ya Kipawa, Kipunguni na Kigilagila katika Jimbo langu la Ukonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda wa miaka sita na kwa kweli kinyume kabisa na sheria za nchi, Serikali imewaweka wananchi hawa karibu 20,000 katika hali ya wasiwasi na mateso makubwa baada ya kuwakataza wasiendeleze maeneo yao ya makazi

wakingojea kuhamishwa ili kutoa nafasi kwa ajili ya upanuzi wa uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema ni kinyume cha sheria kwa sababu ambazo nitazieleza. Mwaka 1997, Serikali ilifanya uthamini bila kuwashirikisha wananchi wa Kipawa wakiambiwa kwamba watahama na kwa hiyo watafidiwa. Lakini kama nilivyosema, hawakushirikisha wananchi na hata wananchi wachache sana wale walioelewa suala hili likaleta migongano na hata wakati fulani karibu wananchi wenyewe kwa wenyewe wakatane mapanga kule Kipunguni Mashariki, kama ilivyoripotiwa katika gazeti la Heko la tarehe 30 Juni, 1997.

Lakini sio hilo tu, Serikali vile vile haikuwapa wananchi thamani ya nyumba zao ili wajue watafidiwa kiasi gani na wakawaacha wananchi hawajui nini kinaendelea kwa miaka mitatu. Mwaka 2000 Serikali ikatuma Askari tena wenye silaha kuja kuweka alama za X kwenye nyumba za Kipawa zipatazo 1,125 na hawa Askari walikuja na silaha na wananchi wakaogopa kweli kweli. Lakini sio hivyo tu, mwaka huo upande wa Kipunguni, Waziri wa Ardhi, kwa kutumia *Notice* ya Gazeti la Serikali, alitoa taarifa kwamba, eneo hilo la Kipunguni limeiva kuendelezwa na kwa hiyo wananchi wasifanye maendelezo mengine zaidi. Sasa ni miaka sita toka uthamini ulipofanyika na miaka mitatu toka X zipowekwa, pale Kipawa hakuna kinachoendelea, wananchi hawajui hatima yao na yote haya wakati mwingine kwa kweli yamekuwa yakifanywa na Serikali kwa vitisho. Kwa hiyo, wananchi hawajapewa fidia, hawajaonyeshwa viwanja mbadala na wala hawajui hatima yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, zimetokea athari nyingi sana kutokana na hili kwa sababu wananchi wa maeneo yale ya Kipawa, Kipunguni na Kigilagila, wameshindwa kukarabati nyumba zao na matengenezo. Kama unavyojua wale ni wananchi maskini, uwezo wa kukarabati au kutengeneza nyumba huku akijua wakati wowote anaweza kuhamishwa, hana. Kwa hiyo ni mateso makubwa. Lakini vile vile wengi wa wale wananchi pale hasa Kipawa, wenye nyumba, mategemeo yao makubwa kama kipato ni pango. Sasa wapangaji wamehama, wamekataa kuwekeana mikataba mingine kwa sababu hawajui hizo nyumba zitabomolewa lini na kwa hiyo hawa watu hawana vipato. Lakini kutokana na kutokarabati nyumba na hasa vyoo, vyoo vingine vimeanguka na nyumba zimeanguka na vyoo viko katika hali mbaya sana na hii imesababisha magonjwa mengi kwenye maeneo yale kwa sababu hawa wananchi kama nilivyosema ni maskini, hawawezi kukarabati vile vyoo kwa kiwango ambacho kinatakiwa kwa sababu nyumba zinaweza kubomolewa wakati wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindupindu kimelipuka pale Kipawa na maeneo ya jirani na kwa kweli inakisiwa kwamba, kwa muda wa miaka miwili hii ambapo watu 12 wamekufa pale Kipawa, baadhi yao inadhaniwa wamekufa kwa kipindupindu kutokana na vyoo vile vibovu ambavyo wale wananchi wanaogopa kuvikarabati kwa sababu wanaweza kuhamishwa wakati wowote. Biashara zinazotegemea nyumba imara kuongeza jengo, hawawezi kuongeza majengo yale ili waweze kufanya biashara nyingine, kwa hiyo vile vile imewaathiri kiuchumi. Lakini vile vile wameshindwa kushiriki katika huduma za jamii, kujenga miundombinu kwa sababu wanasema

tunajengea nini na huku tunahama? Sasa ukiwahamasisha wale wananchi kuhusu maendeleo, hawana hamu kwa kweli. Wana shule moja pale ya Kipawa, iko katika hali mbaya. Toka mwaka 2000 ilishasitishwa kwamba wanafunzi wasiende, kwa hiyo kwa sasa hivi kuna Darasa la Nne mpaka la Saba. Kwa sababu shule hiyo itabomolewa, iko katika hali mbaya, wale wanafunzi wa Darasa la Nne mpaka la Saba hatujui wakati gani wanaweza kubomokewa na ile Shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale wakuu wa familia wanashindwa hata kufanya safari kwenda kwa mfano Mwanza, miezi miwili akijua kwamba labda nikiondoka familia yangu huku inaweza ikabomolewa nyumba wakati wowote. Kwa hiyo, yeye kama ndio anayetafuta riziki anashindwa kuondoka kutafuta riziki kama ni riziki ambayo inapatikana mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna masuala ya urithi. Hawa wananchi walitegemea wawarithishe watoto wao nyumba hizi, lakini sasa hawawezi kufanya hivyo kwa sababu nyumba karibu zinabomoka, hawawezi kuzitenengeza. Inaweza ikafika mahali yeye hana nguvu sasa anakufa, watoto hawajapata nyumba, hawajapata urithi na mambo kama hayo. Lakini wengine wangependa vile vile kupata mikopo kwa njia ya kuhalalisha nyumba zao ili wapimiwe waweze kupata hati na baadaye waweze kupata mikopo kwa sababu sasa hivi kuna vyombo vya kutoa mikopo ili wapate mikopo au mitaji ya kuweza kufanyia shughuli za kuondoa umaskini. Lakini wanashindwa kwa sababu nyumba zile haziwezi kudhaminiwa kwa maana ya kupewa hati. Lakini vile vile nyumba kama ile unaishi vipi kwa raha na amani na familia yako? Kwa hiyo, nasema ni kero kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili tumelifuatilia sana viongozi wa ngazi zote kuanzia Serikali za Mitaa, Kata kwa maana ya Diwani, mimi kama Mbunge, tumefuatilia sana. Tumefuatilia kwa *DC, RC,* Mawaziri mpaka Ikulu, lakini kwa kweli imeshindikana. Mimi na Mbunge mwenzangu, Mheshimiwa Martha Wejja, tumeuliza maswali mara nyingi sana hapa Bungeni kuhusu hatima ya watu hawa, lakini kwa kweli hatujapata majibu ambayo yanaridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa uvumilivu lazima unakuwa na mwisho. Sisi kama Wabunge na vile vile kama wale wananchi, tumevumilia kiasi cha kutosha na sasa tunadhani lazima tupate majibu ya kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ya Serikali kwa suala hili yamekuwa hayaridhishi kwa sababu kwa miaka sita Serikali haiwezi kushindwa kupanga mipangilio ya kuweza kutoa fidia na kutoa viwanja mbadala ili wananchi hawa waweze kuhama na kwenda maeneo mengine na mradi huo ukaendelea. Hata kama hela za mradi hakuna, lakini basi wananchi wahamishwe na eneo hilo lizungushiwe ili lijulikane kwamba kuna mradi utakuja baada ya hela kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasema wananchi hawakutendewa haki pale na kwa maana hiyo Serikali imevunja sheria kwa kuwaonea hawa wananchi. Ukiangalia hata kwa sheria za nchi, ukichukua *Land Acquisition Act* ya mwaka 1967 hata

*Town and Council Planning Ordinance* ya 378 utakuta kwamba, pamoja na Rais kupewa haki ya kutwaa ardhi kwa manufaa ya umma, lazima fidia itolewe kwa wale wanaoishi pale. Sasa hili halikufanyika na inatakiwa wajue ni fidia kiasi gani. Lakini hayo yote hayakufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria Mpya ya Ardhi inasema kwamba, baada ya miezi sita ya uthamini kama hujalipa fidia lazima urudi kuthamini upya kutokana na bei kubadilika. Hili halijafanyika. Vile vile kuna asilimia 25 ambazo lazima ulipe kama *disturbance allowance, resettlement costs* na ardhi yenyewe ina thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa ingawa Serikali inatuambia kwamba, inatafuta shilingi bilioni 22 kwa ajili ya kuwafidia hawa, hii ni bei ya miaka ya 1997 mpaka 2000. Sasa hivi iko sheria mpya, sina hakika, lakini wataalam wanasema sasa hivi Serikali inatakiwa itafute zaidi ya shilingi bilioni 100. Sasa ni gharama kwa Serikali vile vile. Wananchi wa Kipunguni wameamua kuishitaki Serikali na wanayo haki na wanaweza wakashinda na imeshatokea pale ambapo Rais, anatwaa ardhi lakini wananchi wanapinga Mahakamani na wanashinda. Kwa mfano, ukichukua kesi ya *Government Industries* na *Tanzania Manufacturing* ya mwaka 1979, ambapo Rais alitwaa ardhi, kesi ile Rais alishindwa. Kwa hiyo, wananchi hawa vile vile wanaweza wakashinda. Sasa je, wananchi twende Mahakamani ili Serikali ishindwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, mbaya zaidi ni chuki ambayo sasa imejengeka katika eneo lile. Wananchi wanaichukia Serikali yao, Chama chao na viongozi wao. Kwa kweli mimi nachukiwa sana pale, Mama Martha Wejja, anachukiwa sana eneo lile na ushahidi ni tarehe 28 Septemba, 2002 wakati mimi na Mheshimiwa Martha Wejja, tulipoitisha kikao cha wananchi pale Kipunguni, ilikuwa karibu tupigwe mawe. Mheshimiwa Martha Wejja,
alitukanwa matusi ya nguoni na mimi kidole kilifika kwenye jicho. Nikasema kumbe Wabunge wa Tanzania tuweke hoja ya kutembea sasa na Askari. Lakini wameahidi kwamba, hawatoi kura mwaka kesho na wala mwaka keshokutwa na nadhani watatekeleza hilo kama Serikali haiwezi kutoa msimamo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, lazima niseme kwamba, mimi kama Mbunge na hata wale wananchi, tunapenda sana uwanja ule wa ndege upanuliwe, kwa sababu utaleta maendeleo sio kwa Tanzania tu, lakini hasa hasa kwa Jimbo la Ukonga, kwa sababu Uwanja wa Ndege wa Kimataifa uko kwenye Jimbo langu na ukipanuliwa utaleta *investments* na tutafaidika. Lakini tunachosema, kucheleweshwa wananchi hawa kufidiwa hela zao ili wahame, kunawaathiri vibaya sana kiuchumi, kisaikolojia na kijamii. Sasa Serikali kwa kweli lazima itoe tamko. Vile vile Serikali kuchelewa huku kwa sababu hii ni Bajeti ya Taifa ilikuwa shilingi bilioni 22, sasa hivi tunaambiwa inakaribia shilingi bilioni 100; je, hiyo si hasara? Nani atawajibika kwa hasara hiyo kubwa kama gharama zitaongezeka kwa kiasi hicho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kubwa zaidi na mimi kama Mbunge, nataka nirudi hapa mwaka 2005, lakini inavyoonekana hapa sipati kura kama hali ndio hii. Kwa hiyo, maombi na ushauri wangu, wananchi wa Kipawa, Kipunguni na Kigilagila

wamenituma na mimi naungana nao kuomba Serikali itoe tamko moja kati ya haya mawili. Kwanza, Serikali itoe tamko kwamba, itafanya uthamini upya mara moja kwa sababu uthamini uliofanyika ni wa zamani kwa Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 na kwamba watalipa hiyo fidia na kuwaonyesha viwanja vipya huko vinakopimwa na zoezi hili lifanyike katika kipindi cha mwaka mmoja. Kama wanashindwa hilo, basi Serikali itamke kwamba, imeahirisha mradi ule na wananchi waendelee kuendeleza makazi yao na kama huko baadaye Serikali itafufua Mradi ule wa Uwanja wa Ndege, basi itathamini upya na kuwalipa kwa viwango vya wakati huo. Inaweza ikaamua kufanya hivyo kwa sababu uchumi wa Serikali ni mdogo na kwa hiyo, hawana pesa au uwezekano upo labda wa kujenga uwanja wa ndege mahali pengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimezungumza sana, hata jana nimezungumza na Waziri, lakini ninachotaka ni kauli mojawapo kati ya haya mawili ili wananchi wa Kipawa, Kipunguni na Kigilagila, wapatao 20,000 waweze kujua ni nini hatima yao na kwamba Serikali inasema nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, siko tayari kuunga mkono Bajeti ya Wizara hii kama sitaridhishwa au kama Waziri hatatoa tamko la kuridhisha. Baada ya kusema hayo, nangojea hayo majibu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita mchangiaji anayefuata, naambiwa hapo mbele kwenye *gallery* ya Spika, ambayo inakabiliana na Kiti hiki, tunaye Mheshimiwa H. Pohamba, Waziri wa Ardhi wa Serikali ya Namibia. Yeye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Chama Tawala cha *SWAPO,* ambacho nadhani wote tunakijua. *I have been assuming that Honourable Pohamba knows some words of Kiswahili, because he has been here several time. (Makofi)*

Pamoja naye, amefuatana na Dr. Shivute, ndio *Valuer* wa Mkuu wa Wizara hiyo. Kwa wale akina mama ambao hawamwoni, yeye ni mama. *(Kicheko/Makofi)*

Pia tunaye Dr. Wolambi, yeye ni *Surveyor General,* wamefuatana na wenyeji wao wa hapa ambao ni *Counterpart* wao wa hapa, Waziri yupo na *Valuer* yupo. Wote *Counterpart* wapo. *(Makofi)*

Haya Tunaendelea. Sasa namwita mchangiaji anayefuata, Mheshimiwa Faustine Rwilomba.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Kwanza kabisa, naomba niishukuru Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, kwa kazi inayoifanya katika nchi hii. Nina imani Wabunge wote wanafahamu kwamba, Mheshimiwa Waziri, amekuwa ni mfano mzuri wa kutembea kila kona, hata kwetu ambako ni kona ngumu ameweza kufika. *(Makofi)*

Namshukuru Naibu wake, wote wawili, kwa kweli ni wasikivu. Nina imani na hili la Mheshimiwa Mahanga, ambalo amelizungumza, kwa kuwa Waziri huyu ni mwelewa na msikivu, litafanyiwa kazi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga, asiwe na wasiwasi.

Kwa kweli cha kusema, kwa niaba ya watu wa Busanda ni kumshukuru sana. Mheshimiwa Waziri, ahadi zake zimekuwa ni za kweli na amekuwa akitekeleza. Kwa niaba ya wananchi wa Busanda namshukuru sana kwa kujenga Gati ya Bukondo, ambayo tuna imani baada ya muda itatoa matunda na watu wake wanafanya kazi. Wameniomba nije niseme ahsante kwa kazi hiyo. Tunakuomba urudi tena uone kazi inavyoendelea. Napenda kumshukuru Katibu Mkuu, pamoja na Wakurugenzi wote wa Wizara. Hii Wizara ni kubwa na inahitaji umakini na uangalifu mkubwa na ni nyeti na ninafikiri kama moyo wa nchi, kwa sababu inagusa kila kona. Kwa hilo, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Pamoja na shukurani, nina imani kwa sababu Mheshimiwa Waziri ahadi zake huwa zinatekelezeka. Sasa baada ya kutoka Bukondo, utafika Muharamba na penyewe uliwahi kuahidi kwamba utafika, ukimaliza Bukondo utahamia Muharamba na Nkome kutengeneza gati. Nina imani Kiondo anayo taarifa hiyo na kazi hiyo itafanyika. Sisi hatuna wasiwasi. *(Makofi)*

Tunashukuru aliahidi simu katika Jimbo la Busanda, zimefika. Lakini kuna tatizo, japokuwa katika kitabu chake ameeleza kwamba, kutoka Mwanza - Bukoba kuna mawasiliano, sehemu ya Katoro kuna tatizo bado. Hizi simu za *Vodacom* kuipata mpaka upande kwenye mti. Sasa utakuta mwanamama amepanda juu ya mti ndio apate mawasiliano, inakuwa ni shida. Tunaomba katika sehemu za Katoro, Nyarugusu, Lwamgasa, tuweze kupata mnara wa *Celtel* na *Vodacom*. Kwa kweli ukienda kule ni wachimba madini, wana hela na wana simu, lakini utakuta watu wako mitini utafikiri wanakula matunda kumbe wanapiga simu. Tuna imani kwa ahadi zake atakamilisha hilo. Naomba sana, ni vizuri tu uweze kufahamu hili japokuwa tuko mbali na dunia, wanasema dunia ni Dar es Salaam. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nia yangu kuzungumza hapa, napenda nizungumzie chombo kimoja cha mawasiliano nacho ni *TAZARA*. Nina imani wote mnafahamu jinsi *TAZARA* ilivyoanza. Ilianza awamu ya kwanza enzi za Marehemu Baba wa Taifa na enzi za Mheshimiwa Kaunda, kwa uhusiano mzuri na China. Naomba niieleze Serikali kuwa sasa hivi reli hiyo kwa kweli ina hali mbaya. Ina hali mbaya kwa sababu Serikali ni kama imeiweka pembeni. Tunaiomba Serikali sasa iangalie, ni kweli ilianza wakati huo ambapo kulikuwa na matatizo ya mawasiliano upande wa Kusini na migogoro lilijengwa kwa ajili ya kuhudumia upande wa Kusini. Sasa hivi njia zinapitika, lakini si busara kuitupa na kuiacha kwa sababu inaweza kutumika ikazalisha. Kuna watu bado inawahudumia na kuna mizigo bado inahitaji kutoka kule kuja Bandarini na huwezi kujua, baadaye kunaweza kutokea mabadiliko. Hatukujua kwamba Marekani inaweza kuivamia Iraq.

Kwa hiyo, bado tunaihitaji hii reli na maendeleo ya nchi yanategemea barabara, reli, simu, usafiri wa anga na umeme. Vitu hivi vinategemeana sana viwepo. Inasikitisha

inapoonekana hii reli ni kama imeachwa. Tunaomba *at least* Serikali iweke *injuction. Yes*, kuna wazo la kubinafsisha, lakini huwezi kubinafsisha kitu kiko katika hali ambayo sio nzuri. Kama unabinafsisha, basi iwekwe katika hali nzuri. Hata binti yako kama unataka kumwoza lazima umvalishe, umpe sidiria, umuweke nywele vizuri na watu watamwona. Sasa unaweza kumuoza kwa debe la udaga tu kama utamwacha hivi hivi unasema aah, binti nenda tu, kama umemchukia! Ni vizuri iwekwe katika hali nzuri reli hii. *(Kicheko)*

Sasa hivi treni ya abiria inahudumia wananchi kwa upande wa Kusini na kuna barabara. Kuna ushindani wa barabara na treni ya abiria. Lakini kwa taarifa nilizopewa, *running costs* ya treni ya abiria kwa mwaka ni shilingi bilioni kumi. Lakini faida inayoingia au pesa inayoingia ni shilingi bilioni tano. Sasa unakuta wanachota kwenye pesa ya reli ya mizigo wanahamishia huku, matatizo sasa yanajitokeza pale. Inabidi watumishi wachelewe kulipwa, mabehewa yasikarabatiwe au *Loco* kama wanavyoita zisikarabatiwe. Sasa naiomba Serikali iangalie hili, tusiwe na ile *culture* ya kuona kwamba tumemaliza. Kama ndugu zangu Wazaramo wao wanaangalia mambo ya nyuma, hawaangalii mbele. Anaangalia mambo ya nyuma, basi yamekwisha. Lakini lazima tuangalie mbele kwamba itatusaidia huko tunakokwenda. *(Kicheko/Makofi)*

Napenda nimweleze Waziri au niieleze Serikali kwamba, reli hii ina-*survive* kwa sababu China ndio inatoa msaada. Pesa ya China ndiyo inasaidia kununua *locomotives*, inaweza kununua baadhi ya mashine na vipuli. Lakini tatizo kubwa linalokuja, hata ile fedha inayotoka China inakatwa *fuel levy.* Sasa Wachina kwa kweli hawasemi, lakini kwa mahusiano, mimi nimeona wale Wachina walioko pale *they are not comfortable*, hawana raha. Walete fedha wakusaidie wewe, halafu wewe ndio aah, hapa nimegue kodi. Tunaomba Serikali hii, kama fedha ifanye kazi yake kama ilivyoileta. Nafikiri tujaribu angalau kuona wenzetu wanapoleta fedha zao, basi isaidie kazi iliyolengwa badala ya hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuiomba Serikali ya hapa, naomba kuwe na mawasiliano na Serikali ya Zambia iweke nguvu katika reli hii. Naiomba Serikali ijaribu kuangalia ni namna gani reli hii inaweza ikaendelea ku-*survive* vizuri.

Sehemu za Kusini ni *very productive*, lakini *feeder roads* zilizopo hazitoshi. Ni vizuri kuweka *feeder roads* kusudi mizigo inayoletwa kwenye njia ya reli isafirishwe na kuipa nguvu reli hii na ikiwezekana kuwe na *godowns* za kutosha Dar es Salaam. Mtu anapoleta mizigo yake anaweka kwenye *godown* anajua mizigo iko salama inangoja kusafiri ng'ambo au kusambazwa Mikoani na sehemu nyingine, biashara hiyo itakwenda.

Sasa kuiachia hivi hivi kwa kweli nafikiri tutakuwa kama hatumuenzi Baba wa Taifa. Hatujali hao ndugu zetu walioanza kama Mheshimiwa Kaunda na waliofikiria kwamba reli hii ni muhimu. Mimi kwa kweli inanitia uchungu na kuona kwamba sasa inaenda peke yake.

Mimi sikatai kubinafsisha, ibinafsishwe tu sawa, lakini iwe katika hali nzuri, hata gharama yake itakuwa na thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa ninapozungumza, mizigo mingi iko Makambako kwa sababu ya kukosa *Loco* za kwenda kuvuta ile mizito na kwa sababu ya kukosa *fuel* ya kutosha ya kuweza kusafirisha mizigo. Sasa hiyo biashara ni biashara ya Pwagu, kama mizigo inakwenda inakaa na watu wanapoteza imani.

Inatakiwa mzigo unafika na unaondoka, mtu anafuata na ikiwezekana viwepo vifaa vya kisasa kwamba, mzigo unafika mahali fulani unajulikana mzigo wangu sasa hivi umefika labda Mbeya, umekaribia kufika watu wanaona. Serikali, wanunulieni hata *radio calls,* badala ya kutokea ajali za ovyo ovyo hivi, angalau rubani aweze kuwasiliana na rubani mwenzake.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilikuwa nasoma gazeti kwa upande wa reli ya kati kwamba, watu wanakwenda kwa baiskeli kuangalia kama behewa linakuja. Hiyo *style* ya baiskeli ni hatari. Sijui kama ni kweli hiyo! Lakini ikifikia hatua hiyo ni tatizo. Kuwe na simu. Naomba sana Serikali itupie macho vyombo kama hivyo ambavyo vimejengwa kwa gharama kubwa na sasa hivi vinaelekea kufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi ilitolewa hoja kidogo kwamba, tutafute ndege ya Rais, ambayo si ya gharama kubwa kwa sababu sisi ni maskini sana, iwe ndege ya kuchukua watu sita, saba tu. Lakini mimi nafikiri hatutaki *a bid differ* kwa kweli. Ndege ya Rais, iwe nzuri, iwe ndege ya Rais. Tulipitisha wenyewe hapa. Sasa tunatafuta ndege ya kwenda kufika pori la Tabora ipotee tuanze kutangaza kwenye magazeti!

Tunaposema ni masikini, mimi nafikiri wakati mwingine tuanze kuangalia, tuseme labda tuna-*mismanage* fedha. Lakini fedha tunayo, dhahabu ipo, kila kitu kipo, tunapata bilioni moja na ushehe upo, tunaanza kutafuta ndege ya Rais inayochechemea upande mmoja, labda *secondhand*! Hapana. Mimi nasema kama tulipitisha fedha, tununue kitu kitakachodumu ambacho *we are sure hundred percent* kitasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninavyomwangalia Rais, huwa najaribu kuangalia jengo hili, nafikiri labda ni kale kapira ka katikati, anayefuata kule juu ni Mungu. Kale ka katikati ndio Rais, wengine tuko huku, labda kule juu yake kuna Mungu. Sasa unataka kale kapira kaende. Siku moja nilipanda ndege za madini kutoka Mwanza kwenda huko Vijijini. Yaani unaona mara na upepo unaipuliza inakwenda, sijui ndio ndege tutafute ya namna hiyo?

Tunahitaji kununua ndege nzuri ya Rais kama tulipitisha fedha zile. Tunahitaji ndege nzuri ambayo *motor cab* yake wakiwemo mle ndani wako salama wanakokwenda. Mimi sisemi tutumie fedha ovyo, lakini zitumike vizuri, ipatikane ndege ya uhakika. Vinginevyo kama hatuwezi tuache. Tusije tukafika mahali Rais wetu akaanza kuwa anaomba *lift* kwa wenzake. Anakwenda Australia ndege inakuwa ya wasiwasi anaomba *lift.* Sasa huyo Rais wa namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha tuliyopitisha ni kwa ajili ya kununua ndege nzuri. Tutasikitika tukisikia kwamba ndege ya Rais inakwenda inababaika babaika safarini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja hii iliyo mbele yetu, lakini nina imani kubwa kuwa maombi yangu niliyoyapeleka kwa Mheshimiwa Mwandosya, atayafanyia kazi na tunakukaribisha sana tena urudi na hilo alilosema ndugu yangu Mheshimiwa Mahanga, kwa kulisikiliza linasikitisha lakini kwa usikivu wako tulivyo na imani na wewe, utalifanyia kazi na Mheshimiwa Mahanga, tuna hakika atarudi tena ule mwaka alioutaja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuniruhusu nichangie. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Mwandosya kwa Bajeti yake aliyoileta. Lakini vile vile kama walivyokwishasema wenzangu, binafsi napenda kumshukuru kabisa kwa sababu mwaka 2001 nilikaribia kukosa simu kwenye Ofisi yangu ya Ubunge. Sasa wakanizungusha wakaniambia na wewe ufanye kama wengine. Lakini nilipomwambia ndani ya saa 24 nilipata simu hiyo, waliniwekea. Kwa hiyo, huo ni uthibitisho kwamba, anafanya kazi yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, amegusia suala la kubinafsisha *Marine Services Company,* ambayo kwayo sisi tunadhani wamechelewa kwa sababu, kwa Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na Ziwa Victoria, kuendelea kuwa na meli inayotumia saa 24 katika kipindi hiki cha karne ya sayansi na teknolojia, nadhani si sahihi. Kwa sababu lazima tujali muda, kama kuna *Sea Bus* inatoka Dar es Salaam kwenda Zanzibar saa mbili imefika, sioni kama ni tatizo la watu hawana pesa za kuwekeza kwamba kunaweza kuwa na *Sea Bus* katika Ziwa Victoria ili iweze kutoka Mwanza ndani ya saa mbili imefika Bukoba.

Sasa tunachokipata hapa ni kwamba, tuko mbioni, tuko mbioni, sijui ndiyo mbio za sakafuni au mbio za kuelekea bahari ya mafu. Kwa hiyo, ningependa Waziri, atakapokuwa ana-*summarize* hapa, atuambie *time frame* ya hizo mbio zinakwenda vipi, kwa sababu Walatin wanasema *temp sespecunior, protailasure, time is money.* Sasa hatuwezi kuwa tunachelewa katika masuala kama haya kwa sababu nadhani kuna watu wanafanya urasimu mahali fulani.

Kwa sababu mimi siamini kwamba, Serikali imetangaza na watu wa kununua *Sea Bus* wakakosa ya kuweka Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Ziwa Victoria. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri, aangalie na atujibu hapa kwamba litachukua muda gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala yanayohusu simu jimboni kwangu, nimekwisha mwandikia Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo, kwa vile naamini sidhani kama kuna haja tena ya kulisema hapa. Lakini suala la *TRC* imechelewa kubinafsishwa na nadhani wanaomba Serikali ichukue hela nyingine iwape. Watu ambao wame-*enjoy transport* ya kuhudumia nchi kwa miaka 30. Wasije wakasingizia madawa

yaliyoanguka pale juzi, mpaka tunachelewa chelewa na tunavyochelewa chelewa hii barabara ikishajengwa kwa lami, mizigo mingine itapungua na wasafiri watapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini *in connection to that*, nilikuwa naomba kwamba, sasa kwa kuwa tumeingia katika soko la pamoja la nchi za Afrika Mashariki, mimi nita-*enjoy* tu kwa sababu niko pale mpakani, basi na wenzetu ili waweze ku-*enjoy* basi ile reli inayoishia Isaka mngei-*extend* ikaenda kuishia Mrongo ili iweze kusaidia *TRC* kwa upande ule, iweze kusaidia Uganda na pale Rwanda. Wakati mwingine kama Waganda watapata mafuta pale au mkaweza kuchukua mafuta kutoka kule Sudan, nadhani mnaweza mkafanya *business*. Kwa hiyo, mliangalie kwamba mnapomaliza barabara hii ya lami *business* hapa itapungua, kwa hiyo, *I think you have to act in a business manner like fasion.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije kwenye hili moja la *TTCL.* Niliwahi kuliarifu Bunge lako kwamba, mwekezaji wa *TTCL* alikuwa anadaiwa shilingi bilioni 60 na nikaliambia Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali isingepata hizo hela na kama ingezipata ningejiuzulu. Sasa naomba kufuta *statement* yangu kwamba, sitajiuzulu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sitajiuzulu kwa sababu nimehongwa wala nimetishwa. Niliposema vile nilikuwa na sababu tatu, ya kwanza nilijua kwamba nikisema hawatapata wangeniambia ni mwongo. Kwa hiyo, nikaweka rehani Ubunge wangu kwamba, zipatikane halafu nijiuzulu na nilijua Chama Cha Mapinduzi kingefurahi nijiuzulu Jimbo libaki wazi kwa sababu nisingegombea, kwa hiyo, wangekazana kuhakikisha kwamba linapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hazikupatikana na hata zingepatikana nikawa nimejiuzulu ningefurahi sana kwa sababu tungepata hizi shilingi bilioni 60 ni nyingi, kwa sababu hata Bajeti ya Waziri ya Wizara nzima ni shilingi bilioni 45, pungufu ya shilingi bilioni 15. Kwa hiyo, hata kama ningepoteza Ubunge ningeshukuru tu kule kwangu kwamba, nimefanya kazi kubwa sana. Sasa mambo hayakwenda hivyo. *(Makofi)*

Sasa siyo kwamba natengua msimamo wangu huu bure bure tu. Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua hatua zaidi tena kali sana. Ya kwanza, mambo wakati ule wa chama kimoja, kikiwa kimeshika hatamu, yalikuwa yanakwenda barabara, anayevuruga anadhibitiwa. Kwa sababu kuna watu kama nilivyokuwa nasema katika Mkataba ule, amekwenda Afisa mmoja, Mwanasheria, ndiye aliyeweka pale mambo ya ajabu ajabu akatukosesha hizo shilingi bilioni 60 wala siyo Mheshimiwa Mwandosya. Mtu mmoja na kundi lake. *(Makofi)*

Sasa Mheshimiwa Magufuli, hao anawawajibisha, kwa sababu Mzee Kiula, alikuwa anashitakiwa, unadhani hela zile alikuwa anakula yeye, anavuruga yeye? Lakini Mheshimiwa Magufuli anawawajibisha na wenzake. Sasa kwenye Wizara hii mtu mmoja anavuruga halafu tunakuja hapa tunasema *collective responsibility*, *if there were no collective conspiracy, why should there be collective responsibility. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninachosema chama kimoja kilikuwa kinasimamia kweli, baadaye vyama vingi, kama mngekuwa mnakataa mfumo, Mwalimu wakati huo hajafa, alisimamia kweli wanaotaka kuvuruga anawawajibisha. Sasa hayupo. Chama kimoja hakipo. Sasa sijui nani anamwajibisha nani? Lakini nadhani Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, iko wazi, ni kazi ya Bunge kuisimamia na kuishauri Serikali. *(Makofi)*

Sasa mtu unapomsimamia si unamsimamia kweli. Sasa katika hatua ninazotaka kutangaza ni mbili katika hatua hizo. Ya kwanza, nitaliomba Bunge tutakapokuwa tumalizia hapa. Nitaleta hoja hapa ya binafsi ya kutaka tuunde Kamati Teule ya Bunge ya kuchunguza kulikoni huko. Sasa kama Wabunge watakataa lakini wao huwa wanapiga kelele hapa kwamba tuchunguze, basi jamii itatushitaki. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko taarifa kuhusu huyu ambaye Mheshimiwa Profesa Mwaga, pale amemsema kwamba, kuna mtu amelipa asilimia 35 ya hisa zake, lakini ni mjeuri. Sasa Serikali ya Tanzania imemwambia akaenda kushtaki Ulaya. Sisi tukamshtaki huku baadaye tukasema tu-*negotiate* hapa. Tunatumia hela za walipa kodi. Sasa maelezo yaliyokuwepo ni kwamba, Kampuni tanzu ya *CELTEL* aliianzisha kwa kutumia shilingi bilioni 55 kutoka zile shilingi bilioni 60, sijui kama naeleweka! *A subsidiary company*, akaanzisha hizi ambazo zilipaswa kwenda *Treasury* kule ndiyo wakahamishia kwenye hii kampuni na yeye akakaa pale akasema na mimi hii nina *share!*

Sasa nitaka maelezo Mheshimiwa Waziri, utakapokuwa una-*wind up,* ni kweli au si kweli? Ameambiwa alipe shilingi 120 bilioni akalipa shilingi 60 bilioni. Hizi shilingi bilioni 60 ngoja ziende huko zikafanye mipango mingine, akachukua mkaweka pale mnaanzisha *subsidiary company CELTEL* shilingi bilioni 55. Sijui yeye alichangia nini. Sasa tunataka kujua wananchi yeye aliweka ngapi au na pale anataka mgao, anataka *dividend?*

Sasa hiyo, inakazia ile hoja yangu ya kutaka kuleta hoja hapa kwamba sisi ndiyo tunasimamia Bunge na wananchi nje wanatusikiliza. Tuje tuunde Kamati Teule hiyo iende ichunguze, haiwezekani watu wanakaa pale wanamchafua chafua Waziri wetu, hatuwezi kukubali! *(Makofi)*

Sasa baada ya kuyasema hayo, nilidhani ...

**WABUNGE FULANI:** Unga mkono hoja.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wewe unasema unga mkono shilingi bilioni 60 hazipo, sasa niunge mkono! *(Kicheko/Makofi)*

*CELTEL* wamechukua shilingi bilioni 55 zetu, wewe unasema unga mkono. Kwa hiyo, Mhehsimiwa Naibu Spika, naku-*address* wewe. Siwezi kuunga mkono kitu

ambacho sijapata maelezo ya kutosha, kwa sababu nimeshakusudia kushtaki hapa. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa nilisema nachukua hatua mbili kali kweli. Kwa hiyo, hiyo ya kwanza, nitashtaki hapa ili wote tuamue na jamii itajua tumeamua nini kwamba sisi kama Wabunge, tunaunda Kamati tunachunguza au tumekataa tunaogopa.

Lakini hatua ya pili kama Bunge litakataa, nitakwenda kuwatafuta Waandishi wa Habari na wale wanaoandika makala na wale wanaokereketwa kule nje, tunachanga hela tunaishtaki Mahakamani Serikali ya Tanzania, pamoja na mwekezaji hawawezi kutupoteza hizo hela. *(Makofi)*

Sasa baada ya kuyasema hayo, wala sitanii, siwezi kujiuzulu kwa sababu mngelipa ningejiuzulu, sasa hamkulipa. Kwa hiyo, sitajiuzulu nitakaa humu humu. *(Kicheko/Makofi)*

Baada ya kuyasema hayo, nasubiri majibu, nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika. *(Kicheko/Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Jang'ombe, sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi na wataalamu wao wote kwa pamoja, kwa kukaa na kuandaa Bajeti ya Wizara yao kwa kuonyesha utendaji wao na matendo yao ya baadae kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata maelezo kuhusu mtandao wa *ZANTEL* kama yalivyoelezwa kwenye hotuba ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kupata wateja wengi zaidi Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata faraja hiyo kwa *ZANTEL* kwa ongezeko la wateja, lakini bado lile tatizo ambalo wengi wetu tunaotoka Zanzibar tunapenda kupata ufafanuzi zaidi kuhusu kuenea kwa utendaji wa *ZANTEL* kwa nchi nzima na sio sehemu moja tu ya Muungano, kwani mpaka hii leo bado Wizara yako haijatueleza kwa ufasaha na tukaelewa tatizo linaloifanya isienee nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kuipongeza Kampuni ya *VODACOM,* kwa jitihada zao za kuleta Upinzani wa Biashara *(Business Competition)* na kwa sasa wameamua kwa makusudi kupunguza bei kwa mtandao wao ili wananchi wafaidike zaidi na huduma za *VODACOM* na kwa mawazo yangu hilo ndilo lengo la Serikali yetu ya CCM kuwaondolea shida wananchi wake ambao wengi wao ni maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kipindi hiki imejitahidi kuimarisha sehemu nyingi muhimu hasa zile za Uwanja wa Ndege na Bandarini, kwa kuweza kuzidisha shughuli zile zote muhimu hasa zile za Usalama wa Vyombo na abiria. Kwa

hatua hiyo, naipongeza sana na kuyaombea hayo yote waliyoyapanga yafanikiwe ili tupunguze kukaribisha lawama za kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, roho za Watanzania wengi zimepotea na zinazidi kupotea kutokana na ajali nyingi za nchi kavu na Bandarini zilizotokea na zinazozidi kujitokeza mara kwa mara hapa nchini. Pamoja na mikakati inayowekwa na Wizara hii, lakini bado tatizo hili halijapata ufumbuzi wa kueleweka. Kwa hiyo, naiomba Wizara iongeze juhudi zake ili kuhakikisha yanabaki yale ambayo Mwenyezi Mungu, ameshayapanga yawe na hayawezi kuepukika na isiwe kwa sababu za kibinadamu ambazo zimo ndani ya uwezo wetu hasa uchakavu wa vifaa na ushughulikiaji wa matengenezo madogo madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya machache, napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika vifungu vifuatavyo: Kif. 106 - Uk. 55, naipongeza Wizara kwa kufanya matengenezo katika viwanja kadhaa vya ndege kwa upande wa Tanzania Bara. Ni vyema Wizara ikafikiria kufanya matengenezo kwa Kiwanja cha Ndege cha Karume kilichoko Chake Chake Pemba, ili kiweze kufanya kazi hata wakati wa usiku ili ndege ziweze kutua na kuruka wakati wote. Pia pawepo na vyombo vya kuzimia moto vya uhakika na si vya kubahatisha.

Kif. 128 - Uk. 68, tunaomba Kampuni ya Simu za Mkononi ya *ZANTEL,* iruhusiwe kufikisha huduma zake huku Bara kama vile ilivyo kwa *MOBITEL, VODACOM, CELTEL* na kadhalika.

Kif. 130 - uk. 68, Jimbo langu la Ziwani bado hatujapata simu za ndani za *TTCL.* Namwomba Mheshimiwa Waziri, akishirikiana na Naibu wake, atufanyie mpango wa kutuunganishia simu za majumbani za *TTCL* kwenyeJimbo langu la Ziwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kukupongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa hotuba ambayo hakuna shaka imelenga kuiendeleza Tanzania katika Sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi. Ni vyema watendaji nao wakapokea pongezi hizi kwa matayarisho maridhawa. Natamka wazi kwamba, hoja hii naiunga mkono kwa asilimia zote.

Nichukue tena fursa hii kuipongeza Wizara, pamoja na Waziri, kwa ushirikiano wa karibu uliopo baina ya Wizara na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ya Zanzibar. Hili ni muhimu hasa katika kudumisha Muungano na njia nzuri ya kuondoa kero ndogo ndogo ambazo bila shaka zitaondoshwa kwa ushirikiano wa karibu baina ya Wizara zetu. Kwa upande wa Sekta ya Mawasiliano, tumepiga hatua nzuri. Suala la kuiondoa *TAMSA* kutoka kwenye *SUMATRA* ni mfano mzuri jinsi Wizara hizi mbili zilivyoshirikiana na hatimaye sote tumeridhika na matokeo yake.

Suala ambalo mpaka sasa bado ni chembe ya mchanga kwenye jicho hasa kwa wananchi wengi Visiwani limebaki kuwa ni suala la Mawasiliano ya Simu za Mkononi la *ZANTEL* kuweza kutoa huduma upande wa pili wa Muungano. Hili bila shaka inabidi lisubiri kukamilika kwa *monopoly* iliyowekwa ili imvutie mwekezaji atakayeinunua *TTCL. (Exclusivity).*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *Radar* naliunga mkono na nalipongeza. Ingawa ningeshauri kuanza kutumika kikamilifu ili kuepusha matukio, kama lile la karibuni la upoteaji wa ndege ndogo yenye Marubani wawili. Matukio kama haya ni vyema tukayafungia mlango ndani ya mipaka yetu. Hoja hii naiunga mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. SULEIMAN JUMA OMAR:** Mheshimiwa Spika,

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ujenzi wa barabara nyingi nchini kwa kiwango cha lami, mambo mengi ya maendeleo na ya kijamii yatafika sehemu hizo zote za nchi na hasa pembezoni au mipakani mwa nchi yetu. Hivyo, mtandao wa simu kufika katika sehemu hizo za mipakani ni muhimu sana kwa kuharakisha maendeleo ya nchi ki-uchumi na kijamii. Mfuko wa Simu Vijijini ufanye kazi haraka na kwa ufanisi kwa lengo hilo.

Pili, ninaipongeza sana Wizara kwa juhudi za uimarishaji wa viwanja vya ndege. Jambo ninaloshauri ni kwamba, Wizara iangalie uwezekano wa uwekaji wa zana zitazoweza kuifanya ndege iweze/ziweze kutua viwanjani kwa dharura endapo haja ya kufanya hivyo itatokea, isiwe kwa viwanja vikubwa tu.

Sera ya *ICT,* ambayo Serikali imekwisha kuiidhinisha nakubali ifanyiwe sheria husika. Hata hivyo, Serikali iwe mbioni sana kuanza kuweka fedha kwa kuanza kujenga mtandao huu muhimu kwa maendeleo ya nchi na kuongeza ufahamu kwa wananchi wetu juu ya matukio. Maendeleo na kuelimisha watu wa rika tofauti za Watanzania. Hatua hii ya kujenga mtandao huu sijui kama utaiingiza Zanzibar hasa kwa vile mambo yanayohusika na Anga na Simu, Posta na kadhalika ni ya Muungano. Ningeliomba sana kuwa Zanzibar isiachwe pembeni kwenye jambo hili la *ICT* ambalo ni Funua Ulimwengu kwa watu wetu wote.

**MHE. KARIM SAID OTHMAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, hivi kuna sababu gani ya msingi ya kuwaeleza Watanzania kwa nini hadi leo Kampuni ya Simu ya *ZANTEL* haijapatiwa leseni ya kuendeleza mtandao wake huku Tanzania Bara. Kampuni ya *VODACOM, MOBITEL* na *CELTEL* zote zimepewa leseni kwa Tanzania nzima na Waziri bila kuona aibu ametangaza kwenye hotuba yake kwamba Kampuni ya *ZANTEL* imejitanua mtandao wake. Zanzibar tu, Kampuni zote ni sawa, zote zinafanya biashara ni wapi na wapi Kampuni ya *VODACOM* kuwa na wateja 500,000 lakini *ZANTEL* ina wateja 42,000; je, kuna sababu gani au kwa sababu Kampuni hii inatokea Zanzibar, je hii si kasoro za Muungano? Mheshimiwa Waziri, ni lazima ajibu hili kama hakujibu nazuia mshahara wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri katika jitihada zake za kuendeleza viwanja vya ndege, lakini ningemwomba aongeze jitihada katika kiwanja cha Dodoma. Dodoma ni Makao Makuu ya nchi, wageni mashuhuri huwa wanatembelea hapa Mabalozi, Marais na kadhalika. Kiwanja hiki kiwe na huduma za kutosha, pia ni aibu kwamba Dodoma hakuna usafiri wa ndege za abiria wa kutegemewa, hivyo Wizara ingefanya kila mpango kuona kuna ndege ya abiria japo mara tatu kwa wiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ingefanya kila mpango wa kukarabati mabehewa ya abiria angalau mabehewa ya daraja la kwanza. Wasafiri wa mabehewa ya daraja la kwanza ni abiria wenye hadhi zao na nafasi zao lakini mabehewa haya hayana taa, mafeni ni mabovu, vitanda ni vibovu, mende na wadudu wanatembea kama wanaofugwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingi naiomba Wizara inipatie simu katika Jimbo langu, wananchi zaidi ya 35 na maofisi ya Serikali wanaomba simu, Waziri alinijibu nisubiri uwezo wa Serikali, sasa leo nakumbusha tena nipatiwe simu zile za kisasa *(Wireless Local Loop)* na sio zile za kukoroga.

Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 20, kuhusu Usafiri na Uchukuzi wa Barabara Mikoani na Vijijini kwa kweli Mheshimiwa Waziri kilio cha shida ya usafiri wa abiria na mizigo kimepotea, hakuna tena tatizo hilo na inafaa lishughulikiwe. Lakini ukishawapakia abiria na mizigo yao, sikuona kauli yako katika kudhibiti usalama wa safari zao. Ingefaa utoe kauli ya vidhibiti mwendo viendelee kutumika au ilikuwa ni povu la soda. Hivi sasa Mheshimiwa Waziri magari ya abiria yanatembea mwendo wa kilomita 160 kwa saa au zaidi. Hivyo, nakuomba kama mpango huu ni wa kudhibiti mwendo haufai basi shauri mpango mwingine, wewe ndiye mtunga sheria ya kuhifadhi usalama na raia katika safari na Wizara ya Mambo ya Ndani kazi yake ni kusimamia sheria yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli shukrani zangu kwa Mheshimiwa Waziri, pamoja na watendaji wote ni nyingi mno. Ahsante.

**MHE ALLY SAID JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sina wasi wasi na makadirio na matumizi ya Wizara hii. Lakini wasi wasi wangu mkubwa juu ya Wizara hii ni ubaguzi unaotisha katika kusambaza huduma za simu hasa za mkononi. Kuna minong'ono kwa simu za *ZANTEL* isiruhusiwe kuweka minara yake kote Tanzania Bara, wakati ambapo simu zote za Tanzania Bara zimeweka minara yao kote Tanzania Zanzibar, bila hoja yoyote. Hii eti inatokana na kwamba, itaharibu biashara ya simu zote za Tanzania Bara na kwamba mapato ya simu hizi pindi ikiruhusiwa *ZANTEL* yataporomoka, hasa ningependa nipate ufafanuzi wa wazi kuhusiana na hofu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Mheshimimiwa Waziri, haoni kwamba kwa tendo hili ni kuwadhalilisha wawekezaji wa Zanzibar ki-mawasiliano?

Pia Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba kisiasa ni hatari kwani suala hili wananchi wanaweza kuliingiza na kulioanisha na kisiasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupata jawabu sahihi kutoka kwa Waziri muhusika, basi Bajeti yake itakuwa haina kombo na nitakubaliana nayo mia kwa mia. Kinyume na hivyo nitakuwa na wasi wasi kidogo. Ni vyema nijibiwe hadharani katika Bunge.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Hotuba ni nzuri, imewasilishwa kwa muhtasari nadhifu na ya kueleweka. Hongera sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazidi kuisisitiza Wizara iwe na uangalifu sana katika ubinafsishaji. Wasisukumwe sana na mawazo ya kupotosha ya *PSRC* yanayozingatia ufundi zaidi kuliko madhara yatakayolikumba Taifa kwa siku za baadaye. Ni budi tuzingatie maslahi ya Taifa, kuliko matokeo ya muda mfupi kama vile fedha za kuisaidia Serikali hususan katika kuiendesha. Lazima wawekezaji wawekeze na fedha zitakazopatikana kutokana na ubinafsishaji ziimarishe miundombinu iliyopo na kujenga mipya na kuongeza uwezo zaidi.

Naomba kupitia Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, kuishukuru *CELTEL* kwa kuweka mtandao Lushoto. Naomba mtandao huo upanuliwe ufike kwenye maeneo ya Kwekanga, Mlola, Kwamakame, Mkuzi, Jimbo la Lushoto na Bumbuli, Mgwashi, Tamota katika Jimbo la Bumbuli. Pia simu hizo zifike, Mlalo Mtae Mnazi katika Jimbo la Mlalo, hiyo ni kuboresha huduma ya simu za mkononi Wilayani Lushoto. Gharama za matumizi ya simu zidhibitiwe, wawekezaji wasituumize jamani uchumi wa watumiaji unaathirika sana. Ahsante sana.

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi na ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa kazi nzuri sana wanayoifanya kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Kyela ninayo maombi mawili kwa Wizara. Ombi la kwanza ni kupatiwa simu za *TTCL (landline)* katika Mji Mdogo wa Kasumulu. Mji Mdogo wa Kasumulu unakua kwa haraka sana na hivi sasa una wakazi zaidi ya 2,500. Zipo Ofisi za Idara zote za *TRA* pamoja na Vituo vya Polisi na Uhamiaji. Kasumulu iko mpakani na nchi ya Malawi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la pili linakwenda sambamba na shukrani za wananchi wa Kyela kwa Serikali yao, kwa kuwapatia mawasiliano ya simu za mkononi za *VODACOM* na *CELTEL*. Ombi ni kwamba, simu hizi za *VODACOM* na *CELTEL* hazishiki Tarafa yote ya Ntebela yaani Mji Mdogo wa Ipinda hadi Matema. Tunaomba Wizara iwasiliane na Makampuni husika yarekebishe hali hii.

Ninarudia kuwapongeza wafanyakazi wa Wizara kwa kazi nzuri. Ninaunga mkono hoja.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza Mama Maua na Mheshimiwa Mwandosya.

Naipongeza *TTC*L na uongozi wake, kuna matukio madogo, madogo juu ya bili za simu za *TTCL.* Mfano simu huwa mbovu kwa miezi mitatu kisha bili inaletwa, huwa juu sana. Naomba sana kuwe na ushirikiano mzuri kwa Shirika letu.

Kuna migogoro inayojitokeza kwa wafanyakazi wenu. Nini hatima yake mfano, migogoro ya Kampuni ya Simu na kundi la watu wa Makamba, Msindo na wenzake? Nimefanya *study* juu ya suala hili. Naomba nijulishwe hatima yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wimbi kubwa la wizi wa simu za mkononi. Hii nafikiri inatokana na sababu kuwasimu yoyote, yaani *Line,* huwekwa kwenye jumba lolote yaani *Siemen, CSS, Motorola, Samsung, Alcatel, Ericson* au Phillips. Simu na chombo cha simu. Kuna vyombo na *Lines*, njia za simu. Njia ni kama *VODACOM, CELTEL* na *MOBITEL.* Kwa hali hii uwezekano upo kwa mtu akanunua chombo kama *Samsung* akaweka *line* zote mbili au moja kwa kubadilisha *line* ya zamani. Hali hii ikifanywa kiholela itaimarisha wizi wa vifaa vya simu na vyombo vya simu ila waweke njia za simu mpya *(Lines).* Ninashauri kwamba, mteja asiruhusiwe kununua *line* tupu bila ya kuwa na stakabadhi ya chombo au apate *Police Message.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nauli za watoto na vijana katika mabasi, meli, treni na Daladala, Serikali ingeingilia kikamilifu katika kusimamia nauli za watoto kwenye Mabasi. Tabia ya Mabasi huuza viti badala ya umri wa mtu, jambo ambalo watoto hawathaminiwi. Kawaida watoto hulipa nusu ya tiketi ya mkubwa ingawa mtoto hana uzito mkubwa. Chini ya miaka 18 au hata 20 au zaidi kama anasoma shuleni. Mara nyingi masuala haya huachiwa Wakuu wa Mikoa kusimamia kama ilivyo Dar es Salaam ambapo Mwaibula na Makamba, hufuatilia suala la nauli za Daladala.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada vita vya Iraq mafuta yalipanda ghafla vile vile iliendelea kwa muda wa wiki tano hivi. Hali hii ilifanya baadhi ya vyombo vya usafiri hasa Daladala za miji mbalimbali nchini zikapandisha nauli kutoka Sh. 150/= hadi Sh. 200/=, kutoka Sh. 400/= hadi Sh.700/= au kutoka Sh.700/= hadi Sh. 1,000/=, kuzingatia ongezeko la bei ya mafuta kipindi cha vita. Ingawa Dar es Salaam Daladala zilibakia na bei ile ile ya Sh.150/= mbona hadi sasa miji mingine bado hawajashusha bei ya nauli ingawa vita imeisha na mafuta yameshuka bei?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara, kwa kazi nzuri wanayofanya na Bajeti walioyawasilisha kwetu. Nawapongeza wao, Mheshimiwa Rais wetu na Chama cha Mapinduzi, kwa sera nzuri na maendeleo yaliyopatikana katika mawasiliano ya simu, Viwanja vya Ndege, Posta na Bandari.

Pamoja na pongezi hizi, mchango wangu katika Hotuba ya Bajeti ya Mawasiliano na Uchukuzi ninauelekeza katika kuboresha huduma ya mawasiliano ya Simu, Posta,

Viwanja vya Ndege na mchakato uliotumika katika ubinafsishaji wa Mashirika yaliyoko chini ya Wizara hii hususan Kampuni ya *TTCL.*

Mawasiliano ya Simu na Posta ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi yoyote. Huduma hii ya simu za *TTCL* au simu za mkononi imesambaa nchi nzima ya Tanzania na kusahau Wilaya yangu ya Same Mkoani Kilimanjaro. Kule katika Wilaya yangu asilimia 80 ya wananchi wetu wanaoishi milimani ambapo usafiri wa barabara ni shida na mawasiliano ya simu hakuna. Tarafa za Mwembe-Mbagga, Same, Gonja, Mamba-Vunta, hakuna mawasiliano ya simu. Ili kupata mawasiliano wananchi wanalazimika kutembea kwa miguu umbali wa kati ya km 10 - 30 kufuata mawasiliano ya simu Mji wa Wilaya Same. Karne hii ya kupashana habari kwa *electronic* sisi bado tunalalamika kutembea kwa miguu umbali nilioutaja kufuata mawasiliano ya simu. Ninaiomba Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, kwa makusudi kabisa, ielekeze nguvu zake katika Wilaya ya Same, ili kutupatia mawasiliano ya simu katika Kata na Tarafa nilizozitaja hapa. Huduma hii iwe ya njia zote za mawasiliano ya simu za mkononi *CELTEL, TTCL* na hata *VODACOM*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kwa simu za mkononi ni Makampuni ya Simu za Mkononi waunde *charger* za *solar power*, ili kuwawezesha watumiaji wa simu za mkononi mahali ambapo hakuna umeme, waweze ku-*charge* simu zao kwa kutumia *solar power.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa pili ni huduma za Posta. Katika Posta yetu ya Wilaya huduma ya kutuma fedha kwa njia ya *Money Fax* bado ni duni. Kwa ujumla huduma zote za kutuma fedha kwa njia ya Posta kule Same ni duni sana. Huduma hizi ni duni kwa sababu mteja anapotumiwa fedha na ikawa kima cha fedha aliyotumiwa na wateja wengine ukijumlisha ni kikubwa basi wengine wanalipwa fedha na wengine hawalipwi. Tunaomba uwepo utaratibu mahsusi wa kuhakikisha mteja anayetumiwa fedha kwa Posta halazimiki kulala Same, Posta ya Wilaya ilipo, ili alipwe fedha zake alizotumiwa. Kama nilivyosema, wananchi wetu wengi wanaishi milima ya Same ambapo usafiri ni wa shida. Hivyo, tunaomba kero hii ya fedha inayotumwa kwa Posta iondolewe. Pia tunaomba huduma ya kutuma fedha kwa njia ya *Western Money Transfer Union* ifunguliwe katika mji wetu wa Wilaya ya Same.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine unahusu Kiwanja cha Ndege cha Mji wa Same. Kiwanja hiki hakina huduma yoyote na ningeomba kumfahamu mmiliki wa hiki kiwanja na ni kwa nini ametelekeza kiwanja hiki? Bado kiwanja hiki ni muhimu sana kwa wananchi wa Wilaya ya Same kwa mawasiliano ya ndege zinazoleta baadhi ya watalii katika Hifadhi ya Mbuga ya Wanyama ya Mkomazi. Zipo pia ndege za watu binafsi na za Mashirika ya Dini zinashuka katika kiwanja hiki. Ninaiomba Wizara itoe maelezo na kutupia macho kiwanja hiki ili kiweze kuendelezwa kama viwanja vingine vilivyotajwa ukurasa wa 55 vya Mpanda na Biharamulo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa mwisho ni kuhusu ubinafsishaji wa Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Mfano ni Shirika la *TTCL,* ambalo limekuwa na mgogoro huu. Ninaiomba Wizara na Serikali iwe makini

sana inapoweka mipango na mikataba ya ubinafsishaji ili isiathiri maendeleo ya huduma husika za simu kwa wananchi wetu. Mgogoro uliotokea ndani ya ubinafsishaji wa Shirika la *TTCL* umezorotesha kwa kiasi kikubwa maendeleo ya huduma ya simu nchini. Ninaiomba hali ya namna hii inapotokea Serikali iweke *Transitional Measures,* ili kukabili hali ya kuathirika kwa maendeleo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naunga mkono hoja na kumwomba Mheshimiwa Waziri au Naibu wake, watembelee Wilaya yangu ya Same ili kuona kilio cha wananchi na kero sugu za mawasiliano nilizozitaja hapa.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia kuwa wazima na salama na kuendelea na shughuli zetu za Bunge kwa salama. Vile vile napenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, kwa namna unavyoliendesha Bunge letu mpaka hivi sasa. Mimi kwa upande wangu nashukuru. Pia nachukua nafasi hii kumshukuru Waziri na Wizara hii, pamoja na watendaji wenzake wote. Mwisho nawashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Micheweni, kwa kunichagua kuwa Mbunge wa Jimbo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza kuchangia kwenye hotuba yenyewe, mimi nitaongelea sehemu nne muhimu. Sehemu ya kwanza ni usafiri wa baharini. Kama tunavyoelewa usafiri ni jambo muhimu sana kwani bila ya usafiri mambo mengi hayawezekani, kwa hiyo usafiri ni kitu muhimu sana mimi imenibidi niliweke mwanzo kabisa susla hili katika mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kuwa siku za nyuma tulikuwa na chombo muhimu sana katika usafiri wa baharini, chombo hicho si kingine ila ni *M.S. SEPIDEH*. Chombo hiki kilikuwa kinatoa huduma za usafiri katika sehemu za Mwambao mzima wa Afrika Mashariki. Chombo hiki kilikuwa kikifanya safari za Dar es Salaam kwenda Zanzibar, Zanzibar kwenda Pemba. Pemba kwenda Tanga, Tanga kwenda Mombasa na safari kama hizo kwa kurudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la muhimu zaidi ambalo mimi nimekusudia ni hii safari ya Dar es Salaam/Zanzibar /Pemba kila siku na kurudi, jambo ambalo lilikuwa likitusaidia sana sisi wasafiri wa Pemba ambao hatuna usafiri wa uhakika kama wenzetu wa Zanzibar/Dar es Salaam ambao wana vyombo vingi. Kwa hiyo, kwa faida ya Watanzania walio wengi ninamwomba Mheshimiwa Waziri, atupe maelezo ya kina ili tuelewe kuhusu chombo hiki kiko wapi na kitarudi tena au vipi? Mheshimiwa Waziri, tafadhali usiniweke kapuni kwa majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ningependa kuzungumzia kuhusu Simu za Mkononi, hizi simu nazo vile vile ni muhimu kwa hiyo ningependa ziboreshwe ili ziweze kufanya kazi Tanzania nzima na sio baadhi ya sehemu tu na wengine wakiwa hawana mawasiliano hayo, kwa mfano, nasikia Wabunge wengine wanalalamika mpaka leo bado wana simu za kukoroga katika Wilaya na Majimbo yao. Vile vile ningependa kuelewa je, kuna sababu zipi za kimsingi mpaka leo *ZANTEL* hawajaingia Tanzania Bara au ni wao wenyewe hawajawa tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, napenda kuongelea kuhusu Posta, katika miaka ya 1980, Shirika la Posta likiwa pamoja na simu lilikuwa likifanya kazi sana na lilikuwa na ofisi zake hata vijijini lakini sasa naona limedorora sana limebakia majengo matupu na baadhi ya mijini tu. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali iliangalie ili lifanye kazi kama zamani au sasa watu hawapendi tena mambo ya barua na vifurushi wanatumia simu tu?

Mwisho namalizia kuhusu usafiri wa barabarani. Kuhusu sehemu hii mimi napenda kutoa maoni yangu kwa wanaotoa leseni hususan za madreva wa magari ya abiria. Mdereva wengine wanaopewa leseni huwa ni watoto sana na wanapoendesha magari huwa hawajali sana wamebeba nini, wanajali zaidi kupata abiria na fedha tu. Dreva anaweza akaovateki ingawa sehemu hiyo haruhusiwi kufanya hivyo ili mradi yeye anaweza kupita tu. Kwa hiyo, hii sehemu ni muhimu kwani dreva akishaua watu hutoka na kupewa leseni yake akaendelea kutesa na huku wenzake ameshawaua na wengine kuwaweka vilema. Kwa hiyo, naomba suala hili liangaliwe sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nifikie hapa kwa leo. Ahsante.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa pongezi kwa hotuba iliyotolewa na Waziri wakati akiwasilisha hotuba yake Bungeni. Baada ya shukrani hizo, ninayo machache ya kuchangia. Kwanza, Wizara ilikwishatoa ahadi ya kupatiwa mtambo wa kisasa wa simu Mji wa Sikonge. Ahadi hiyo ilisema ifikapo mwishoni mwa mwaka 2003 Mji wa Sikonge utapata mtambo wa kisasa. Nakumbusha kwamba hili ni jambo muhimu kwa kuiweka Wilaya ya Sikonge iwe na mawasiliano na Wananchi wengine hapa nchini. Ni matumaini yangu kutokana na usikivu wa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara, wataondoa kero hii.

Pili, Wilaya ya Sikonge ina Kituo kidogo cha Posta. Mahali kituo hiki kilipo hapastahili kupaita Kituo cha Posta chenye hadhi ya Wilaya. Naomba tena kuikumbusha Wizara kwamba, Sikonge kama Makao Makuu ya Wilaya, mahali ambapo pana Taasisi kadhaa zinazohitaji huduma hii nyeti, hii ikiwa ni pamoja na Wananchi ambao wanaihitaji sana huduma hii.

Mwisho, naomba kero hizo nilizozitaja hata kama hazijafika Sikonge, Viongozi wa Wizara ni vizuri wafike wajionee hali ilivyo na vile vile kuwapa imani Wananchi kuhusu hatua za Serikali katika kumaliza kero hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. BATILDA S. BURIAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Katibu Mkuu, pamoja na timu nzima ya Wataalam wa Wizara yake kwa hotuba nzuri iliyowasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kupitia Wizara hii, napenda kuzipongeza jitihada zinazofanywa na Serikali katika kutekeleza mambo mbalimbali hususan katika kuimarisha Sekta ya Mawasiliano na ile ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yafuatayo ni baadhi tu ya mambo ambayo napendekeza yaangaliwe kwa ukaribu zaidi:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu kuipa kipaumbele Sekta ya Mawasiliano hasa kufuatia kuendelea kwa kasi kwa masuala ya mawasiliano na teknolojia ya habari *(ICT).* Ili kuwawezesha Wananchi kufanya biashara zao bila vikwazo na ili kuimarisha uuzaji wa mazao na bidhaa zingine nje *(export)* ni lazima kuwepo na miundombinu ya ku-*support ICT,* miundombumu inayoaminika, ili kuwezesha kupatikana kwa taarifa za maeneo ya masoko na bei za bidhaa.

Vile vile, ni lazima kuwepo kwa bandari na viwanja vya ndege vyenye huduma bora na ya kuaminika. Hii ni pamoja na kuwepo kwa mtandao mzuri wa mawasiliano ya simu na *internet*. Hivyo, napendekeza kwamba, Serikali itoe kipaumbele cha kipekee kwa masuala ya *ICT.* Hivyo, Wizara iangalie uwezekano wa nchi yetu kujenga *ICT incubation centre*, *smart village* ili kusaidia ukuaji wa *ICT,* kama walivyofanya wenzetu wa Uganda, kwenye Bajeti yao ya mwaka huu wa 2003/2004.

Ni vizuri ikafahamika kwamba, kuboreshwa na kuimarishwa kwa *ICT* hakutasaidia tu utoaji na upatikanaji wa habari, bali pia itasaidia sana katika kutoa mchango mkubwa katika Pato la Taifa. Mchango huu ni wa moja kwa moja kutokana na uuzwaji wa huduma na bidhaa za *ICT*. Pia, *ICT* inasaidia Sekta zingine za uchumi (biashara na utalii), kuboresha huduma na bidhaa zao na hivyo kuongeza tija na mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupendekeza kupitia Wizara hii kwamba, ni vizuri Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, ikaangalia upya mfumo au *formula* inayotumika katika kuchanganua na kikadiria mchango wa kila Sekta katika Pato la Taifa. Kwa mfano, ni vigumu sana kuamini kwamba, Sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi imekuwa ikikua kwa asilimia 0.1 yaani 1992 - 5.2%, 1993 - 5.3%, 1994 - 5.1, 1999 - 5.4%, 2000 - 5.4%, 2001 - 5.4% na 2002 - 5.5%. Kwa takwimu, hizi nashauri Serikali iangalie upya utaratibu wa kuchanganua mchango wa kila Sekta kwani Sekta ya Mawasiliano kwa upande wa simu tu, ninayo *study (200)* inayoonyesha kuwa na mchango wa Dola za Kimarekani milioni 136 kwa mwaka.

Pia katika mchanganuo inaonyesha kwamba, msisitizo umewekwa kwenye huduma za simu *(fixed, mobile)* Posta na kadhalika. Hata hivyo, kuna huduma zinazofanywa kama huduma ya *International Gateways* ambazo haziwekwi kwenye makadirio. Huduma hii ya ku-*transit calls* ndiyo inayoingiza mapato makubwa sana kwa baadhi ya Makampuni kama *TTCL* na *Zantel.*

**MHE. SHAMIM P. KHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wote, kwa kazi nzuri wanayofanya. Hongereni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *ICT Policy*, kwanza, natoa pongezi kwa kuwa na Sera hiyo *in place*. Ni kati ya nchi chache tu za Bara la Afrika kuwa na Sera hiyo. Nilipata bahati ya kuhudhuria mkutano Uganda pamoja na Ndugu Kowelo kuhusu *Feminization of the IT Policy.* Katika dudu zima dhana ya kijinsia imejitokeza katika mistari miwili au mitatu tu. Kwa imani yangu Sera hiyo ni *gender blind*. Nashauri kwa vile kila Wizara sasa ina *gender desk,* basi huyo Afisa ashirikishwe kikamilifu katika shughuli zote za Kiwizara ili dhana ya kijinsia ijitokeze.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara iwe inatumia *gender lens*. Katika mkutano huo wa Kampala baada ya kusomewa takwimu mbalimbali zilizomo katika *ICT Policy*, Wajumbe walitaka kufahamu kati yao Wanawake ni wangapi? *Unfortunately we did not have*. Nashauri tuwe na *disaggregated data which I strongly agree.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninashauri wakati wa kuandaa *Strategic Planning* ya *ICT Policy,* Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wadau wengine wote, washirikishwe ili dhana ya kijinsia ijitokeze *boldly.* Nia ni kuwasaidia wote kuhusu Wanawake na Vijana walioko Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaweza kupata taarifa kamili ya mkutano huo kutoka kwa Ndugu Kowelo. Namshukuru sana alinisaidia kupitia Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Wizara kwa uamuzi wake wa kupeleka simu Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina maswali. Katika hotuba yake amesema atafanya ukarabati/matengenezo katika Viwanja vya Ndege vya Musoma, Tabora, Dodoma, Shinyanga na kadhalika:-

(a) Je, Wizara ina mpango gani wa kuvifanya ukarabati/matengenezo viwanja vilivyoko Wilayani? Mfano ni Nzega.

(b) Je, kwa Kiwanja cha Nzega, kimepangiwa Shilingi ngapi?

(c) Je, Wizara ipo tayari kuzungumza na Kampuni ya *Resolute* ili iruhusu kutumia uwanja hasa kwa *Flying Doctors?*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, ameeleza juu ya Kampuni ya *ATCL* kutumia Nembo ya Twiga. Inasemekana *Precision Air* tayari walishalipia ada ya kutumia nembo hiyo, hivi ni nani *National Carrier*? Kwa

nini Kampuni iliyonunua hisa 49% inakuwa na sauti/maamuzi katika Serikali yenye hisa 51%

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya simu imejielekeza zaidi katika kupeleka Makao Makuu ya Mikoa, Wilaya na barabara kuu. Kwa kuwa Wananchi wengi wapo zaidi Vijijini. Je, *TTCL* ina mpango gani wa kuwapa huduma hii Wanavijiji walio mbali na Makao Makuu ya Mikoa, Wilaya na barabara kuu? Katika Wilaya yangu ya Nzega sehemu kama Ndala, Puge, Mambali na Magengati zipo mbali na hazipati *network* za simu za mkononi, *Vodacom* na Celtel. Namalizia kwa kuwatakia heri, baraka na kazi njema.

**MHE. MWADINI ABASS JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa kupata fursa hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi. Aidha, napenda nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya, Naibu Waziri wake, pamoja na Watendaji wa Wizara hiyo kwa kuandaa na kuwasilisha hotuba nzuri yenye kuonyesha mwelekeo mzuri wa kumkomboa Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia suala zima la Huduma ya Simu za Mkononi. Mheshimiwa Waziri, amekiri katika hotuba yake kwamba, Makampuni ya Simu za Mkononi yameendelea kupanua mitandao ya simu zao katika sehemu mbalimbali nchini. Makampuni hayo yametajwa kuwa ni *Celtel, Mobitel, Vodacom* na *Zantel.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali inavyoonekana ni Makampuni ya Simu za Mkononi yale tu yaliyosajiliwa Tanzania Bara ndiyo yanayoonekana kuwa na mtandao mkubwa katika sehemu zote mbili za Jamhuri ya Muungano (Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar).

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kushangaza na kwa kweli linalozua malalamiko ni kule kuonekana Kampuni ya *Zantel* kutopatiwa kibali cha kupanua mtandao wake katika upande huu wa pili wa Jamhuri ya Muungano (Tanzania Bara). Inavyoonekana ni kwamba, Kampuni ya *Zantel* imewekewa mipaka maalum isivuke bahari kuingia Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, inakuwaje mpaka hivi leo ikawa mtandao wa *Zantel* haujaingia Bara? Nafahamu kwamba *satellite dish* iliyowekwa na *Zantel* ni *more powerful* kuliko hata ile iliyoko Mwenge Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, taswira ambayo watu wengi wameijenga ni kwamba, kwa kuwa Kampuni hii ya *Zantel* imesajiliwa Zanzibar ndiyo maana inawekewa vikwazo vya makusudi ili Kampuni hii isipanue mtandao wake huku Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sisi tunafahamu kwamba, *Zantel* inanyimwa kibali kuwepo Bara kutokana na sababu ya kuikandamiza kwa makusudi kiuchumi Kampuni hii na kuyalinda Makampuni ya Simu yaliyosajiliwa huku Tanzania Bara

kutokana na ushindani wa kibiashara. Kila mtu pengine anafahamu kwamba, huduma ya simu za mkononi ya Kampuni ya *Zantel* ni rahisi kulinganisha na Makampuni mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda hii ndiyo sababu kuwa mpaka hii leo *Zantel* haijapewa kibali kupanua mtandao wake Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, anipatie maelezo ya kina ni lini Kampuni hii ya *Zantel* itaondolewa pingamizi zote zinazozuia kupanua mtandao wake wa simu za mkononi huku Tanzania Bara.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutoa pongezi kubwa sana kwa Waziri, Naibu Waziri na Wafanyakazi wake wote, kwa jinsi wanavyoshirikiana na kuifanya kazi yao kwa makini na kwamba taarifa imechambuliwa na imegusa maeneo mengi ikiwemo katika Wilaya. Naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wanawake wa Mkoa wa Mtwara, natoa shukrani kwa Serikali kupitia Wizara hii ya Mawasiliano na Uchukuzi, kutuletea mtambo mkubwa Mtwara ambao tulishuhudia ufunguzi wake tarehe 15 Aprili, 2003, mtambo ambao una matumaini ya ukombozi wa miundombinu ya kisasa katika kupata mawasiliano mazuri kati ya mtu na mtu, ofisi na ofisi na kadhalika. Lakini nashauri mambo machache yafanyike:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, mtambo baada ya kufunguliwa tu unapofanya mawasiliano ya kuongea na simu sauti inajirudia na kuwa ni kero kwa watumiaji. Pili, simu zinakatika kila unapotaka kuitumia, hata kusababisha kuacha kabisa na ni watu wengi wamelalamikia tatizo hili wakiwemo Wakuu wa kazi, wafanyabiashara hasa ukiwa nje ya Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, upelekaji wa simu za *TTCL* unakwenda polepole sana kwa Wananchi na zikiwemo simu za mkononi. Nne, Wilaya ya Tandahimba iko mbali na Makao Makuu ya Mkoa na kwa vile ni Wilaya mpya huduma zao nyingi lazima wakimbie kwenda Newala kama Benki, hospitali, maduka na kadhalika na laiti wangekuwa na simu wangefanya mawasiliano haraka. Hivyo, nataka kujua ni lini huduma za simu zitafika Tandahimba na ni kitu gani kinachosababisha Wizara kutotekeleza mara moja kauli zake kule nyuma kuwa watapatiwa simu haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa pia zipo Shule za Sekondari ambazo zipo mbali na Makao Makuu ya Wilaya kama maili 35 - 40 hivi, nazo ni Ndwika, Wilaya ya Masasi ya bweni na Mnyambe ni ya bweni ipo Wilaya ya Newala, nashauri wapatiwe simu haraka kikiwemo na Chuo cha Elimu Kitangari. Mahali penye mkusanyiko kunakuwa na mambo mengi inapotokea tatizo inakuwa ngumu sana kufanya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TTCL* katika Mkataba wake unasema wataweka simu kila penye watu 3,000 hivi na mpaka saa hawajatimiza malengo, je, tuwaache tu wakati wanatuchelewesha? Nashauri washtakiwe au waache Mkataba na apewe mtu mwingine

ili huyo mpya tushirikiane naye kutimiza malengo. Pia, nashauri Miji Midogo na sehemu za Taasisi zilizo mbali na Makao Makuu ya Wilaya zipewe kipaumbele mara moja kwa kufungiwa simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kununua rada baada ya muda mrefu kupita ili nchi iwe na uhakika wa ndege inayotua na inayotoka kwa usalama. Nashauri kuwe na utaalam wa utumiaji, tuandae vijana wetu kuwapeleka mafunzoni ili kuwaongezea elimu itakayowasaidia kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuhakikishe ulinzi wa kuaminika wa kulinda mitambo yetu ukilinganisha wapo wengi wenye mawazo potofu kuwa kununua rada ni kupoteza fedha za Wananchi bila kujali usalama pia kuwa ni gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache naunga mkono hoja moja kwa moja na kwamba, Waziri asimamie malengo aliyojiwekea kuhakikisha yanatekelezwa.

**TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, sikupenda kuchangia sababu niliona aliyochangia Msemaji Mkuu wa Upinzani, yanatosha sana, lakini kutokana na wachangiaji wengine kutaka kufanya ubishi usio wa lazima *for the sake of argument* tu, ndiyo nimeona nichangie kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala ninalotaka kuchangia ni suala la ndege ya Mheshimiwa Rais. Kweli Mheshimiwa Rais anahitaji ndege imara na bora na siyo bora ndege, hili halina mjadala, lakini siyo ughali wa bei ya ndege ndiyo ubora wa ndege. Ndege yetu ni lazima iwe bora, lakini siyo ya fahari sana. Tusiwe kama ndugu zangu enzi zile za kale, Wasukuma walikuwa wanakwenda dukani kununua shati, koti, gauni au chochote kile, wakifika wanasema nataka koti, shati, gauni, khanga ya Shilingi 150,000/= wakati koti au khanga bei yake inaeleweka, lakini kwa sababu hajui, anajua koti la bei ghali ndiyo bora, ndiyo hivyo. Sasa, wakati huo haupo tena umepita, ni lazima tuangalie hali halisi. Hivyo, tununue ndege ya kufuatana na hali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna matatizo mengi sababu ya umaskini uliokithiri, kama mtu anaweza kula nyama kila siku ili apate *protein,* lakini hana fedha za kununua nyama kila siku ili apate *protein*, basi inabidi anunue kilo chache na agawe mafungu madogo madogo ili apate *protein* kila siku au ale maharage ili mradi apate *protein.* Kwa misingi hiyo suala la ndege ya Rais ni muhimu, ila tupate ndege *to our standards.* Waswahili husema jikune unapofika.

**MHE. ABDULLATIF H. ESMAIL:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya, Naibu wake, Mheshimiwa Dr. Maua A. Daftari, pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Salim Msoma, kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuchangia mambo yafuatayo: Kwanza, ni kuhusu tiketi ya *ATC Limited*. Kwa hivi sasa tiketi hizo ni za *South African Airline* na

hazina alama yoyote ya utaifa wetu, nashauri tiketi hizo ziwe zina sura za ubia pamoja na ndege zote ziwe na Nembo ya Taifa yaani Twiga.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, *TTCL* bado haijasambaa Vijijini Zanzibar, kwa hivi sasa Utalii umeendelea na kuzidi hasa kwenye fukwe za bahari kama Nungi, Paje, Matemwe na kadhalika. Ni muhimu kuwepo kwa simu za *TTCL,* zisitegemewe simu za mkononi ambazo husaidia, lakini hazina *reception* nzuri hasa wakati wa mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, naishauri Wizara kuwahamasisha wenye ndege *(Air Services),* kuweka safari za Dodoma - Dar es Salaam, Dar es Salaam - Dodoma - Bukoba na kuongeza safari za Dar es Salaam - Arusha, Dar es Salaam - Mwanza ambazo zina abiria wengi ili kuwepo na ushindani na hatimaye nauli kupungua *due to harsh competition.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ninaishauri Wizara kuwa macho na Kampuni za nje za Simu za Mkononi. Kwa mfano, kuondoka kwa *Tritel* kumewatia hasara kubwa wafanyabiashara kwa kubakiwa na *lines (Sim Cards)* na *voucher* za malipo ambazo walikuwa bado hawajaziuza kutokana na uondokaji wa ghafla wa Kampuni hiyo. *Voucher* na *Sim Cards* zimerudishwa kwa *Tritel*, lakini hawakulipwa fedha zao *(refund)* na wala hawakupata maelezo yoyote. Kwa hiyo, Wizara iwe macho na kuwalinda wafanyabiashara wa nchi yetu. Kwa hivi sasa huduma za *Mobitel (buzz)* zinazorota, Wizara isikae kimya ilifuatilie suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, naishauri Wizara idumishe na ihakikishe kwamba, sigara hazivutwi ndani ya ndege wakati wa safari *(No Smoking Flight).*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi na natoa pongezi kubwa kwa hotuba nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kuishukuru sana Wizara kwa kutuletea simu katika Mji/Kijiji cha Mtamba (Matombo) kwenye Tarafa ya Matombo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafadhali naomba sana simu hizo ziendelezwe kwenye Vijiji vya Mvuha, Duthumi, *Kisaki Station* na Kisaki - Gomero.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi kwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa kufanikisha hotuba yao.

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusema tangu awali kuwa naiunga mkono hoja hii. Vile vile, nampongeza sana Mheshimiwa

Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza madreva wote wa magari makubwa ya mizigo na abiria wapate mafunzo na vyeti kutoka Chuo cha Usafirishaji cha Taifa *(NIT)*. Hii itasaidia sana kupunguza ajali barabarani. Kwa wale wa Mikoani, *NIT* ishirikiane na *VETA* kutoa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza ili kuondoa kabisa tatizo la abiria kujazana katika mabasi, sasa hivi wao abiria ndio watozwe *fine* ya papo kwa papo, angalau mara mbili au tatu ya gharama alizotoa ili iwe fundisho kwa wale waliokosa kiti, wasisimame.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Zantel,* naomba sasa hilo tatizo la *exclusivity* litazamwe *critically* ili maslahi ya Taifa yatazamwe na ushindani wa kibiashara ufanyike vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana jitihada za Wizara kuimarisha Chuo cha *NIT*. Lakini bado naomba fedha ziongezwe ili wakufunzi na hata wanafunzi waweze kufanya tafiti zaidi ili kuboresha huduma za usafirishaji katika nchi yetu na hata nchi jirani na *SADC.* Tukumbuke hiki ni Chuo cha aina yake hapa Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara. Hivyo, huduma zake lazima ziwe za kiwango cha Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. SHAMSA S. MWANGUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, kwa kazi kubwa ya kutayarisha Bajeti nzuri na ambayo imegusa sehemu zote muhimu. Pia, natoa pongezi kwa Naibu Waziri na Kamati nzima iliyoshughulikia Bajeti hii. Napenda kuchangia kuhusu yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu uwanja wa ndege wa Arusha. Juu ya hali mbaya ya uwanja huu wa ndege ambao Wizara imekiri na kuipangia Bajeti ya Shilingi 100 milioni, lakini uwanja huu hauna chumba au sehemu ya abiria kusubiria mizigo baada ya kuteremka kutoka katika ndege. Mimi nimeshuhudia, tunasubiri mizigo nje, pembeni ya *gate* la kutokea. Hakuna utaratibu wowote! Nashauri fungu hilo pia lijenge sehemu ya kufikia abiria wakati wakisubiri mizigo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni kuhusu *computer* kama chombo muhimu cha mawasiliano. Kampuni za kuuza na kutoa mafunzo ya *computer* zimekuwa nyingi hapa nchini. Hiyo ni dalili nzuri sana ya mbio zetu za kuingia katika ulimwengu wa teknolojia ya kisasa. Lakini basi sifahamu kama kuna chombo maalum cha kudhibiti au kufanya *monitoring* na ushauri kuhusu *computer* ikiwemo matumizi, ubora, masomo na athari mbalimbali. Tusipoangalia, badala ya kunufaika na teknolojia ya mawasiliano kwa *computer,* tutajikuta tumekuwa *dumping ground* ya *junks* na *rejects* za *computer* kutoka nchi zilizoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Wizara hii ichukue hatua zinazofaa kuratibu teknolojia ya *computer.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Bajeti hii.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Wataalam wote kwa hotuba yao nzuri, yenye matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipitishie shukrani zangu kwako kwa Mheshimiwa Waziri kutenga Shilingi 250 milioni kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa gati Bandari ya *Mbamba Bay.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya *Mbamba Bay* ni ya Kimataifa inayohudumia pia nchi jirani kama Msumbiji na Malawi. Bandari zaidi ya kutokuwa na gati, pia haina umeme wa uhakika, eneo halijazungushiwa uzio na matatizo ya mawasiliano kama simu. Mheshimiwa Waziri, ni vizuri matatizo haya na mengine yakatafutiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ziwa Nyasa tunahudumiwa na meli mbili, MV Songea na Iringa. Meli hizi zimezeeka na zinafanya kazi kwa taabu sana. Ingefaa kwa sasa zikanunuliwa meli mpya ili huduma ya usafiri wa maji Ziwa Nyasa iboreke.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, naomba meli hizi zitoe huduma katika Bandari ya Ndumbi ili Wananchi wa maeneo hayo wafaidike na huduma hii muhimu kwa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru sana Mji wetu wa Mbinga kupata simu za kisasa aina ya *digital,* lakini Miji yetu Midogo ya Mbamba Bay, Liuli, Litembo na Maguu bado wanatumia simu za kukoroga. Tunaomba sana simu zote za kukoroga ziondolewe na tuwekewe simu za kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uwanja wa Ndege wa Songea ni mzuri, lakini hautumiki kwa ndege za abiria. Tunaomba ndege zinazokwenda Mtwara zisirudie hapo, zifike hadi Songea na zirudie njia hiyo hiyo (Songea, Mtwara, Dar es Salaam).

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini maombi yangu yatakubaliwa na Mheshimiwa Waziri kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuchangia hotuba hii naomba kwanza kutamka kwamba ninaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii inafahamika na kutoa kwa kina maelezo yahusuyo utekelezaji, mafanikio, pamoja na mapungufu yanayoikabili Wizara hii katika utekelezaji wa mipango yake na malengo ya utekelezaji.

Kwa maana hii kujipangia vyema mipango yake katika kipindi cha mwaka 2003/2004 katika Makadirio yake na hivyo ni matumaini yangu kwamba, Bajeti hii itapewa kipaumbele kwa ajili ya mafanikio yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na mafanikio yaliyokwishafikiwa na mipango mizuri ya mwaka huu, yapo mambo machache ambayo ningependa kuchangia zaidi katika hotuba hii ya Bajeti ikiwa kama ni kuboresha maendeleo ya nchi yetu kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naipongeza Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, kwa mashirikiano yao na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuwapatia huduma wananchi wao na kuwapelekea kutoka katika enzi ya teknolojia ya kizamani na kuingiza katika karne mpya ya Sayansi na Teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri sana Wizara hii iendelee kuishauri Kampuni ya Simu ya *ZANTEL* (Zanzibar). Kampuni ambayo inaonyesha kuwa gharama zake ni nafuu ikilinganishwa na Kampuni nyingine za simu za mkono hapa Tanzania, iongeze huduma zake hadi kufikia Tanzania Bara kwa haraka ili kutupunguzia gharama na kuzishawishi Kampuni nyingine kupunguza gharama ya huduma zao kutokana na ushindani wa kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningeomba Serikali kwa maana ya Wizara hii ya Mawasiliano na Uchukuzi, kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kulizingatia zaidi ni suala la usafiri wa bahari na kuona kuwa kunakuwepo usafiri salama katika bandari zetu kwa kuzikagua ngazi zinazotumika wakati wa kuingia na kutoka katika vyombo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninaomba kuchangia ni suala la mpango wa kuanzishwa kwa maeneo huru *(EPZ),* ili kuchochea maendeleo ya shughuli zenye maslahi kwa wananchi wake. Bandari ya Zanzibar ni pahali pazuri pa kuchochea maendeleo kwa Zanzibar, Tanzania, Afrika Mashariki na hata kwa dunia nzima, kwa kuzingatia mtandao wa biashara wa dunia *(globalization).* Kwa maana hii ninaishauri sana sana Wizara hii ilitupie macho suala la kuifikiria Zanzibar katika mashirikiano ya kuona kuwa katika mipango ya kimaendeleo ya Tanzania Bara, Bandari ya Zanzibar inafikiriwa na kupewa nafasi ya kuendelea na huduma zake kwa faida ya Tanzania kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hayo kwa maana nyingine nawatakia kila la kheri na mafanikio na ninaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei za simu za mkononi ni kubwa sana, *dollar* tano ni sawa na shilingi 5,000 au zaidi. Ni vema Sh. 5,000/= ziwe sambamba na *TTCL* ambayo ukitumia shilingi 5,000/= unaongea sana muda wa kutosha kwa hapa ndani. Gharama hiyo iwe kubwa tu kama unapiga nje ya nchi.

**MHE SALIM OMAR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake ambayo imekuwa na dira ya safari tunakoelekea. Lakini napenda nipate majibu sahihi ya ukusanyaji wa mapato yanayofanywa na *TRA* Zanzibar, ambayo sasa wafanya biashara wengi Zanzibar hawateremshi mizigo yao katika Bandari ya Zanzibar na badala yake huteremsha bidhaa zao katika Bandari ya Dar es Salaam na Tanga. Hivi kuna siri gani kati ya Serikali au chombo hiki cha *TRA* kuwafanya wafanyabiashara wasiteremshe bidhaa hizo katika Bandari ya Zanzibar na kuiacha Zanzibar hoi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nipate majibu ni kwa sababu gani simu za mkononi nyingi zimepanua mtandao wake hapa Tanzania na zinasikika kwa kiwango kikubwa. Lakini je, sababu gani Kampuni ya *ZANTEL* bado haijapata kibali cha kupanua mawasiliano yake? Je, Mheshimiwa Waziri, huoni ya kuwa huko ni kuwanyima mawasiliano Wazanzibari na ndugu zao walioko Tanzania Bara?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamtakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri, katika kazi zake kwa Taifa hili na kazi nyinginezo. Majibu ni muhimu. Ahsante.

**MHE. SUMRI A.S. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa asilimia mia moja. Pili, natoa shukrani kwa yote yahusuyo maendeleo yaliyofikiwa na yanayotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri ni kuhusu gati huko Karema kando ya Ziwa Tanganyika. Katika ziara ya Mheshimiwa John Malecela, akiwa Waziri Mkuu, huko Karema mnamo mwaka 1994, aliahidi tujengewe gati, ili pawe soko huria kati yetu na nchi za jirani. Tangu wakati huo hadi sasa hatujaona utekelezaji wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hiyo inaleta kero kwa wasafiri wa Karema na vitongoji vyake, kiusalama kuingia na kutoka melini, Karema ina wavuvi wengi na kilimo cha mpunga kwa wingi. Naomba tufikiriwe.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wote wa Wizara hii, chini ya Katibu Mkuu, kwa kuandaa hotuba nzuri yenye maelezo ya kina iliyowasilishwa kwa ufasaha na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usafiri wa reli na meli kwa wasafiri wa Kanda ya Ziwa ndio usafiri salama na wa nafuu, ingawa si wa haraka, lakini inavyoelekea usafiri huu utapata ushindani mkubwa kwa jinsi barabara zinavyozidi kuboreshwa. Kwa

hiyo, nashauri mikakati ya makusudi ifanywe ili kuboresha huduma mbalimbali katika treni na hata meli. Huduma kama vile ya chakula kiwe kizuri na kwa bei nafuu. Usafi katika sehemu zote liwe ni jambo la msingi, matandiko yawe safi wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa chakula kinachoandaliwa ndani ya treni ni bei ya ghali na hasa ni kwa ajili ya wasafiri wa daraja la I na II, je, Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba huduma ya chakula inayotolewa na mama lishe pale Stesheni ya Salenda inastahili kuboreshwa kwa kuwa wasafiri wengi huifurahia huduma hiyo?

Ningeomba na kushauri uongozi wa reli uwasaidie akinamama hao na vijana kwa kuwajengea mabanda ambapo wasafiri wanaweza kupata chakula kwa utulivu zaidi na kwa heshima zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupongeza hatua zote za kufanyia matengenezo ya viwanja vya ndege hasa kile cha Bukoba. Matumaini ya Wana-Kagera ni kupanuliwa kwa uwanja huo na kuuwekea lami. Tusubiri hadi lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Makampuni ya simu za mkononi ambayo yameuwezesha Mkoa wa Kagera kuwa karibu na sehemu nyingine za dunia kutokana na uwezo wa kuwasiliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja hii.

**MHE. STANLEY H. KOLIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri na napongeza utekelezaji wa shughuli za Wizara yake katika kipindi cha mwaka 2002/2003. Hata hivyo, nataka kumkumbusha Mheshimiwa Waziri, mambo machache yanayoitatiza Wilaya ya Ludewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Wizara kwa kuanza sasa kutazama hali ya uchukuzi wa Ziwa Nyasa hususan kwa ujenzi wa magati katika Bandari ya *Mbamba Bay*, uamuzi huo unapongezwa kwa dhati kabisa. Hata hivyo, tunaiomba Wizara kuanza kushughulikia Gati la Bandari ya Manda, ambalo limebomoka kwa asilimia mia moja kwa vile halijashughulikiwa kwa muda wa miaka mingi. Bandari ya Manda, *Mbamba Bay* na Itungi ndiyo zenye abiria wengi katika Ziwa Nyasa. Tunashauri gati litakalofuata liwe la Manda.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado lipo tatizo sugu la uendeshaji wa meli ya MV Iringa, meli pekee inayotoa huduma kwenye vituo/Bandari za Tarafa za Mwambao wa Lumbila, Makonde, Kilondo, Lupingu katika Wilaya ya Ludewa. Meli hiyo kabla ya ukarabati ilisimama kufanya kazi kwa kipindi cha miaka takriban minne. Baada ya matengenezo mwaka 2002 huko Malawi, imefanya kazi miezi mitatu ikasimama hadi leo. Je, Serikali inatamka nini kuhusu meli hii ya MV Iringa?

Habari nilizonazo ni kwamba, meli hiyo matengenezo yake yamekamilika. Je, ni lini itaanza kazi ili kuwaondolea dhiki na kero wakazi wa Tarafa ya Mwambao. Aidha, kwa nini meli ya MV Songea isifanyiwe uchunguzi upya wa kuiwezesha meli hii

angalau kutua katika Bandari za Makonde (Nsisi) Kilondo (Ifungu) kwa Tarafa ya Mwambao - Ludewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo malalamiko kutokana na utaratibu wa muda wa kuanza kuondoka meli kwenye Bandari ya Itungi, miaka ya nyuma meli zilikuwa zinaondoka Bandari ya Itungi mapema asubuhi, hivyo meli zilikuwa zinapita kwenye bandari mchana, lakini utaratibu wa sasa unawaweka abiria kwenye Bandari ya Itungi kwa muda wa saa zaidi ya nane na eneo hilo halina huduma za hoteli. Tunaomba meli ziondoke asubuhi kama huko nyuma. Utaratibu wa kuondoka Itungi saa kumi ufutwe hauna maslahi kwa abiria ila unawaongeza mateso tu kwa wahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaombwa kuanzisha huduma za simu za *TTCL* kwenye Vijiji/Miji ya Mlangali, Lugarawa, Manda, Mundindi, Maranga na Mawengi. Uchunguzi wa awali ulikwishafanywa na Kampuni ya simu.

**MHE. MWADINI ABASS JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ya Mawasiliano na Uchukuzi pia ina jukumu la kusimamia usalama wa vyombo majini, abiria na mizigo. Wizara hii imekuwa inawaelekeza na kuwakumbusha wenye vyombo wote vya majini wakati wote kufuata sheria na taratibu zote za usalama wa vyombo vyao. Aidha, wenye vyombo hivyo wanatakiwa kuhakikisha kuwa vyombo hivyo vinakaguliwa katika muda unaotakiwa. Napenda kuipongeza Wizara hii katika utekelezaji wa jukumu lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuchukua hatua zote za tahadhari kuepusha ajali za vyombo vya majini, lakini bado kuna ongezeko kubwa la ajali hizo na maisha ya Watanzania walio wengi yamepotea. Kama tunavyofahamu kwamba, uchumi wa wananchi wa Pemba unategemea zaidi kilimo na biashara. Kumekuwa na biashara kubwa baina ya Pemba, Tanga na Mombasa. Bidhaa nyingi za vyakula na vifaa vinginevyo mara nyingi watu wa Pemba huwa wanajipatia kutoka Tanga na Mombasa. Lakini kwa bahati mbaya ni muda mrefu sasa wafanyabiashara hawa kutoka Pemba huwa wanatumia vyombo vyao vya asili (Mashua, Jahazi na Ngalawa) kuvuka kutoka Pemba kwenda Tanga, Mombasa na hata Unguja.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya vyombo hivi hasa yanakuja kutokana na sababu kwamba, hakuna vyombo vya kisasa (meli, boti), ambazo zina ratiba maalum ya safari za kwenda Tanga na Mombasa. Sasa kwa sababu wananchi wa Pemba wanatumia vyombo vya asili kufanya shughuli za kibiashara baina ya Tanga na Mombasa, mara nyingi hutokezea ajali za vyombo hivyo na kusababisha kupotea kwa maisha ya watu na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya nyingine Serikali mpaka hivi leo bado haijaona umuhimu wa kuweka vyombo vya uokozi pale ambapo panatokea ajali za vyombo vya baharini. Lakini la kushangaza zaidi ni pale ambapo Serikali inapoonekana kutojali panapotokea ajali za vyombo vya baharini hasa baina ya Pemba, Tanga na Mombasa. Si mara nyingi kusikia Serikali ikitoa walau mkono wa pole au kutoa fidia kwa wanaopata ajali. Hali hii inathibitishwa na hii ajali iliyotokea Pemba hivi karibuni,

mashua iliyopotea kwa muda wa siku tatu na kupoteza maisha ya Watanzania wasiopungua 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Waziri, azingatie taratibu za kiusalama za vyombo vya baharini ikiwa ni pamoja na vyombo vya asili ambavyo ndiyo vingi na maarufu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, afikirie na hatimaye atupatie boti au chombo ambacho kitasaidia kutoa huduma za uokozi pale ajali za baharini zinapotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, ninaiomba Serikali basi kama ambavyo inajali ajali zinazotokea katika maeneo mengine ya Jamhuri, kwa mfano, ajali za treni, MV Bukoba na vivuko vingine, pia ijali na kuona ni miongoni mwa Watanzania kwa ajali zinazotokea baharini katika Visiwa vya Unguja na Pemba. Aidha, waathirika nao pia wapatiwe fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. OMAR JUMA OMAR**: Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mawasiliano katika dunia sio starehe bali ni ukombozi wa wanadamu katika dunia, kwa hiyo, simu ni muhimu sana hasa simu za mkononi kwani hata mkulima akiwa shambani anaweza kuwasiliana na mtu yeyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa simu ni muhimu, lakini watu wengi hushindwa kununua simu kwa ughali wa simu hizi, hivyo tunaomba hizi simu zipunguzwe ughali ili watu waweze kumudu matumizi ya simu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo gani ambalo hadi leo Kampuni ya Simu za Mkononi ya *ZANTEL* haijafika hata Mkoa mmoja wa Tanzania Bara bali inaishia kule kule Zanzibar tu wakati Kampuni nyingine zinafanya kazi karibu Tanzania nzima? Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iiruhusu *ZANTEL* ienee Tanzania nzima kama Kampuni nyingine.

Hali ya usafiri wa baharini sasa hivi ni wa kubahatisha kwa sababu karibu vyombo vyote vya baharini vimechakaa na vimetumika kwa muda mrefu bila kufanyiwa matengenezo, kwa hiyo, ipo haja ya Serikali kuvifanyia ukaguzi vyombo hivyo ili usalama wa wananchi na mali zao upatikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Tanga - Pemba bado mpaka sasa hakuna usafiri wa uhakika na kupelekea watu wengi kupoteza maisha yao, kwa hiyo, tunaiomba Serikali kwa kupitia Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, iweke chombo cha uhakika ili watu wapate usafiri wa usalama na Serikali iweze kupata mapato mengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usafiri wa ndege, ipo haja ya kuboresha viwanja vyake vya ndege ili wananchi wakidhi haja zao, kwa sababu mpaka sasa katika

Kiwanja cha Ndege cha Pemba hakuna taa na hivyo mwisho wa kutua na kuruka kwa ndege katika kiwanja hicho ni saa 12 jioni. Kwa hiyo, ipo haja ya kukiboresha kiwanja hicho kwa kukiwekea taa ili kiweze kufanya kazi kwa muda wa saa 24 kwani kufanya hivyo ni kuiongezea Serikali yetu mapato.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Napenda pia kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake, nikiwajumuisha na wataalam wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa mwanzo ni kuhusu udhaifu wa huduma wa baadhi ya Makampuni ya simu. Mfano hivi sasa Kampuni ya *Mobitel,* imekuwa inasumbua wateja hasa katika utiaji wa kadi, hivyo naomba Wizara ifuatilie kwa makini huduma za Kampuni hatimaye kuzishauri kitaalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tunakumbuka ajali mbaya ya treni iliyoua mamia ya Watanzania, hivyo Wizara haina budi kuhakikisha usalama wa reli yetu kiutawala, haiwezekani hadi leo abiria wasafiri ndani ya mabehewa ambayo yana giza, ni kweli Wizara haina uwezo wa kuweka *bulb* ndani ya mabehewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, dunia hivi sasa ipo ndani ya utandawazi wa soko huria, ni aibu kwa Wizara kuzungumzia suala la *ZANTEL* kutokufanya kazi ndani ya Tanzania, hii inapunguza sifa ya Wizara nzuri inayofanya kazi siyo kwa kubahatisha. Jimbo langu la Mfenesini ni sehemu moja inayotumia huduma ya mtandao wa simu za mkononi katika kiwango kikubwa. Kwa niaba ya wananchi, naiomba Wizara itazame kuweka simu za vibandani katika Soko Kuu la Mfenesini kwani ni sehemu moja kubwa ya kibiashara iliyokua, kwani lipo soko, Mahakama ya Wilaya na Shule ya Sekondari na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kukamilisha ufungaji wa *radar* na hatimaye inafanya kazi. Naomba Wizara iwaangalie watalaam wa mitambo hii yenye nguvu za *electronic* katika kuwapatia chakuala maalum na pia kufundisha mafundi wa kutosha kukabiliana na kudhibiti afya za mafundi *(Technicians).*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nachukua fursa hii ya mwisho kupongeza huduma ya simu zinazotolewa katika Ukumbi wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja tena kwa asilimia mia moja, ahsante.

**MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa uchambuzi wa Bajeti hii kama inavyohitajika na kugusia maeneo yote. Naanza kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuchangia kwenye huduma ya simu za mkononi. Napenda niwashukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kusikiliza

kilio changu cha muda wa miaka miwili iliyopita kuhusu kupata huduma hii muhimu ya mawasiliano ya simu katika Jimbo langu, nashukuru tatizo hili limeondoka. Naishukuru Kampuni ya *ZANTEL,* lakini ningependa Kampuni hii izidi kupanua mawasiliano yake kwa sababu kuna baadhi ya sehemu nyingine hazipati mawasiliano vizuri kama inavyotakiwa. Mheshimiwa Waziri, nimepigiwa simu ni kwamba, wananchi wa Jimbo la Kiwani wanashukuru sana kwa kuwaondolea tatizo hili, lakini wanakuomba uzungumze na Kampuni ya *ZANTEL* waongeze kupanua mawasiliano ili wapate mawasiliano mpaka watakapokuwa wamo ndani wamelala, isiwe lazima watoke nje.

Mheshimiwa Naibu Spika na mimi nataka niungane na wenzangu kuhusu kilio hiki cha gharama kubwa kwa simu za mkononi. Naomba Mheshimiwa Waziri, tuwafikirie wananchi wetu tukilinganisha na huduma hii ya lazima kwa kila mwananchi. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali punguzo kubwa hili la gharama ya bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka kuchangia kwenye usafiri wa baharini, hususan usafiri wa Tanga na Pemba. Bado upo usumbufu mkubwa wa usafiri wa Pemba na Tanga kwani boti inayokwenda Pemba/Tanga bado hakukidhi haja, kunahitajika kupangiwa usafiri mwingine wa uhakika wa meli zetu hizi tulizonazo, kupangiwa ratiba maalum ya kufanya safari ya kwenda huko ili kuwaondolea tatizo la usafiri wananchi wanaokwenda Tanga/Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu ni machache, lakini narudia kumwomba Mheshimiwa Waziri, aangalie sana usafiri huu wa Pemba/Tanga na kupanua zaidi mawasiliano ya Kampuni ya *ZANTEL* kwenye Jimbo la Kiwani ili wananchi wangu wazidi kunufaika na huduma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, narudia kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, kwa hotuba yenye mwelekeo na matumaini. Naunga mkono hoja hii na nina ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Usalama ya Viwanja vya Ndege, haithaminiwi na kupewa umuhimu unaostahili. Watumishi wake wanaonekana kama ni *Security Guards,* hasa kwa wale walioajiriwa zamani ambao mishahara yao bado ni midogo na wanazidiwa na wahudumu walioajiriwa na *TCAA* na *TAA*. Kufanyike *harmonization* ya mishahara ili walioajiriwa zamani na wana sifa za masomo/elimu hasa za *ICAO* wapandishiwe mishahara. Hivi sasa *TAA* hawajui wako wapi kimaslahi ingawa wanapata mishahara. Kwa jinsi ya kazi zao, napendekeza waajiriwe na *TCAA* ambao wanajua umuhimu wao.

Kumekuwa na mtindo wa kutoa vifuta machozi, pale kunapotokea ajali za treni, meli na vivuko. Thamani ya vifuta machozi hivyo ni ridhaa ya Serikali na msafiri huwa hana uhakika kama atapata chochote au la. Ni vema sheria zitazamwe upya ili vyombo hivyo viwekewe Bima na waathirika walipwe kwa mpango huo wa Bima badala ya ridhaa ya msafirishaji. Hii ni muhimu hasa tunapobinafsisha vyombo hivyo.

Naiomba Wizara iiboreshe Bandari ya Kigoma ili iweze kutoa huduma bora kwa nchi jirani za *DRC* na Burundi ili washawishike kuitumia. Ni vyema pia *TRC* iharakishe kusafirisha mizigo kwa mabehewa ili *turnround* iwe ndogo hata kwa mabehewa machache yaliyopo. Inachukua muda mrefu sana behewa toka Kigoma kwenda Dar es Salaam na mara nyingi mabehewa ya mizigo upatikanaji wake umegubikwa na rushwa. Kwa kuwa Kigoma ni mpakani, usafiri wa treni kuhudumia wasafiri toka *DRC* na Burundi na wasafiri toka pia Mkoa wa Kagera walioogopa kusafiri kwa meli. Tunaomba mabehewa ya abiria yaongezwe kwa kuzingatia hali hii. Chini ya Mpango wa *TTCL*, maeneo kama ya Mamba, Kasanda, Kakonko, Muhange na Nyabibuye kulikuwa kuwekwe huduma ya simu. Huduma hii itafikishwa lini katika maeneo haya?

Mwisho, ili tuweze kutumia ipasavyo Soko la *DRC* na Burundi, ni vyema tukapanua Uwanja wa Ndege wa Kigoma. Hii pia itakuza utalii wa eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema tena naunga mkono hoja hii.

**MHE. KHADIJA SALEH NGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, kwa hotuba yake nzuri, nami naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Nami naomba kutoa mchango wangu kuhusu simu za mkononi. Ukweli ni kwamba, wakati simu za mkononi zilipoanza kufanya kazi, sote tulifurahia huduma hizi, maana ziliwawezesha wananchi wa Tanzania, hasa wale wafanya biashara wadogo kuweza kumiliki simu hizo. Maendeleo haya si madogo ukizingatia kuwa asilimia kubwa ya watanzania wanatumia simu hizo. Kampuni hizi za simu za mkononi hivi sasa wanapata faida maradufu siku hadi siku.

Umefika wakati Serikali itoe kauli kwa Kampuni husika *CELTEL, Mobitel* na hasa *VODACOM,* wapunguze gharama ya ununuzi wa kadi. Kwani ukiweka *dollar* tano hasa nia na madhumuni ni kwa ajili ya kuwahi kuzungumza na mwenzio. Je, huku ni kumnufaisha Mtanzania, ambaye naye ni haki yake kutumia matunda ya nchi yake au ni kumfanya awe fukara; ikiwa sisi Waheshimiwa Wabunge tunapiga kelele; je, wananchi wa kawaida watasema nini au tuseme Serikali inajali maslahi ya Makampuni kuliko kuwajali wananchi wake? Hebu tuige mfano hai wa Kampuni ya Simu ya *ZANTEL* inavyowajali wateja wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. KIJAKAZI KHAMIS ALI:** Mheshimiwa Spika na mimi napenda kuchangia hoja hii. Naanza kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa hoja nzuri yenye mwelekeo wa kuinua na kuboresha hali ya maendeleo katika nchi yetu. Vilevile napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge wanzangu, kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya wa CCM na *CUF,* kwa ushindi wao katika chaguzi ndogo zilizopita mwezi Mei, 2003.

Huduma za simu za mkononi, *VODACOM,* imepanua mtandao wake mpaka umefika katika sehemu nyingi za Tanzania. Kwa hiyo, napenda kuipongeza sana Kampuni hiyo pamoja na Kampuni ya *CELTEL*. Kwa upande wangu naomba sehemu ya Zanzibar Mkoa wa Kaskazini Unguja, tufikishiwe huduma ya simu hizi kwa sababu ukienda Mjini ukipiga simu unapata na ukipigiwa unapokea, lakini ukifika Kibweni ukipiga simu wala hupati na ukipigiwa simu huwezi kupokea. Kwa hiyo, hilo ombi langu naomba lizingatiwe.

Kwa hayo machache, sina zaidi. Napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupewa nafasi hii, kwanza naomba nianze kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Kama ilivyojitokeza kwenye ukurasa wa 31 wa hotuba yako kwamba bado ajali katika njia ya reli zinazomilikiwa na mashirika yote mawaili *TRC* na *TAZARA* zinaendelea hivyo ninaishauri Serikali ipange mikakati ya makusudi ya kukabiliana na tatizo hili ili kuweza kuepusha ajali za mara kwa mara zinazopelekea vifo na ulemavu kwa raia wetu.

Mheshimiwa Spika, pia nielezee kuhusu kunyimwa kwa kampuni ya simu ya *ZANTEL* upande mmoja wa Muungano Tanzania Bara ni kero kubwa na kuinyima haki kampuni hii, huo ni udhalilishwaji wa makusudi kwani inafahamika lakini Serikali ya Jamhuri ya Muungano wanalifumbia macho, hivyo kero hii inadhoofisha maelewano ya Muungano wetu kwani manung'uniko haya yanaweza yakatatuliwa kwa njia ya kukubaliwa kampuni hii kufanya shughuli zake huku Tanzania Bara, inaonekana kuna siri au kigugumizi kwa Serikali juu ya maamuzi ya suala hili, hivyo Serikali ikae kitako, sasa wakati umefika kupunguza au kuondoa kabisa kero za Muungano.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa anga kutoka sehemu mbalimbali ya Tanzania Bara kwenda Visiwani Unguja na Pemba hauridhishi hivyo ninaiomba Serikali ikatafakari kwa makini zaidi ili kuweza kupanga ratiba katika viwanja mbalimbali vya Tanzania Bara kusafirisha abiria hao Unguja na Pemba kwa mfano Dar es Salaam kwenda Pemba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali na Wizara husika sasa wakati umefika wa kuunda mamlaka ya kusimamia usalama wa vyombo vya usafiri majini na siyo kauli ya maandalizi hii kauli imechosha kwani baadhi ya vyombo hivyo havifuati sheria na taratibu zinazotakiwa, hivyo inapelekea vifo vya abiria na majeruhi kadhaa. Naomba Serikali itilia maanani na uamuzi muafaka.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote kwa kuandaa hotuba hii ya Bajeti kwa umahiri mkubwa sana. Vile vile pongezi zangu Mheshimiwa Waziri aziwasilishe kwa kampuni ya simu za mkononi *Celtel* kwa kuwa kampuni ya kwanza kuweka simu Wilaya ya Mbinga.

Kitendo hiki kiwe changamoto kwa makampuni ya *Vodocam* na *mobitel* kuwekeza katika Wilaya hiyo. Baada ya kutoa pongezi na shukrani zangu naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hotuba ya kusisimua na yenye kuleta matumaini makubwa ya ushirikiano wa maendeleo na Malawi pamoja na makubaliano ya kuendeleza kukuza uchumi wa nchi hizi mbili, mbona Serikali hasa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kuchukulia maendeleo ya Ukanda wa Mtwara kwa kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya mradi wa *"study on berths development on lake Nyasa"* nashauri mwaka ujao wa fedha za mradi huo upewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuhusu Kiwanja cha Ndege Songea licha ya uwanja huo kuwa katika hali nzuri hakuna huduma za ndege katika uwanja huo. Je, Serikali inaweza kufanya utafiti ambao utawezesha kuufanya uwanja huo kuwa wa manufaa. Naamini matokeo ya utafiti huo utasaidia pia viwanja vipya vinavyojengwa kwa mfano Songwe na Singida.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na nawatakia utekelezaji mwema wa bajeti ya 2003/2004 kama mlivyojipangia.

Napenda kuipongeza Wizara kwa *TRC* kujenga *waiting shed* katika *station* yetu ya Shinyanga. Nashukuru sana. Ninaiomba Serikali pamoja na kununua ndege ya Rais ipange kununua *Helicopter* mpya yenye *engine* mbili kwa matumizi ya viongozi wanapotakiwa haraka mahala ambavyo havina viwanja vya ndege.

Kuhusu hali ya hewa miaka ya nyuma kulikuwepo na ripoti ya kila mwaka ya *Hydrological Annual Report* ambayo ilikuwa inatolewa kila mwaka, taarifa hii kwa miaka mingi haitolewi ni vyema, taarifa hii iwe inatolewa hasa kwa watumiaji wa hali ya hewa kwa kilimo nakadhalika. Hapo awali *rain gauges* zilikuwepo kwenye Ofisi za Serikali zote na mashule ikiwa pamoja na *Wind Gauge.* Utawala ulikuwa mzuri ni vyema ukarudiwa.

Mheshimiwa Spika, katika uwanja wetu wa Shinyanga naomba sana kwa Bajeti ya mwaka ujao 2003/2004 Wizara isaidie kuweka lami na kupanua ili ndege kubwa ziweze kuwa zinatua, kubeba wasafiri na hata mizigo. Ninaomba sana tukumbukwe maana mchango wa Mkoa wa majirani zetu kwa Taifa letu ni mkubwa sana kiuchumi.

Vile vile kutokuwa na umuhimu wa *TRC* kwenye uchumi wa Tanzania ni vyema ikaendelea kuwatafutia misaada na mikopo kwa ajili ya kuboresha huduma ya reli. Baada ya kuwa na barabara ya lami kuelekea Mikoa ya Ziwa *TRC* itabidi iboreshe huduma zake na tariff zake kuboresha ili kuhimiri ushindani. *TRC* na *THA* ni vyema vikawa pamoja ili fedha za rahisi kutoka *THA* zisaidie katika ku-subsidize taarifa na gharama kubwa za kuendesha *TRC* ili taarifa zake ziweze kuwa za chini zaidi kuzidi gharama za barabara kama ilivyokuwa zamani wakati wa *Tanzania Railways and Harbours or East African Railways and Habours.*

Ubinafsishaji wa *TRC* lazima uangaliwe kwa makini sana maana Waingereza walibinafsisha railway lakini ikashindikana. Nawatakia kazi njema katika kutekeleza Bajeti na malengo mliojiwekea mola awe nanyi katika kuboresha maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

**MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, katika maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Profesa Mark J. Mwandosya Mbunge kuhusu ubinafsishaji wa Shirika la Reli *(TRC)* amesema tenda ilipotangazwa ilipata wawekezaji sita ambao kati ya hao wawekezaji sita wote walijitoa amebaki mmoja. Serikali imeona si vizuri akaachwa mmoja peke yake na kuamua tender hiyo itangazwe upya.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kubakia mwekezaji mmoja kati ya waombaji sita hakileti picha nzuri. Kwa hiyo, nashauri Serikali ifikirie kukubali kuwekeza katika Shirika Reli badala ya kutangaza tender kwa mara ya pili. Tabia ya wawekezaji sifa zilizofanya wawekezaji watano wajitoe zitakuwa zimetangazika. Jambo hilo ni kudhalilisha shughuli za shirika letu na Serikali yetu. Kwa kuwa Shirika la Reli linatumia sana mafuta ya *diesel,* ninapendekeza kama Hazina inavyotoa fungu kwa *TANROADS,* ifanye hivyo kwa Shirika la Reli.

Mheshimiwa Spika, uzoefu umetufundisha sera ya ubinafsishaji imefanya vizuri katika baadhi ya sekta za mashirika ya umma, lakini upo ushahidi sera hii ya ubinafsishaji haikufanikiwa katika baadhi ya sekta nyingine. Kwa hoja hii iwapo shirika la reli litabinafsishwa na matokeo yake ya utekelezaji yakawa mabaya kama ilivyo kwa mashirika mengine yaliyobinafsishwa, hali ya matokeo hayo yataathiri sana pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utekelezaji wa Shirika la Reli unaliingizia pato kubwa katika uchumi wa Taifa letu na kwa kuwa tayari wawekezaji wamekwamisha onyesho *negative response,* Serikali lazima ikubali, isipokuwa na uangalifu mwekezaji atakayekuja ni kampuni tanzu yaani *subsidiary company* ya *holding National Company in their country.* Hali ikiwa na sura hiyo Shirika letu la Reli ya Taifa ambayo ni mali ya umma, itakuwa *owened by another National Railway holding company.* Kwa kuzingatia *history* ya upatikanaji wa uhuru wa nchi yetu na namna ambavyo tulivyosaidia katika ukombozi wa Bara letu la Afrika Kusini mwa *Sahara Desert,* haitakuwa vizuri kama nchi tulizozisaidia kupata uhuru wao leo waendeshe njia kuu za uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napendekeza aina yeyote ya ubinafsishaji wa Shirika la Reli, kama Serikali haijaingia kufunga mkataba na mwekezaji ni muhimu hiyo mikataba ya wawekezaji kabla ya kutiwa saini, Serikali ipeleke mikataba hiyo kwa Kamati ya Bunge ya Miundombinu na baada ya Kamati ya Miundombinu kupitia hiyo mikataba kwa kuzingatia umuhimu wa Shirika la Reli katika pato la uchumi wa Taifa letu, mapendekezo ya Kamati ya Miundombinu yaletwe mbele ya Bunge Zima kujadiliwa na kutolewa maamuzi. Ahsante.

**MHE. JANETH E. MASHELLE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ningependa kuzungumzia suala la mashirika ya sekta ya uchukuzi kama vile Shirika la Reli, *TAZARA* nakadhalika. Kwa kweli mashirika haya yana matatizo yanayokabiliwa nayo mfano uchakavu wa vifaa Mindombinu na raslimali. Vyombo hivyo vya usafiri kwa kweli vimechakaa vinafanya hata kuwatia wasiwasi wananchi. Vilevile husababisha kukosa mwekezaji/mkodishaji kuwa ni vigumu sana.

Lakini ninapenda kuishauri Wizara au Serikali ifanye utaratibu mzuri wa kuyasaidia mashirika hayo hasa kwa kuyasaidia yaendelee kutoa huduma ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu. Kwani mashirika hayo hutusaidia hasa kwa wafanyabiashara. Nchi jirani mfano Zambia, Malawi, Congo, Rwanda, Burundi na kadhalika.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri. Nawatakia utekelezaji mzuri. Naomba kutoa ushauri ufuatao kuhusu *TAZARA:-*

Reli hii inakwamishwa na wenzetu wa Zambia kwa kufanya yafuatayo: Wanapendelea kutumia reli za *South Africa* kuliko reli yao (ubinafsi), ni wafujaji wa mali ya umma na watumiaji ovyo wa mabehewa ya *TAZARA,* ni wategaji kazi na wabaguzi, wanapenda kuvuna kuliko kupanda mbegu, mishahara ya watumishi haina uwiano na mapato ya *TAZARA,* Shirika halikuzi maeneo yanayosaidia mapato kwa *TAZARA* kama Makambako na Bonde la Kilombero.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo napenda kutoa mapendekezo yafuatayo:

(i) Watumishi wakuu wa *TAZARA* wawe wanapatikana kwa kutangaza magazetini na wapatikane kutoka mahali popote duniani badala ya kutoka Zambia wakati wote.

(ii) *TAZARA* iwe na mifuko miwili na kila nchi isimamie mapato yake ili kuongeza ufanisi Dar es Salaam - Tunduma.

(iii) Makambako iongezewe huduma na kupanua eneo la mizigo karibu na *depot* ya mafuta mikakati gani? Mbao zimejaa kwa kukosa mabehewa? Kuweko na mikakati ya kujenga *feeder roads* katika maeneo ya Bonde la Kilombero, Mbarali, Mufindi, Njombe ili kuongeza mizigo ya kusafirisha.

(iv) Kama ni lazima *TAZARA* ibinafsishwe basi ni vizuri kuwakaribisha rafiki zetu Wachina.

(v) Kuna haja ya kufanya review ya management ya *TAZARA* na mishahara ya watumishi ili ilingane na mapato. Idara nyingine ziunganishwe ili upunguzaji gharama.

(vi) Tazara isiendeshwe kisiasa, bali izingatie misingi ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu Reli ya Mwambani (Tanga) hadi Musoma, Reli hii ilibuniwa kwanza na *East African Community* miaka ya 1970. Ni reli yenye faida kuliko reli zote katika Afrika. Ilijengwa itahudumia nchi za Congo, Uganda, Burundi, Rwanda na Tanzania. Kenya hawaipendi lakini Rais Museveni, anapenda reli hii ijengwe. Tatizo ni sisi. Kama inawezekana tuuze wazo ili ijengwe kwa njia ya *BOT* au *BOOT. It is now or never*. Hii ni reli ya kiuchumi. Tafadhali iwekewe mikakati ya ujenzi.

Tatu, kuhusu *Mtwara Corridor,* ukurasa wa 45 *much is being said but very little or nothing is being done.* Vuguvugu lililokuweko limeanza kupungua kwa nini? Hakuna *action plan* wala msukumo. Mratibu ataratibu nini? Je, sote tunaongea lugha moja mbele ya wahisani? Tafadhali Wizara zote zisukume utekelezaji wa *Mtwara Corridor* ili Watanzania wafaidike na mali asili iliyoko Ludewa. Muuza mawe na chuma.

**MHE. TATU NTIMIZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Naomba kuchangia machache kwa kutoa ushauri wa maandishi maalum.

Jimbo langu la uchaguzi, reli ya kati inapitika katika eneo kubwa lenye urefu wa takribani kilomita 140 kuanzia mpaka unaotenga Singida na Tabora. Kati ya stesheni ya Kaskazi na Ibulo kwenye eneo hili kuna vituo vya Magenge na vya stesheni. Vituo hivyo vinafanya kazi na familia zake ambao ni wapiga kura wazuri katika chaguzi zote aidha za Chama wakipendacho na za Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu.

Nimekuwa Mbunge wao kwa kipindi cha pili sasa. Hata hivyo nimekuwa kiongozi ninayewatembelea wapiga kura hawa kama kuwashukuru na pia kuona mazingira wanayokaa na wanavyofanya kazi. Waziri katika ziara hizo mbili nilizowahi kufanya kuwatembelea wananchi hao nimekuwa ninazunguka na uongozi wa reli kama vile *DME, DTM* hawa wote wakisiliza maelezo ya wafanyakazi wao na kuahidi kuyashughulikia. Cha ajabu Mheshimiwa Waziri, hakuna kinachoshughulikiwa kikamilifu. Wananchi hao walitoa malalamiko yao wanachokiomba ni kuona matatizo yao yanafanyiwa kazi au, wanajibiwa kwa maelezo, vipi imeshindikana?

Mheshimiwa Spika, ni kitu cha kuudhi sana kama humthamini mfanyakazi. Wafanyakazi hawa wanaishi maporini ni vituo vichache sana viko kwenye maeneo ya vijiji labda iwe ni *station* lakini siyo Magenge. Wafanyakazi na familia zao wana matumaini sana na uongozi ukifika lakini tulizunguka na kupiga porojo bila kuona matokeo ya ziara inakuwa ni aibu kwa uongozi. Matatizo yao ni kama haya yafuatayo:-

(i) Maji ya kutumia hawapelekewi kama ilivyo kawaida Magenge mengine yapo sehemu ambazo ni zaidi ya kilomita 9 hadi 15 ndiko wanapata maji ambayo si safi wala salama. Ni tatizo ambalo limekuwa la kuduma. Wanauliza waache kazi, treni zianguke kwa ajili ya kutafuta maji?

(ii) Vifaa vya kufanyia kazi kama *Gloves, boots,* kwenye reli inabidi ung'oe majani, wapange mawe, kuna wadugu, kuna kinyesi cha wanyama na binadamu. Aidha wasipange mawe au kufanya usafi au waambukizwe magonjwa kutokana na kushika kinyesi? *Boots,* aidha watembee na kufanya kazi katika maeneo ya reli bila *boots,* ili

wachomwe na miiba, misumari, waumwe na nyoka waingie kwenye maji wapate *fungus* au wajiepushe na madhara haya kwa kukaa magengeni ili reli isipate huduma?

(iii) Nyumba zao bado wanakaa kwenye nyumba za misonge. Bati zinachemka, sakafu zimebomoka, wadudu kana nge, nyoka na tandu ndiyo mahali pa kukaa. Nyumba hizi hazifanyiwe ukarabati tangu mwaka 1975 hata zile zilizojengwa vizuri kidogo na kuezekwa vigae lakini hali yake ni mbaya. Magenge ya Igalula, Malangwe yako Mbugani wakati wa masika, watoto na familia inabidi watoke ndani waingie kwenye mitumbwi ili wavuke. Hayo ni machache tu Waziri, angalau moja kati ya hayo yangeanza kutekelezwa, Wizara ingeonekana inajali wafanyakazi wake. Hii reli ni agenda ya uchaguzi wana haki zote. Hakuna juhudi za kuwasaidia, kuwatembelea tu viongozi wao inakuwa shida. Sasa je kutatua shida zao ndiyo itawezekana? Si rahisi kwa yote kutekelezwa lakini miaka 10 sasa hata moja halijashughulikiwa kikamilifu?

Mheshimiwa Spika, kichekecho miaka 2 iliyopita walipelekewa viatu namba 10 *pair* zote bila kuja huyu anavaa namba ngapi? Angalau eneo la Dodoma wafanyakazi walipatiwa vifaa wakati wa mvua. Sasa hata mapanga ya kufyekea pia inakuwa taabu, je wang'oe nyasi kwa mikono ambapo hata gloves hawana? Waziri panga ziara hata tukiwa hapa Bungeni kiasi cha siku 2 zinatosha twende ukasikie kilio chao la sivyo tukimaliza Bunge iwe agenda yako ya awali.Wasikilizeni wafanyakazi hawa kuwa na reli imara na pamoja na wafanyakazi hawa kupata mahitaji ya muhimu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na kungoja jibu la hatua za utekelezaji.

**MHE. SHAIBU AHMADA AMEIR:** Mheshimiwa Spika, na mimi napenda kujumuika na wenzangu kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi. Kabla sijaanza kuchangia na mimi nitaanza kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake aliyoitoa ambayo ina mwelekeo wa kuifanya Wizara hiyo ifikie malengo. Pia nampongeza Naibu Waziri pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuanza kuchangia mimi kwanza nitachangia suala la usafiri wa baharini. Vyombo vya baharini vilianza miaka mingi kwa kiasi na vyombo hivyo wakati viliponunuliwa vilikuwa vimetumika na baadhi ya vinginge vilikuwa vimeanza kuchoka, vingi ya vyombo hivi vinahitaji kufanyiwa matengenezo. Lakini vilikuwa vinatembea basi matajiri wanaona bado haujafika wakati wa kuvipeleka vyelezoni kufanyiwa ukaguzi na matengenezo.

Sasa tunaiomba Wizara ipange utaratibu maalum kwa kusimamia ukaguzi wa vyombo hivyo. Chombo kitakachokwepa kufanyiwa ukaguzi au matengenezo kinyimwe leseni kama vyombo hivyo vitaachwa kufanyiwa ukaguzi huenda siku moja vikasababisha maafa kwa wananchi wetu wanaosafiri kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, suala jingine ambalo nataka kuchangia ni tatizo la *ZANTEL.* Kila siku tunapata masuala kuhusu huduma za *ZANTEL* kwa nini huduma zake hazianzishwi kuenea Tanzania nzima kama makampuni mengine yanavyofanya? Suala

hili Mheshimiwa Waziri hebu limalize, suala hili lisizungumzwe tena hapa Bungeni, kuendelea kuzungumzwa suala hili watu watatafsiri kama ni kero ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, vile vile nitazungumzia kuhusu simu za mkononi ambazo siku hizi zimekuwa zinaibiwa sana. Mheshimiwa Waziri nakuomba ukutane na wenye makampuni ya simu hizi mfano *vodacom, mobitel, celtel* na *zantel,* ili warekodi *serial number* ya kila simu wakati ikiingia katika mitandao ya makampuni yao. Mfano kampuni ya *mobitel* idhibiti *serial number* zote za simu zenye kutumia *mobitel* na vile vile idhibiti *serial number* vile vile.

Baadaye kila kampuni impe *serial number* mwenzake na baadaye kama endapo simu itaibiwa baada ya mtu aliyeibiwa ataripoti kama kampuni yake, basi kampuni hizi zote ziambizane ya kuwa simu yenye serial namba fulani imepotea na kwa hivyo atakayeiba simu hiyo akitoa line na kutaka kuchukua line nyingine asipewa kwa kampuni zote. Mimi nafikiri hatua hii huenda ikapungua wimbi hili kubwa la wizi wa simu hizi. Nakuomba Mheshimiwa Waziri washauri wenye makampuni wabuni mtindo kwa njia ya kutumia serial number.

Mheshimiwa Spika, mwisho nampongeza kwa mtandao mzuri wa usafiri wa njia zote yaani anga na baharini au maziwa na reli. Mtu anajipangia safari na kufika alikotaka kufika kwa wakati kama anavyojipangia kwa suala la usafiri Tanzania tumepiga hatua sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia na mimi naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri yenye dira sahihi.

Aidha pamoja na changamoto ya hotuba hii naomba tu nizungumzie kero moja kubwa inayowagusa wananchi na hasa waendesha shughuli za uvuvi katika ziwa Victoria na kwamba nitashukuru kupata maelezo ya Serikali juu ya suala hili. Kero hii imesababishwa na Serikali kumteua wakala wa kuthamini na kudhibiti viwango vya ubora wa vyombo vya majini.

Ni kweli kuwa udhibiti wa vyombo hivi ni muhimu sana kwa usalama wa maisha ya watumiaji wa vyombo hivi pamoja na mali zao. Tatizo lililojitokeza ni kwa wakala huyu *Mbondo Marine Transport Project Limited* kuendeleza zoezi hili kinyume kabisa na matakwa ya sheria. Yaani amekuwa akifanya yafuatayo:-

(i) Kutumia vyombo vya dola kama polisi kwenda kusaka vyombo vya majini yaani mitumbwi na kutoza *fees* ya kuanzia shilingi 37,000/= kwa ajili ya ukaguzi tu.

(ii) Kutishia kuwakamata wamiliki wa vyombo hivi na kuwatoza faini yakushindwa kulipa papo hapo ada hiyo.

(iii) Kuharibu mitumbwi ambayo wananchi wameshindwa kulipia ada zake kwa siku hiyo.
(iv) Kulazimisha kununua maboya anayouza kwa bei ya juu kinyume kabisa na matakwa ya sheria.

(v) Kutumia lugha chafu na kubugudhi sana wananchi kwa mgongo wa dola, kitendo amacho kimekuwa ni kero sana miongoni mwa wananchi.

Sasa basi mimi mwenyewe pamoja na uongozi wa Wilaya ya Magu tulimwita na kumhoji kuhusu tuhuma hizo ambazo licha ya kushindwa kukiri mapungufu haya, bado ilionekana kuwa zoezi lake linafanyika kwa msingi wa wingu la rushwa. Si Serikali ya Mkoa wala mamlaka yoyote ilionekana kushirikishwa katika hatua hii. Aidha afisa kutoka Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, Mama Rhobi alikiri kukiukwa kwa zoezi hili na hasa katika Wilaya ya Magu ambapo yeye na Bwana Mbondo walihudhuria kikao hicho. Pia ilionekana dhahiri Bwana Mbondo yeye mwenyewe na maofisa wake hawana sifa za kitaalam kufanya kazi hiyo. Hivyo basi:-

(i) Naiomba Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi itoe tamko la kusitisha zoezi hili katika Wilaya ya Magu na kwamba kampuni hii ya Mbando itathiminiwe upya juu ya utendaji kazi wake ikiwa pamoja na wasifu wa maofisa wake.

(ii) Wizara itoe waraka wa kuwataka viongozi wa Wilaya washirikishwe ikiwa pamoja na kupambana juu ya sheria hii na ile ya maliasili kufuatia udhibiti wa vyombo vya majini ikiwa pamoja na ukataji wa leseni.

(iii) Wizara itumie maofisa wake ili walitazame suala hili kwa kushirikisha wadau.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. YETE S. MWALYEGO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wa Wizara yake kwa kazi nzuri wanayofanya na hotuba nzuri aliyowasilisha leo hii. Napenda kuchangia hoja ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege Songwe. Kama Mheshimiwa Waziri alivyobainisha kwenye hotuba yake kuwa asilimia 98 ya wakazi wamelipwa fidia ya nyumba, mazao na makaburi, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri. Hao waliobaki asilimia 2 natoa ushauri ufuatao:

Mheshimiwa Spika, iundwe kamati ya kusikiliza malalamiko. Kamati hiyo iwe na watu wafuatao. Wizara, *Tanzania Airport Authority,* Halmashauri ya Wilaya Mbeya, Mwakilishi wa Mshauri consultant, Mkoa.

Mheshimiwa Spika, wote wanaolalamika waandike barua kwa kupitia Serikali ya Kijiji, Kata na Halmashauri ili barua hiyo iende *T.A.A.* Barua za makundi ya watu zisiruhusiwe. Kila mwenye shamba, nyumba au kaburi aandike mwenyewe. Aeleze

malalamiko yake na anadai nini? Kamati ikae na kuchambua kila moja na kutoa maoni baada ya kufika kwenye site na kuonana na wahusika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la maji ya uwanja wa ndege kuna njia tatu za kupata huduma hiyo. Mto Songwe *(SOWACO),* Kisima, Mto Mbalizi. Chanzo cha mto Mbalizi kipo Kata ya Igale na kipo mlimani. Maji yatateremshwa kwa *gravity scheme* na kufaidisha wakazi wengi wa kata zifuatazo; Igale, Iwindi, Utengule/Usongwe Mji mdogo wa Mbalizi, Bonde la Songwe na Mshewe - Kijiji cha Ilota.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninaomba sana Wizara, Tanzania *Airport Authority* na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kuangalia uwezekano wa kutoa maji Mto Mbalizi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SIJAMINI MOHAMED SHAAME:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa na taadhima nataka nichukue fursa hii adimu sana kukushukuru sana wewe binafsi kwa namna unavyoliendesha vizuri sana Bunge hili Tukufu. Aidha nataka kwa kuanzia kuchangia bajeti hii nianze kwa kutamka tena kwa tahadhari kuunga mkono kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi na nina hakika kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Kitope, wanakubaliana nami kwani hotuba hii imeeleza kwa undani na fasaha mkubwa namna ambavyo inatekeleza maelekezo ya sera ya CCM kwa kuwatendea haki wananchi wa Tanzania hii bila ya kujali maeneo na itikadi zao.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii kwa muundo wake siyo ya Muungano wa moja kwa moja ila ninapenda kumshkuru Waziri kwa kuonyesha imani na upendo wake huko Zanzibar kwa kuimarisha kwa mtandao mzuri wa *Civil Aviation Authority a*mbabyo inakwenda kisayansi.

Pia napenda sana kuwashukuru wataalam wake kwa namna ambavyo wanatusaidia kuangalia usalama wa viwanja vyetu vya ndege vya Unguja na Pemba kwa hakika huu ni uungwana unaonyesha kukomaa kwake katika kuimarisha Muungano wetu wa Tanzania. Bado naomba Serikali kuipa msaada mkubwa wizara hii katika hatua za kupatiwa malipo ya deni sugu ambalo limezonga Mamlaka ya Ndege za Serikali ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa ingawa deni hili linaitwa deni sugu kwani nina hakika kuwa Serikali haina nia kudhoofisha kwa huduma za mamlaka hii kushindwa kutoa huduma nzuri ila sisi watu maskini kusema, “maskini hapendi mwana”.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imeonyesha juhudi kubwa sana katika eneo la kusambaza simu nchini ingawa bado hali yetu inahitaji watendaji waadilifu kiasi cha leo kupewa lawana ambazo wasingelistahili wanayopewa na kutia doa jeusi na kampuni ya simu ya *TTCL,* Tanzania inakosa uwezo wake kwa baadhi ya maeneo kwa ukorofi huu ambao nina hakika Serikali haikutegemea kupata tatizo hili. Hata hivyo nina hakika siku itafika na Wizara hii utawafikishia huduma za simu kwa wananchi wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaomba wizara hii sasa ionyesha ukali wake kwa kuruhusu wakorofi ambao kwa makusudi wameona watie doa katika mamlaka ya utabiri wa hali ya hewa. Nasema haya kwa sababu imeonekana kuwa hakuna sababu ya mamlaka hii kupata lawana sizizo za msingi kwani utendaji wake ni nafuu simu na kutoa taarifa za uhakika.

Leo inakuwaje baadhi ya vyombo vya habari kwa makusudi hutoa taarifa zisizo sahihi kinyume na taarifa za uhakika zinazotolewa na mamlaka hii. Wizara hii iwadhibiti hawa wanaovuruga taarifa hizi kwa kupokea taarifa kutoka vianzio ambavyo ni batili kwa kuwa hawataki kuitumia mamlaka hii labala kwa kukwepa ada ndogo na kupata taarifa ya mhakiki ambazo wananchi wanazihitaji sana kwa maisha yetu ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kurejea tena shukrurani zangu kwa Mheshimiwa Waziri Profesa Mark Mwandosa, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari Naibu Waziri na Watendaji wote wanayoipa sifa Wizara hii. Kuunga mkono bajeti hii ni tendo la lazima na mimi naunga mkono asilimia mia kwa mia.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi yeye binafsi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wake wote kwa juhudi na kazi nzuri za kujituma mnazofanya ambazo zinaridhisha na inaonekana katika Wizara hiyo. Vile vile nikupongeze kwa kusimamia vizuri mashirika yaliyo chini ya Wizara yako na kuwezesha eneo kubwa la Tanzania kupata mawasiliano.

Mheshimiwa naomba niishauri Serikali kwa mambo yafuatayo:- *TRC* mabehewa yanunuliwe mapya na yale ya zamani yakarabatiwe kupunguza msongamano wa wasafiri, usafiri ndani ya treni ufanyike mara kwa mara ili kuepuka magonjwa yakuambukizwa, Reli ya Singida - Dodoma iimarishwe, ratiba za treni ifutwe ili kuondoa usumbufu unajitokeza kwa wasafiri, utendaji wa kazi wa watumishi wa *TRC* usimamiwe vizuri kwani wanaonekana kutowajibika kikamilifu na kusababisha ratiba kutofuatwa, ajali nakadhalika. Vile vile maslahi ya watumishi yaangaliwe kwa suala la matengenezo yalikuwa yanafanyika mchana na usiku na kero nyingi hazikuwa zinajitokeza.

Usafiri wa anga. Naiomba Serikali kuangalia upya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Dodoma ukizingatia hapa ni Makao Makuu ya Serikali. Dodoma sasa hivi kuna wageni mbalimbali kutoka nje ya nchi wakiwemo Waheshimiwa Marais wa nchi mbalimbali. Si hivyo tu hata Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Mawaziri na Mheshimiwa Rais, sasa hivi muda mwingi wanakuwa Dodoma mrefu na hata Watendaji wa Wizara mbalimbali, viongozi hawa wanahitaji usafiri wa haraka kwenda katika maeneo yao. Si hivyo tu hata mashirika yasaidie kuleta usafiri wa ndege. Naomba kijengwe kiwanja kipya kulingana na master plan ya Mji wa Dodoma. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya katika kusimamia kazi hii ya mawasiliano. Naishauri Serikali kuhakikisha mawasiliano haya yafike vijijini hasa katika Wilaya zilizobaki kama Kondoa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Mheshimiwa Waziri kwenda kutembelea Kondoa na kujionea hali halisi ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja

**MHE. FRANK G. MAGHOBA:** Mheshimiwa Spika, nakupongeza kumpongeza Waziri kwa kazi nzuri na yenye mwelekeo mzuri kwa Taifa letu. Mheshimiwa Waziri kwa kuwa dunia ya sasa ni kama kijiji kimoja, kutokana na kuwa na mawasiliano mazuri na kwa kuwa mawalisiliano yanaharakisha maendeleo ya kiuchumi popote duniani ni vyema niseme haya yafuatayo ili maendeleo ninayoyasema labda yaanze kuonekana jimbo langu la Kigamboni ni miongoni mwa majimbo yaliyopata neema ya kuwa kandokando mwa Bahari ya Hindi. Sasa hivi imekuwa kitega uchumi kikubwa kwa Taifa hili kama tutafanya haya. Nashauri kijengwe Kiwanja cha Ndege kidogo kitachowarahishia watalii kufika kwenye mahoteli kwa urahisi zaidi, kwani hivi sasa kuna helkopter zinazotua kule karibu mara nyingi kwa ajili ya watu mbalimbali wanaokuja kustarehe kandokando mwa bahari hiyo nina maana kwenye mahoteli yalioko Kigamboni na sina uhakika kama Serikali inajua hivyo na kama inajua basi utanieleza faida tupatayo kwa huduma hiyo. Naamini helcopter na ndege ndogo ndogo zilikuwa zinatua huko nyuma labda utanijulisha kama wameacha kwa sasa. Pia hiyo kiusalama ni hatari kwa taifa letu lenye utulivu na amani kubwa,

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri jambo la pili maeneo haya hapa chini hakuna mawasiliano kabisana kwa kuwa tunahitaji maendeleo ya kiuchumi haraka haraka hatuna budi kuweka mawasiliano haraka maeneo haya ni kuanzia Mji Mwema, Muongozo, Pemba Mnazi, yale yale Puna, Kimbiji nakadhalika. Ikipatikana minara mitatu au miwili utakuwa umeunganisha sehemu kubwa ya Jimbo hilo la Kigamboni na Wilaya yetu ya Temeke na Dunia nzima nasema hivyo kwa kuwa kuna mahoteli ya kisasa kabisa na ya hali ya juu na watalii na wananchi hupendelea kwenda huko kila weekend mwishoni mwa wiki kwa mapumziko ya hapa na pale lakini tatizo ni mawasiliano hakuna.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja hii ya Wizara yako.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa hotuba nzuri yenye mwelekeo mzuri wa utendaji katika sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi na taasisi zake kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, napongeza sana mpango wa kuboresha usafiri katika Jiji la Dar es Salaam bus rapid transit. Dhamira ya utekelezaji wake kati ya 2003/2005 inaonyesha jinsi tunavyodhamiria kubadilika kimaendeleo kuelekea katika mfumo wa usafiri kwa nchi zilizoendelea. Tusiwe watu wa kutazama wenzetu na kushangaa kuwepo hata kwa usafiri wa treni chini ya ardhi *(underground trains).*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pendekezo kwamba simu zote za mkononi sasa ziweke gharama zake kwa thamani ya fedha za Tanzania. Nawashukuru sana *Celtel*

kwa kuanza mfano huo mapema na pia mobitel ambao wameahidi kuanza katika wiki moja ijayo. Hivyo kampuni nyingine zifuate mpango huo. Ni kinyume cha sheria hata hivyo kampuni iliyoandikisha Tanzania kufanya biashara ndani ya Tanzania kwa mfumo wa fedha za kigeni. Naomba pia kuwasilisha maombi ya wananchi na wafanyakazi wa Amani Wilaya ya Muheza kuhusu mawasiliano ya simu za mkononi. Amani ina zaidi ya wafanyakazi 5000 katika mashamba ya chai, taasisi ya maleria na hifadhi ya msitu wa Amani. Miongoni mwao zaidi ya wafanyakazi 100 wana simu za mkononi za Vodocam au *Celtel*. Hivyo kwa wastani lipo soko la matumizi ya simu hizo kwa wastani wa shilingi 10,000 kwa wiki kwa simu moja au shilingi 40,000,000/=. Tatizo ni kwamba simu za mkononi katika eneo hilo zinapatikana kwa nadra sana katika maeneo machache sana ya mlima huo. Hivyo tunaomba angalau moja kati ya makampuni hayo mawili liboreshe upatikanaji wa mawasiliano hayo kwa kuweka mnara mlimani hapo. Tukumbuke pia Amani sasa ni eneo kuu la utalii na pia eneo kuu la utafiti vinaoshirikisha wageni wengi kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, huduma ya benki kwa msingi nilioeleza hapo juu ipo haja ya kufikiria kuanzisha mfumo wa benki katika eneo la Amani. Kwa kuanzia na huduma ya benki ya posta. Wafanyakazi hao wote ambao hupata mishahara yao kwa fedha taslimu hawana chombo chochote cha kuhifadhi fedha zao za akiba. Wanalazimika kufuata huduma hiyo Muheza umbali na wastani wa kilo mita 47.

Mfumo wa makampuni ya simu kuweka gharama zake za simu za mkononi kwa kipimo cha dakika. Mfumo huu ni mbaya sana na unawatia hasara wateja. Kwa kawaida kampuni nyingi za simu za mkononi nje ya Tanzania hupanga rates zake kwa sekunde. Hii ndiyo njia pekee ya haki kwa mteja kwani atalipia gharama halisi. Mara nyingi wateja wanalazimika kupoteza haki yao ya muda wa mazungumzo wakati kwa mfano akitumia muda wa dakika tatu na sekunde 20 kwa mfano huo wa rates za dakika anakuwa amelipia dakika tatu badala ya muda halisi aliotumia. Tofauti hii ya muda siku zote inakuwa faida kwa kampuni ya simu. Hii siyo halali. Kampuni zinatakiwe kubadili mfumo huu ili kuwatendea haki wateja.

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa mabehewa ya treni yaliyopata ajali Dodoma. Nawapongeza Wajerumani kwa msaada wa fedha ukarabati wa mabehewa hayo. Lakini tujishauri kama kweli mabehewa yale yataweza kukarabatiwa na kurudia katika hali yake halisi au ni bora kutumia fedha hizo kununua mabehewa mapya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kutuwezesha leo kukutana hapa kujadili hoja ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Napenda niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote walioshinda katika uchaguzi uliopita na nawasihi tuendelee kushirikiana katika kuondosha kero za wananchi wetu na kuleta maendeleo yao. *(Makofi)*

Nimefarijika sana na naendelea kufarijika kwa kupata support kubwa kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambayo imenisaidia sana kutekeleza majukumu yangu ya

kumsaidia Mheshimiwa Waziri. Napenda niwaahidi kuwa nitajihidi kuendelea kushirikiana nanyi katika kutafuta ufumbuzi wa kero zinazowagusa wapiga kura wenu ambazo kwetu sisi ni changamoto zinazohitaji kupewa uzito unaofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa Wizara hii katika kuchangia uchumi wetu na pia katika kuendeleza na kuboresha Sekta nyingine unaeleweka wazi. Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi inachochea ukuaji wa sekta nyingine. Hivyo tuna wajibu wa kuongeza juhudi katika utekelezaji wa majukumu yetu ili tuweze kukidhi mahitaji ya Sekta na Wizara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja hii naomba nichangie kwa kutoa ufafanuzi na pia kujibu hoja mbili tatu zilizojitokeza katika maeneo yafuatayo: Hoja zinazohusu viwanja wa ndege. Hoja inayohusu Mamlaka ya Hali ya Hewa, Usafiri wa Bahari, Mambo ya Bandari, Usafiri katika maziwa. Usafiri wa nchi kavu, *TAZARA, TRC,* Usafiri na Usalama wa Anga, Chuo cha Usafirishaji, Posta na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na hoja ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Tulipewa hoja ya kwamba kuna haja ya kupatikana maji kwa kiwanja cha ndege cha Songwe. Sisi tunakiri kwamba kuna umuhimu wa maji kwa ajili ya uendeshaji wa viwanda vyote nchini kikiwemo hiki cha Songwe na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imeshafanya *study* ya kuona vyanzo vya maji na tumeona ziko alternatives tatu Mto Songwe, Mto Mbalizi na *alternative* nyingine ni kuchimba kisima. Kati ya hivyo, chanzo cha Mto Songwe kimeonekana kufaa zaidi. Hivyo makubaliano yameshafanyika na kampuni ya maji ya Songwe yanayoitwa *SOWACO* kufanya usanifu wa mfumo wa maji pamoja na visima vya kuhifadhi maji. *(Makofi)*

Lilitolewa wazo Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba tuweke taa kwenye viwanja vyote vya ndege tulivyo navyo. Mtakumbuka kwamba tuna viwanja vya ndege 62 Tanzania nzima na kama mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge tulishawahi kuahidi kwanza hapa tutaweka taa kiwanja cha ndege cha Dodoma. Tunakiri kwamba tumechelewa kidogo utekelezaji wake lakini shughuli za matayarisho zinaendelea vizuri. Taratibu za zabuni zimekwishafanyika, na tunategemea zabuni hizi zitafunguliwa tarehe 17 mwezi huu, kazi itaanza mwezi wa September na inshallah mambo yakienda vizuri baada ya mwezi mmoja taa zitawekwa katika kiwanja cha ndege cha Dodoma. *(Makofi)*

Aina ya taa hizi ni zile semi-permanent system na zitakuwa na gharama ya shilingi milioni 220. Sasa Waheshimiwa Wabunge kama hali ya fedha itaruhusu itategemea kukua kwa shirika, mapato na hali ya Mkoa kibiashara, hali ikiruhusu kifedha basi sehemu nyingine zilizosalia tunaweza tukaweka kwa awamu.

Tuje kwenye masuala ya bandari. Lilitolewa wazo Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba kuna wizi wa vifaa kutoka kwenye magari yanayoingizwa nchini. Sasa napenda niseme kwamba Waheshimiwa Wabunge uchunguzi uliofanywa umebainisha kwamba wenye magari makuu kuu hasa yanayoingia bandarini, yanakutwa na matatizo ya wizi wa vifaa mbalimbali. Lakini asilimia kubwa ya magari mapya yanayokuja yakiwa timilifu na kukabidhiwa kwa wenyewe hivyo hivyo yalivyopokelewa.

Baada ya tatizo hili kubainika Mamlaka ya Bandari ikaanzisha utaratibu wa kufanya ukaguzi magari hayo na makabidhiano baina ya wenye meli, bandari na mpokeaji. Sasa utaratibu huu umeonyesha kwamba hitilafu nyingi zinatokea ama kabla au wakati magari hayo yakiwa melini. Baada ya kuanzishwa utaratibu huo wa magari mengi makuukuu yamekuwa salama kwa kiasi kikubwa na mteja yeyote anapopokea gari yake hufanya ukaguzi wake pamoja na bandari ambao hulinganisha na ule uliofanywa gari lilipopokelewa wakati linatoka melini. Takwimu za robo mwaka wa kwanza huu zinaonyesha ni gari moja tu kati ya gari 5,181 yaliyopokelewa bandarini lililokabidhiwa kwa mteja likiwa tofauti na lilivyopokelewa. *(Makofi)*

Hata hivyo, waagiaziaji wa magari wanashauriwa pia kuhakikisha kwamba wanapata taarifa za ukaguzi wa magari yao yalivyopokelewa na wakala wake alivyokabidhiwa. Na imedhihirika pia kwamba magari mengi yanaondoshwa bandarini na wakala wenye meli ambao hawawapi wenye meli nakala za ukaguzi ambazo tumezianzisha. Tunaomba tu tulisisitize hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala lililochangiwa la ukaguzi wa vyombo vya majini. Napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara kupitia kwa Wakaguzi wa Meli wanakagua vyombo vyote vilivyosajiliwa mara moja kila mwaka. Aidha, katika ukaguzi huo Serikali hujiridhisha kwamba chombo husika kimepelekwa kwenye chelezo, kwa ukaguzi wa sehemu zote melini. Aidha chombo ambacho hakikidhi viwango vyote vya usalama ikiwemo kupelekwa kwa chelezo kwa wakati, au kuwa na vifaa vya kuokolea maisha hunyimwa cheti cha usalama. Wamiliki wote wa vyombo pia huandikiwa barua za taarifa pale tarehe ya ukaguzi inapokaribia ili kuwezesha ukaguzi kufanywa Utaratibu huu umesaidia sana Wizara kufanikisha usalama wa vyombo. *(Makofi)*

Wakaguzi pia huingia katika vyumba wakati wowote hata kabla ya ule wakati wenyewe unaotakiwa yaani *Annual Survey,* tunafanya *periodic* na kufanya *inspection* kuhusu usalama wa chombo husika na Serikali iliweza kusimamisha meli kadhaa kutokana na utaratibu huu wa kufanya survey bila kutarajia. Hata hivyo napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, kwamba Wizara itazidi kuimarisha shughuli za ukaguzi wa meli ili kuhakikisha kwamba meli mbovu hazifanyi kazi kwa ajili ya usalama wa abiria mali na kuzuia uharibifu wa mazingira. Napenda kuchukua fursa hii kuwakumbusha wakimiliki wote wa vyombo vya majini kuwa ni uvunjaji wa sheria na ni marufuku kutumia chombo kibovu au kisichokuwa na cheti cha sheria cha usalama kwa shughuli za usafirishaji majini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lilitolewa ombi la kuboresha bandari ya Kigoma. Tunaahidi tutaendelea kufanya hivyo na pia tunajua kwamba Kigoma ni kiungo muhimu kwa biashara kati yetu na Congo, Burundi, Rwanda na Zambia. Kwa hivyo, tunayo nia ya kuongeza vifaa vya kupakia na kupakilia mizigo katika bandari hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo lilitolewa la kuibua meli ya MV Bukoba ambayo ilizama. Naomba radhi, ni wazo jema, tunaliona Wizara. Lakini napenda niliarifu Bunge

lako Tukufu kwamba meli hii imezama kwenye kina cha maji ya mita 30 na kwa sasa tunadhani kwamba meli hii imejikita kwenye tope. Kwa sababu Ziwa Victoria lina tope sana na ni ukweli ulio wazi. Lazima tuwe wa kweli kwamba hatuna vifaa na nyenzo za kuweza kufanya kazi hii na kama tutataka kufanya kazi ya kuibua, itabidi tukodi makampuni kutoka nje ambayo ni gharama kubwa na kwa hivi sasa fedha hizo hatunayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, limetolewa wazo la kujenga gati la Karema. Tunasema nakubali na mimi nilipata nafasi ya kutembelea, usafiri kutoka Kigoma hadi Kasanga. Nilijionea mwenyewe hali halisi ya usafirishaji katika maeneo haya. Napenda tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kweli tumeanza mwaka jana na gati tulizoanzisha na mwaka huu tumeweza kuweka ma-*gat* machache. Hali ya bajeti ikiruhusu hapo baadaye hakuna sababu yoyote ya kukosa kujenga gati katika eneo hili la Karema ambayo Mheshimiwa Mbunge amelielezea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye masuala ya usafiri wa nchi kavu na lilitolewa wazo kwamba Serikali iingilie kikamilifu katika kusimamia nauli za watoto, wanafunzi kwenye mabasi, wenye mabasi wanatoza nauli kwa mujibu wa kiti badala ya kuwalipisha nusu nauli kama sheria inavyotaka.

Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kuwa tulipitisha Sheria ya Maadili ya Biashara ya mwaka 1994 yaani katika *Trade Practice Act of 1994* na Serikali ikajitoa kupanga bei za bidhaa na huduma na bei hiyo sasa inapangwa na mzalishaji na nguvu ya soko ndiyo inayochukua mkondo wake.

Ndiyo sababu Dar es Salaam daladala zilitangaza nauli ya shilingi 200/=, nyingine shilingi mia moja na hamsini. Lakini abiria waliposita wakaamua kwenda kwa miguu mabasi yaliteremsha bei yakafikia sh.100/= na huduma zikaendelea. Ili kupunguza mzigo wa nauli kwa abiria, Mamlaka ya Leseni ya Mkoa wa Dar es Salaam imebuni utaratibu wa kutumia mabasi makubwa aina ya *City Bus or City Trains* kama alilivyosema Mheshimiwa Waziri asubuhi leo yatakayosafiri masafa marefu. Kwa mfano, yatatoka Mbagala kwenda Tegeta na kumwezesha abiria kulipa nauli moja tu ya sh.150/= na kumwondoshea kero ya kubadilisha mabasi mawili au manne kwa safari moja.

Tunaamini zoezi hili la kubuni safari ndefu litakapokamilika litapunguza kero kubwa sana tu kwa wasafirishaji na wasafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko ya wananchi wa Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Mtwara kutoza gharama za kusafirisha vifurushi vidogo vidogo lilizungumzwa. Tuseme tu kwamba sheria inaruhusu vifurushi vidogo vidogo vyenye uzito usiozidi kilo 20, kusafirishwa bure. Lakini nafikiri tatizo linalojitokeza ni kwamba wengi wenye shughuli hizi huwa hawana mizani ya kupimia vifurushi hivyo. Kwa hivyo, tunasema Mamlaka ya Leseni ya Usafirishaji na Polisi wa Usalama Barabarani, wataendelea kutekeleza Sheria hii ipasavyo na Wizara pia kwa upande wake itawahimiza wasafirishaji wawe wanatumia mizani kupima vifurushi hivyo.

Lilitolewa wazo na hoja ya kuimarisha Ofisi za Kanda, ikiwa ni pamoja na kuzipa nafasi ili zitoe leseni. Hili tunasema linazingatiwa. Sheria Na. 5 ya Simatra ya mwaka 2001, inaitambua Sheria Na. 1 ya Usafirishaji ya mwaka 1973 kama ni *Principle Act* na hivyo Sheria hiyo ya Leseni inafanyiwa marekebisho. Moja ya mapendekezo ni kuzipa Kanda mamlaka ya kutoa leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hilo limezingatiwa. Pia kuna suala la msongamano wa abiria kwenye mabasi. Abiria wapigwe fine za papo kwa papo. Sisi tunameleta mapendekezo ya Mheshimiwa Mbunge ni zuri. Lakini hata hivyo kwa vile suala hili linagusa taasisi zaidi ya moja, tutawasilisha kwa wadau kwa lengo la kuona njia bora au uwezekano wa kuweza kulitekeleza bila kuleta matatizo. Usafiri wa mijini na Mikoani msongamano wa magari jijini Dar es Salaam ni mkubwa. Tumesema mapendekezo yaliyotolewa ni mazuri, na Wizara yangu itashirikiana na vyombo vingine katika kulitekeleza hilo. Hasa na Wizara ya Viwanda na Biashara itaangalia namna bora ya kutekeleza masuala hayo.

Ipo hoja ambayo aliitoa Mheshimiwa Shoka, kwamba baadhi ya madereva wanapewa leseni za kuendesha magari ya abiria akiwa na umri mdogo na hivyo kuleta matatizo na adhabu wanazopewa ni ndogo mno. Kwa hiyo, hawajali. Tunasema ni kweli kwamba baadhi ya madereva wanapoendesha magari ya abiria, wana umri mdogo, wanapoendesha hujali fedha zaidi kuliko sheria na kwamba adhabu kwa wanaobainika na makosa hayo ni ndogo. Wizara inashirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili kusaidia kuhimiza usimamizi wa utoaji leseni na kubainisha adhabu kali kwa wakosaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa sitaweza kukidhi haja za Waheshimiwa Wabunge wengi, lakini nitajitahidi. Tuje kwenye masuala ya Posta. Lilitolewa wazo kwamba kule Same Magharibi huduma za kutuma pesa katika Posta Wilaya ya Same ni duni. Wananchi wa Same wanapotumiwa fedha nyingi hulazimika kusubiri hadi fedha za kutosha zinapopatikana. Kwa hivyo wanaomba kuwe na huduma ya *The Western Union Money Transfer* kama ziliko sehemu nyingine. Sisi tunasema sio wazo baya, lakini kuna vipindi vya msimu. Si wakati wote masuala haya yanajitokeza. Kama vile mwanzo wa mwisho wa mwezi ambapo Ofisi ya Same ya Posta inapokea hati nyingi za fedha kutoka Mikoa mbalimbali na kulazimika kusubiri taratibu za kuhamisha fedha kutoka Ofisi Kuu ya Posta Moshi na Ofisi ya Kanda Arusha au Dar es Salaam.

Hali inatokana na Ofisi ya Same kuzalisha kiwango kidogo cha fedha na hivyo kuwa na Ofisi iliyopewa fedha nyingi kuliko inavyopokea kutoka kwa wakazi wa Same. Taratibu zinafanyika kuongeza mtaji wa Ofisi ya Same kupunguza tatizo hilo na wakala wa *Western Union Money Transfer* utaanzishwa Ofisi ya Same maandalizi yakikamilika baina ya Shirika la Posta Tanzania na Benki ya Posta Tanzania ambao ndiyo wakala wakuu wa *West Union Money Transfer.* Sisi ni wakala wa kulipa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulitolewa wazo la jimbo la Buchosa lenye wakazi wapatao laki halina huduma za Posta. Tunasema jimbo la Buchosa hadi March 2002 lilikuwa linahudumiwa na wakala wa *Nyanguge Bus Service* ambaye aliacha kutoa huduma hizo kutokana na kuhama. Lakini uongozi wa Posta Kanda ya Ziwa unafanya

majadiliano na Kahunda kwa lengo la kuanzisha wakala mpya wa Posta katika mji wa Buchosa.

Kwa sasa Sekondari ya Kahunda na Shirika la Ma-*Sister* wamepewa vibali vya kuuza stamp kwa wananchi katika maeneo hayo. Nina uhakika baada ya mawasiliano ya kutosha wananchi wa Buchosa watapata mbadala na baada ya yule aliyekuwepo kuondoka. Kulitolewa wazo la kujenga Ofisi za Posta Mkwajuni na Makongolosi. Kwa sababu maeneo haya yana watu wengi. Ni kweli maeneo haya yana watu wengi. Lakini huduma katika eneo la Mkwajuni, Shirika la Posta linatoa huduma zake kama Posta kamili. Pale Makongolosi kuna Posta ndogo inayotoa huduma kwa wananchi. Shirika la Posta limejenga na litaendelea kujenga majengo ya Posta kwenye miji mikuu ya mikoa na wilaya. Lakini kutokana na uhaba wa fedha Shirika kwa hivi sasa halina uwezo wa kujenga majengo katika maeneo mengine. Kwa hivyo, tunamwomba tu Mheshimiwa Mbunge wa Mkwajuni na Makongolosi itabidi wasubiri kidogo hali ya shirika itakapoendelea kuwa nzuri, tutaweza kufanya hivyo. Lakini kwa hivi sasa tutaendelea na utaratibu wa kukodisha majengo na kuyafanyia marekebisho ili huduma hizi za Posta ziweze kuendelea kutolewa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kondoa, aliomba tu iimarishwe huduma za Posta pale Pereko na Bahi. Mheshimiwa Mbunge, mwenendo wa kibiashara katika Posta ya Bereko na Bahi hauridhishi kabisa. Kwa hivi sasa na Shirika linaendesha huduma katika maeneo hayo kwa hasara. Lakini mawasiliano yanafanyika kati ya Posta na tutafanya na wewe Mheshimiwa Mbunge ili tuhamasishe wanavijiji wa maeneo hayo ili waweze angalau kupangisha masanduku yaliyopo na kutumia huduma nyingine za Posta. Kwa hivyo, maendeleo ya juhudi hizi yatakapopelekea kuwa mazuri, mipango ya kuboresha na kuimarisha Posta hizo yataboreka zaidi na kuhusu Kata ya Kisese ipatiwe Posta ndogo. Shirika linafanya mipango ya kufanya utafiti wa kimasoko na wa kimahitaji kwa lengo la kubaini mahitaji ya huduma za Posta katika eneo la Kisese baada ya hapo utekelezaji utaingizwa kwenye mpango huu wa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Esha Stima alitoa hoja kubwa tu ya wafanyakazi wa Shirika la Posta. Lakini kama tunavyosema, suala likifika Mahakamani, sidhani kama tunayo nafasi ya kulijadili ipasavyo. Lakini kwa manufaa yake, naweza tu kukaa naye kujadiliana naye kumpa undani wa hali halisi ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuje kwenye masuala ya Shirika la Reli Tanzania. Tulitakiwa tuboreshe na kuendeleza usafiri wa reli. Tunakubali na tunafanya hizo jitihada, ni nyinyi wenyewe Waheshimiwa Wabunge ambao mnasafiri na reli ya Kati mtakubaliana nasi kwamba shughuli hizo zinafanywa.

Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, tutaboresha huduma za treni za Kigoma baada ya kukarabati hayo mabehewa yetu 11 yaliyopata ajali. Tunategemea treni itaongezwa kutoka siku tatu hadi nne kwa wiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapenda tumhakikishie Mheshimiwa Tatu Ntimizi kwamba tunajali sana maslahi ya wafanyakazi wetu wa magenge na tunahakikisha

kwamba wanapata maji kwa kuwatengenezea matanki ya kuhifadhia maji na tunawapelekea mara nyingine maji kwa kutumia treni zetu ndogo ndogo. Kwa hiyo, tutaendelea kufanya hivyo. Pia tutahakikisha wanapata vitendea kazi kama *gloves na boots.* Lakini napenda nikiri kwamba hatuwezi kusambaza vifaa hivyo kwa watu wote kwa hiyo tunagawa kwa awamu kwa Wilaya kama hivi sasa tuko katika Uhandisi Tabora na tumewapelekea boots 1,250 na makoti ya mvua 500 na tutafanya hivyo kwa Wilaya nyingine kwa zile Wilaya kireli na siyo hizi Wilaya za Kimkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeambiwa muda wangu umekuwa mdogo, naomba niseme machache kuhusu *TRC* kuwa iboreshwe kwa kuwa na tariff zenye ushindani. Tunakuahidi Mheshimiwa Leonard Derefa tutafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, isipokuwa ombi la kuunganisha *TRC* na *THA* ili itoe subsidy kwa *TRC,* sisi tunafikiria hilo kidogo litakuwa ni ngumu. Ili mapato ya nchi yaongezeke ni vema hii miundombinu tofauti ikabaki kama ilivyo hivi sasa. Kuunganisha haya mashirika mawili kunaweza kuleta ufanisi tegemezi, ili kukidhi haja hii ndiyo maana mashirika haya mawili yanabinafsishwa tofauti ili kuleta ufanisi mzuri zaidi. Lakini nafikiri mtakubaliana nami ubinafsishaji kwa namna nyingine umesaidia, anayeiona *Dodoma Hotel* leo na ilivyokuwa, nadhani kuna tofauti kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo masuala mengi yaliyozungumzwa ya *fuel levy,* yanashughulikiwa. Napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge tahadhari inayochukuliwa katika suala zima la ubinafsishaji wa *TRC* kwa sababu tunaelewa hiki ni kiungo kikubwa na ni kiungo ambacho kinawasaidia wanyonge wengi. Sehemu nyingi za katikati hakuna barabara, wanategemea sana Shirika la Reli la Tanzania kwa hiyo ndiyo maana alipobakia mwekezaji mmoja tukasema hapana ni vizuri tutoe nafasi uwigo upanuke, wapatikane wengi ili tupate ushindani wa ubora zaidi. Kwa hiyo, huduma hizi zitashughulikiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mawazo yaliyotolewa na Mheshimiwa Abdullatif Hussein Esmail kuhusu tiketi za Kampuni ya *ATCL* kwa hivi sasa ni *The Southern Airways,* hazina alama yoyote ya Utaifa wetu na akashauri tiketi hizo ziwe zina sura na ubia pamoja na ndege zote ziwe na nembo ya Taifa ya Twiga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, matayarisho yamekamilika ya tiketi mpya za *Air Tanzania* zenye nembo mpya ya *ATCL.* Hata hivyo *coupon* za ndani ambazo tiketi zenyewe zinafanana na zile za *SAA,* ni kwa sababu za kibiashara tu na wala si sababu nyingine ya kihasibu, ni katika kuongeza ufanisi tu na katika mauzo na kuna kudhibiti mapato yake kwa kutumia kompyuta, haya masuala yote yanashughulikiwa. Ninapenda niwahakikishie kwamba nembo ya twiga itarejeshwa hivi karibuni kwenye ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili pia lilizungumziwa na Mheshimiwa Lucas Selelii kwamba nembo ya twiga ionekane. Napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba hili litashughulikiwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nikiri kwamba muda wangu ni mfupi sitokidhi kuweza kujibu masuala yote ambayo yako mbele yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima naomba niunge mkono hoja iliyo mbele yangu. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuanza kwa kutoa shukrani zetu za dhati kabisa kwa michango mizuri sana iliyoletwa hapa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge kwa maandishi na vile vile kwa kusema kama walivyosema kuanzia asubuhi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu kwa niaba ya wenzangu wote katika Sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa jinsi mlivyotusemea, kwa jinsi mlivyowasifia wenzangu na pia mlivyotambua kazi zao, kwa kweli wale wote walio huku nyuma wanaotusaidia kazi wamefarijika na mimi na Mheshimiwa Dr. Maua Daftari mnatufanya tuwe wanyenyekevu zaidi. Ahsanteni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia. Napenda nianze kwa kuwataja wale ambao wamechangia kwa kusema nao ni Mheshimiwa Henry D. Shekiffu, Makamu Mwenyekiti wa Miundombinu, Mheshimiwa Ismail J. R. Iwvatta, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Prof. Daimon M. Mwaga, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Esha H. Stima, Mheshimiwa Prof. Henry Mgombelo, Mheshimiwa Samwel M. Chitalilo, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Dr. Milton M. Mahanga, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Benedicto M. Mutungirehi na Mheshimiwa Dr. Maua A. Daftari. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vile vile niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi, nao ni pamoja na Mheshimiwa Shamim P. Khan, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, Mheshimiwa Dr. Batilda S. Burian, Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, Mheshimiwa Semindu K. Pawa, Mheshimiwa Mizengo K. P. Pinda, Mheshimiwa Shamsa S. Mwangunga, Mheshimiwa Ireneus N. Ngwatura, Mheshimiwa Prof. Pius P. Mbawala, Mheshimiwa Dr. Diodorus B. Kamala, Mheshimiwa Dr. Chegeni R. Masunga, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa William J. Kusila, Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Prof. Daimon M. Mwaga, Mheshimiwa Sumri A. S. Mohamed, Mheshimiwa Leonard N. Derefa, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Emmanuel E. Kipole, Mheshimiwa Beatus R. Magayane, Mheshimiwa Paul E. Ntwina, Mheshimiwa Margareth A. Mkanga,

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Philip A. Magani, Mheshimiwa Omar Said Chubi, Mheshimiwa Salim Omar Ali, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mheshimiwa Remidius E. Kissassi, Mheshimiwa Halimenshi K. R. Mayonga, Mheshimiwa Frank M. Mussati, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa John E. Singo, Mheshimiwa Abdullatif Hussein Esmail,

Mheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya, Mheshimiwa Yete S. Mwalyego, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa Khalid S. Suru, Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mheshimiwa Stanley H. Kolimba, Mheshimiwa John L. Mwakipesile, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Ali Said Juma, Mheshimiwa Shani, Mheshimiwa Karim Said Othman, Mheshimiwa Henry D. Shekiffu, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Khan Khan, Mheshimiwa Omar Juma Omar, Mheshimiwa Robert J. Buzuka, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Dr. Aisha O. Kigoda, Mheshimiwa Capt. Theodos J. Kasapira, Mheshimiwa Dr. Thadeus M. Luoga, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mheshimiwa Janeth E. Mashele, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, Mheshimiwa Khadija Saleh Ngozi, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Ally A. Karavina, Mheshimiwa Kijakazi Khamis Ali, Mheshimiwa Teddy L. Kassella-Bantu na Mheshimiwa Prof. Henry R. Mgombelo vile vile namtambua Mheshimiwa Frank G. Magoba. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi tukiwa nje ya Bunge wananchi wanafikiri kwamba kazi inafanyika ndani ya Bunge tu, kumbe Waheshimiwa Wabunge ni Wabunge wakati wote wa mwaka nzima. Sasa hilo nathibitisha kwani nina *list* ya Waheshimiwa Wabunge wengine 37 ambao katika kipindi cha miezi kama tisa (9) tu wameniletea hoja nikiwa Wizarani na nimewajibu kadri nilivyoweza. Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba Waheshimiwa Wabunge ni Wabunge kila siku wala siyo wakati wa Bunge tu. Sasa majina yao ni mengi kidogo kama utaniruhusu nisome maana yake wananchi wajue kwamba kazi inaendelea wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Chegeni R. Masunga, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Venance M. Mwamoto, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Dr. Hussein A. Mwinyi, Mheshimiwa Dr. John S. Malecela, Mheshimiwa Athumani S. M. Janguo, Mheshimiwa Omar Said Chubi, Mheshimiwa Lydia T. Boma, Mheshimiwa Hadija K. Kusaga, Mheshimiwa Dr. Aaron D. Chiduo, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mheshimiwa Oscar T. Mloka, Mheshimiwa Dr. Amani W. A. Kabourou, Mheshimiwa Ali Mussa, Mheshimiwa Mathew T. Ole-Timan, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Bujiku K. Sakila, Mheshimiwa Njelu E. M. Kasaka, Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mheshimiwa Dr. Amani W. A. Kabourou, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, Mheshimiwa Leonard N. Derefa, Mheshimiwa Basil P. Mramba, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Charles H. Kagonji, Mheshimiwa Anatory K. Choya, Mheshimiwa Robert J. Buzuka, Mheshimiwa Prof. Pius P. Mbawala, Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu na Mheshimiwa Mizengo K. P. Pinda. Naomba vile vile kumtaja na kumtambua Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, sijui nilimsahau namna gani Msemaji Mkuu anayejiita Waziri Mbadala, hamna cheo cha namna hiyo wewe ni Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani tu. Nawashukuru wote. (*KichekoMakofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze moja kwa moja na lile ambalo unaweza kuliita ni jinamizi, wenzetu wanaita ruhani. Lakini ruhani au jinamizi la *TTCL*

bado linatuandama, *inshallah* siku moja litakwisha tu. Kwa hiyo, naomba nianze nalo hilo kwa maelezo ya ziada. Mwaka jana nilisimama hapa mbele yenu kwa unyenyekevu mkubwa kabisa nilijibu maswali, nilijibu hoja na pia niliitwa kwenye Kikao cha Kamati ya Uchumi na Fedha nikawekwa kiti moto kwa muda zaidi ya masaa sita, nilielezea, kamati ilipitia huo mkataba, ni wakati nadra ambao Kamati zinapata nafasi ya kupitia mkataba mzima.

Kwa hiyo, Serikali iliruhusu huo mkataba na ulipitiwa tena kwa undani kabisa ndiyo maana leo Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi anakumbuka kwamba kulikuwa na maandishi pembeni pale, nayo ilikuwa ni hoja. Tuliweza kuyajibu na Kamati iliridhika na ilitupa maelekezo ambayo tumeyazingatia. Lakini kwa kuwa limezungumzwa hapa naomba nichukue nafasi kidogo tu kwa maana ya wananchi waweze kujua tumefika wapi na kwa sababu gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa mkataba na mwekezaji kwa kweli tulikuwa na matumaini makubwa na sisi wengine kila wakati ni watu wa matumaini, *we were born with hope* kwamba yatakuwa mazuri tu na Taifa letu litazidi kuendelea, haiwezekani kwamba tukaenda chini. Kwa hiyo, tulikuwa na matumaini makubwa kwamba hili suala kwa kweli lingekwisha hasa baada ya kupata ile Ripoti ya George Fumbuka na baada ya *Price Water Coopers* kuipitia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika haya mambo ya biashara ndiyo tumeingia katika biashara sasa tufanyeje, ni mapambano tu na tutaendelea kupambana. Tulipofika wakati wa kuyapitisha na wenzetu wakasema hapana, wakasema tunaona hapa huyu mswahili ni mwenzenu na wakasema huyu bila shaka, huyu Fumbuka huyu ni rafiki wa *professor* aliteuliwa na *professor* . Kwa hiyo haiwezekani, kwamba akawa ni mtu ambaye ataweka mambo sawa, akatufanya wote tuwe katika mizani moja. Kwa hiyo wakakataa wakasema hapana bila shaka Serikali imependelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi tukasema nini? Kwanza, tukasema ngoja tuwawekee ngumu. Mtakumbuka tulisema hapa na mbele yenu tulikiri kwamba hawa watu wasipokubali mwisho wake tutawanyang'anya hizi hisa. Hilo nililisema mbele ya Bunge ni mimi mwenyewe hapa, likatuponza tukashtakiwa London. Wakasema ooh tunataka kunyang'anywa hisa, kwa nini? *Professor* ameliambia Bunge kwamba tusipokamilisha au tusipokubali basi tutanyang'anywa hisa, Mahakama Kuu London ikaweke pingamizi. Lakini tuna wanasheria wetu hapa tena wazuri tu wakiongozwa na Mheshimiwa Andrew Chenge. Wakalipitia lile pingamizi wakaona kwamba kwa kweli lazima hata Tanzania kisheria, Sheria za Kimataifa lazima tuiheshimu. Lazima nikiri kwamba pingamizi hilo lipo mpaka leo kwa hiyo ndiyo maana tunapojaribu kuzungumza hili la *TTCL* tunakuwa kidogo na tahadhari kwa sababu tulichofanya sasa hivi ni kusitisha tu, tuangalie mkondo wa kupatana lakini tumesitisha, Mahakama Kuu Tanzania kesi bado ipo na Mahakama Kuu London kesi bado ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wameturuhusu wamesema hebu tuwape muda endeleeni, mkifika tamati ya suala hili basi mje mtuambie katika Mahakama Kuu ya London na Dar es Salaam kwamba mmekubaliana. Hili ndiyo linalofanyika hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulifikiria ya kwamba kwa nini tusiende kwenye Mahakama ya Kimataifa ya Usuluhisho. Lakini tukakumbuka kwamba inaweza ikachukua miaka minne hata mitano, hizi Mahakama za Kimataifa za usuluhishi zinaweza zikachukua muda tu. Sasa tukasema miaka mitatu ya usuluhishi au miaka hata minne hakuna kitu kitachofanyika katika *TTCL* labda maadam tumeingia na tulikubaliana kuna vipengele tunaweza tukakubaliana nje ya Mahakama, ngoja tuone kama tunaweza lakini wakati kesi zetu zikiwa zinaendelea yaani tumezisitisha tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili ndilo ambalo Serikali iliamua kulifanya na si vibaya kukiri kwamba hatuko duniani peke yetu, tulikuwa na wenzetu kama washirika wetu kama vile *European Investment Bank.* Wao wametuambia jamani sisi tunazo milioni 100 tumezitenga kwa ajili ya maendeleo ya *TTCL* tunaomba mlikamilishe hili jambo haraka ili ziweze kupatikana zikatumika. Huyu si mwakilishi tu isipokuwa ni *Vice President,* Makamu wa Rais wa *European Investment Bank.*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa *CDC* wakasema jamani sisi tunataka ku-invest katika *Telecommunications Tanzania,* jamani malizeni hili jambo haraka. Sasa tukasema hivi twende tukaanza mambo ya *IPTL* miaka minne, tukasema ndiyo tumeingia katika biashara, wakasema basi ngoja tuyape chance haya mazungumzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika kufanya hivyo Serikali kwa ujumla wake tukiongozwa na Mheshimiwa Rais ikasema kwamba hili suala ni zito siyo la kuiachia sekta moja au sekta mbili ya ubinafsishaji na sekta ya mawasiliano, hili ngoja apewe Katibu Mkuu Kiongozi ili alisimamie kwa maana ya mazungumzo na ndiyo maana Mheshimiwa Lumbanga, Katibu Mkuu Kiongozi amepewa jukumu hilo. Kwa umahiri wake na utendaji kazi wake sisi tuna matumaini makubwa, kama labda mlidhani wanasiasa hawawezi kuangalia maslahi ya nchi basi huyu Katibu Mkuu Kiongozi na Kiongozi wa Shughuli za Serikali kwa maana ya kiongozi wa wafanyakazi wote wa Utumishi wa Serikali basi nadhani atasimamia vizuri zaidi hayo maslahi ya nchi. Kwa hiyo, hapo ndipo tulipofikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tulichokubaliana na wenzetu ni kwamba tumwombe Mheshimiwa Rais wa *The Institute of Chartered Accountants of United Kingdom and Wiles* yeye amteuwe mtaalam, yeye hana habari na mlumbano yetu haya, baada ya kumweleza tatizo atamteua mtaalam, tumempa *terms of reference* na amemteua mtaalam. Amesema katika wataalam watatu yeye anafikiri kwamba John Helson wa

Kampuni ya *CEMG* ya London apewe nafasi ya kupitia taarifa za Fumbuka na Ripoti za *Price Water House Coopers.* Lakini sisi tukasema hapana hii tukubaliane naye lakini katika maelekezo yetu tukubaliane na hawa wawekezaji kwamba kila mtu amechoka na hili jambo atakayotueleza huyu bwana sasa ndiyo mwisho tumefikia kikomo, hatutaeleweka. Kwa hiyo, hilo tumeliingiza katika *terms of reference.* Kwa hiyo, huyu bwana ndiye atakayekata shauri au zamani walikuwa wanasema ndiye Jaji Kata, siyo Kata hizi lakini anakata shauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, atamaliza kazi yake kwa kipindi kama nilivyosema katika miezi mitatu kuanzia 8 Julai, 2003. Kwa nini 8 Julai, 2003? Kwa sababu ndipo ambapo Ndugu Lumbanga anakutana na wawakilishi wa wawekezaji ili kumpa kazi rasmi, kumkabidhi kazi rasmi. Kwa hiyo, imechukua muda kwa sababu tulikuwa tunamtafuta huyu mtu ambaye wote tungekubaliana naye ambaye ameteuliwa na huyu Rais wa *Institute of Chartered Accountants of United Kingdom and Wales.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunathamini sana michango mizuri iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, wananchi wa kawaida wameandika sana katika magazeti na pia wana taaluma nao wamelifuatilia sana suala hili. Mimi naamini kwamba sijui nani atatangulia, sijui mimi au wao wana taaluma, kuna kitabu tutaandika kuhusu *TTCL,* hii "saga" hii, litakuwa ni fundisho kwa vizazi vinavyokuja. Waingereza wanasema: "katika wingu lolote lilo jeusi ukiangalia pembeni unaona matumaini". Kwa hiyo, nami naamini hata katika hili wingu la *TTCL* bado kuna matumaini kwa ajili ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa sababu mmekuwa wazi sana katika suala hili na ni kwa nia njema kabisa mmeonyesha uzalendo kwa sababu wakati wote mtuasa kwamba tuzingatie maslahi ya nchi, sasa nani akatae kuzingatia maslahi ya nchi. Sisi ambao mmetupa dhamana ya kuendesha haya mambo tunachoweza kuomba ni msaada tu wa Mwenyezi Mungu atusaidie tufanikishe hili suala na masuala mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunashukuru sana. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Prof. Daimon Mwaga hili suala amelifuatilia kwa makini sana, si leo tu ila katika Kamati na hata tukikutana akija Ofisini na kila mahala. Yote haya anafanya kwa mapenzi kwa nchi yake wala si kwamba anajitafutia umaarufu wa aina yoyote ile, yeye anachotafuta hapa leo ni simu Kibakwe basi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa yanayotokana na hili suala kwa sababu tumechelewa lakini kwa bahati nzuri kweli tumejitahidi, hapa mlikuwa mnaona menejimenti yote ilikuwepo ni ya Wazungu wale lakini kwa bahati nzuri tukaweza kumpenyeza Mheshimiwa Mzee wetu Mbowe. Wale ambao mnamkumbuka Jumamosi iliyopita alikuwa nadhifu kama siku zote akiwa kama mpambe wa Mheshimiwa John Malecela. Sasa tuna bahati kwa sababu anaelewa matatizo haya, amewasikia Waheshimiwa Wabunge, yuko hapa, angekuwepo yule mtu wa nje haya yote tunayoyasema hayaelewi, unamwambia siku Kibakwe anasema Kibakwe ni wapi huko, lakini Ndugu Mbowe anayaelewa haya, ameyasikia na ameona jinsi mnavyozungumza, yanaingia moyoni. Kwa hiyo, inshallah tutatekeleza yote haya, tupewe tu uwezo na uwezo tutaupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa lililojitokeza ni kwamba kuna hili suala la *exclusivity.* Sasa kwa sababu miaka miwili tulikuwa tunalumbani, vikao vya bodi haviitishwi, kwa kweli mpaka tulipompata Ndugu Mbowe ndipo mambo yameanza kuendelea, amesukuma sasa ndiyo kwa mara ya kwanza tunaanza kuagiza vifaa kwa ajili ya ile miradi niliyoitaja leo asubuhi. Nimeitaja ile miradi kwa makusudi kwa sababu kila mwaka tunakuja hapa tunatoa ahadi tu na ahadi za *TTCL* zamani zilikuwa zinatekelezeka

lakini kwa sababu ya haya matatizo siku hizi tunakuwa na wasiwasi kweli kutoa ahadi. Kwa hiyo, mtaona tunapamba maneno tunasema pale fedha zitakapopatikana. Kwa hiyo, siku hizi hatutoi kwamba mwaka 2004, hapana, tutaongezea iwapo hali ya shirika itakuwa nzuri ili mkitubana mwaka kesho tunasema lakini hamkuona kile kipengele cha mwisho?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini leo nilikuwa jasiri kabisa kusema miradi hii na hii itatekelezwa kwa sababu vifaa vimekwishaagizwa, viko njiani. Kwa hiyo, miradi yote niliyoitaja leo asubuhi napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba itatekelezwa. *(Makofi)*

Sasa kwa sababu walichelewa kwa hiyo wameshindwa kutekeleza yale yaliyowafanya wapewe *exclusivity,* ni kweli. Sasa *exclusivity* kwa kweli wengi hatuipendi lakini sasa tulikubaliana kwamba tukiwapa *obligation* kubwa namna hii tunawapa na *exclusivity* ili waweze kutimiza, tulidhani mambo yangekwenda vizuri lakini kama nilivyosema hayakwenda vizuri. *Exclusivity* inadumaza ushindani, inarudisha nyuma maendeleo na kwa kweli inapingana na dhana zima ya soko huria kwa sababu haiweki ushindani sawa labda iwe *exclusivity* ya kulinda maslahi ya nchi na sisi tulifikiri kwa kufanya hivyo tutalinda maslahi ya nchi, tutawafanya hawa watu waeneze simu haraka haraka lakini imeshindikana. Sasa *exclusivity i*nakwisha Januari, 2005, tuna mwaka mmoja na nusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tulichosema na wametusikia, kwamba wasije hata siku moja wakafikiri tutaiongeza *exclusivity* hata kwa siku moja, hilo wasahau. Halafu vile vile tumewaagiza *TCC* waanze maandalizi ya awali ya kumpata *operator* mwingine au ma-*operator* wengine wa simu za msingi ili kuleta ushindani kama ulio katika simu za mkononi katika simu za msingi. Sasa kwa sababu mikataba inachukua kama miaka miwili hivi ili mtu atafute fedha, aje, apate vibali vya Serikali na kadhalika. Tunafikiri huu muda uliobaki ni muda mzuri wa *TCC* kuanza kufanya matayarisho. Kwa hiyo, hakuna lililopotea. Hata leo hii tungesema *exclusivity* hakuna ingetuchukua miaka kama miwili kuja kumpata mwekezaji mwingine, kwa hiyo hakuna lililopotea. Kwa hiyo, tunataka *TCC* ianze huo mchakato ili tuweze kumpata huyu mwekezaji mwingine. Lakini hili la exclusivity vile vile linazungumzika. Tumechukua mawazo ya Waheshimiwa Wabunge kwamba kama *TCC* watazungumza na *TTCL* ili waangalie, sasa wewe umeshindwa kutekeleza hii exclusivity haya basi tufanye nini, kama itabidi kuwaondolea mapema. Lakini kama nilivyosema itachukua kama mwaka mmoja na nusu hata kumpata mwekezaji mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa *TCC* wana mamlaka ya kuipata hiyo faini ya dola milioni 18 lakini si ndogo. Sasa wachukue wao au iende kupeleka simu Kibakwe kwa masharti fulani fulani pamoja na kubadili simu za kukoroga, hayo sasa ni mambo ambayo *TCC* inabidi wakae kwa sababu wao bilioni 18 watazifanyia nini; na simu nchini. Kwa hiyo, hili tumewaagiza. Wana mamlaka, kwanza wanaweza hata kuwapeleka *TTCL* Mahakamani lakini wao wenyewe wakaona baada hata ya kupata ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye aliwaambia mna mamlaka lakini angalieni namna ya kuyatumia mamlaka yenu kwa sababu jiulizeni tu na sisi tunajua nao

wanajiuliza kwamba ni tofauti kumpeleka Tritel Mahakamani na kumpeleka *TTCL* kwa sababu ukweli ni kwamba mpaka sasa *TTCL* ni mali ya Tanzania, ni mali ya Serikali tutake tusitake, achana na mgogoro huu wa management lakini *TTCL* ni mali ya Serikali. Kwa hiyo, *TCC* kabla haijaipeleka Mahakamani TTCL inabidi ipate ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani hili ndiyo limewapa ugumu. Sasa likiwapa ugumu mara nyingine wanasema tumelisukuma tumelipeleka Wizarani, hapana, wana mamlaka ambayo Bunge liliwapa, nadhani ndiyo tatizo hili. Lakini tumewaeleza kwamba wakae waangalie jinsi gani wote tunaweza tukafaidika na simu hasa ziende Vijijini haraka sana. Hii *exclusivity* vile vile imeathiri suala la *ZANTEL* ku- *rule out* huku Bara. Lakini pamoja na hii *exclusivity* tumewataka *TTCL* na *ZANTEL* washirikiane kibiashara kwa sababu maisha yanaendelea, migogoro ipo lakini maisha yanaendelea na biashara lazima ishamiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa faida tu ya Waheshimiwa Wabunge *ZANTEL* ni nini na lazima niitaje hapa niseme *ZANTEL* ni nini? Kwa sababu *ZANTEL* inamilikiwa na Emirates Telecommunications ya Durban, *MEHECO International* ya Dar es Salaam, *Cantibar Investment ya United Kingdom* na Serikali ya Zanzibar. Kwa hiyo, *ZANTEL* ni ya kwetu, wakati mwingine tunailalamikia, tunasema ooh inatuibia nini? Hapana, *ZANTEL* ni ya kwetu kabisa. ZANTEL ni ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wako wanaosema *TTCL* inataka kuuwawa na *ZANTEL* kwa sababu ya ku-*route traffic*, hapana. Kwa mfano jana tu huyu Bwana Salim *El-kindi* wa *ZANTEL* amenieleza mambo muhimu tu kwamba kwa kweli uhusiano wa *TTCL* na *ZANTEL* ni mzuri sana. *TTCL* inapitisha simu zake nyingine kwenda Uganda na Kenya kupitia *ZANTEL* na *ZANTEL* vile vile inapitisha simu nyingine toka nchi za nje kupitia gate way ya Dar es Salaam kwa hiyo biashara inaendelea kushamiri. Hivi karibuni *ZANTEL*itaenda Rwanda, Sudan, Ethiopia, Burundi, Malawi moja kwa moja kwa nini *TTCL* iende Ulaya na isiende Zanzibar kwenda Malawi au Rwanda au mahali popote ambako inaweza kwenda moja kwa moja? Hili ndio suala la *TTCL,* Mheshimiwa Mutungirehi ameamua kutojiuzulu na mimi nampongeza sana kwa sababu wananchi wa Kyerwa watapata uwakilishi mpaka mwisho wa kipindi cha Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna miradi mingi, tutaitolea maelezo kwa maandishi kwa wote wale ambao wameuliza. Mheshimiwa Chitalilo tutamjibu, tutazungumza kusaidia Jimbo lake la Buchosa. Hatuna haja ya kumsindikiza mgombea mwingine aje kwa Mheshimiwa Chitalilo, hapana.

Mheshimiwa Haroub ameomba Mheshimiwa Maua Daftari aende naye Jimboni kwake, mimi sina matatizo isipokuwa namshauri aombe ruksa kwa mume wake. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Kigwalilo amezungumza kwa uchungu sana kuhusu Liwale, Liwale inaniuma sana mimi vile vile kwa sababu kila nikimkumbuka Simba wa Vita, nasema

afadhali kwa kweli tujitahidi kupeleka simu Liwale kwa ajili ya kumpa heshima. Ndugu Mbowe yuko hapa ananisikiliza tutajitahidi na sehemu nyingi Ruangwa, Simanjiro, Kondoa nilikuwa huko tutapeleka, Kilindi, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Itigi naambiwa mwaka 2004 iwapo hali ya fedha itakuwa nzuri, tutafika Itigi. Nashukuru kwamba amesema na mimi ni Mbunge wa Manyoni, Mbunge wa tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilidhani nina saa nzima, kiwanja cha ndege ni kitovu cha biashara, kiwanda muhimu sana kwa hiyo ni muhimu tukiongeze kwa sababu traffic inakuwa ni 5.5% kwa mwaka ili tufike 2015 kwa kweli lazima tukifanye kiwe kikubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tathmini, tathmini ilifanywa nataka kumhakikishia Mheshimiwa Makongoro Mahanga kwamba ukifika wakati wa kulipa tutafanya tathmini mpya kufuatana na viwango vya sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tumepima viwanja 1700 Pugu Kajiungeni na hivi sasa tunapima viwanja Pugu Mwakanga 1800, tutatengeneza Hati tutakabidhi mkono kwa mkono unahama unapata Hati yako, hamna usumbufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikia kilio cha wananchi wa Kipawa, Kipunguni, Kigilagila na namhakikishia Mheshimiwa Mahanga kwamba Serikali itatoa uamuzi thabiti na wa mwisho katika kipindi kisichozidi miezi miwili. Nasema hivyo kwa sababu taratibu za Serikali mnazijua na suala hili ni zito, fedha ni nyingi na Serikali nzima lazima iseme katoe tamko hilo. Hilo ndilo linangojewa lakini tutazingatia sana kilio cha Mheshimiwa Mahanga na Mheshimiwa Wejja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Mahanga kwa sababu alivyonieleza jana anatekeleza kwa vitendo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mengine nitajibu wakati wa kipindi cha Kamati ya Bunge Zima.

**NAIBU SPIKA:** Endelea tu.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Naomba niendelee, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, toa hoja tu.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba niendelee. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hili limewasumbua wenzetu wanaotoa hoja, Kanuni inawataka wajibu kwa saa moja kwa hiyo wenyewe wanafanya utaratibu wa

kugawana. Kama ni nusu saa kwa nusu saa, dakika 20 kwa dakika 40 hiyo ni uamuzi wao. Lakini hoja imetolewa, hatua inayofuata, Katibu!

*(Hoja iliamuliwe na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 62 - WIZARA YA MAWASILIANO NA UCHUKUZI**

Kif. 1001 - *Administration and General* ..Sh.1,061,748,300/=

**MWENYEKITI:** Kabla hamjachangia, nimepeta taarifa kutoka kwa mtoa hoja kwamba kuna marekebisho ya mahesabu sasa utayasema pale tutakapofika kwenye kifungu ambacho ungependa kirekebishwe.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 1001, 250100, nimetoa maelezo hapa suala la *TTCL* nimelielewa kwa jinsi nilivyolielewa kwa hiyo sitaki majibu ya ziada. Lakini katika suala la *Celtel* nimesema kwamba kati ya bilioni 60 zilitolewa ni bilioni 55 ambazo zilipaswa kwenda Hazina lakini hizo hizo zikatumika kuanzisha Kampuni Tanzu ya *Celtel*. Sasa nataka ufafanuzi kama huo ndio ukweli mwekezaji aliwekeza nini kwa sababu zile ni za Serikali ya Tanzania tulikuwa tunalipwa na kama aliweka, aliweka asilimia ngapi?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba zaidi kidogo ya dola 50 milioni zilitumiwa kuanzisha *Celtel.* Sasa ikumbukwe kwamba *TTCL* ilikuwa tayari imeshapata leseni toka Serikalini ya kuanzisha huduma ya simu za mkononi na makubaliano yalikuwa ni kwamba fedha zitaingia *TTCL* ili kuboresha huduma za simu nchini haikuwa kwamba zinakwenda Hazina, Serikalini, hapana. Kwa hiyo, *TTCL* kwa ujumla wake maana yake pamoja na Serikali ya Tanzania tulikubali kwamba wanaweza kuanzisha huduma ya simu za mkononi ikiwa ni Kampuni Tanzu ya *TTCL* matokeo yake, matunda yake wote mmeyaona, ahsante.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani katika *logic* ya kawaida ya kimahesabu hizo ni hela tulimwambia yeye atachangia hisa kiasi fulani na ni kampuni mbili tofauti sasa kama ndivyo mlisema zitaingia zikaboresha, yeye huyo bado anahesabu na hiyo ni sehemu ya hisa zake katika *Celtel* au anasema ni hisa ile ambayo kwenye *TTCL?* Maana tunataka logic ya mahesabu hayo ili tuone yeye aliweka ngapi kwa sababu zile alishatulipa ni za kwetu.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleweke kwamba makubaliano yalikuwa ni kwamba fedha zote ambazo zimelipwa na huyu mwekezaji, zingeingizwa *TTCL* kuendeleza huduma za simu zisingekwenda Hazina kwa hiyo hizi shilingi milioni 60 zilikwenda *TTCL*. Sasa namna

*TTCL* itakavyozitumia ilikuwa si mwekezaji tena isipokuwa ni *TTCL* kwa ujumla wake wenye hisa ikiwa ni pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Vote* ni hiyo hiyo, *program 10, subvote 1001, item 250100,* Mimi nina tatizo dogo, naomba kupata ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri, kwanza namshukuru kwa kutenga hizo pesa kwa ajili ya Bandari ya *Mbambabay.*

Mheshimiwa Spika, katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 43 juu ya mradi wa gati *Mbambabay* amesema fedha zitakazotumika kwa ujenzi wa gati hiyo ni shilingi 250 milioni lakini kwenye Kitabu cha Maendeleo, Kitabu cha Nne, ukurasa 168, imeelezwa kuwa mwaka wa fedha wa 2002/2003, Wizara ilipata shilingi milioni 60 hazikutumika na mwaka huu 2003/2004, Wizara imepewa shilingi 100 milioni ni chini ya kiasi walichoomba cha shilingi 760 milioni. Kitu ninachotaka kufahamu kuna tofauti kati ya data kwenye Kitabu cha Nne na fedha alizoeleza Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 43 shilingi 250 milioni, tofauti ya shilingi 90 milioni iko katika item gani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, unazungumzia Kitabu cha Nne au ni *item* hii hii?

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si mshahara wa Waziri unaweza kuzungumzia yote na mimi nimeshika mshahara wa Waziri.

**MWENYEKITI:** Sawasawa.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kufahamu tu, hotuba inaeleza zitatumika shilingi 250 milioni lakini fedha zilizopo kwenye Kitabu cha Nne inaeleza kuwa pesa zote ni shilingi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, Kitabu cha Nne hatujakifikia ni kweli mshahara wa Waziri lakini unazungumzia masuala yaliyopo kwenye *development.* Sasa ni vizuri ukasimama wakati huo ukalinganisha yaliyopo kwenye hotuba na unachoona kwenye Kitabu cha Nne, tutakupa nafasi tu.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Sawa.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nimechangia kwa maandishi na baadhi ya mchango wangu Mheshimiwa Naibu Waziri ameujibu ni juu ya nembo ya Twiga kwenye *ATCL*. Ninavyojua mimi nembo ya Twiga kwenye *ATCL* imeshanunuliwa na *Precision.* Nataka Mheshimiwa Waziri anihakikishie je, hakutakuwa na mgogoro mwingine tena kati ya *Precision* na Wizara na *ATCL?* Kwa sababu ninavyojua *ATCL* ndio *national carrier* sasa ilikuwaje wao ambao ni wabia 49% wakatushinda sisi wabia wa 51% katika maamuzi? Naomba Mheshimiwa Waziri anihakikishie hilo juu ya nembo hiyo kama kweli haitaleta mgogoro kwa sababu tayari *Precision* wameshailipia na wameichukua wanangoja tu kuanza kupaka kwenye ndege zao. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, vile vile nimechangia juu ya ukarabati wa viwanja vya ndege. Nimeafikia nao katika utaratibu wa kukarabati viwanja vya ndege lakini nikaomba ukarabati wa viwanja vya ndege ambavyo viko zaidi ya vile ambavyo vimetajwa kwenye hotuba, viwanja vya ndege vya Wilaya. Nikatoa mfano katika Wilaya yangu kiwanja cha ndege kilichopo kimeharibika lakini kuna kiwanja kingine cha ndege cha *Resolute* cha mgodi *Flying Doctors* wanapokuja hawaruhusiwi kutumia uwanja ule inawabidi waende Igunga. Sasa kama pesa hakuna basi tuombe idhini ya Wizara wawalazimishe wachimbaji wale tutumie uwanja ule kwa ajili ya Madaktari wanapokuja kutibu kwenye Wilaya yetu kuliko kushuka kilomita 60 wakati kipo kiwanja cha kilomita 10.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nembo, naomba kurudia yale ambayo amezungumza Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa anachangia hoja hii kwamba nembo ya Kitaifa yaani Twiga inarudishwa *Air Tanzania* hilo nathibitisha na tumethibishiwa kimaandishi na Mwenyekiti amenithibitishia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba nembo ya Twiga imenunuliwa na *Precision Air,* Wizara haina habari. Nembo ya Twiga itaendelea kuwa ya *ATC*, sasa kama kuna mashindano ya kibiashara hayo wenyewe watapambana katika uwanja wa mashindano lakini katika mashindano hayo najua nani atashinda ingawa wote ni wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hiyo hiyo nembo, wananchi wengi huwa wanazungumzia kuhusu ile bendera iliyo nyuma kwenye mkia wa *ATC.* Ukiangalia vizuri ile bendera sio ya Afrika Kusini zile rangi ni za bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mpangilio umefanana lakini umefanana kwa sababu za kibiashara tu kwa sababu ya wenye hisa wawili. Lakini bendera ile rangi nyekundu haipo ambapo ni mojawapo ya rangi za Afrika Kusini. Sasa mara nyingi mtaona katika hizi nembo za *Airlines* karibu nyingi zinapishanapishana kidogo tu utaona wengine wanachukua bata, wanachukua simba, wengine wanachukua simba anaruka, wengine simba anatembea basi ni biashara tu, kwa hiyo, naomba tulielewe hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukarabati wa viwanja vya ndege, ombi la Mheshimiwa Selelii kwamba tuwaone hawa *Resolute* ili waweze kutusaidia *Flying Doctors* waweze kutua katika kiwanja chao, nalichukua na tutawasiliano nao.

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mgogoro mkubwa isipokuwa tu nataka kauli ya Mheshimiwa Waziri juu ya kutuondolea adha ya simu ya kukoroga iliyowekwa mwaka 47. Kwa sababu katika mazungumzo ya kawaida aliniahidi kwamba mwaka 2002 angeweza kunifikiria kwa kutumia mtandao wa maji (simu kwa njia ya *cable)* na mimi nikaenda kuwaambia wenzangu kwamba mambo yatakwisha lakini mpaka leo tunatumia ile simu ya mkorogo ambayo imepitwa na wakati. Naomba maelezo.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilwa, Liwale, Mafia na Nachingwea ni maeneo ambayo mpaka sasa wana simu za kizamani. Nia ya Wizara na vile vile katika mpango wa *TTCL* ni kwamba ikiwezekana ifikapo mwisho wa mwaka 2004 basi simu zote hizi za kukoroga za mwaka 47 ziwe za kisasi *(digital).* Naomba na nitaendelea kuomba Mheshimiwa Chubi, Mheshimiwa Mwenda, wananchi wa Kilwa, Mafia, Liwale wawe na subira wakati tukijitahidi kutafuta fedha hizo kuhakikisha kwamba tunatekeleza mradi huo. Sisi furaha yetu ni kuona kwamba simu zote za kizamani nchi hii zinaondolewa.

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilwa tangu mwaka jana imekuwa ni sehemu kubwa ya mambo ya utalii na katika hali ya ugonjwa nafikiri unaanza kumpa yule ambayo yuko *ICU.*

Namwomba Mheshimiwa Waziri angewaambia wale wahusika angalau tuwekewe laini mbili tu za *STD* pale hotelini kwa sababu tunakosa *foreign exchange.* Hatusemi kwamba kule kuna umuhimu sana lakini pia katika *priority* nafikiri pale ambapo watu wanatuletea *forex* inakuwa safi zaidi kuliko kule kwa Ndugu yangu Liwale. Simba tu wanakuja, sasa *priority* ya namna hii inafaa. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chubi, ingefaa ujisemee mwenyewe kuliko kusema Majimbo ya watu wengine.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tukifanya mabadiliko ya mitambo, mitambo mengine ni ya *digital,* mitambo mingine huwa tunaihamisha toka mji mmoja na mwingine wakati tukingojea kuboresha huduma zaidi. Kwa hiyo, tunalichukua ombi la Mheshimiwa Chubi kuangalia nini tunaweza kufanya katika kipindi cha mpito kabla hatujaboresha huduma za Kilwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kif.1002 - *Finance and Accounts*.........Sh.617,807,000/=
Kif.1003 - *Policy and Planning*.......... Sh.929,373,900/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kif.2001 - *Transport and Communication* ......Sh.17,850,349,000/=

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hicho cha 2001, wakati Mheshimiwa Waziri akijibu hoja yangu ya wananchi wanaohamishwa Kipawa, Kipunguni na Kigilagila alitoa ahadi kwamba Serikali itatoa tamko ndani ya miezi miwili, namshukuru kwa hilo.

Lakini napenda nijue hapa kuna mambo mawili kuna wananchi kulipwa fidia ili waondoke na kuna kusitisha mradi ule. Sasa kama unalipa fidia na kwenye Bajeti yote ya mwaka huu sioni fungu lolote lililowekwa kwa ajili hiyo, hii kauli ya ndani ya miezi miwili itasaidia nini kwa sababu mwaka huu wote hamna fedha labda aseme kwamba kauli hiyo itaelekea kwenye kusitisha mradi, napenda kupata maelezo kidogo.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza, Wizara imefurahishwa sana na Mheshimiwa Dr. Makongoro, sijui kama nimesema lakini anaanzisha *Website* ya Jimbo lake na tumeahidi kwamba tutashirikiana naye kukiweka kiwanja cha ndege katika *Website* hiyo kwa maana ya *investment* zikazokuja kiwanja cha ndege cha Dar es Salaam.

Kwa maana hiyo, *option* ya kusitisha kabisa mradi huu utapunguza hata ile thamani ya *Website* kwa hiyo tunaelekea kutekeleza sana sana labda gharama iwe ya ajabu kabisa kwamba ni bora kujenga kiwanja kipya kuliko kuendeleza kiwanja hiki. Kwa hiyo, nilitaka kutoa maelezo hayo tu, ahsante.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea labda Mheshimiwa Waziri katika ile ahadi kwamba atafanya marekebisho mahali isije ikapita, ni-*declare* mimi ni mjumbe wa Kamati ya Miundombinu.

Sasa katika *vote* hii, 2001, item 280500 ukurasa wa 228 pale kwenye *transfer and subsidy,* tulipokuwa kwenye Kamati *figure* ambayo ilikuwa inaonekana kwa upande wa Hali ya Hewa *OC* ilikuwa ni 2,350,000,000 lakini kwa sasa na hasa ukienda kule kwenye Kiambatisho Na.1 ukurasa 272 unakuta *OC* ni Sh.903,226,500 lakini ukiangalia kitabu kile ambacho kimetoka Hazina, *Volume* Na.62 pia inaonyesha kwamba *OC* ni sh.2,350,000,0000 sasa naomba ufafanuzi tu kwamba takwimu ipi ni sahihi?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niwie radhi, naomba kufanya masahihisho ukurasa 272 kwa sababu nilidhani tutakwenda mpaka mwisho, Kifungu cha 62, kifungu kidogo 4001, *Tanzania Meteorology Authority* ile *figure* 903,226,500 isomeke Sh.2,350,000,000 na hii inakidhi *observation* ya Mheshimiwa Missanga.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, naona Makatibu wangu hawajaipata vizuri, *Vote* unayosoma, ni kitabu gani?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** *Volume II,* ukurasa 272 ambako inaonyesha *subvention* zote za Serikali kwa Mashirika na taasisi zake, *Vote 62* kule pembeni, kifungu 4001, *Tanzania Meteorology Authority,* kuna *figure* katikati pale ambayo ni *Other Charges* imeandikwa Sh.903,226,5000, kwa ruksa ya Hazina tunaomba isomeke Sh.2,350,000,000.

**MWENYEKITI:** Nadhani wameipata? Mheshimiwa Missanga umeridhika?

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Ndiyo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 - *Central Transport and Licensing* ...Sh.845,481,200/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 62 - WIZARA YA MAWASILIANO NA UCHUKUZI**

Kif. 2001 - *Transport and Communication* ... Sh.22,659,813,000/=

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufanya masahihisho kadhaa ambayo tayari yamesambazwa kutoka Hazina. Katika miradi ifuatayo naomba, ukurasa 166, mradi wa 3218, ule wa *Railway Interim Capacity* ufutwe umewekwa kwa makosa na pesa yake yote ifutwe. Kwa ujumla wake wote ufutwe. Hautabadili figure za mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu ukurasa 167, mradi 6217, umeandikwa *TRC Signaling System* nao naomba ufutwe kwa sababu ni sehemu ya mradi mwingine ambao tayari upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 167, mradi 6224, *Railways Telecom Network Phase III Dodoma-Tabora.* Katika kifungu kidogo 310400, kule mwisho kabisa *donor* ameandikwa na *Germany* mfadhili ni *Netherlands.*

Halafu ukurasa 168, mtuwie radhi, mradi huo huo ukurasa wa pili *donor* ameandikwa *Germany and Netherlands* na mstari wa pili *Germany and Netherlands.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho hayo kwa mradi huu wa *TRC Railways Project* mradi 6224, unaoanzia ukurasa 167, vile vile yako katika ule mstari unaosema *total of project* kwenye *estimate* za mwaka 2003/04. *Local* ni sawa bilioni 200, lakini *forex* ni 1,237, 411,600. Kwa maana hiyo jumla nzima inabadilika na kama nilivyosema haitabadilisha mahesabu huko mbele. Inakuwa 1,437,411,600. Naomba mwendelee kutuwia radhi ni masahihisho ambayo...

Mheshimiwa Spika, *project 6225* ile imeandikwa *TCCIC* kichwa cha mradi ni *ICT (Information and Communication Technology) Strategy and Development.* Sasa pale kwa kweli namba inayohitajika ni moja tu kwenye *total of project* ambayo baadaye

Hazina inapofanya masahihisho itarekebisha vifungu vidogo. Total siyo bilioni mbili kwa kweli ni fedha kidogo, *total of projection* ambayo mwaka 2003/04, *local* ni sifuri, *forex* ni 672, 802,240. Hiyo inabadili hata ile *total* vile vile. Namba hiyo tunaipeleka mbele kule, namba hiyo hiyo ambayo ni *total* sasa inarudiwa tena inakuwa 672, 802,240.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu mradi 6227, kichwa cha habari cha mradi ni *Development of Bukondo, Shirati and Kinesi Bert,* kama Hazina ilivyoleta masahihisho kwa Bunge lako Tukufu isomeke *Development of Bukondo, Shirati,* Kinesi, Kasanga and *Nansio Berths* kama nilivyosoma katika hotuba. Halafu mradi 6228, unasomeka *Study on Berths Development on Lake Nyas a Ports,* naomba kwa mabano iongezwe *(Mbamba Bay Ports).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa 169, ule mradi 6237, *RSPS* Trunk ufutwe upo hapo kwa makosa. Halafu mradi 6239, unaofuata Kaliua *Mpanda Railway* usomeke *Kaliua Mpanda and Manyoni Singida Railway* ili tupate kibali cha kutekeleza yote miwili. Sasa Mheshimiwa Mwenyekiti, katika huu mradi wa Kaliua Mpanda, Manyoni Singida naomba twende kwenye makisio ya 2003/04, tukienda pale kwenye 310990 *Construction of Other Civil Works,* mwaka tunaouombea fedha wa 2003/2004 *forex* ni 16,866,313,000. Kwa maana hiyo kwenye *total of project* kwenye *forex* tunaishusha namba ile ile 16,866,313,000. Ile *line* ya mwisho vile vile imekosewa kwenye *local tu*naishusha inakuwa ni *one hundred million* siyo *five hundred million.* Vitabu hivi vilitolewa kabla ya kufanya masahihisho.

Halafu tunaishusha ile kwenye *total of sub vote* tunaishusha vile vile kwenye *forex 2003/2004,* inakuwa 16,866,313,000. Kwa maana hiyo zile *total* za mwisho huku zitabadilika vile vile. Ukichukua 31099 kifungu kidogo mwisho baada ya *World Bank* tunaileta ile ile 16,866,313,000 halafu nairudia tena kwenye *total of projects.* Kwa hiyo, *total* ya mwisho ya *Sub vote* inakuwa ni 16,966,313,000 kwa *Sub vote* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. CHIFU ABDALLAH S. FUNDIKIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona masahihisho ya namna hii hayafai kwa sababu Bunge linakuwa *confused* ikiwa kuna masahihisho mengi hapa, hapa, hapa. Inaonyesha kwamba kuna *muddle thinking* katika *counterpart of Treasury.* Kwa hiyo, ingefaa kabla ya kufika katika *Committee Stage* iwe wameyaandika yote na yamesambazwa mapema kwa Waheshimiwa Wabunge ili yaweze kuonekana lakini kuleta kwa namna kama hii inabidi tuitikie tu bila kufahamu kinachobadilishwa ni nini.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Chifu Fundikira, ni kweli, utaratibu mzuri ni kwamba iletwe mapema tena kwa maandishi.

**MBUNGE FULANI:** Walileta.

**MWENYEKITI:** Labda Mheshimiwa Chifu hajaona, sijui. Walileta?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, masahihisho hayo wanayo, basi Chifu kumbe walileta. Lakini ni utaratibu mzuri kama alivyosema Chifu, mlifanya vizuri kuleta mapema na iwe ndiyo utaratibu. Kukiwa na marekebisho ya namna hii unaleta mapema ili Waheshimiwa Wabunge waweze kufuatilia vizuri.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nina wazo dogo tu. Ukurasa 168, *Project 6228, item* 310700. Mimi nataka tu kuweka sawa mambo, sina tatizo kubwa ila ni ufafanuzi wa hapa na pale. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 43 ameelezea pesa kwa ajili ya mradi huo ni 250,000,000/= lakini jumla ya fedha zilizotengwa mwaka wa fedha 2002/2003 ni 60,000,000/= hazikutumika na mwaka huu zimetengwa 100,000,000/=. Sasa hapo kuna tofauti kati ya takwimu zilizoelezwa kwenye ukurasa wa 43 na fedha kamili zilizotengwa kwenye kitabu cha maendeleo. Naomba kufahamu hizo 90,000,000/=, tofauti hiyo ipo katika *item* gani, ningeomba tufahamu.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Namshukuru sana Mheshimiwa Dr. Luoga, nikisoma tena hotuba yangu ukurasa wa 43 naona kwamba nilivyoiandika, ile jumla ya miradi yote ni shilingi 250,000,000/= siyo kwa mradi mmoja, ni jumla ya miradi yote niliyoitaja katika ile aya. Ni pamoja na Kinesi, Bukondo, Shirati, ukarabati wa gati ya Nansio, gati ya Kasanga na maandalizi ya ujenzi wa gati ya *Mbamba Bay* katika Ziwa Nyasa ambao umetengewa 100,000,000/=.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 - *Aerodromes* ... ... ... Shs. 1,300,000,000/=

**WAZIRI WA MAWASILIANO NAUCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya rekodi tu, naomba kusisitiza tu kwamba Hazina ilileta marekebisho haya mapema na leo asubuhi yaligawiwa. Ninachorudia ni kwa ajili ya wale ambao na lazima nipitie ili kwa kweli kibali kitoke hapa kwa sababu kibali lazima kitoke kwenye Kamati ili ripoti iende kwa Bunge zima. Sasa sahihisho dogo ukurasa wa 170, ile *Construction of Singida Airport* mradi namba 6226, inaonyesha katika *approved local estimate* pamoja na kwamba mwaka jana 2002/2003, ilikuwa ni sifuri lakini kwa kweli Bunge lako Tukufu liliidhinisha 100,000,000/= ambazo zimetumika. Kwa hiyo, naomba badala ya sifuri kwa rekodi iwe 100,000,000/= kwa ajili ya *Singida Airport* na mwaka huu vile vile tumepata 100,000,000/= si haba. Tutaendeleza kiwanja cha ndege cha Singida polepole. (Makofi)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ya Mwaka 2003/2004, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha pamoja na mabadiliko. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi yalipitishwa na Bunge)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Kuhusu utaratibu Mheshimiwa Mutungirehi.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 104(2). Katika kanuni hiyo wakati nachangia nilisemea mambo mawili, la *TTCL* hilo nimepata maelezo na nimekubaliana nalo. Lakini la *Celtel* kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri mimi sikuafikiana nayo kwa sababu ameniambia ile ilikuwa ni kampuni tanzu ya *TTCL* na mimi nikamwambia kama ni Kampuni Tanzu basi ni ambazo ni tanzu lakini zina mitaji tofauti na wanaita tofauti na kila mmoja ana mtaji wake au hisa zake katika hisa hizo. Kwa hiyo kwa msingi huo nakusudia na natoa taarifa kwamba itakapofika muda nitaleta hoja hapa ili tuweze kuunda Kamati Teule ya kuchunguza hiyo kwamba hizo bilioni 55 zilizokwenda ni za Watanzania wenyewe au na huyo ambaye anatudhulumu na yeye anataka kusema ana hisa hapo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mutungirehi ametumia kifungu cha Kanuni zetu, Kanuni ya 104(2) ambayo inasema hivi: "Kamati Teule yaweza pia kuundwa endapo baada ya Bunge kujadili hoja fulani litaamua kupeleka jambo fulani linalotokana na hoja hiyo kwenye Kamati Teule ambapo utaratibu wake utakuwa kama ifuatavyo:- Mara tu baada ya hoja iliyokuwa ikijadiliwa kuamuliwa na ndiyo hii, mara tu ilipoamuliwa hii hoja, nayo tumeiamua sasa hivi. Mbunge yeyote mwenye nia ya kutoa hoja chini ya Kanuni hii aweza kusimama mahali pake na kutoa taarifa ya mdomo kwamba anakusudia kuleta hoja ya kuunda Kamati Teule. Baada ya hapo Mbunge huyo atatoa taarifa ya hoja yake kwa maandishi kwa Katibu na hoja hiyo itashughulikiwa wakati unaofaa kwa kuzingatia mpangilio wa shughuli uliowekwa na Kanuni ya 23(4)".

Mheshimiwa Mutungirehi amesimama, ametoa taarifa anakusudia kuleta ombi la kuunda Kamati Teule naye atapaswa kufanya hivyo kwa maandishi kwa kumpelekea Katibu na kwa kanuni hii hakuna uamuzi mwingine isipokuwa kuipanga ili iweze kujadiliwa nayo itafuata misingi ya Kanuni ya 23(4). Hii mara nyingi nimeisema sema hapa. Kanuni 23(4) inaelezea tu mpangilio kama unavyoonekana kwenye *Order Paper,*

inaanza kiapo cha uaminifu na yote hayo.  Kwa hiyo, Mheshimiwa Mutungirehi sasa kazi kwako na tunasubiri maendeleo ya hilo ambalo unakusudia.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kufika hapo sasa naahirisha Bunge mpaka Jumanne saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.28 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne Tarehe 8 Julai, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*